

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Thelathini na Tano – Tarehe 24 Mei, 2021**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, *Asalam alaykum.*

**WABUNGE FULANI:** *Waalaykumu s-salam*

**SPIKA:** Bwana Yesu Asifiwe.

**WABUNGE FULANI:** Ameen.

**SPIKA:** Kama mnavyojua wiki iliyopita tulipata msiba wa kuondokewa na ndugu yetu, rafiki yetu, Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde. Tulipata nafasi ya kupumzika siku ile ya msiba kama ambavyo Kanuni zetu zinaelekeza lakini pia tulifanya maandalizi ya mazishi na baadhi yenu mliweza kushiriki kule Pemba, tunawashukuru sana.

Kwa niaba ya Bunge, napenda kutoa salamu za pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na kwa Watanzania

kwa msiba huu mkubwa ambao tumeupata wa ndugu yetu. Alikuwa ni Mbunge mahiri sana aliyelichangamsha Bunge na aliyekuwa akiongea hoja zenye mashiko lakini kama ambavyo Bwana alitoa, Bwana ametwaa, Jina lake lihimidiwe.

**WABUNGE FULANI:** Ameen.

**SPIKA:** Napenda kutoa taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya mabadiliko kama mnavyofahamu tayari na katika mabadiliko kadhaa mojawapo ambalo amelifanya ni la Katibu wa Bunge. Aliyekuwa Katibu wetu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai sasa ni Mheshimiwa Stephen Kagaigai, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro na badala yake ameteuliwa Ndg. Nnelwa Mwihambi kuwa Katibu mpya wa Bunge. Naomba nimtambulishe mbele yenu sasa Katibu mpya, ahsante sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Kama mnavyofahamu Bunge letu lilianza zamani sana. Hivi Makatibu, Bunge lilianza mwaka gani?

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, ndc - KATIBU WA BUNGE:** Mwaka 1926.

**SPIKA:** Nilikuwa natafuta Bunge halisi lilianza mwaka gani, ni mwaka 1926 (*LEGICO*). Kwa hiyo, bado miaka mitatu/ minne kutimiza miaka 100 ya Bunge la Tanzania. Katika miaka hiyo 100 ya Bunge la Tanzania ndiyo mwanamke wa kwanza kuwa Katibu wa Bunge. Kwa hiyo, kwa kweli tunampongeza, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wote tumpe ushirikiano wa kipekee, tuoneshe kweli kwamba wanawake wanaweza, asanteni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Katibu!

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**KIAPO CHA UAMINIFU**

Waheshimiwa Wabunge wafuatao waliapa Kiapo cha Uaminifu:-

1. Mhe. Dkt. Florence George Samizi
2. Mhe. Kavejuru Eliadory Felix

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**SPIKA:** Ahsante sana Mjumbe wa Kamati, Mheshimiwa Khadija Aboud, Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza maswali, nitoe mwongozo tena kwa sababu tunazidi kuwa wazoefu sasa. Kipindi cha maswali kwa wakati huu wa bajeti ni saa moja tu, maswali yote kumi; ni ngumu sana ku-*run* kwa utaratibu huo lakini tutajitahidi sana kwamba twende kwa muda huo uliopangwa ili ratiba nyingine nazo ziweze kwenda kama zilivyopangwa tusile muda wenu wa uchangiaji na kadhalika. Kwa hiyo, naomba tujielekeze kwenye lengo la Kikanuni la muda huu, nao ni kwamba unatakiwa uulize swali, habari ya kujenga hoja, kuzunguka, kufanya hivi ni kutupotezea muda; tuulize swali. (*Makofi*)

Waheshimiwa Mawaziri mjibu maswali, msizunguke. Ni lini jambo fulani wewe sema lini basi umemaliza, sijui kitu gani kitu gani jibu moja kwa moja. Kinachotakiwa ni jawabu na hata majibu yenu yale ya msingi huna sababu ya kuwa na jibu la ukurasa mzima. Zipo Wizara zinajibu vizuri sana zinakwenda moja kwa moja lakini zipo Wizara ambazo yaani ngonjera nyingi, hatuhitaji, hapa ni maswali na majibu basi, hakuna kitu kingine. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba sana kuanzia kesho sasa baada ya kutoa mwongozo huu wote tujielekeze hivyo, unayesimama uliza swali kwa sababu vinginevyo tutakukalisha chini, tukikukalisha chini ni aibu kwa wapiga kura wako, haipendezi, ndiyo maana huwa tunavumilia kidogo lakini sasa usituvute mpaka inafika mahali tukukalishe, jipange uliza swali. Walio wengi wanauliza swali lilelile yaani swali lake la nyongeza linakuwa lilelile la msingi, huwa tunanyamaza tu. Kama umeridhika na jibu unatulia sio lazima uulize swali la nyongeza lakini kama lipo la nyongeza basi linapaswa liwe la nyongeza maana lipo tofauti kidogo na swali la msingi lakini bado lipo katika misingi ya swali la msingi. Kwa hiyo, natumaini mwongozo huu utatusaidia.

Tuwe tunaangalia Mabunge ya wenzetu pia kipindi kama hiki cha maswali na majibu yaani ni swali jibu, ndiyo lengo la kipindi hiki.

Kwa hiyo, baada ya mwongozo huo sasa tunaendelea na maswali, tunaanza na swali la Mheshimiwa Nicholas George Ngassa, Mbunge wa Igunga, karibu sana Mheshimiwa Ngassa.

Na. 283

### **Hitaji la Gari la Wagonjwa - Hospitali ya Wilaya ya Igunga**

**MHE. NICHOLAS G. NGASSA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaipatia Hospitali ya Wilaya ya Igunga gari la kubebea wagonjwa kwa kuwa lililopo limechakaa sana?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa TAMISEMI, hili ni moja ya majibu mafupi na mazuri, hongera Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nicholas George Ngassa, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, gari la wagonjwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Igunga ni chakavu na halifai kuendelea kutumika. Kwa sasa Hospitali ya Halmashauri ya Igunga imepatiwa gari la Kituo cha Afya kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Igunga kutoka katika Kituo cha Afya cha Choma ambalo linatoa huduma katika Hospitali ya Wilaya ya Igunga.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto za uchakavu wa magari ya kubebea wagonjwa katika Hospitali na Vituo vya Afya nchini. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kununua magari ya kubebea wagonjwa na itatoa kipaumbele kwa Hospitali na Vituo vya Afya vyenye uhitaji mkubwa wa magari ya kubebea wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia bajeti ya mwaka 2021/2022 imeweka mpango mahsusi wa kununua magari ya kubebea wagonjwa ambayo yatapelekwa kwenye halmashauri...

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hayo unayoyasema hayapo katika majibu yako ya msingi, ndiyo yale ambayo tunasema mnaongeza muda bila sababu. Lazima twende na jibu lilelile la msingi ambalo umeliweka mezani hapa. Swali la nyongeza Mheshimiwa Ngassa.

**MHE. NICHOLAS G. NGASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Sasa naomba kuuliza swali la nyongeza kwa Serikali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Sera ya Afya ya Mwaka 2007, Sura ya 7 imeweka vigezo kwa Hospitali za Kata na Wilaya na moja ya kigezo ni lazima kuwe na gari la wagonjwa. Sasa Serikali imechukua gari la Kituo cha Afya cha Choma imepeleka Igunga na Kituo cha Afya cha Choma tena kimekosa gari. Je, Serikali haioni tunaendelea kukanyanga Sera ambayo tumejitungia sisi wenyewe? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, magari yame-*swap*.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nicholas Ngassa, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, gari la Kituo cha Afya cha Choma limepelekwa katika Hospitali ya Halmashauri ili kuweza kuboresha zaidi huduma za Halmashauri kwa kuwa Hospitali ya Halmashauri ina wagonjwa wengi zaidi kuliko Kituo cha Afya. Hata hivyo, gari hilo linafanya kazi katika vituo vyote viwili kwa maana Kituo cha Afya na Hospitali ya Halmashauri.

**SPIKA:** Ahsante tunaendelea na swali linalofuata la Mheshimiwa Charles Mguta Kajege, Mbunge wa Mwibara. Mheshimiwa Kajege tafadhali, Mheshimiwa Esther Bulaya kwa niaba yake.

Na. 284

### **Kuzihamishia *TANROADS* Barabara za Mwibara**

**MHE. ESTER A. BULAYA K.n.y. MHE. CHARLES M. KAJEGE** aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuipunguzia mzigo *TARURA* kwa kuzihamishia *TANROADS* barabara za Bulamba – Karukekere – Nakatubai – Igunchi – Mwitende na Busambara - Mugara zilizopo katika Jimbo la Mwibara?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa David Silinde, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles Mugeta Kajege, Mbunge wa Jimbo la Mwibara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya kupandisha hadhi barabara kutoka barabara za Wilaya na kwenda barabara za Mikoa yanatakiwa kuwasilishwa na kujadiliwa kwenye Vikao vya Bodi ya Barabara ya Mkoa. Endapo Bodi

itaridhia mapendekezo hayo, yanatakiwa kuwasilishwa kwa Waziri mwenye Dhamana na barabara ambaye ni Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, hatua inayofuata ni maombi hayo kupitiwa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi chini ya Kamati ya Kitaifa ya Kupandisha Hadhi Barabara ili kuona kama yanakidhi vigezo na Kamati kuridhia au kukataa kupandishwa hadhi barabara husika. Hivyo, nashauri utaratibu huo ufuatwe katika maombi ya kupandisha hadhi barabara za Bulamba – Karukekere - Nakatubai – Igunchi - Mwitende na Busambara - Mugara zilizo katika Jimbo la Mwibara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya na Mheshimiwa Kajege wameridhika, tunaendelea na swali linalofuata. Swali Na. 285 litaulizwa na Mheshimiwa Josephine Johnson Ngenzabuke.

Na. 285

**Ukosefu wa *Ultrasound* na *X-Ray* Kituo cha Afya cha  
Muyama – Buhigwe**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakipatia Kituo cha Afya cha Muyama Wilayani Buhigwe vifaa vya *Ultrasound* na *X-ray*?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, utaratibu wetu wa Bunge ni kwamba kama una swali akimaliza tu Waziri unakuwa umeshasimama palepale ili tuweze kwenda Kikanuni. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Dkt. Dugange, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA  
SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa



Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Muyama katika Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe hakitoi huduma ya uchunguzi wa *Ultrasound* na *X-ray* kutokana na ukosefu wa majengo lakini na vifaa hivyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inamuelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Buhigwe kupanga kununua *Ultrasound* kupitia mapato ya ndani wakati Serikali Kuu inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kununua *X-ray*. Aidha, ikiwa mapato ya ndani ya Halmashauri hayatoshelezi, Serikali inamshauri Mkurugenzi kukopa kupitia *NHIF* na kununua mashine ya *Ultrasound* wakati Serikali inapanga kununua *X-ray*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu unayoyasoma ni mengine na yaliyopo mezani ni mengine, mnachomekea? Napenda twende *consistently*, majibu mnyoyaleta yawe ni yaleyale kwa sababu si mmeshayafanyia kazi na mmeniandikia na nakala ninazo hapa, msichomekee. Nimesema kuanzia sasa hivi masuala ya maswali tutakwenda kama taratibu zinavyotaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Ngenzabuke nimekuona.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Hospitali ya Buhigwe ni mpya, hospitali hiyo haina *Ultrasound*, *X-ray* na gari la kubebea wagonjwa. Je, ni lini hospitali hiyo itapalekewa vifaatiba hivyo? (*Makofi*)

**SPIKA:** Sasa huu ndiyo mfano wa maswali, angalieni kwenye *tablets* zenu mfano wa maswali niliyosema. Swali la msingi Mheshimiwa Genzabuke aliuliza: Je, ni lini Serikali itakipatia kituo cha afya Munyami na mahali pengine; swali

la nyongeza: Je, Serikali ni lini; yaani ni lile lile la msingi. Kwa hiyo, huna swali Mheshimiwa.

Tunaendelea na Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Anatropia Theonest. (*Kicheko/Makofi*)

Na. 286

## **Masoko la Kimataifa la Murongo na Nkwenda**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa masoko ya Kimataifa ya Kitega Uchumi ya Murongo na Nkwenda ili kuongeza chachu ya maendeleo ya Wilaya ya Kyerwa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Viwanda na Biashara, tafadahali.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na masoko ya Kimataifa ya kimkakati kwa ajili ya kukuza biashara na mauzo nje ya nchi kwa maendeleo na ustawi wa wananchi wake. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuhakikisha masoko ya kimkakati hususan ya mipakani yanaanzishwa, kuboreshwa na kuendelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mpaka kati ya Tanzania na Uganda, Serikali iliamua kuanzisha masoko ya kimkakati ya Kimataifa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa masoko ya Nkwendana Murongo yaliyopo Wilaya ya Kyerwa Mkoani Kagera chini ya Mradi wa Uwekezaji wa Sekta ya Kilimo

Wilayani, (*DASIP*) uliokuwa unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Mheshimiwa Spika, Masoko hayo bado hayajakamilika kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo ufinyu wa Bajeti. Aidha, Serikali imeunda timu ya wataalam ili kufanya uchambuzi wa kina kuhusiana na changamoto katika miradi hiyo na hatimaye kuja na mapendekezo ya namna bora ya kukamilisha ujenzi wa masoko hayo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 500 kwa ajili ya tathmini na uendelezaji wa masoko ya kimkakati ya mipakani. Kazi hiyo itafanywa kwa pamoja kati ya Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Kilimo. Aidha, Serikali inaendelea kushirikiana na wadau wengine kutafuta fedha za kukamilisha ujenzi wa masoko ya Murongo na Nkwenda kwa wakati.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Anatropia, nimekuona.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa haya masoko yamesimama muda mrefu, kuanzia mwaka 2013 na maelezo ya Serikali kila siku ni wanatenga bajeti: Sasa swali, Kwa kuwa haya masoko ni *strategic*, Serikali haioni ni umuhimu wa kushirikisha wadau binafsi katika kuendeleza haya masoko? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Serikali imesema tangu mwaka 2019/2020 kwamba itatenga shilingi bilioni 2.9 kujenga hayo masoko, nataka *commitment* ya haya masoko kuanza kujengwa.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, mawili Naibu Waziri, Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli ujenzi wa masoko haya

umesimama kwa muda mrefu tangu mwaka 2013/2014 wa mwaka wa fedha huo, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba ilitokana na changamoto za ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mbunge wa Jimbo la Kyerwa, Mheshimiwa Innocent Bilakwate, ambaye amekuwa akiendelea kufuatia sana ujenzi wa masoko haya kwa muda mrefu na ndiyo maana tumesema tunatafuta wadau wengine ikiwemo na benki, lakini na wadau wengine ambao tulikuwa tunashirikiana nao katika kujenga masoko hayo na ndiyo maana mwaka wa fedha huu 2021/2022 unaokuja Serikali imetenga angalau shilingi milioni 500. Lengo ni kukamilisha ujenzi wa masoko hayo.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kweli *commitment* ya Serikali ni kuhakikisha tunajenga masoko ya kimkakati ya mipakani kwa sababu tunajua lengo la Serikali sasa ni kuanza ku-*access* masoko ya nje baada ya bidhaa nyingi au mazao mengi ya kilimo Tanzania kuongezeka. Kwa hiyo, ni lazima tutafute masoko ya nje. Kwa hiyo, ni mpango mkakati wa Serikali kuhakikisha tunajenga masoko ya mpakani, lakini ku-*access* masoko ya nje kupitia fursa mbalimbali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na swali linalofuata la Wizara ya Maji. Mbunge wa Kwela, Mheshimiwa Deus Sangu, tafadhali uliza swali lako.

Na. 287

### **Kusambaza Maji Kata za Miangalua na Mnokola – Kwela**

**MHE. DEUS C. SANGU** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kusambaza Maji kutoka katika mradi wa Maji Kata za Miangalua na Mnokola katika Jimbo la Kwela: -

(b) Je, ni lini Serikali itapeleka Pesa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika maeneo hayo?

**SPIKA:** Majibu ya Serikali yatatolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Eng. Maryprisca Winfred Mahundi, tafadhali majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa maji katika Kata za Miangalua na Mnokola ni asilimia 51.2. Kata hizi ya Miangalua inapata huduma ya majisafi kupitia mradi wa Maji wa Skimu ya Miangalua ya visima virefu vinavyohudumia vijiji vya Miangalua, Tunko, Movu, Kavifuti na Nampako vya Kata hiyo na kijiji cha Mnokola kilichopo katika Kata ya Mnokola.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha hali ya upatikanaji wa maji Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga inazidi kuimarika, Serikali imeendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji ambapo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya miradi mitano ya maji imetekelezwa na kukamilika katika Vijiji vya Nankanga na Sakalilo (Kata ya Ilemba), Milepa na Kisa (Kata ya Milepa), Kizungu (Kata ya Muze) na miradi minne ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji katika Kata za Mtowisa, Ikozi, Msandamuungano na Mufinga.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 2.76 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi 18 ya maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga. Aidha, Serikali itatoa fedha kwa kuzingatia miongozo ya kupeleka fedha za utekelezaji wa miradi itakayopangwa katika bajeti husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Kwela nimekuona, uliza swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Wizara, naomba kuuliza:-

Serikali ina mpango gani wa kutanua mradi wa maji wa Mji Mdogo wa wa Laela ili uweze kupeleka katika Kata ya Mnokola na Miangalua kwa sababu hivyo visima vimeshindwa kukidhi mahitaji ya wananchi katika Kata hizo?

Swali la pili, katika Tarafa ya Kipeta ambayo ina Kata ya Kapenta, Kaoze, Kilangawana, Kipeta ni Kata ambazo zimekuwa na shida ya maji kwa takribani tangu uhuru wa nchi hii...

**SPIKA:** Mheshimiwa swali lako la pili haliko katika *line* ya swali la kwanza. Jibu swali lile la mwanzo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Serikali inao Mpango wa kusambaza maji kutokana na vyanzo mbalimbali tulivyonavyo, na tutahakikisha tunafanya hivyo hivyo pamoja na chanzo hiki cha Rahela pia tutaenda kukifanyia kazi mwaka ujao wa fedha.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi.

Na. 288

### **Kurasimisha Bandari ya Mbweni**

**MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurasimisha Bandari ya Mbweni kuwa Bandari ndogo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbuge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamamizi wa Bandari Tanzania (*TPA*) imekamilisha kazi ya kutambua Bandari bubu zote zilizo katika mwambao wa Bahari ya Hindi ikiwemo bandari ndogo ya Mbweni kwa ajili ya kurasimishwa kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania kwa kushirikaina na Manispaa ya Kinondoni, zipo katika hatua ya kutambua mipaka ya eneo la bandari hiyo kwa upande wa bahari na nchi kavu ili kuweka miundombinu rafiki kama vile maegesho ya majahazi, barabara, ofisi, choo, maji, umeme na ghala la kuhifadha mizigo.

Mheshimiwa Spika, tangu mwezi Februari, 2020, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania imepeleka wafanyakazi na mashine za *POS* katika bandari ndogo ya Mbweni ili kusimamia shughuli za kibandari na kukusanya mapato. Katika miezi tisa ya mwaka wa fedha 2020/2021 (Julai 2020 hadi Machi 2021), *TPA* imeweza kukusanya kiasi cha shilingi milioni 117. Mapato hayo yanatarajiwa kuongezeka baada ya kuirasimisha bandari hiyo na kuiwekea miundombinu muhimu.

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa ipo katika hatua za mwisho za kumpata Mkandarasi Mshauri ambaye pamoja na mambo mengine, atafanya usanifu katika Bandari za Mbweni na Kunduchi na kushauri aina ya uwekezaji wa miundombinu itakayofaa katika bandari hiyo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi umesimama nimekuona.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, bandari hiyo sasa imesharasimisha na ninaipongeza sana Serikali: Je, Serikali sasa ina mpango gani wa muda mfupi kuboresha eneo hilo ili liweze kufikika?

Swali la pili; kwa kuwa wanawake wa Kata ya Mbweni ni wadau wakuu katika eneo hilo la bandari: Je, Serikali ina mpango gani ya kuwatengea eneo mahususi kabisa ya kufanya shughuli za ujasiliamali ili nao waweze kufahidika na fursa hiyo ya bandari? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Maswali mazuri kabisa. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya muda siyo mrefu sana tutatembelea eneo hilo. Anasema kuna shida ya barabara kwamba eneo halifikiki; tutarekebisha miundombinu ili waweze kupata huduma nzuri pale.

Mheshimiwa Spika, swali la pili amewasemea akina mama wa nchi hii na hasa Mkoa wa Dar es Salaam maeneo ya Mbweni; naomba niseme tumepokea wazo hili nzuri na jema, tutalifanyia kazi akina mama wapate sehemu maalum ya kufanya shughuli zao katika Bandari ya Mbweni. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, swali la Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete.

Na. 289

### **Mkakati wa kuendeleza Shamba la Mifugo Kitulo**

**MHE. FESTO R. SANGA** aliuliza:-

Je, upi ni mkakati wa Serikali wa kuendeleza Shamba la Mifugo la Kitulo?



**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sanga, majibu ya swali hili, Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shamba la Kitulo ni miongoni mwa mashamba matano ya Serikali ya kuzalisha mifugo na ni shamba pekee linalozalisha ng'ombe aina ya Freisian halisi (*pure*). Mkakati uliopo ni wa miaka mitatu (2020/2021 – 2022/2023) ambao umelenga kuendeleza shamba kwa kuongeza ng'ombe wazazi kutoka 350 hadi 700, kununua madume ya ng'ombe wazazi 20, kuboresha malisho kwa kupanda malisho eneo la hekta 150, kuimarisha huduma ya uhimilishaji kufikia uhimilisha wa ng'ombe 300 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mkakati huo, Wizara kupitia Bajeti ya Mwaka 2021/2022 imenunua madume matano ya ng'ombe wazazi kutoka shamba la *Shafa Farm* lililopo mkoani Iringa, kilo 400 za mbegu za malisho kutoka Marekani na kilo 100 kutoka Kenya kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa malisho. Aidha, shughuli nyingine ni uhimilishaji ambapo ng'ombe 135 wamehimilishwa na ununuzi wa tenki la kupoozea maziwa lenye ujazo wa lita 3,000 ambapo utaratibu wa manunuzi unakamilishwa.

Mheshimiwa Spika, Shamba la Kitulo linahitaji uwekezaji wa kiasi cha shilingi bilioni 6.6 ili kufikia kiwango cha juu cha uzalishaji. Aidha, uwekezaji huu utaendelea kufanywa na Serikali kadri ya upatikanaji wa fedha kwa kushirikiana na wadau wengine wa maendeleo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza naishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini nilikuwa naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. La

kwanza, kwenye shamba hili Serikali imeeleza kwamba inaweza ikatenga shilingi bilioni sita kwa maana ya mwaka 2021/2023.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nauliza: Je, Serikali iko tayari kuingia *partnership* kwa sababu Benki ya *TADB (Tanzania Agriculture Development Bank)*, iko tayari kutoa hizi fedha na ikafanya iwekezaji kwenye shamba hilo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni maslahi ya wafanyakazi wa shamba lile kwa maana ya vifaa na madeni ya wafanyakazi wale, kwa muda mrefu hawajalipwa: Je, ni lini Serikali itakuwa tayari kuhakikisha maslahi ya wafanyakazi na pia vifaa vya shamba viwe vinanunuliwa?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Miradi mingine bwana. Mradi ambao kinachoagizwa ni madume matano na nini, halafu eti kuna wafanyakazi kibao, wana madeni wanadai. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, juu ya uwekezaji, tuko tayari na milango yetu iko wazi, karibu sana tuweze kujadili jambo hilo. Jambo la kuboresha maslahi ya wafanyakazi na ununuzi wa vifaa ni sehemu ya pesa zilizopangwa kutumika katika bajeti hii. Kwa hiyo, tunalielekea pia.

**SPIKA:** Wizara ya Mifugo tunawashauri tu mwangalie hili jambo la kumiliki mashamba ya kufuga. Serikali inamilikije? Yaani Serikali inachunga ng'ombe? Mna ranchi, kazi ambayo Msukuma anaweza, Mgogo anaweza; Serikali ifanye mambo ya maana ya Serikali. Haya mashamba mengine haya kama *Kongwa Ranch* na kadhalika, wapewe wananchi wafanye. Tuvuke yaani twende kwenye *opening-up* tuwape watu wafanye hivi vitu. Serikali inachunga ng'ombe! Hii haiwezekani. Serikali ibakie na *Research* na vitu vingine basi. Kwa hiyo Wizara ya Mifugo angalieni haya mambo, tubadilike tutoke huko. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, kwa niaba yake, nakuruhusu Mheshimiwa.

Na. 290

## **Kukabidhi eneo la Mifugo Ruvu kwa Halmashauri-Chalinze**

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE K.n.y. MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapima eneo la mifugo la Ruvu na kulikabidhi kwa Halmashauri ya Chalinze?

**SPIKA:** Bado tuko Wizara ya Mifugo, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali, majibu ya Swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mbunge wa Chalinze kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshapima na kutoa kipande cha ardhi chenye ukubwa wa hekta 2,208 kutoka Ranchi ya Ruvu kwa ajili ya matumizi ya wananchi. Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze ilikatiwa hekta 1,488 kwa ajili ya vijiji sita ambavyo ni Kijiji cha Ruvu Darajani hekta 200; Kijiji cha Kidogozero hekta 200; Kijiji cha Kitonga hekta 480; Kijiji cha Magulumatali hekta 200; Kijiji cha Vigwaza hekta nane; na Kijiji cha Milo-Kitongoji cha Kengeni hekta 400.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imepima na kutoa kipande cha ardhi chenye ukubwa wa hekta 120 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kwa ajili ya vijiji vitatu vya Kidomole hekta 40; Fukayosi hekta 40 na Mkenge hekta 40. Pia, Serikali imepima na kutoa ardhi yenye ukubwa wa hekta 600 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha Vijijini kwa ajili ya Kijiji cha Mperamumbi Kitongoji cha Waya.

**SPIKA:** Nimekuruhusu Mheshimiwa Mwuliza swali, ongeza swali la nyongeza.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na maswali mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, tatizo lilolopo Chalinze ni sawa na tatizo lililopo Bagamoyo na hasa katika Vijiji vya Mkenge Kidomole pamoja na Vijiji vya Milo. Sasa swali langu ni kwamba, kutokana na tatizo la wakulima na wafugaji eneo lillilotengwa halitoshi, ni dogo sana kwa vijiji hivyo. Ni lini Serikali itaongeza hili eneo? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo. Sijui mtapata wapi eneo la ziada kama lipo? Majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, Serikali inazingatia sana maoni na ndiyo maana hata maoni uliyoyatoa ni katika sehemu ya mpango wetu wa bajeti tunayokwenda ya kuboresha zaidi *NARCO* ili iweze kukidhi haja ya kuhakikisha kwamba wadau wetu mnafurahi na kuweza kutumia fursa ya ardhi hii kubwa na nzuri ya Serikali kuweza kufanya shughuli za uzalishaji kupitia mifugo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa hili la Bagamoyo Serikali iko tayari kupokea tena maombi ya wananchi na kuyafanyia kazi kwa ajili ya kuweza kuondoa kabisa migogoro ya wakulima na wafugaji.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri, tunasubiri bajeti yenu ije tuone lakini *NARKO* imeshindwa tangu mwaka 1967 ilipotaifishwa hayo mashamba mpaka leo, hakuna kitu. Mnafikiri ninyi ndio mtaweza? Binafsisheni, binafsisheni! Hiyo peke yake ndiyo njia ya kwenda. (*Makofi*)

Wizara ya Nishati swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Nsimbo.

Na. 291

## Hitaji la Umeme Kata ya Ugalla – Nsimbo

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Je, ni lini wananchi wa Kata ya Ugalla watapatiwa umeme wa *REA* III?

**SPIKA:** Majibu ya swali hili, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Nsimbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) inaendelea na utekelezaji wa miradi ya kupeleka umeme vijijini kwa nchi nzima kwa kupeleka umeme katika vijiji ambavyo havijafikiwa na umeme.

Mheshimiwa Spika, vijiji tisa vya Jimbo la Nsimbo ambavyo havina umeme ikiwa ni pamoja na Vijiji vya Kata ya Ugalla vya Katambike, Mnyamasi na Kasisi vitapatiwa umeme kupitia Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu mzunguko wa pili unaoendelea. Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwezi Machi, 2021 na unatarajiwa kukamilika Desemba, 2022.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kupeleka umeme katika vijiji hivyo inahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33, urefu wa kilomita 63.6; msongo wa kilovoti 0.4, urefu wa kilomita 3.0; na ufungwaji wa transfoma tatu, pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali zaidi ya 66. Gharama ya mradi ni Shilingi bilioni 2.46

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mbunge wa Nsimbo, Mheshimiwa Anna Lupembe.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Hii Kata ya Ugalla na huo mradi anaosema umeanza mwezi Machi, lakini hakuna dalili yoyote ya mradi, hakuna kitu chochote; na wananchi katika kata hiyo wamesubiri kwa muda mrefu, ni kata; kuna Kata ya Litapunga na Ugala wana miaka mingi wanaona wenzao wanapata umeme lakini wenyewe hawajawahi kupata umeme wala dalili ya nguzo hamna, lakini hapa ameniambia kuwa mwezi Machi mradi umeanza. Sasa hapo kidogo napata wasiwasi kwa sababu hamna dalili kabisa, hakuna dalili ya umeme. Sasa naomba basi Naibu Waziri aji-*commit* twende akaone ili ajue hali halisi ya wananchi kwa jinsi wanavyopata tabu.

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; wananchi katika vijiji vingine wanalipia umeme Sh.27,000, lakini wanachukua muda mrefu sana miezi sita, saba mpaka nane hawaingiziwi umeme, basi Waziri atueleze wakilipa inachukua muda gani ili wananchi wanaweza kupata umeme? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri umesema utekelezaji wa mradi huu umeanza mwezi Machi, Mheshimiwa Mbunge anasema hakuna kitu kama hicho hata nguzo moja hakuna, unachotakiwa kujibu hapa je umelidanganya Bunge? Majibu tafadhali Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Lupembe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa upelekaji umeme wa awamu ya tatu, mzunguko wa pili, ulisainiwa na kuzinduliwa rasmi mwezi Machi na hatua kwa hatua zimekuwa zikianza sehemu moja moja kuendelea. Kwa mfano Mtwara wameendelea, Jumamosi iliyopita Mheshimiwa Waziri alizindua tena Arusha, kwa hiyo kufikia Disemba mwakani ndio maeneo yote yatakuwa yamekamiliika. Kuna maeneo mengine yameshaanza, mengine bado yanaendelea, lakini

hatua za kupeleka nguzo zimeanza. Kwa hiyo uzinduzi ndio ulikuwa mwezi Machi mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kwenye maeneo mengine kama alivyosema kwake, watu wanapolipa umeme zinachukuliwa zile hatua sasa za kupeleka vifaa mbalimbali kwa wale wananchi waliolipia kama nguzo kama waya kwa pamoja ili sasa tuweze kufunga kwa pamoja. Hata hivyo, tunachofanya tunaweka utaratibu angalau tuseme ndani ya mwezi mmoja, kila mtu aliyelipia umeme awe ameupata kulingana na mazingira aliyokuwa nayo. Pengine kwenye *three phase* inachukua hadi pengine siku 90, lakini tumekuwa tukijitahidi kuhakikisha kwamba kila aliyelipia umeme anaupata na anaupata kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri sasa urudi ujibu swali. Umeeleza habari ya Machi sijui kulikuwa na uzinduzi na nini, swali la Mbunge linasema, je, ni lini wananchi wa Kata ya Ugalla watapatiwa umeme wa *REA III*? Ndio swali la msingi tangu mwanzo.

Mheshimiwa Waziri jibu swali.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Mbunge na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jibu lake la msingi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli utelekezaji wa mradi kambambe wa awamu ya tatu, *round* ya pili umeanza rasmi toka mwezi Machi mwaka huu na wakandarasi wote wameshakwenda *site*. Kesho tuna mkutano wa wakandarasi wote hapa Dodoma, kuwaarifu watoe taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge na Madiwani katika maeneo yao. Kwa hiyo inawezekana Mheshimiwa Mbunge kweli hajakutana nao, lakini wameshaanza kazi rasmi na wanakwenda kila eneo kwenye maeneo ambako wamepangiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, nitoe taarifa tu kwa wakandarasi kupitia Bunge lako Tukufu kwamba, wakandarasi wote wakaripti kwa Waheshimiwa Wabunge wanapoingia katika maeneo yao ili Waheshimiwa Wabunge wapate taarifa hizo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa Mheshimiwa Waziri usimame tena ujibu swali sasa. Je, ni lini wananchi wa Kata ya Ugalla watapatiwa umeme wa REA III? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kata ya Ugalla pamoja na vijiji tisa, wataanza kupatiwa umeme kuanzia mwezi Juni mwaka huu mpaka mwezi Mei mwaka ujao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana.

Mheshimiwa Waziri niwaambie tu ukweli, yaani tumekuwa tukivumilia hapa majibu ya blabla na ya uswahilishahili. Majibu hayajibiwi, yaani Waziri jibu swali, ukijibu swali una tatizo na meza, wala na nani na nani, pamoja na kwamba unaweza ukapamba kidogo, lakini swali lijibiwe, kwa sababu wananchi wanasikiliza, wanataka jibu lao, sio la Mbunge, ni la wananchi. Kwa hiyo tukijikita kwenye kujibu maswali itatusaidia sana. *(Makofi)*

Tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Zaytun Seif Swai.

Na. 292

### **Ufumbuzi wa Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto**

**MHE. ZAYTUN S. SWAI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mikakati gani dhidi ya vitendo vya Ukatili vinavyofanywa kwa wanawake na watoto?



**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Mwanaidi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. MWANAIDI ALI KHAMISI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaytun Swai, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo wa tatizo la ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto na kuendelea kuchukua hatua mbalimbali za kutokomeza ukatili huo. Moja ya hatua hizo ni pamoja na kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Mpango kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto wa mwaka 2017/2018 hadi 2021/2022. Mpango huu wa miaka mitano unalenga kupunguza kiwango...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumsikilize Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. MWANAIDI ALI KHAMISI):** Mheshimiwa Spika, Mpango huu wa miaka mitano unalenga kupunguza kiwango cha ukatili dhidi ya wanawake na watoto katika jamii yetu kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, jitihada nyingine ni pamoja na kuanzishwa kwa Kamati 16,343 za Ulinzi na usalama wa wanawake na watoto kwenye ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zina jukumu la kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Pia kuanzishwa kwa madawati 420 ya Jinsia na watoto katika vituo mbalimbali vya Polisi nchini ambayo huwezesha wahanga wa ukatili kuripoti aina mbalimbali ya ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imewezesha kutungwa kwa Sheria za Msaada wa Kisheria Na.1 ya mwaka 2017. Sheria hii inatoa fursa kwa wanawake waliofanyiwa unyanyasaji au kudhulumiwa kupata haki zao kupitia vyombo vya usimamizi wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhakikisha utekelezaji wenye ufanisi wa Mpango kazi wa Taifa wa kutokomeza ukatili, sheria zilizopo pamoja na kuimarisha Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri safari ijayo majibu yawe mafupi. Swali la nyongeza, Mheshimiwa Zaytun.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri kwanza niipongeza Serikali kwa kuona kuna haja ya kuwa na mpango mkakati wa Taifa wa kutokomeza ukatili. Hata hivyo, inashangaza kuona Serikali yenyewe imejiwekea asilimia 50 tu kutokomeza matendo haya, ifikapo 2022.

Mheshimiwa Spika, malengo haya bado yako chini na tunawapa mwanya...

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun nenda kwenye kuuliza swali.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; je, Serikali haioni kama kuna haja ya kujiwekea malengo ya juu ambayo yatadhibiti matendo haya na kukomesha?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kwa kuwa vitendo hivi vingi vinafanyika kwenye ngazi za kata na za vitongoji lakini madawati ya kijinsia mengi yapo kwenye ngazi za wilaya. Je, Serikali haioni kama kuna haja ya kushusha huduma hii kwenye ngazi za chini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana kwa maswali hayo. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo mawili, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. MWANAIDI ALI KHAMISI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zaytun kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nilieleza kuwa, mpaka sasa Serikali imeshaanzisha madawati 420 ya jinsia ya watoto kwa vituo mbalimbali nchini. Aidha, ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa huduma za wahanga wa ukatili zinafanyika katika kila Kituo cha Polisi na kila Kituo cha Polisi kimewekwa chumba maalum kwa ajili ya kuwahudumia wahanga hao.

Mheshimiwa Spika, vilevile wahanga hao wa ukatili uhudumiwa na Polisi ambao masuala yao yote huanzia katika Vituo Vidogo vya Polisi na kumalizia Vituo Vikubwa vya Polisi kwa ajili ya kushughulikiwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili Mheshimiwa Zaytun, ni kweli kuwa kuna sababu ambazo zinasababisha vitendo vya ukatili wa kijinsia ni uwepo wa imani za ushirikina. Serikali ishaanza kushughulikia suala hili ili kutekeleza mpango wa Taifa na kutokomeza ukatili dhini ya wanawake na watoto. Aidha, nimuahidi kuwa nitalifuatilia suala hili na kuhakikisha wanawake wote wa Arumeru na Monduli wanakuwa salama pasipo na kunyanyaswa. Pia ni watake Maafisa wa Maendeleo ya Jamii Arumeru na Monduli kupanga mpango kazi maalum ili kuwaendeleza wananchi wa Arumeru kukabiliana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaelekea Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Vicent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini, endelea.

Na. 293

## **Mgogoro wa Hifadhi ya Lwafi – Nkasi Kusini**

**MHE. VINCENT P. MBOGO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro kati ya Hifadhi ya Lwafi iliyopo Nkasi Kusini na wananchi wa Vijiji vya Mlambo, King'ombe, Tundu na Kata ya Wampembe?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Francis Masanja, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Paul Mbugo, Mbunge wa Nkasi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Pori la Akiba la Lwafi liliwahi kuwa na mgogoro wa Kijiji cha King'ombe ambapo baadhi ya wananchi wake walivamia eneo la hifadhi kwa ajili ya shughuli za kilimo. Hata hivyo, mgogoro huo ulitatuliwa na Serikali baada ya kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo wananchi kupewa elimu na kuonyeshwa mipaka halisi.

Mheshimiwa Spika, aidha, mgogoro huo ulikwisha, lakini kuna mgogoro mwingine kwa sasa ambao ni kati ya Msitu wa Hifadhi ya Loasi yaani *Loasi River Forest Reserve* na Vijiji vya Mlambo, King'ombe na Tundu, ambapo wananchi walivamia msitu huo kwa ajili ya makazi na shughuli za kilimo. Serikali imefanyia kazi mgogoro huo kupitia mapendekezo ya Kamati ya Mawaziri Nane ambapo maamuzi ya mgogoro huo yameshatolewa na utekelezaji wake utafanyika katika bajeti ya mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa rai kwa Mheshimiwa Mbunge na wananchi wanaozunguka eneo hilo

kuendelea kutoa ushirikiano katika kuhimiza, kulinda na kutatua migogoro hiyo inayohatarisha uwepo wa maliasili zinazowazunguka.

**SPIKA:** Majibu marefu Mheshimiwa Naibu Waziri, safari ijayo uyafupishe.

Muuliza swali Mheshimiwa Mbunge wa Nkasi, Mheshimiwa Mbogo, uliza swali lako au umeridhika?

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, nimeridhika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Liwale.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Hali ya madhara yanayotokana na wanyamapori yamekuwa ni makubwa sana. Leo hii kwenye Vijiji vya Ngumbu, Kibutuka, Kiangala na Ngatapa, wananchi wameshahama wamerudi majumbani kwao kutoka mashambani, baada ya tembo kumaliza mazao yote. Sasa naomba Serikali ituambie, je, ina mkakati gani wa kuhakikisha usumbufu huu wa wanyamapori unapungua hasa kwenye hivi vijiji vichache nilivyovitaja? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, usumbufu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mbunge wa Liwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwapa pole wananchi wa Liwale, lakini pia niendeele kutoa pole kwa wananchi wengine wote wanaozunguka maeneo ya hifadhi, zikiwemo Hifadhi ambazo nimezitembelea jana za Mwanga na Same.

Mheshimiwa Spika, changamoto hii inasababishwa na wananchi kusogelea maeneo ya hifadhi, hasa maeneo yenye ushoroba, njia za wanyama pori hususani tembo, wanatembea kwa *speed* ndefu na wanatembea katika maeneo marefu na shoroba hizi zimezibwa na wananchi ambao wanafanya shughuli za kilimo lakini wengine wamejenga kwenye maeneo ambayo ni mapito ya wanyama.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaweka mkakati wa kufanya mafunzo kwa wananchi ya namna ya kudhibiti hawa tembo, lakini pia tunagawa vifaa, lakini pamoja na hilo tumeimarisha dolia za askari, kuhakikisha kwamba hawa wanyama wanapoingia kwenye maeneo ya wananchi basi askari wa doria wanakuwepo kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, nimtoe wasiwasi Mbunge kwamba suala hili Serikali inalitambua na tunaendelea kufanya kazi na hatulali mchana na usiku tunahakikisha wananchi waishi kwa amani. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsate sana. Mheshimiwa Mheshimiwa Nape Nnauye nimekuona, uliza swali la nyongeza.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na jitihada ambazo zinafanywa na Serikali, Wizara imekuwa ikisema kwamba upandaji wa pilipili kwenye maeneo ambayo yanakaribiana na vijiji una uwezo wa kuzuia tembo kuingia vijijini. Sasa, je Serikali hiko tayari kupitia *TANAPA* na taasisi zake wakapanda wao hizi pilipili ili wawasaidie wananchi wetu wasihangaikie, mazao yao yasiliwe na wao wasiuliwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mary Fransis Masanja, mnaonaje mkimwaga mbegu za pilipili mnazo ndege kule mnaweza mkasambaza tu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nape, Mbunge wa Mtama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tulishabuni mbinu mbadala za kuhakikisha kwamba hawa wanyama wakali wanapunguza kasi ya kuathiri wananchi ikiwemo pilipili lakini pia kuna mizinga ya nyuki ambao ni njia bora zaidi ya kuwafanya hawa wanyama wasiweze kusogelea makazi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, tunalipokea wazo lake, lakini kulingana na gharama Serikali itaendelea kuangalia tathmini na tunaweza tukafanya kwa awamu, kwenye maeneo ambayo yameathirika Zaidi. Hata hivyo, niwaombe tu Waheshimiwa tuendeleo kushirikiana kwenye hizi mbinu ambazo tunaendelea kuzielekeza wakati Serikali sasa inaangalia mbinu ya kudumu ambayo inaweza ikasaidia wanyama hawa kuishi katika maeneo yao na wananchi wakaishi kwa amani.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii. Waheshimiwa Wabunge natumaini tukienda hivi kipindi chetu cha maswali kitakuwa na tija Zaidi na kutakuwa na maswali ya nyongeza mengi Zaidi, kwa sababu tutajikuta tuna muda, basi nyongeza zinaweza zikapatikana kama mnavyoona. Saa moja ni mambo machache sana tunayoweza kuyafanya na sababu yake ni kwamba Bunge hili tangu lina Wabunge kama hamsini hivi enzi hizo, muda wa maswali ni huu huu.

Leo tuko karibu 400 muda wa maswali ni saa moja kwa hiyo hata uwe na bingwa namna gani hapa labda awe anaongeza muda na kwa hiyo anakula muda mwingine kwa ajili ya shughuli nyingine jambo ambalo halipaswi kuwa hivyo.

Nina mambo mawili matatu *including* matangazo na kuwatambulisha wageni; la kwanza. Waheshimiwa Wabunge Kamati zetu zifanye kazi zake, mjitahidi sana kufanya kazi zenu ambazo mnahusika hasa wale ambao

mna Kamati za Kisekta na nyingine. Msikae tu fuatilieni mambo, ninyi ndio Bunge msichae mambo yanakwenda tu hivyohivyo.

Nitatoa mfano, mtakumbuka kipindi kilichopita tulikuwa na ajira za Walimu sijui nadhani, 8,000 si ndio? Wangapi mnajua wapiga kura wenu wangapi wamepata nafasi? Mnawezaje kuwa na uhakika kwamba mchakato huu umekwenda inavyopasa? Ni kazi ya Bunge hili kufuatilia na kuwaita nyoni tuelezeni, tupe majina, ni nani na ametoka wapi? (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hii ni kazi yenu, kama sio kazi yenu ni kazi ya nani? Mnasubiri Spika awaambie? Kamati husika ninyi mnaniambia kwamba tunataka tuwaite hawa kwa ajili ya kupata taarifa hii, ninyi ndio kwa niaba ya wananchi. (*Makofi*)

Tusipoangalia tutajikuta nchi hii badala ya kuwa na utumishi wa umma wa Watanzania wote tukawa na utumishi wa umma wa baadhi ya watu katika nchi hii. Hatuwezi kwenda hivyo, Sisi tuna wajibu wa ziada wa kuhakikisha siyo tu ajira elfu ngapi, halafu basi; zimekwenda wapi na kivi? (*Makofi*)

Safari hii tunazo 6,270, kitu kama hicho, hizo 8,000 tusifuatilie wala hakuna shida kwa sababu limeshapita, lakini hizi 6,000 tuwaambie kabisa Serikali kwamba tutazifuatilia kindakindaki. (*Makofi*)

Mfumo wake uwe na uwazi, uwe unaoeleweka, uwe ambao hauna mambo mengine. Na ni vizuri kuja na *formula* huko tunakokwenda ambazo ni *inclusive*. Hata kama ni walimu basi wawepo Wamasai, Wamakonde, Wahaya, Waha, Wagogo, wote. (*Makofi*)

Tutafute mfumo ambao ni *inclusive*, unajaribu kuingiza watu wa aina mbalimbali katika nchi yetu. Tuwe na mfumo wa utumishi ambao unatoa sura ya nchi yetu ilivyo. Tujaribu kuangalia *formula* mbalimbali ambazo zinaweza



zikatusaidia, vinginevyo unaweza ukakuta tuna watumishi, maana wanavyoripoti unawaona, na wewe, na wewe na yule na yule, ohoo, unaanza kuona vitu ambavyo kidogo... tuwe makini sana katika eneo hili, ni eneo muhimu. (*Makofi*)

Hoja yangu ni kwamba Kamati zinazohusika mjitahidi kuwa macho na mambo haya ya Kitaifa katika ufuatiliaji wake. Msilibiri Spika peke yake ndio awaambie nini cha kufanya. Kwa hiyo, hizi zikishakamilika Kamati husika mtatakiwa mpate taarifa ya zoezi liliendaje ili tujiridhishe na tuishauri Serikali kama kuna maeneo ya kuweza kurekebisha.

La mwisho kabla ya matangazo Waheshimiwa, juzi Jumamosi pale Dar es Salaam, Uwanja wa Mkapa, palikuwa na mambo makubwa pale. (*Makofi*)

Kama Bunge lazima tupongeze Timu yetu ya Simba (*Simba Sports Club*) kututoa kimasomaso. Kuweza kufika Robo Fainali ya Kombe la Mabingwa wa Mpira wa Miguu Afrika nzima si padogo, si haba. (*Makofi*)

Kwa hiyo na wale marafiki zetu wengine nao wajitahidi, badala ya ligi ya hapahapa tu wajitahidi kidogo, waige wasiogope. Tunategemea mwakani, hata Namungo wamejitahidi, ni mara ya kwanza wameingia kwenye mashindano makubwa, wamejitahidi. Sasa wengine mko wapi? Badala yake tunakuwa tunashangilia wageni tu jamani, hii haipendezi hata kidogo. (*Makofi*)

Lakini mwisho wa haya si tarehe 03, Julai jamani? Ndiyo majibu yatapatikana, baada ya hapo tutakutana humuhumu kwenye Ukumbi huu tusikie mambo yakoje. Vinginevyo jamani tunawapongeza kwa kweli *TFF*, Wizara, Viongozi wa Klabu na wengine, wote wanaohusika, tunaiweka sasa Tanzania kwenye ramani ya mpira.

Tutakubaliana kwamba wale *South Africans, Kaizer Chiefs*, wameendelea, lakini yeyote aliyefuatilia mechi hizi mbili atakwambia klabu bora katika klabu zile mbili ni ipi, kabisa. Kwa hiyo, ni kuziba sasa kuangalia tu namna

ambavyo siyo tucheze tu mpira, chenga twawala, hapana, na magoli pia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naamini huku tunakokwenda, akina *Sports Pesa* nani, wote, Mheshimiwa Tarimba, naamini tunakokwenda ni kuzuri zaidi. Tutafika mbali zaidi katika malengo tuliyojiwekea kama Watanzania. *(Makofi)*

Inatupa heshima kubwa tukiimarisha katika masuala ya michezo, siyo tu mpira wa miguu lakini na michezo mingine yote. Kwa hiyo wadau wote, wapenzi, mashabiki, kwa kweli sisi kama Bunge tunawapongeza sana na tujiandae kwa mwakani. *(Makofi)*

Wageni tulionao Bungeni ni wageni 90 wa Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda, Waziri wa Kilimo, ambao ni, kwanza mke wa Mheshimiwa Waziri ambaye namuomba asimame; anaitwa Dkt. Beatrice Mkenda. Hongera sana. *(Makofi)*

Endelea kusimama mama, sijakuruhusu ukae, ili Waheshimiwa wakuone wakufahamu; jamani ndio shemeji yetu huyu. Hapana, muhimu kwa ajili ya afya, ila muhimu mjue tu kwamba hii familia ni ya Profesa na *doctor* humo nyumbani. Hongera sana shemeji yetu, karibu sana, tunakupongeza kwa kufika. *(Makofi/Kicheko)*

Katibu Mkuu, Ndg. Andrew Masawe; karibu sana Katibu Mkuu, leo na kesho tuko na wewe hapa na kilimo ndiyo uti wa mgongo, kwa hiyo leo na kesho kivumbi kitatimkwa hapa. *(Makofi)*

Naibu Katibu Mkuu, Prof. Siza Tumbo; karibu sana Naibu Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Pia wako wakurugenzi wa Wizara na wakuu wa taasisi chini ya Wizara hiyo, pale mlipo wote msimame, wakuu wa taasisi, wakurugenzi, bodi; karibuni sana wapendwa wetu. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Spika kutoka Benki ya CRDB wakiongozwa na Ndg. Chabu Mishwaro; Chabu na timu yake, karibuni sana. *(Makofi)*

Hawa ni wadau wetu CRDB na tutumie nafasi hii kuwashukuru jamani. Siku ile ya futari, nafikiri futari ya CRDB, kwa wale mliondohuria, walijiandhaa vizuri, mtupelekee salamu za shukrani, tunawakaribisha sana. CRDB ni benki ambayo Wabunge wengi wanaitumia. Tungewaomba wananchi tuendeleo kuitumia benki yetu hii. Hii ni benki ya wananchi, siyo Benki ya Yanga, hapana, ya wananchi. *(Makofi/Kicheko)*

Ahsante sana Chabu na wenzako.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 70 wa Mheshimiwa Hussein Bashe, Naibu Waziri wa Kilimo, ambao ni viongozi wa CCM kutoka Nzega, Mkoani Tabora, wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa, Ndg. Hassan Wakasuvi. Wale Wanyamwezi naomba msimame; karibuni sana Wanatabora, Wabunge wenu wa Tabora wako hapa wanafanya kazi nzuri, pamoja na Mheshimiwa Bashe mwenyewe nafikiri mnamuona kwenye kona pale; karibuni sana watani zangu, karibuni sana. *(Makofi)*

Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa, Ndg. Hassan Wakasuvi yuko upande gani? Yuko wapi? Sijamuona bado. Huyu aliyenyoosha mikono, safi sana. Karibu sana Ndg. Wakasuvi, hiki ndicho kigingi cha Tabora. Karibu sana Dodoma mtani, kabisa. Hawa ndiyo wazee, basi, nisiseme sana, ndio wazee wenyewe, ukisikia CCM ndio wenyewe hawa. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Tumaini Magesa ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Jimboni Busanda, wakiongozwa na Ndg. Joseph Mathayo. Haya, Busanda; karibuni sana. Inaandikwa Busanda lakini unapotamka unasema Usanda, unamezea ile B; ahsante sana. *(Makofi)*

Wageni 24 wa Mheshimiwa Tarimba Abbas ambao ni viongozi wa CCM Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam, wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Kinondoni, Ndg. Harold Maruma. Wale wa Dar; karibuni sana viongozi wa kutoka Dar es Salaam, karibuni sana Makao Makuu ya Nchi. Hapa ndiyo mjini, mliotoka Dar es Salaam ni mkoani, kwa hiyo hapa na sisi tuna stendi ya mkoani, mabasi yanayokwenda Dar es Salaam; karibuni sana. ((*Makofi/Kicheko*))

Mgeni wa Mheshimiwa Florent Kyombo, Mwenyekiti wa Chama cha Walimu Jijini Dodoma na Afisa Uthibiti Ubora, Ndg. Prosper Mutungi. Karibu sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Mwantumu Zodo ambaye ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania (*TSC*) kutoka Kongwa, Ndg. Rehema Mapuga. Eh, karibu dada, karibu sana. Aisee, Katibu wa *TSC*; hongera sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Fatma Toufiq ambaye ni Mkurugenzi Asasi ya Kiraia ya *Tanzania Human Rights Defenders* kutoka Jijini Dar es Salam, Ndg. Onesmo Olegurumwa. Ahsante sana Onesmo, wewe ni mtu maarufu bwana, karibu sana. (*Makofi*)

Wageni sita wa Mheshimiwa Athumani Maige ambao ni wanachama wa Muungano wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA) wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji, Dkt. Steven Ruvuga; karibuni sana MVIWATA, wale kule juu kabisa, karibu sana. (*Makofi*)

Hawa ni vikundi vya wakulima ambao wanafanya kazi nzuri sana nchi nzima; karibuni sana MVIWATA, Ndg. Dkt. Ruvuga, karibuni sana. Na mmekuja siku nzuri ambayo leo masuala ya kilimo yanajadiliwa hapa. Nawakaribisha leo na kesho muwepo ili mfuatilie vizuri Waziri wa Kilimo na Naibu wake wakishusha mambo yao hapa.

Wageni sita wa Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma ambao ni wawakilishi wa MVIWATA mikoa mbalimbali

Tanzania wakiongozwa na Mwenyekiti wa MVIWATA, Ndg. Apolo Chamwela; karibuni sana popote pale mlipo. Wale kule juu, ahsante. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Festo Sanga ambao ni wafanyabiashara wa vifaa vya umeme au *electronics* katika Jiji la Dar es Salaam ambao ni Ndg. Frank Mushi, Ndg. Issa Ibrahim na Ndg. Safiei Sekule; karibuni sana, wale kule. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Eric Shigongo ambao ni washonaji wa nguo kutoka Kampuni ya *Carenitho Cadia Company Limited* ya Jijini Dodoma wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu Ndg. Caren Ibrahim; karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa hawa ni mafundi washonaji wataalam kabisa wanakutolea suti *original* za kila aina, za kike na za kiume, wako Dodoma hapahapa na wana vitambaa vizuri sana. Kwa hiyo, baada ya hapa waoneni ili muweze kujua *address* yao na mkipata tabu ya kuwapata basi Mheshimiwa Eric Shigongo yupo kuwaelekeza vizuri. Vile mnavyomuona Eric Shigongo anavyopendeza, ni vijana wetu wa Dodoma hapahapa.

Wageni sita wa Mheshimiwa Flatei Massay ambao ni wanamaombi kutoka Mkoa wa Manyara wakiongozwa na Ndg. Maglan Mollel; karibuni sana wanamaombi, wale pale. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Najma Giga na Mheshimiwa Bahati Ndingo, ambaye ni Katibu Mkuu wa Umoja wa Wazazi Tanzania, Ndg. Erasto Sima; karibu sana Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Kama utaendelea kuwepo basi baadaye kidogo uhamie kule kwenye viti vyekundu kule. *(Makofi)*

Wageni 36 wa Mheshimiwa Florence Samizi ambao ni ndugu na marafiki zake, wakiongozwa na Ndg. Sadock Mugendi; karibu sana Sadock, wale kule. Ni ndugu zake

Mheshimiwa Florence Samizi, wako 36; ukoo mkubwa huu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 16 wa Mheshimiwa Kavejuru Felix – ahaa, ninyi mmetoka Muhambwe? Simameni tena. Karibuni sana kutoka Muhambwe, hongereni sana kwa yote, mtupelekee salamu Muhambwe. Ahsante, mnaweza kukaa. *(Makofi)*

Katika wageni hawa, japo sikuandikiwa hapa, lazima atakuwepo mume wake Mheshimiwa Florence; karibu sana shemeji yetu, mama ameshafika salama, sasa baada ya hapa wewe endelea na shughuli zako; yuko katika mikono salama ya Mheshimiwa Spika. *(Makofi/Kicheko)*

Wageni 16 wa Mheshimiwa Kavejuru Felix ambao ni ndugu na rafiki zake wakiongozwa na Ndg. Geremana Felix, hawa watakuwa wanatoka, Buhigwe, karibuni sana kutoka kule Kasuli, Jimbo la Buhigwe; karibuni sana na Mungu awabariki sana muweze kurudi salama. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Mwita Waitara... naam?

**WABUNGE FULANI:** Wifi!

**SPIKA:** Ahaa, tena kweli. *(Makofi)*

Mama Kavejuru Felix kama upo usimame. Aah! Mnaona sasa haya mambo. Kazi maalum, amekwenda Mtera. *(Makofi/Kicheko)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Mwita Waitara, Naibu Waziri wa Ujenzi ambao ni jamaa zake, wakiongozwa na Ndg. James Matari. Wale kule; ahsanteni sana.

Mgeni wa Mheshimiwa Venant Protus ambaye ni mchungaji wa Kanisa la KKKT, Tabora, Mch. Stanley Mteule; karibu sana mchungaji, msitusahau kwenye maombi yenu.

Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, wageni wawili wa Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda ambao ni Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Kogoma, Ndg. Amandus Nzamba na Katibu wa CCM wa Mkoa wa Kigoma, Ndg. Kajoro Vyohoroka. Wale kule; karibuni sana. *(Makofi)*

Kama mtaendelea kuwepo Mwenyekiti na Katibu, baadaye kidogo mtahamia viti vyekundu vile; karibuni sana.

Basi nataka tuendelee sasa.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Zungu nimekuona.

### MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Hivi karibuni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, alitoa angalizo kuhusu bili za maji.

Mheshimiwa Spika, nimepata malalamiko kutoka kwa baadhi ya watu katika Mkoa wa Dar es Salaam, na inawezekana nchi nzima, kwamba bili za maji zinaendelea kuwa kaa la moto. Familia ya watu wawili wanaletewa bili za maji ya 150,000 kwa mwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kuhusu hoja hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri au Naibu, mna cha kusema kuhusu hilo?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru sana kwa nafasi hii. Lakini kubwa, kwanza nilishukuru Bunge lako Tukufu katika bajeti yetu hili jambo lilikuja na tumetoa maelekezo mahususi kabisa kwa watu

ambao wanaidhinisha bili hizi za maji kwa maana ya *EWURA*. Wanaifanyia kazi na ripoti watatukabidhi tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Tutalifuatilia kupitia Kamati yetu ya Maji, Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, mlifuatilie hili la bili za maji, ni la muda mrefu, kwa kweli bili ni kubwa sana kila mahali, wanaumia sana.

Kama mnavyojua wengi wanaoathirika na jambo hili ni akina mama, kwa hiyo linahitaji kipaumbele cha aina yake. Ni bili kubwa kwa kweli, karibu kila mahali, sijui kwa nini. Kwa hiyo, tulifuatilie Kamati, tunawakabidhi mtaendelea nalo kama Kamati.

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Tarimba, Mstahiki Meya Songoro wa Kinondoni; karibu sana. (*Makofi*)

Ujumbe wetu Meya, aste aste, taratibu, polepole Meya. Unapofanya kazi na wanawake kuna utaratibu wake. Meya, ndiyo, nilishaeleza humu ndani na ujumbe ufike kwenu pia; yaani siyo umwamba wala nini unamfokea mwanamke kwenye *public*. Jaribu sana kuwa-*handle* vizuri, utapata utumishi mzuri tu. Pamoja na kwamba unaweza ukawa uko *right*, lakini *the way* unavyofanya na kufokea, hapana, siyo sawasawa, rekebisheni mambo yenu, taratibu tu mtafika. (*Makofi*)

Kama yanawashinda yuko Mbunge wenu pale atasaidia kuweka mambo sawa. Nashukuru na Mkuu wa Mkoa naye ameingilia, angalau. Jaribuni kuchapa kazi kwa pamoja na kwa urafiki kwa pamoja.

Pia kuna wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ambao niliwasahau; ni Baraza la Madiwani la Rombo. Waheshimiwa Madiwani wote simameni; ahsanteni sana kwa kufika. (*Makofi*)



Ni mara ya kwanza Baraza la Madiwani Rombo linatembelea Bunge; hongereni sana. Mbarikiwe sana. Na Mbunge wenu yupo, anachapa kazi. Leo ndiyo shughuli hapa. Msitoketoke sana muone anavyoshusha maneno ya kilimo, naamini hata kahawa kidogo ataiongelea, na biashara ya mazao mpakani huko. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mwenyekiti wa Halmashauri, Mheshimiwa Tarimo asimame; karibu sana Mheshimiwa Tarimo. Yeye ndio Mwenyekiti wa Baraza la Madiwani. *(Makofi)*

Lakini pia wapo marafiki wa Mheshimiwa Waziri, yupo Deo Marandu, yuko Ndg. Tarimo, yuko Singo Swai na Deo Tarimo; karibuni sana pia popote pale mlipo. *(Makofi)*

Katibu, sasa tuendeleo.

**NDG. NENELWA JOYCE MWIHAMBI – KATIBU WA BUNGE:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

#### **MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**SPIKA:** Ahsante sana. Kwa heshima sasa nimkaribishe Mheshimiwa Waziri wa Kilimo aje atuwasilishie hotuba yake ili tuweze kuipokea na tuweze kujijadili. Na ni vizuri kujua kwamba Watanzania asilimia kubwa sana leo wanafuatilia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri ambayo naamini itakuwa na matumaini makubwa kwenye eneo la kilimo. Mheshimiwa Waziri, Profesa Adolf Mkenda, sasa uwanja ni wa kwako.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa ya Utekelezaji ya Mpango wa Maendeleo ya Wizara na kwamba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo ya Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, ninaomba hotuba yote iliyowasilishwa Mezani iingie kwenye kumbukumbu za Bunge lako Tukufu, ila mimi niokoe muda kwa kusoma tu muhtasari wa hotuba hiyo, ambayo pia inapatikana katika tovuti ya Wizara ya [www.kilimo.go.tz](http://www.kilimo.go.tz).

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, naomba kufanya marekebisho kidogo kwenye hotuba nzima kwenye ukurasa wa 128, aya 275, kwenye *text* kuna rejea ya Jedwali Na.8, naomba *text* isomeke rejea Na. 9.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba tena kuungana na Wabunge wote kutoa pole kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa msiba mkubwa tulioupata wa kuondokewa na aliyekuwa Rais wetu, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Natoa pole pia kwa Mheshimiwa Janeth Magufuli, Mama Mzazi Suzana Magufuli, watoto na ndugu wote wa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Watanzania wenzangu wote. Tutaenzi mchango mkubwa wa Rais wetu wa Awamu ya Tano katika ujenzi wa Taifa letu na tutajitahidi kuendeleza uthubutu, uchapakazi na uzalendo kama alivyotufundisha Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni pia tulimpoteza aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Hayati Maalim Seif Sharif Hamad. Maalim Seif Sharif Hamad alikuwa ni kiongozi maarufu sana hapa nchini na atakumbukwa kwa mengi. Tutamkumbuka sana kwa kushirikiana na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuleta maridhiano na mshikamano wa Zanzibar baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2020. Natoa tena pole nyingi kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, familia ya Hayati Seif Sharif Hamad na Watanzania wenzangu wote kwa msiba huu mkubwa wa kuondokewa na Hayati Seif Sharif Hamad.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba sana tumsikilize Mheshimiwa Waziri, wengine mtachangia baadaye mtaanza kurudia mambo yaleyale ambayo kumbe ameshayaeleza. Kwa wale ambao wanataka kuzungumza mnaruhusiwa tu kwenda kupata chai kidogo, lakini tumpe nafasi Mheshimiwa Waziri awasilishe na tunaotaka kusikiliza tupate nafasi ya kusikiliza. Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kipindi hiki pia tumempoteza aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Hayati Balozi John William Herbert Kijazi. Sote tunamkumbuka Balozi Kijazi kwa uchapakazi wake na karama yake kuu ya kuwaheshimu watu wote aliofanya nao kazi kwa ukarimu na uwezo wake mkubwa wa kuelewa na kuusimamia utumishi wa umma kwa uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu limepata pia pigo la kuondokewa na Wabunge watatu; Hayati Atashasta Justus Nditiye aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Muhambwe, Hayati Martha Jachi Umbulla, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Manyara na Hayati Khatib Said Haji aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Konde. Naungana tena na wewe na Wabunge wenzangu wote kuomboleza misiba hii mikubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pigo kubwa sana na huzuni kuu ya kuondokewa na aliyekuwa Rais wetu, Taifa letu limehimili vyema kwa sababu ya misingi imara ya kikatiba ya nchi yetu na utamaduni wa kisiasa ambao uliasisiwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere na Chama cha Mapinduzi. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekamata hatamu za uongozi wa nchi yetu, ametuongoza na kutufaraji sana katika majonzi na amefanikiwa kuleta matumaini makubwa. Namuombea afya njema na mafanikio makubwa katika kazi hii nzito ya kuliongoza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pongezi za dhiti kwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango na Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi kwa

nafasi za uongozi wa juu katika Taifa letu ambazo wameaminiwa na kukabidhiwa. Nawaombea afya njema na mafanikio makubwa katika kutekeleza majukumu haya makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa kuendelea na wadhifa wake huo katika uongozi wa Awamu ya Sita. Pia namshukuru kwa kutusimamia na kutuongoza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi pia kwako wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kwa kuchaguliwa kuendelea kuliongoza Bunge letu hili Tukufu. Nawapongeza wabunge wenzangu wote kwa kuaminiwa na vyama vyetu na kuchaguliwa kuwa Wabunge. Kwa namna ya kipekee, nawapongeza Waheshimiwa Eliadory Felix Kavejuru na Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge wa Majimbo ya Buhigwe na Muhambwe mtawalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi nakishukuru sana Chama cha Mapinduzi kwa kuiteua kugombea Ubunge katika Jimbo la Rombo na nawashukuru sana wananchi wa Rombo kwa kunichagua. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuiteua kuwa Waziri wa Kilimo. Naahidi kwa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Rais, wananchi wa Rombo na Watanzania wote kwa ujumla kwamba nitatumikia nafasi za Ubunge na uwaziri kwa bidii, maarifa, weledi na uadilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee namshukuru sana mke wangu, Beatrice na familia yangu kwa ujumla kwa upendo na uvumilivu wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum na

Makamu Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Almas Athuman Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, kwa ushirikiano mzuri na ushauri makini ambao wameendelea kuutoa kwetu katika kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2020/2021 na Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2021/2022. Ushauri wao umezingatiwa na tunaahidi kuendelea kushirikiana kwa karibu na Kamati katika kuendeleza kilimo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, nawashukuru viongozi na watumishi wote wa Wizara ya Kilimo kwa ushirikiano na bidii yao katika kazi na maandalizi ya hotuba hii. Namshukuru sana Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Mbunge, kwa jinsi tunavyosaidiana kwa karibu katika kutekeleza majukumu ya Wizara tuliyokabidhiwa. Namshukuru pia Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Bw. Andrew Wilson Massawe na Naibu Katibu Mkuu, Prof. Siza Donald Tumbo kwa kazi nzuri na ushirikiano mkubwa ambao wao pamoja na Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi, Bodi na Wakala zilizo chini ya Wizara na watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano wanaoendelea kuutoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipomshukuru aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo Bw. Gerald Musabila Kusaya ambaye kwa sasa ni Kamishna Jenerali wa Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya kwa kunikaribisha na kufanya naye kazi kwa karibu kwa kipindi chote nilichokuwa hapa Wizarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020 mchango wa kilimo katika Pato la Taifa ulikuwa ni asilimia 26.9. Aidha, katika kipindi hicho sekta ya kilimo imekua kwa asilimia 4.9 ikilinganishwa na asilimia 4.4 ya mwaka 2019. Vilevile uzalishaji wa sekta ndogo ya mazao umekua kwa asilimia 5 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.4 katika mwaka 2019. Pia katika mwaka 2020 sekta ya kilimo imechangia kwa asilimia 58.1 katika kutoa ajira nchini na kuchangia zaidi ya asilimia 65 ya malighafi za viwanda nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, Wizara ilikadiria kukusanya shilingi bilioni 5.79 kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi Aprili, 2021, Wizara imekusanya shilingi bilioni 2.69 ambayo ni sawa na silimia 46.48 ya makadirio.

Mheshimiwa Spika, Kilimo kupitia Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24 iliidhinishiwa shilingi bilioni 229.89. Kati ya Fedha hizo, shilingi bilioni 79.76 ni za Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 150.07 za Miradi ya Maendeleo. Wizara ya Kilimo chini ya Fungu 43 iliidhinishiwa shilingi bilioni 202.50, ambapo shilingi bilioni 65.23 ni fedha za Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 137.27 ni Fedha za Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Mpango na Bajeti wa mwaka 2020/2021 umezingatia mambo yafuatayo:-

- (i) Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchuguzi 2015/2020;
- (ii) Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano Awamu ya Pili; na
- (iii) Programu ya Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (*ASDP II*).

Mheshimiwa Spika, miongozo hiyo imezingatiwa katika kuboresha mifumo ya kitaasisi, bodi na sheria za kilimo, kuunganisha wakulima wadogo na wakulima wakubwa, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagaliaji, ghala, masoko kuimairisha upatikanaji wa pembejeo na huduma za ugani, kuimarisha maendeleo ya ushirika, kuongeza matumizi ya teknolojia bora, kuimarisha vituo vya utafiti, vyo vya mafunzo na vyo vya wakulima na huduma za upimaji matabaka na ubora wa udongo.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutumia mfumo wa utoaji wa vibali kwa njia ya kielektroniki na mfumo wa usajili wa wadau wa sekta ya kilimo na mfumo wa M-Kilimo (Mobile Kilimo). Mifumo hiyo imerahisisha utoaji wa

huduma zikiwemo vyeti vya usafi wa mazao ya mimea na vibali vya kuingiza na kuuza mazao nje ya nchi kwa wakati, huduma za ugani, usajili wa wadau wa sekta ya kilimo na upatikanaji wa takwimu za kilimo.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeendelea na ukarabati na ujenzi wa miundombinu ambapo skimu 13 kupitia mradi wa *SSIDP* na skimu tatu kupitia mradi wa *ERPP* zimekamilika. Vilevile Tume kupitia *EIDF* imekamilisha ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji iliyoharibiwa na mafuriko katika skimu ya Ruaha Mbuyuni. Aidha, ukarabati wa skimu ya Mlenge na Magozi umefikia asilimia 80.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi unaotekelezwa na *NFRA*, imeendelea kujenga vihenge vya kisasa katika maeneo ya Babati, Shinyanga, Songea, Makambako, Mbozi Sumbawanga, Mpanda na Dodoma ili kuongeza uwezo wa kuhifadhi nafaka kutoka tani 250,000 hadi tani 501,000, ambapo hadi Mei 2021, ujenzi umekamilika kufikia asilimia 80.1.

Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2021 upatikanaji wa mbegu bora nchini umefikia tani 50,589.43 zisizojumuisha miche, vikonyo na vipando ambapo tani 27,330.37 zimezalishwa nchini, tani 15,758.92 zimeingizwa kutoka nje na tani 7,500.14 ni bakaa ya msimu wa 2019/2020. Aidha, *TARI* kwa kushirikiana na wadau imezalisha na kusambaza miche milioni 13.56 ya mazao ya viazi vitamu, zabibu, minazi, parachichi, miwa na mkonge na vilevile pingili za muhogo milioni 40.9. *ASA* nayo imezalisha miche 242,000 ya michikichi.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu uzalishaji na uingizwaji wa mbolea nchini ambapo hadi Aprili 2021, upatikanaji umefikia tani 678,017 sawa na asilimia 94.4 ya mahitaji ya tani 718,051 kwa msimu wa 2020/2021. Kati ya kiasi hicho tani 426,572 zimeingizwa kutoka nje ya nchi, tani 32,239 zimezalishwa nchini na tani 219,206 ni bakaa ya msimu wa 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2021, upatikanaji wa viuatilifu vya kudhibiti visumbufu vya milipuko umefikia lita 113,066 na kilo 5,000. Kati ya hizo, lita 100,000 ni kwa ajili ya kudhibiti viwavijeshi, lita 5,000 kwa ajili ya kudhibiti kweleakwelea, lita 7,000 kwa ajili ya kudhibiti nzige na lita 1,000 ni kwa ajili ya kudhibiti nzi wa matunda na kilo 5,000 za kudhibiti panya waharibifu.

Mheshimiwa Spika, Wizara imedhibiti makundi ya nzige wa jangwani, kweleakwela na panya. Wizara imefanikiwa kudhibiti makundi yote ya nzige wa jangwani waliovamia nchi yetu, pamoja na nzige wachanga walioanguliwa katika Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie Bunge lako Tukufu kuwashukuru sana Mheshimiwa Dkt. Anna Mgwira aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mheshimiwa Idd Kimanta aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha na Mheshimiwa Joseph Mkirikiti aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Wakuu wa Wilaya za Simanjiro, Siha, Longido, Mwangi na Monduli, Waheshimiwa Wabunge wote wa Wilaya na majimbo hayo na wananchi wote wa maeneo hayo kwa ushirikiano wao mkubwa waliotoa wakati wa kupambana na janga la nzige. Aidha, natoa shukrani za dhati kwa Jeshi la Polisi, Mamlaka ya Anga na hasa Meneja wa Kiwanja cha Ndege Arusha, Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (*TANAPA*) na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (*FAO*) kwa ushirikiano wao katika zoezi la kudhibiti nzige hao.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika imekagua Vyama vya Ushirika 4,494 kati ya vyama 9,185. Aidha, ukaguzi maalum umefanyika kwa vyama 35 na hatua stahiki zimechukuliwa kwa waliojijhusisha na wizi na ubadhirifu wa mali na fedha za Vyama vya Ushirika. Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*) limekagua Vyama vya Ushirika 6,021 na Serikali imechukua hatua stahiki kwa vyama vyote ambavyo vimebainika kuwa na ubadhirifu wa fedha na mali za vyama.



Mheshimiwa Spika, Tume imefuatilia mali za Vyama vya Ushirika zilizochukuliwa kinyume na utaratibu ambapo mali zenye thamani ya shilingi bilioni 68.9 zimerejeshwa. Aidha, Tume imehamasisha uanzishwaji wa viwanda vya kuchakata mazao ambapo viwanda vimeongezeka kutoka 374 mwaka 2019 hadi 452 mwaka 2020. Pia ajira katika Vyama vya Ushirika imeongezeka kutoka 90,090 mwaka 2019 hadi 100,100 mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021 matumizi ya trekta yameongezeka kutoka asilimia 20 mwaka 2019 hadi asilimia 23 mwaka 2020 na ongezeko hilo limepunguza matumizi ya jembe la mkono kutoka asilimia 53 mwaka 2019 hadi asilimia 50 mwaka 2020. Katika kipindi hicho sekta binafsi imeingiza nchini matrekta makubwa 1,124 na matrekta madogo ya mkono 459 hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha huduma za ugani, Wizara imeandaa Rasimu ya Mwongozo wa Usimamizi wa Uratibu wa Huduma za Ugani utakaotumiwa na sekta ya umma na binafsi ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma. Wizara kupitia *TARI* imetoa mafunzo kuhusu teknolojia bora za kilimo kwa wakulima 51,304 na Maafisa Ugani 982 kupitia vituo 11 vya *TARI* na Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Nyakabindi *AgriTech*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, uzalishaji wa mazao asilia ya biashara ya tumbaku, pamba, kahawa, chai, pareto, korosho, mkonge na sukari umefikia tani 8,076,510.83. Katika mwaka 2019/2020, uzalishaji wa mazao ya mafuta umefikia tani milioni 1.58 ikilinganishwa na tani milioni 1.23 mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021 upatikanaji wa mbegu bora za alizeti na ufuta umefikia tani 441.42 na 90.52 mtawalia. Aidha, mbegu milioni 3.82 za mchikichi zimezalishwa. Uzalishaji wa mazao bustani umeongezeka kutoka tani milioni 6.59 mwaka 2018/2019 hadi tani milioni 7.56 mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mazao ya chakula yanajumuisha mahindi, mpunga, mtama,uwele, mikunde, ngano, ndizi, muhogo na viazi kwa msimu wa kilimo kwa mwaka 2019/2020 umefikia tani 18,196,733. Katika mwaka 2020/2021, Wizara imeendelea kufuatilia masoko ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi. Wizara kupitia Bodi ya Korosho imeratibu minada 70 ya uuzaji wa korosho ambapo tani 206,718.88 za korosho ghafi zenye thamani ya shilingi bilioni 473.17 zimeuzwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho tani 8,517 za chai zenye thamani ya dola za Marekani milioni 11.69 zimeuzwa nje ya nchi na tani 1,795 za chai zenye thamani ya shilingi 16.19 zimeuzwa katika soko la ndani. Pia tani 61,306 za kahawa zenye thamani ya dola za Marekani milioni 123.8 na tani 1,346.7 za choroko zenye thamani ya shilingi bilioni 2.4 zimeuzwa.

Mheshimiwa Spika, katika kufungua masoko mapya ya mazao, Wizara ilifanya mkutano wa wafanyabiashara wa mazao ya nafaka ulioshirikisha Mabalazi wetu wa Nchi za Rwanda, Misri, Burundi, *DRC*, Zambia, Sudan Kusini, Malawi, Kenya, Uganda na Msumbiji ili waweze kuunganishwa na masoko katika nchi hizo. Vilevile, Wizara imefungua masoko ya mazao mapya ya parachichi katika nchi za India, Marekani na inakamilisha taratibu za kufungua soko la zao hilo katika nchi ya China, maharage ya soya katika nchi ya China vilevile, ambapo hadi Aprili, 2021 jumla ya wafanyabiashara 49 wamesajiliwa kwenye Mamlaka ya Forodha ya China kwa ajili ya kuuza soya.

Mheshimiwa Spika, ili kuleta ufanisi katika matumizi ya chokaa kama virutubishi vya udongo, Wizara imeandaa Mwongozo wa Matumizi ya Chokaa katika Kilimo utakaotumiwa na Maafisa Ugani kufundishia wakulima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vipaumbele vya kimkakati kwa mwaka, 2021/2022; Mpango wa Bajeti ya Mwaka, 2021/2022 ya Wizara imezingatia mambo makuu yafuatayo: kwanza, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka, 2020/

2025, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa miaka mitano wa awamu ya III na *program* ya kuendeleza sekta ya kilimo awamu ya II (*ASDP – II*). Miongozo yote hiyo iliyoainishwa, imesisitizwa katika hotuba ya Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, alipolihutubia Bunge lako Tukufu tarehe 22 Aprili, 2021.

Mheshimiwa Spika, hotuba hiyo imeweka dira kwa kuainisha vipaumbele vikubwa na vya kimkakati. Katika kupanga mipango ya mwaka 2021/2022 tumezingatia vipaumbele hivyo kama zilivyosisitizwa pia kwenye maelekezo ya Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi Mheshimiwa Daniel Chogolo tarehe 20 Mei, 2021 aliyotoa wakati akiongea na waandishi wa habari na kuzungumzia Wizara tatu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake, Mheshimiwa Rais, aliainisha tija ndogo kama tatizo kubwa linaloikabili sekta ya kilimo. Hili linaonekana wazi kwenye takwimu zinazohusu mchango wa sekta ya kilimo, katika pato la Taifa ambapo kwa sasa umefikia asilimia 26.9 kwa mwaka 2020 na wakati huo huo ukichangia ajira kwa asilimia 58.1. Hii ina maana kwamba, takribani theluthi mbili ya nguvu kazi hapa nchini, inachangia takribani theluthi 1 tu ya pato la Taifa. Hiki ni kielelezo tosha kwamba tija ni ndogo sana katika sekta ya kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mpango mkubwa wa kimkakati ni kuongeza tija katika uzalishaji. Hivyo kipaumbele cha kwanza kikubwa cha kimkakati katika kuongeza tija, ni kuweka mkazo katika utafiti utakaozingatia ugunduzi wa aina za mbegu bora na mbinu bora za kilimo. Ili kufikia malengo haya tutafanya yafuatayo: moja, kufanya utafiti wa mbegu bora zenye tija kubwa; na mfano mmoja tu, kupitia utafiti wa *TARI* wa kituo chetu cha Kibaha, tumeweza kupata mbegu zinazoweza kuzalisha tani 22 mpaka tani 50 kwa hekta, ikilinganishwa na wastani wa tani nane kwa sasa hivi ambapo wakulima wengi wanapata.

Mheshimiwa Spika, vile vile, ukiangalia upande wa pamba, sasa hivi tija ni kilo 250 mpaka 300 kwa ekari,

ikilinganishwa na uwezo wa kufikia wastani wa kilo 1,000 mpaka 2,000 kwa ekari; pili, tumeongeza bajeti ya *TARI* kutoka shilingi bilioni 7.35 mwaka 2020/2021 hadi shilingi bilioni 11.63 mwaka 2021/2022; na tatu, kuimarisha upatikanaji wa fedha za maendeleo ya utafiti wa kilimo kwa kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Utafiti kwa mujibu wa kifungu Na. 26 cha Sheria Na. 10 ya Mwaka 2016 iliyoanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (*TARI Act No. 10, 2016*).

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha pili cha kimkakati cha kuongeza tija ni kuongeza uzalishaji wa mbegu bora. Sote tunafahamu nchi yetu bado hatujajitosheleza kwa mahitaji ya mbegu, hivyo kulazimika kuagiza mbegu nyingi kutoka nje ya nchi. Ili kuongeza uzalishaji wa mbegu bora nchini, Wizara imepanga kuendeleza mashamba 13 ya mbegu ya *ASA* kwa kuweka miundombinu ya umwagiliaji, kwa kutumia fedha za Mfuko wa Maendeleo wa Umwagiliaji, kuongeza bajeti ya uzalishaji wa mbegu bora kutoka shilingi bilioni 5.42 mwaka 2020/2021 hadi shilingi bilioni 10.58 mwaka 2021/2022 na kuendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kuzalisha mbegu bora hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha tatu cha kimkakati ni kuimarisha huduma za ugani. Idadi ya Maafisa Ugani wanaotoa huduma za ugani nchini katika ngazi ya kata na vijiji ni 6,704, idadi hiyo ni ndogo ikilinganishwa na mahitaji ya wagani 20,538. Pamoja na idadi hiyo kuwa ndogo, Maafisa Ugani hao wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwepo ukosefu wa vitendea kazi pamoja na mafunzo rejea.

Mheshimiwa Spika, upungufu huo wa Maafisa Ugani pamoja na changamoto wanazokabiliana nazo, huchangia wakulima wengi kukosa huduma za ugani, ikiwepo matumizi ya mbegu bora, matumizi sahihi ya viuatilifu, zana bora, mbinu bora za kilimo na taarifa za masoko. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imeongeza bajeti katika eneo hilo kutoka shilingi milioni 603 kwa mwaka 2020/2021 hadi shilingi bilioni 11.5 mwaka 2021/2022. Fedha hizo zitatumika kuimarisha huduma za ugani nchini ikiwa ni pamoja na kununua pikipiki 1,500, vifaa vya kupima afya ya udongo,

visanduku vya ufundi (*extension kit*), simu janja, kuwezesha uanzishwaji wa mashamba ya mfano na kutoa mafunzo rejea kwa Maafisa Ugani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Maafisa Ugani watasimamiwa katika kuanzisha mashamba darasa kulingana na mahitaji ya wakulima kwa ajili ya kuendeleza kilimo katika maeneo yao. Tutaianza safari yetu ya kuboresha huduma za ugani katika mikoa mitatu ya kielelezo ambayo ni Dodoma, Singida na Simiyu. Tutaanza hasa katika mikoa ya Dodoma, Singida na Simiyu. Mikoa hiyo ina fursa kubwa ya kuzalisha mazao ya mafuta hususani alizeti na pamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mikoa hiyo Maafisa Ugani wote watapewa pikipiki, vifaa vya kupima afya ya udongo, visanduku vya ufundi, simu janja kuwawezesha kuanzisha mashamba ya mfano, kwa kila Afisa Ugani na kutoa mafunzo rejea yatakayozingatia mazao yote yanayolimwa katika maeneo hayo. Pia, Maafisa Ugani hao watawezesha kuanzisha mashamba darasa katika maeneo yao. Maelezo zaidi ya jinsi tunavyopanga kuendeleza shughuli ya ugani yapo katika hotuba kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha nne cha kimkakati ni kuimarisha kilimo cha umwagiliaji. Kama tunavyofahamu, kilimo chetu nchini kinategemea mvua kwa asilimia kubwa ambazo hazitabiriki kutokana na mabadiliko ya tabia nchi. Aidha, kilimo cha umwagiliaji kinakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo ubovu wa miundombinu, kutokamilika kwa baadhi ya miradi ya umwagiliaji, kukosekana kwa miundombinu ya umwagiliaji kwenye fursa za umwagiliaji, mitaji ya ujenzi wa miundombinu na kadhalika. Tutafanya hivyo kwa kuendeleza Mfuko wa Umwagiliaji ambao unaanzishwa kulingana na Sheria ya Umwagiliaji Na. 4 ya mwaka 2013, ambayo tayari tunatarajia kukusanya zaidi ya shilingi bilioni 30 kwa shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha tano, ni kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo hapa nchini.

Kipaumbele cha sita, itakuwa ni kuanzisha na kuimarisha kilimo anga ili kupambana na tatizo kama ambalo tulipambana nalo la nzige hapa nchini. Kupitia huko tutahakikisha kwamba tunatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuhudumia shughuli za kilimo anga. Hivyo, Wizara imeongeza bajeti ya kilimo anga kutoka shilingi milioni 150 kwa mwaka 2020/2021 hadi shilingi bilioni tatu mwaka 2021/2022. Fedha hizo zitatumika pamoja na mambo mengine, kununulia ndege moja kwa ajili ya kudhibiti visumbufu hivyo.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha saba cha kimkakati ni kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa mitaji, upatikanaji wa fedha katika shughuli za kilimo. Sasa hivi fedha zinazopatikana kwenye kilimo zinatozwa riba kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizopo zinaonyesha kuwa ni asilimia 30 tu ya wakulima wanaofikiwa na huduma za mikopo. Aidha, ni asilimia kati ya saba na tisa ya mikopo inayotolewa na mabenzi ya biashara katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, imeelekezwa kwenye kilimo. Ili kutatua changamoto hii, Wizara imeunda jopo maalum linalohusisha watendaji wakuu wa taasisi za fedha, ambalo tumeamua litaongozwa na Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, kwa ajili ya kupitia minyororo ya thamani ya mazao na kushauri namna bora zaidi ya upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya kuendeleza kilimo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naambiwa muda umeisha, ningeomba *record* nyingine ibaki kwenye kumbukumbu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka, 2021/2022 Wizara ya Kilimo inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishhe jumla ya shilingi 294,162,071,000/= kupitia Fungu - 43, Fungu - 05 na Fungu - 24.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO MHESHIMIWA PROF. ADOLF FAUSTINE MKENDA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA 2021/2022**

**1. UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

2. **Mheshimiwa Spika**, ninaomba hotuba yote iliyowasilishwa mezani iingie kwenye kumbukumbu za Bunge lako Tukufu, ili mimi niokoe muda kwa kusoma tu muhtasari wa hotuba hiyo. Aidha Hotuba yote inapatikana pia kwenye tovuti ya Wizara, [www.kilimo.go.tz](http://www.kilimo.go.tz)

3. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote ninapenda tena kuungana na Wabunge wote kutoa pole kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa msiba mkubwa tulioupata wa kuondokewa na aliyekuwa Rais wetu, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Ninatoa pole pia kwa Mheshimiwa Janeth Magufuli, Mama Suzana Magufuli, watoto na ndugu wote wa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Watanzania wenzangu wote. Tutaenzi mchango mkubwa wa Rais wetu wa Awamu ya Tano katika ujenzi wa Taifa letu na tutajitahidi kuendeleza uthubutu, uchapakazi na uzalendo kama alivyotufundisha Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

4. **Mheshimiwa Spika**, hivi karibuni pia tulimpoteza aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Hayati Maalim Seif Sharif Hamad. Maalim Seif Sharif Hamad alikuwa ni kiongozi maarufu sana hapa nchini na atakumbukwa kwa mengi. Tutamkumbuka sana kwa kushirikiana na Rais wa Serikali ya

Mapinduzi ya Zanzibar katika kuleta maridhiano na mshikamano wa Zanzibar baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Ninatoa pole nyingi kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, familia ya Hayati Seif Sharif Hamad na Watanzania wenzangu wote kwa msiba huu mkubwa wa kuondokewa na Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad.

5. **Mheshimiwa Spika**, kipindi hiki pia tumempoteza aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Hayati Balozi John William Herbert Kijazi. Sote tunamkumbuka Balozi Kijazi kwa uchapakazi wake na karama yake kuu ya kuwaheshimu wote aliofanya nao kazi kwa ukarimu, na uwezo wake mkubwa wa kuelewa na kuusimamia utumishi wa umma kwa uadilifu Mkubwa.

6. **Mheshimiwa Spika**, Bunge lako Tukufu limepata pia pigo la kuondokewa na wabunge watatu; Hayati Atashasta Justus Nditiye aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Muhambwe, Hayati Martha Jachi Umbulla, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Manyara na Hayati Khatibu Said Haji aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Konde. Ninaungana tena na Mheshimiwa Spika na wabunge wenzangu wote kuomboleza misiba hii mikubwa.

7. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na pigo kubwa sana na huzuni kuu ya kuondokewa na aliyekuwa Rais wetu, Taifa letu limehimili vyema kwa sababu ya misingi imara ya kikatiba ya nchi yetu na utamaduni wa kisiasa ambao uliasisiwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, na Chama cha Mapinduzi. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekamata hatamu za uongozi wa nchi yetu, na ametuongoza na kutufariji katika majonzi na amefanikiwa kuleta matumaini makubwa. Ninamuombea afya njema na mafanikio makubwa katika kazi hii nzito ya kuliongoza Taifa letu.

8. **Mheshimiwa Spika**, kama nitakavyoeleza katika hotuba hii, mikakati yetu katika sekta ya kilimo



tumeipanga kwa kuzingatia maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, aliyoyatoa kupitia hotuba yake hapa Bungeni ya tarehe 22 April, 2021.

9. **Mheshimiwa Spika**, ninaomba nitoe pongezi za dhati kwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi kwa nafasi za uongozi wa juu katika Taifa letu ambazo wameaminiwa na kukabidhiwa. Ninawaomba afya njema na mafanikio makubwa katika kutekeleza majukumu haya makubwa.

10. **Mheshimiwa Spika**, ninampongeza pia Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa kuendelea na wadhifa wake huo katika uongozi wa Awamu ya Sita, na ninamshukuru kwa kutusimamia na kutuongoza vizuri.

11. **Mheshimiwa Spika**, pongezi nyingi pia kwa Spika, Mheshimiwa Job Ndugai na Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kwa kuchaguliwa kuendelea kuliongoza Bunge hili tukufu. Ninawapongeza wabunge wenzangu wote kwa kuaminiwa na vyama vyetu na kuchaguliwa kuwa wabunge. Kwa namna ya kipekee nawapongeza waheshimiwa Eliadory Felix Kavejuru na Dkt. Florence George Samizi kwa kuchaguliwa kuwa wabunge wa majimbo ya Buhigwe na Muhambwe mtawalia.

12. **Mheshimiwa Spika**, mimi binafsi ninakishukuru sana Chama cha Mapinduzi kwa kunitewa kugombea ubunge katika Jimbo la Rombo na ninawashukuru sana wananchi wa Rombo kwa kunichagua. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kunitewa kuwa Waziri wa Kilimo. Naahidi kwa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Rais, wananchi wa Rombo na Watanzania wote kwa ujumla kwamba nitatumikia nafasi za ubunge na uwaziri kwa bidii, maarifa, weledi na uadilifu.

13. Kwa namna ya pekee namshukuru sana mke wangu, Beatrice, na familia yangu kwa ujumla kwa upendo na uvumilivu wao wakati wote.

14. **Mheshimiwa Spika**, ninapenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, na Makamu Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Almas Athumani Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, kwa ushirikiano mzuri na ushauri makini ambao wameendelea kuutoa kwetu katika kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2020/2021 na Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2021/2022. Ushauri wao umezingatiwa na tunaahidi kuendelea kushirikiana kwa karibu na Kamati katika kuendeleza kilimo hapa nchini.

15. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee ninawashukuru viongozi na watumishi wote wa Wizara ya Kilimo kwa ushirikiano wao na bidii yao katika kazi na maandalizi ya hotuba hii. Ninamshukuru sana Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe (Mb), kwa jinsi tunavyosaidiana kwa karibu katika kutekeleza majukumu ya Wizara tuliyokabidhiwa. Ninamshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Bw. Andrew Wilson Massawe na Naibu Katibu Mkuu, Profesa Siza Donald Tumbo kwa kazi nzuri na ushirikiano mkubwa ambao wao pamoja na wakurugenzi, wakuu wa taasisi, Bodi na Wakala zilizo chini ya Wizara na watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano wanaoendelea kuutoa.

16. **Mheshimiwa Spika**, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipomshukuru aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo Bw. Gerald Musabila Kusaya ambaye kwa sasa ni Kamishna Jenerali wa Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya kwa kunikaribisha na kufanya naye kazi kwa karibu kwa kipindi chote nilichokuwa naye Wizara ya Kilimo.

## 2. MCHANGO WA KILIMO KATIKA UCHUMI

17. **Mheshimiwa Spika**, kilimo kimeendelea kuwa muhimu katika kuchangia Pato la Taifa (GDP) na uchumi wa nchi hususan katika kuhakikisha usalama wa chakula, upatikanaji wa ajira na malighafi za viwanda. Katika mwaka 2019, mchango wa kilimo katika Pato la Taifa ulikuwa ni asilimia 26.9.

18. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020, sekta ya kilimo imekua kwa asilimia 4.9 ikilinganishwa na asilimia 4.4 ya mwaka 2019. Aidha, uzalishaji wa sekta ndogo ya mazao umekua kwa asilimia 5.0 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.4 katika mwaka 2019. Vilevile, katika mwaka 2019, sekta ya kilimo imechangia kwa asilimia 58.1 katika kutoa ajira nchini na kuchangia zaidi ya asilimia 65 ya malighafi za viwanda nchini.

## 3. HALI YA CHAKULA, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA

### 3.1 *Hali ya Chakula*

19. **Mheshimiwa Spika**, uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2019/2020 na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2020/2021 umefikia tani 18,196,733 kwa mlinganisho wa nafaka (*Grain Equivalent*) ambapo nafaka ni tani 10,869,596 na yasiyonafaka tani 7,327,137. Uzalishaji huo ukilinganishwa na tani 16,293,637 za msimu wa 2018/2019 unaonesha ongezeko la tani 1,903,096 sawa na asilimia 11.7 ambapo uzalishaji wa nafaka umeongezeka kutoka tani 8,896,830 hadi 10,869,596 sawa na asilimia 22.2.

20. **Mheshimiwa Spika**, mahitaji ya chakula kwa mwaka 2020/2021 ni tani 14,404,171 ambapo tani 9,191,116 ni za nafaka na tani 5,213,055 ni mazao yasiyonafaka. Mahitaji hayo yakilinganishwa na uzalishaji yanaonesha kuwa nchi imezalisha ziada ya tani 3,792,562 za chakula ambapo tani 1,678,480 ni za mazao ya nafaka na tani 2,114,082 za mazao

yasiyonafaka (**Kiambatisho. Na. 1**). Kutokana na hali hiyo, Taifa limejitosheleza kwa chakula kwa asilimia 126.

21. **Mheshimiwa Spika**, kimkoa, hali ya chakula imekuwa ya kiwango cha ziada (kati ya asilimia 120 na 238) katika mikoa 14; Utoshelevu (kati ya asilimia 110 na 118) katika mikoa 11; na Upungufu wa asilimia 2 katika Mkoa wa Dar es salaam. Hivyo, hali ya uwepo na upatikanaji wa chakula nchini ni nzuri.

22. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (*National Food Reserve Agency - NFRA*) imeendelea kuimarisha hifadhi ya chakula nchini ambapo katika mwaka 2020/2021, Wakala umenunua tani 58,813.401 za nafaka zikiwemo tani 51,832.502 za mahindi, 850.908 za mtama na tani 6,129.991 za mpunga. Kiasi hicho cha nafaka pamoja na akiba ya tani 52,724.73 za nafaka ya mwaka 2019/2020 zimefanya wakala kuwa na jumla ya tani 110,389.057 ya akiba katika ghala zake (**Kiambatisho Na 2**). Hadi Aprili 2021 akiba iliyopo kwenye ghala za Wakala ni tani 109,231.057 baada ya mauzo ya tani 1,167.



*Hifadhi ya nafaka katika ghala linalomilikiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula Nchini (NFRA)*

### 3.2 Umwagiliaji

*Waziri wa Kilimo Mhe. Prof. Mkenda (wa pili Kushoto) akikagua skimu ya umwagiliaji ya Msolwa Ujamaa iliyopo Kilombero Mkoani Morogoro.*

**23. Mheshimiwa Spika**, eneo linalomwagiliwa limeongezeka kutoka hekta 694,715 mwezi Mei, 2020 hadi hekta 695,045 Machi, 2021 na hivyo kufikia asilimia 58 ya lengo la hekta 1,200,000 ifikapo 2025. Pia, Wizara kupitia Tume ya



Desemba, 2020 sawa na ongezeko la asilimia 2.9. Aidha, idadi ya Vyama vya Ushirika imefikia 9,185 ikilinganishwa na vyama 11,626 mwaka 2019. Upungufu huo umetokana na kufutwa kwa vyama 3,317 vilivyokosa sifa baada ya kufanyika ukaguzi.

25. **Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2021 mikopo yenye thamani ya Shilingi trilioni 1.63 imetolewa kwa wanachama wa Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*Savings and Credit Cooperative Societies-SACCOS*) ikilinganishwa na mikopo yenye thamani ya Shilingi trilioni 1.5 mwaka 2019. Aidha, thamani ya hisa na akiba za wanachama zimeongezeka kutoka Shilingi bilioni 819 mwaka 2019 hadi Shilingi bilioni 891 mwaka 2020.

#### 4. UTEKELEZAJI WA MALENGO NA BAJETI KWA MWAKA 2020/2021

26. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2020/2021, umezingatia Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2020/2021; Mpango wa Maendeleo wa Taifa Awamu ya Pili (2015/2016- 2020/2021) na Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

27. Aidha, utekelezaji umezingatia na Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II). Pia, imezingatia masuala mtambuka ya jinsia, mazingira, lishe, mabadiliko ya tabianchi, UKIMWI, vijana na kutokomeza ajira kwa watoto katika sekta ya kilimo.

28. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inatekeleza malengo mkakati tisa (9) ambayo yanaweka msisitizo katika kilimo kinachohakikisha usalama wa chakula na lishe pamoja na upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda. Malengo Mkakati hayo ni pamoja na: -

a) Kuendelea kutekeleza Progamu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II);

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

- b) Kuboresha mifumo ya kitaasisi, Bodi na Sheria za Kilimo;
- c) Kuunganisha wakulima wadogo na makubwa;
- d) Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji, masoko na miundombinu ya kuhifadhi mazao ya kilimo;
- e) Upatikanaji wa pembejeo (mbegu bora za mazao, mbolea na viuatilifu);
- f) Kuimarisha uhamasishaji na usimamizi wa maendeleo ya ushirika;
- g) Kuongeza matumizi ya teknolojia bora katika uzalishaji wa mazao;
- h) Kuimarisha Vituo vya Utafiti, Vyuu vya Mafunzo ya Kilimo na Vituo vya Mafunzo kwa Wakulima; na
- i) Kuimarisha huduma za upimaji wa matabaka na ubora wa udongo.

### 4.1 Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2020/2021

#### 4.1.1 Makusanyo ya Maduhuli

29. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/2021, Wizara ilikadiria kukusanya jumla ya Shilingi **5,793,400,000** kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi Aprili 2021, Wizara imekusanya Shilingi **2,693,218,390.45** sawa na asilimia **46.48** ya makadirio na ukusanyaji unaendelea hadi mwishoni wa mwaka 2020/2021. Inatarajiwa kuwa malengo yaliyowekwa yatafikiwa ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha.

#### **4.1.2 Fedha Zilizoidhinishwa**

30. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Kilimo kupitia Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24 iliidhinishwa Shilingi **229,839,808,000** ili kutekeleza majukumu yake. Kati ya Fedha hizo Shilingi **79,765,084,000** ni kwa Matumizi ya Kawaida na Shilingi **150,074,324,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

31. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Kilimo kupitia Fungu 43 iliidhinishwa Shilingi **202,504,117,000**. Kati ya Fedha hizo, Shilingi **137,273,144,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo na Shilingi **65,230,973,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (Fungu 05) iliidhinishwa jumla ya Shilingi **17,726,845,000** ambapo Shilingi **4,925,665,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **12,801,180,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Tume ya Maendeleo ya Ushirika (Fungu 24) ilitengewa Shilingi **9,608,446,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

#### **4.2 Utekelezaji wa Malengo Mkakati**

##### **4.2.1 Kuendelea kutekeleza Progamu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II)**

32. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/2021 Wizara imeendelea kusimamia mikakati ya uendelezaji wa mazao ya kipaumbele kama yalivyoanishwa kwenye ASDP II. Mazao hayo ni pamoja na pamba, kahawa, miwa, korosho, chai, mahindi, mpunga, mtama, uwele, muhogo, mazao ya bustani, mazao ya mafuta, viazi, mazao ya mikunde na migomba. Vilevile, Wizara imeendelea kuimarisha miundombinu ya vyo na vituo vya mafunzo na utafiti wa kilimo, udhibiti wa visumbufu vya mimea, huduma za ugani, usajili wa wakulima na kuhamasisha matumizi ya bima ya mazao.

##### **4.2.2 Kuboresha Mifumo ya Kitaasisi, Bodi na Sheria za Kilimo**

###### **a. Mifumo ya Kielektroniki ya kutoa huduma katika Sekta ya Kilimo**



**i. Mfumo wa Utoaji Vibali**

33. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutumia mfumo wa kielektroniki (*Agriculture Trade Management Information System-ATMIS*) ambao unatoa huduma za utoaji wa vyeti vya usafi wa mazao ya mimea na vibali vya kuingiza na kuuza mazao nje ya nchi kwa njia ya mtandao. Mfumo huo wa utoaji wa vibali unapatikana kwenye tovuti kupitia *atmis.kilimo.go.tz* Matumizi ya mfumo yamerahisisha upatikanaji wa vibali kwa wafanyabiashara kwa wakati na umeongeza ufanisi wa upatikanaji wa mapato ya Serikali. Ufanisi huo umetokana na mfumo huo kuziba mianya ya udanganyifu wa nyaraka na umewezesha maduhuli ya Serikali yanayotokana na ada za usafirishaji na uingizaji wa mazao toka nje ya nchi kuongezeka kutoka Shilingi 2,213,946,466 mwaka 2018/2019 hadi Shilingi 3,150,947,979 mwaka 2019/2020.

34. **Mheshimiwa Spika**, hadi Aprili 2021, wafanyabiashara 9,800 wamejisajili na wanatumia mfumo huo. Pia, vibali 19,727 vya kusafirishia tani 489,998.547 za mazao nje ya nchi (*phytosanitary certificates*) na vibali 1,742 vya kuingiza tani 62,088.899 za mazao nchini (*plant import permits*) vimetolewa. Serikali inaendelea kuhimiza wafanyabiashara wa mazao kuendelea kutumia mfumo huu ambao umeonesha ufanisi ambapo wafanyabiashara wa mazao ya kilimo hawalazimiki kuja Makao Makuu ya Wizara kwa ajili ya kuomba vibali.

**ii. Mfumo wa Usajili wa Wadau wa Sekta ya Kilimo**

35. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuhamasisha na kuratibu usajili wa wadau wa sekta ya kilimo kupitia Mfumo wa Usajili wa Wadau wa Sekta ya Kilimo unaofanyika kupitia tovuti *assd.kilimo.go.tz*. Hadi Aprili 2021, miradi 115 inayotekelezwa ndani na nje ya mfumo wa bajeti kwa ufadhili wa Wadau wa Maendeleo imesajiliwa. Aidha, wadau 589 wakiwemo wasambazaji wa pembejeo, wazalishaji na wasindikaji wamejisajili. Mfumo huo umewezesha Serikali kutambua mchango wa Wadau

mbalimbali katika utekelezaji wa ASDP II pamoja na maendeleo ya sekta ya kilimo kwa ujumla.

**iii. Mfumo wa M-Kilimo (Mobile – Kilimo)**

**35. Mheshimiwa Spika**, Wizara imekamilisha mfumo wa kutoa huduma za ugani kwa njia ya mtandao (M-Kilimo) ambao unamuwezesha mkulima kupata huduma na ushauri wa kitaalamu kupitia simu yake ya kiganjani bila kulazimika kukutana na Afisa Ugani. Huduma hiyo imelenga kupunguza changamoto ya uwepo wa idadi ndogo ya Maafisa Ugani hivyo kumuwezesha mkulima kupata mrejesho wa haraka wa msaada wa kitaalamu. Aidha, mfumo huo unamwezesha mkulima kupata taarifa za masoko ikiwemo bei na mahali yalipo masoko kwa wakati husika. Hadi Aprili 2021, maafisa ugani 6,419, wakulima 134,568, wauzaji 712 na wanunuzi 407 wa mazao wamesajiliwa katika mfumo wa M-kilimo.

**b. Bima ya mazao**

**37. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/2021, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Bima la Taifa (*National Insurance Corporation - NIC*), *Jubilee Insurance*, *AUP*, *MGen Insurance*, *Reliance Insurance*, *Acre Africa Limited* na *Alliance Insurance* imeendelea kuongeza wigo wa huduma kwa kuongeza bidhaa kwa ajili ya wakulima. Hadi Aprili 2021, NIC kupitia bima ya 'LIMA SALAMA' inayopatikana kwa mfumo wa vocha (*scratch card*) imetoa fidia ya Shilingi 23,000,000 kwa wakulima 32 wa Wilaya ya Mvomero katika Mkoa wa Morogoro ambao mashamba yao yaliathiriwa na mafuriko.

**38. Mheshimiwa Spika**, Kampuni ya bima ya MGen imetoa huduma ya bima ya mazao kwa wakulima 940. Kati ya hao wakulima 844 wanajishughulisha na zao la mtama katika Mkoa wa Dodoma na wakulima 96 wanajishughulisha na mazao ya chai, mahindi, alizeti, mpunga, maharage, kahawa na muhogo katika Mikoa ya Iringa, Kigoma, Songwe, Manyara, Singida, Tabora, Ruvuma, Shinyanga, Geita na Kigoma. Jumla ya thamani ya bima za mazao walizokata wakulima kupitia kampuni ya bima ya MGen ni Shilingi 107,828,719.

39. **Mheshimiwa Spika**, Kampuni ya Bima ya Jubilee imetoa huduma za bima ya mazao kwa vikundi vya wakulima 167 ambapo thamani ya bima zilizouzwa kwa wakulima ni Shilingi 27,032,634,740. Vilevile, Kampuni hiyo imezindua bidhaa mpya ya bima ya mazao ititwayo 'BIMA PIMA' kwa ajili ya wakulima wa mahindi. Wadau wengine waliojikusha na huduma ya bima ya mazao ni AGRA, TAPBDS, ACRE AFRICA, QUINCEWOOD pamoja na Taasisi za fedha za CRDB na NMB. Pia, Wizara ya Kilimo inashirikiana na wadau wengine kukamilisha Mpango wa Taifa wa Bima kwa ajili ya Sekta ya Kilimo unaoratibiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (*Tanzania Insurance Regulatory Authority - TIRA*).

#### 4.2.3 Kuunganisha Wakulima Wadogo na Makubwa



Waziri wa Kilimo Prof. Adolf Mkenda (Mwenye suti nyeusi) akiangalia mashine ya kisasa ya kuvunia zao la chai katika shamba la wakulima wadogo mkoani Njombe.

40. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/2021, Wizara kwa kushirikiana na ORTAMISEMI imehakiki mashamba 126 yenye ukubwa wa kuanzia hekta 20 yenye hati miliki kwa matumizi ya kilimo katika Halmashauri za Wilaya ya Bahi, Kongwa, Mpwapwa, Chamwino na Kondoa Mkoani Dodoma. Lengo la uhakiki huo ni kuwaunganisha wakulima wadogo na mashamba makubwa kwa lengo la kujifunza na kuendeleza kilimo biashara.

41. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ofisi ya Msajili wa Hazina, Bodi ya Mkonge Tanzania, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, OR – TAMISEMI na Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa imehakiki na kuandaa taarifa za Mashamba 124 ya uwekezaji wa zao la Mkonge katika Wilaya ya Kilosa ili kuwagawia wakulima wadogo wayaendeleze.

42. **Mheshimiwa Spika**, uhakiki wa mashamba hayo umetatua mgogoro kati ya wananchi na mwekezaji wa shamba la Chanzuru lenye ukubwa wa ekari 1,598, Wilayani Kilosa. Utatuzi huo umewezesha umilikishwaji wa ekari 340.12 kwa wananchi kwa ajili ya shughuli za kilimo na makazi, ekari 856.66 kwa ajili ya Bodi ya Mkonge, ekari 20.61 kwa ajili ya ujenzi wa reli ya mwendokasi (*Standard Gauge Railway - SGR*), ekari 32.87 kwa wananchi wa kijiji cha Muungano waliopata mafuriko mwaka 1998 kwa ajili ya makazi na ekari 339.08 kwa ajili ya mwekezaji. Aidha, Serikali imepata eneo lingine lenye ekari 1,251.5 kwa ajili ya fidia kwa mwekezaji.

#### 4.2.4 Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Umwagiliaji, Masoko na Miundombinu ya Kuhifadhi Mazao ya Kilimo

##### a) *Uendelezaji wa Miundombinu ya Umwagiliaji*



*Miundombinu ya umwagiliaji ambayo imeendelea kukarabatiwa katika skimu ya umwagiliaji ya mbegu la ASA la shamba la Kilangali lillilopo wilaya ya Kilosa Mkoani Morogoro*

43. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeendelea na ukarabati pamoja na ujenzi wa miundombinu katika skimu 21 za umwagiliaji. Kati ya skimu hizo, 16 ni kupitia mradi wa Uendelezaji Wakulima Wadogo (*Small Scale Irrigation Development Project - SSIDP*) unaofadhiliwa na JICA na skimu tano (5) ni kupitia mradi wa Kuongeza Uzalishaji wa Zao la Mpunga (*Expanded Rice Production Project-ERPP*). Hadi Aprili 2021, skimu 13 kupitia mradi wa SSIDP zimekamilika kwa mujibu wa mkataba; na skimu tatu (3) zinaendelea kujengwa na kukarabatiwa kwa kutumia *force account* ambapo ujenzi umefika asilimia 46. Aidha, ujenzi na ukarabati wa skimu tano (5) kupitia mradi wa ERPP umekamilika kwa asilimia 95 ambapo 5% zilizobaki zitakamilishwa katika kipindi cha matazamio kwa mujibu wa makubaliano na Benki ya Dunia (**Kiambatisho Na. 3**).

44. **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imekamilisha ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji iliyoharibiwa na mafuriko katika skimu ya Ruaha Mbuyuni (Kilolo). Aidha, ukarabati wa Skimu za Mlenge na Magozi katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa umefikia asilimia 80. Vilevile, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu ya Luiche iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Ujiji umekamilika kwa asilimia 90.

45. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha miundombinu ya umwagiliaji inatunzwa na kudumu kwa muda mrefu, Tume imetoa mafunzo kwa wakulima 714 na wataalam wa kilimo sita (6) kuhusu uimarishaji wa Vyama vya Umwagiliaji na ukusanyaji wa ada za huduma ya umwagiliaji katika skimu 22 zilizopo katika Mikoa ya Mbeya, Ruvuma, Manyara, Kilimanjaro, Dodoma, Pwani na Morogoro.

46. Pia, Tume imefufua mitambo mitatu (3) na kuifanyia matengenezo ya kawaida mitambo mitatu (3) ambayo inatumiwa na Tume katika shughuli za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji. Lengo ni kupunguza gharama za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji. Aidha, mitambo hiyo inakodishwa katika shughuli za ujenzi na kuwa moja ya vyanzo vya mapato.

47. **Mheshimiwa Spika**, kupitia Mradi wa Kusimamia Maliasili na Kuendeleza Utalii Kusini mwa Tanzania (*Resilient Natural Resource Management for Tourism and Growth Project - REGROW*), Tume imeandaa Mpango wa Usimamizi wa Mazingira na Masuala ya kijamii, Mpango wa Usimamizi wa Visumbufu vya Mazao (*Integrated Pest Management Plan*) ili kupunguza matumizi yasiyo sahihi ya viuatilifu na mbolea yanayosababisha uharibifu wa maji na udongo katika bonde la Usangu. Kadhalika, Tume imetoa mafunzo ya usimamizi wa fedha na Uendeshaji wa Vyama vya Umwagiliaji kwa wakulima viongozi 120, katika skimu saba (7) za Hermani, Igumbilo/Isitu, Gonakuvagogolo, Makangarawe, Njombe, Matebete na Isenyela.

**b) Uendelezaji wa Miundombinu ya Hifadhi na Masoko**

48. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi (*Storage Capacity Expansion Project*) unaotekelezwa na NFRA, inaendelea kujenga vihenge vya kisasa (*Silos*) katika maeneo ya Babati (Manyara), Shinyanga, Songea (Ruvuma), Makambako (Njombe), Mbozi (Songwe) Sumbawanga, Mpanda (Katavi) na Dodoma. Lengo la mradi ni kuiongezea NFRA uwezo wa kuhifadhi nafaka kutoka tani 250,000 hadi tani 501,000, ambapo hadi kufikia Aprili 2021, ujenzi umefikia asilimia 80.1. Vilevile, Wakala umekarabati ghala nne (4) zenye uwezo wa kuhifadhi tani 63,500 katika kanda za Arusha (tani 30,000), Songwe (tani 5,000), Sumbawanga (tani 18,500) na Dodoma (tani 10,000).



49. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia mradi wa ERPP unaotekelezwa mkoani Morogoro imekamilisha ujenzi wa ghala tano (5) zenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 6,700 za nafaka. Ghala hizo zimejengwa katika skimu za Msolwa Ujamaa (tani 1,700); Njage (tani 1,700); Mvumi (tani 1,300); Kigugu (tani 1,000); na Mbogo Komtonga (tani 1000). Ghala hizo zitatumwa na Vyama vya Umwagiliaji vya skimu za maeneo hayo chini ya usimamizi wa Halmashauri.



*Ghala la Mvumi Mpunga uliohifadhiwa katika ghala la Mvumi*

50. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa Udhhibiti wa Sumukuvu nchini (*Tanzania Initiative for Preventing Aflatoxin Contamination – TANIPAC*) unaolenga kupunguza athari za sumukuvu katika mazao ya chakula hususan karanga na mahindi. Lengo la mradi huo ni kuimarisha usalama wa chakula, kulinda afya ya mlaji na kuongeza biashara ya nje. Mradi huo unahusisha ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Kibaiolojia (Kibaha); Kituo Mahiri cha usimamizi wa mazao ya nafaka baada ya kuvuna (Mtanana, Kibaigwa); Maabara Kuu ya Kilimo (Dodoma); na ghala 14 (Tanzania Bara 12 na Zanzibar 2) kwa ajili ya kuhifadhi mazao.

Hadi Mei, 2021 usanifu wa ujenzi wa miundombinu hiyo umekamilika na mikataba mitano ya ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Kibaiolojia (Kibaha) na ghala nne (Nyakatoto - Kasulu; Kagezi - Kibondo; Msagila – Bukombe) imesainiwa na wakandarasi wamekabidhiwa maeneo yote na kazi ya ujenzi imeanza.

51. **Mheshimiwa Spika**, Vilevile, TANIPAC imetoa Mafunzo ya Kilimo Bora (smart Aflatoxin *Good Agricultural Practices* - GAP) yanayolenga kudhibiti uchafuzi wa sumukuvu kwenye mazao ya mahindi na karanga. Mafunzo hayo yametolewa kwa Maafisa Ugani 261 katika Wilaya za Kiteto (58), Babati (60), Kilosa (105) na Gairo (38). Katika mafunzo hayo wajumbe wote wa Timu ya Uongozi (*Council Management Team* - CMT) katika Halmashauri hizi walipewa elimu ya ufahamu wa sumukuvu na kuelekezwa kazi zitakazofanyika na majukumu ya Halmashauri ili kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa kikamilifu ndani ya muda wa mradi.

52. Aidha, waandishi wa habari 30 wa vyombo vya habari vya Zanzibar wamepatiwa mafunzo maalum ya namna bora ya kuhabarisha umma juu ya uwepo wa sumukuvu na madhara yake kwa afya ya binadamu na biashara ya nje. Mafunzo kama hayo yatafanyika Tanzania Bara kwa kuhusisha waandishi wa habari zaidi ya 105.

53. **Mheshimiwa Spika**, kupitia maonesho ya Nanenane na Siku ya Chakula Duniani jumla ya watu 4,470 wamepatiwa elimu kuhusu uelewa wa sumukuvu. Vilevile, makala, vipindi sita (6) vya luninga na 11 vya redio kuhusu sumukuvu, madhara na udhibiti wake viliandaliwa na kurushwa hewani kupitia vituo mbalimbali vya utangazaji.

#### **4.2.5 Upatikanaji wa Pembejeo (Mbegu bora, Mbolea na Viuatilifu)** **Mbegu bora**

54. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora nchini ambapo hadi



Aprili, 2021 tani 50,589.43 zisizojumuisha miche, vikonyo na vipando zimepatikana. Kati ya hizo, tani 27,330.37 zimezalishwa nchini, tani 15,758.92 zimeingizwa kutoka nje na tani 7,500.14 ni bakaa ya msimu 2019/2020 (**Kiambatisho Na. 4**). Uzalishaji wa ndani umechangiwa na Wakala wa Mbegu za Kilimo (*Agriculture Seed Agency - ASA*) kwa kushirikiana na Kampuni binafsi nane (8) zilizotumia mashamba ya ASA ambao kwa pamoja wamezalisha tani 5,634 (ASA tani 1,750 na Kampuni tani 3,884) na kiasi cha tani 18,789.37 kimezalishwa na Kampuni binafsi pamoja na TARI.

**55. Mheshimiwa Spika**, TARI imezalisha na kusambaza miche 13,568,422 ya mazao ya muhogo, viazi vitamu, zabibu, minazi, parachichi, miwa na mkonge. Kati ya hiyo muhogo ni pingili 4,766,501, viazi vitamu vikonyo 1,833,486, maembe miche 15,765, parachichi miche 15,891, minazi miche 1,072,308, mipapai miche 57,883, mkonge miche 2,896,000, miwa miche 1,515,652 na zabibu miche 9,000, michikichi miche 1,370,133 na pareto miche 15,803.

**56. Mheshimiwa Spika**, Kampuni zinazozalisha mbegu kupitia mashamba ya ASA zimeongezeka kutoka Kampuni nane (8) msimu wa mwaka 2019/2020 na kufikia Kampuni 10 msimu wa 2020/2021 na hivyo kuongeza eneo la ASA linalotumika kuzalisha mbegu kupitia sekta binafsi kutoka hekta 2,031 kwa msimu wa 2019/2020 hadi hekta 2,270 msimu wa 2020/2021. Vilevile, ASA imeongeza eneo la uzalishaji wa mbegu kwa kufungua maeneo mapya manne (4). Maeneo hayo ni Kilimi wilayani Nzega (ekari 1,115), Msungura (ekari 250) na Mazizi (ekari 12) wilayani Chalinze, na shamba la Tanganyika (ekari 500) katika Wilaya ya Tanganyika Mkoa wa Katavi.

**57. Mheshimiwa Spika**, hadi Aprili 2021, ASA imezalisha miche 342,000 ya chikichi katika mashamba manne (4) ya Bugaga - Kasulu, MsimbaKilosa, Mwele-Tanga na Mbozi-Mkoani Songwe. Aidha, ASA kwa kushirikiana na Bodi ya Pamba imezalisha tani 8,270 za mbegu ya pamba.

**58. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora, ASA kupitia mradi wa ERPP imekamilisha ujenzi wa maabara. Maabara hiyo imewekewa vifaa kwa ajili ya kuhakiki na kudhibiti ubora wa mbegu kabla ya kuziwasilisha Taasisi ya Uthibiti wa Ubora wa Mbegu (TOSCI). Pia, matumizi ya maabara hiyo inasaidia Wakala kuwa na uhakika wa ubora wa mbegu zinazopelekwa kwa wakulima. Vilevile, kupitia mradi wa ERPP, ASA imekamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye eneo la hekta 400 katika shamba la Kilangali (Kilosa) pamoja na ukarabati wa tuta la bwawa katika shamba la Mwele Wilaya ya Mkinga.



*Waziri wa Kilimo Prof. Adolf Mkenda (wa pili kushoto waliokaa) akiwa na Kamati ya Bunge ya Kilimo Mifugo na Maji mara baada ya kutembelea ASA, nyuma ni jengo la maabara lilojengwa kupitia mradi wa ERPP*

**59. Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa upatikanaji wa mbegu bora ni kipaumbele, Wizara imeiwezesha ASA kununua vitendea kazi ambavyo ni trekta 2 (HP 95 na HP 125) na viunganishi vyake, Mashine 2 za Kupandia (*Planters*), Mashine 2 za kunyunyiza viuatilifu (*Boom sprayers*) na mashine ya kulainisha udongo (*Rotavator*) ili kuongeza uzalishaji wa mbegu bora nchini. Aidha, Wizara itaendelea kuiwezesha ASA kupata vifaa na kuweka miundombinu ya umwagiliaji ili uzalishaji wa mbegu ufanyike mwaka mzima bila kutegemea mvua.

60. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Kamati ya Mbegu imethibitisha matumizi ya aina mpya za mbegu 28. Mbegu hizo ni migomba (4), mtama (2), viazi vitamu (2), miwa (6), maharage (10), fiwi/ngwara (2), mahindi (1) na mpunga (1) (**Kiambatisho Na. 5**). Kati ya hizo, TARI imegundua aina 20 ambazo ni mtama (2), migomba (4), viazi vitamu (2), miwa (6) na maharage (6). Aidha, kwa mara ya kwanza hapa nchini tumeweza kugundua mbegu za miwa zinazotegemea mvua ambazo ni nafuu kwa wakulima ikilinganishwa na mbegu za awali zinazotegemea kilimo cha umwagiliaji.

61. **Mheshimiwa Spika**, TARI imezalisha tani 481.73 za mbegu bora za mazao ya nafaka, jamii ya mikunde na mafuta (**Kiambatisho Na. 6**). Kati ya hizo, tani 16.08 ni mbegu mama (*breeder seeds*), tani 112.32 ni mbegu za awali (*prebasic Seeds*), tani 22.31 ni mbegu za msingi (*Basic Seeds*) na tani 331.02 ni mbegu zilizothibitishwa (*Certified Seeds*).

62. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, TARI imezalisha tani saba (7) za mbegu za awali za pamba. Mbegu hizo, zina uwezo wa kuzalisha tani 3,888 za mbegu zilizothibitishwa ambazo zinatoshleza hekta 155,520. Aidha, TARI imezalisha mbegu mama tani 1.162 za pamba na kupandwa msimu wa 2020/2021 kwa majaribio na uzalishaji wa mbegu kwa ajili ya msimu wa 2021/2022. Pia, TARI imezalisha tani 36 za mbegu za ufuta zilizothibitishwa ambazo zinatoshleza ekari 42,960.

63. **Mheshimiwa Spika**, TARI imetunza aina 36,706 za vinasaba (*germplasm*) vya mbegu za asili za mazao mbalimbali ili zisipotee na kuzitumia katika tafiti (**Kiambatisho Na. 7**). Aidha, TARI imeendelea kutunza nasaba za vizazi 300 vya mbegu za asili za alizeti ambavyo vitawezesha upatikanaji wa mbegu bora zenye uwezo wa kuzalisha tani 2 kwa hekta. Kwa kutumia mbegu hizo za asili, aina 11 za mbegu za mazao ya maharage (5), ngano (2), mchicha (2) na mpunga (2) zinafanyiwa majaribio ili kupata mbegu bora. Pia, tani 3.58 za mbegu za alizeti aina ya *Record* (1.26 za awali na tani 2.32 zilizothibitishwa) zimezalishwa na

kusambazwa kwa wakulima katika mikoa ya Mbeya, Kigoma, Dodoma, Morogoro na Singida.

64. **Mheshimiwa Spika**, TARI kupitia mradi wa utafiti "*Enhancing Partnership among Africa RISING, NAFKA and TUBORESHE CHAKULA Programs for Fast-tracking Delivery and Scaling of Agricultural Technologies in Tanzania*" imewajengea uwezo wakulima 33,936 katika Wilaya za Mbarali, Iringa, Kilombero na Momba kuhusu matumizi ya mbegu bora za mpunga, kanuni bora za kilimo cha mpunga na utunzaji wa maji na ardhi. Matokeo ya jitihada hizi kwa wakulima waliokuwa wanatekeleza mradi ni kuongezeka kwa tija ya zao la mpunga kutoka tani tatu (3) kwa hekta kabla ya mradi hadi tani tisa (9) kwa hekta baada ya mradi.

65. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Tumbaku (*Tobacco Research Institute of Tanzania - TORITA*) imefanya utafiti wa mbegu mpya ya Yunnan 85 yenye uwezo wa kuzalisha wastani wa kilo 1,585 kwa hekta na imechaguliwa na wakulima. Aidha, TORITA kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Tumbaku Zimbabwe imetafiti mbegu mpya aina ya KRK26R ambayo ina ukinzani dhidi ya ugonjwa wa 'Bandubandu' (*Tobacco Mosaic Virus – TMV*).

### Udhibiti na Uthibiti wa Ubora wa Mbegu



*Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ilipotembelea Taasisi ya Udhibiti na Uthibiti wa ubora wa mbegu TOSCI.*

66. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (*Tanzania Official Seed Certification Institute - TOSCI*) imeendelea kudhibiti ubora wa mbegu nchini kwa kufanya majaribio ya utambuzi (*Distinctness Uniformity and Stability - DUS test*) wa aina mpya za mbegu; kufanya majaribio ya umahiri (*National Performance Trial - NPT*) wa aina mpya za mbegu; kukagua mashamba, ghala na maduka ya mbegu na kuchukua sampuli za mbegu kwa ajili ya vipimo vya maabara.

67. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/2021 TOSCI imekagua hekta 3,977.7 za mashamba ya mbegu, ghala 68 za mbegu na maduka ya mbegu 787 katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Kusini, Kanda ya Ziwa na Kanda ya Mashariki na Pwani ambapo maduka 90 yamefungiwa na kuelekezwa kufanya marekebisho ili kukidhi vigezo vya kuendelea na biashara. Vilevile, TOSCI imepima ubora wa mbegu 2,533 ambapo sampuli 1,981 zimekidhi vigezo. Pia, TOSCI imesajili wafanyabiashara wa mbegu 140 ambapo kati ya hao, 37 ni wenye makampuni na 103 ni wauzaji wa mbegu.

68. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha ubora wa mbegu nchini, TOSCI imetoa mafunzo kuhusu uthibiti na udhibiti wa ubora wa mbegu kwa wagunduzi wa mbegu 26 kutoka katika makampuni binafsi na taasisi za umma, wazalishaji 200 wa Mbegu Zilizothibitishwa Ubora katika Ngazi ya Mkulima (*Quality Declared Seed - QDS*) na wafanyabiashara wa mbegu 457 kutoka Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Geita, Kigoma, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Shinyanga na Songwe.

## Upatikanaji wa Mbolea



*Waziri wa Kilimo Prof. Adolf Mkenda (katikati) alipotembelea kiwanda cha mbolea cha Minjingu kilichopo mkoani Manyara Wilayani Babati. Kushoto; Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) Bw. Japhet Justine*

**69. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuratibu, kusimamia uzalishaji na uingizwaji wa mbolea nchini ambapo hadi Aprili 2021, upatikanaji wa mbolea umefikia tani 678,017 sawa na asilimia 94.4 ya mahitaji ya tani 718,051 kwa msimu wa 2020/2021.

Kati ya kiasi hicho tani 426,572 zimeingizwa kutoka nje ya nchi, tani 32,239 zimezalishwa nchini na tani 219,206 ni bakaa ya msimu wa 2019/2020 (**Jedwali Na. 1**). Aidha, hadi Machi 2021, tani 436,889 za mbolea zimeuzwa kwa wakulima, tani 129,876 zimepewa vibali na kusafirishwa nje ya nchi na tani 111,252 zitaendelea kuuzwa.

**Jedwali Na. 1: Upatikanaji wa Mbolea hadi Aprili 2021(tani)**

Aina ya Mbolea	Bakaa ya Msimu 2019/2020	Kiasi kilichoingizwa	Uzalishaji wa ndani	Jumla ya Upatikanaji	Mahitaji ya 2020/2021
UREA	87,626	101,574	-	189,201	229,126
DAP	33,975	93,244	-	127,219	185,321
NPKs	43,867	83016	252	127,135	157,417
Mbolea zingine za N.	6,681	27,570	-	34,251	9,423
SA	15,477	54,655	-	70,132	27,729
CAN	20,661	47,707	-	68,367	84,901
MoP	3,608	14,282	-	17,890	1,334
Minjingu	3,993	-	23,914	27,908	12,588
Mbolea zingine	1,767	4,524	-	6,291	10,212
Chokaa (Lime)	1,297	-	6,082	7,379	-
Dolomite	169	-	1,259	1,428	-
Gypsum	85	-	732	817	-
<b>Jumla</b>	<b>219,207</b>	<b>426,572</b>	<b>32,239</b>	<b>678,017</b>	<b>718,051</b>

*Chanzo: Wizara ya Kilimo*

**70. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia TORITA imefanya utafiti wa mbolea ya Minjingu (N10:P18:K24) na Minjingu CAN 27% zilizoboreshwa. Matokeo ya awali shambani yanaonesha kufanya vyema kwa ukaribu na mbolea ya NPK (10:18:24) na CAN 27% ambayo inatumika kwenye tumbaku (*standard*). Utafiti unaoendelea sasa ni kufuatilia matokeo ya mbolea ya Minjingu kwenye ukaushaji na ubora wa tumbaku. Iwapo matokeo ya ufuatiliaji huo yatakuwa mazuri, yatawezesha kampuni kuhamasisha matumizi ya mbolea hiyo kwenye zao la tumbaku na hivyo kuongeza uzalishaji wa ndani. Aidha, TORITA kwa kushirikiana na Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela (*Nelson Mandela Agricultural Institute of Science and Technology - NMAIST*) imekamilisha utengenezaji wa kikaushio cha tumbaku kinachotumia nishati ya jua ili kulinda mazingira.

## Udhibiti wa Ubora wa Mbolea

71. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2020/2021, Wizara kupitia TFRA imesajili wafanyabiashara wapya 387 na kuhisha usajili wa wafanyabiashara 533 na hivyo kufanya jumla ya wafanyabiashara wa mbolea waliopewa leseni kuwa 920. Pia, imekagua usajili, leseni, uingizaji wa mbolea, utunzaji wa mbolea na bei elekezi kwa wafanyabiashara 1,148 nchini. Vilevile, TFRA imetoa elimu kuhusu kanuni za utunzaji na uhifadhi wa mbolea kwa wafanyabiashara 1,038 wa mbolea kutoka Dar es Salaam (177), Pwani (106), Arusha (112), Kilimanjaro (142), Manyara (86), Morogoro (345) na Tanga (70).

72. **Mheshimiwa Spika**, TFRA imesajili aina 17 za mbolea mpya (**Kiambatisho Na. 8**). Vilevile, imetoa mafunzo kuhusu ukusanyaji wa takwimu za mbolea na matumizi yake kwa Wakaguzi 30, Maafisa Pembejeo 17 na Vyama vya Ushirika wa Mazao (*Agricultural Marketing Cooperatives Societies*- AMCOS) 146 vilivyopo Mwanza (27), Mara (29), Simiyu (34), Shinyanga (12), Geita (31) na Kagera (13). Aidha, kupitia vyombo vya habari TFRA imetoa elimu kuhusu matumizi sahihi ya mbolea, mchango wa tasnia ya mbolea kwenye ujenzi wa uchumi wa viwanda, umuhimu wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja na Mifumo ya usambazaji wa mbolea.

## Upatikanaji wa Viuatilifu vya Mimea na Mazao

73. **Mheshimiwa Spika**, hadi Aprili 2021, upatikanaji wa viuatilifu vya kudhibiti visumbufu vya milipuko umefikia lita 113,066 na kilo 5,000. Kati ya hizo, lita 100,000 ni kwa ajili ya kudhibiti viwavijeshi, lita 5,000 kweleakwelea, lita 7,000 za kudhibiti nzige, lita 1,000 nzi wa matunda na kilo 5,000 za kudhibiti panya. Hadi Aprili, 2021 lita 9,900 za Duduba zimetumika kudhibiti viwavijeshi vamizi katika eneo lenye ukubwa wa hekta 24,750 katika mikoa ya Kilimanjaro, Dodoma, Singida, Tanga, Mara, Arusha na Morogoro. Aidha, lita 2,800 za fernithion zimetumika kudhibiti nzige katika mikoa ya Kilimanjaro, Manyara na Arusha. Vilevile, kilo 2,288.5 za *zinc phosphide* za kudhibiti panya katika mikoa ya Morogoro, Pwani, Iringa na Singida katika eneo la hekta 86,989.



74. Wizara pia, imesambaza lita 66 za *Methyl Eugeno* katika mikoa ya Pwani (lita 10), Dar es Salaam (lita 50), Njombe (lita 5) na Kigoma (lita 1) kwa ajili ya kudhibiti nzi wa matunda. Kadhalika, wakulima 20 wa zao la parachichi katika mikoa ya Kigoma, Kagera, Iringa, Njombe, Mbeya na Shinyanga wamepewa chambo aina ya *Methyl Eugeno* kwa ajili ya kudhibiti nzi wa matunda.

### **Udhibiti wa Ubora wa Viuatilifu vya Mimea na Mazao**

75. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu vya Kitropiki (*Tropical Pesticides Research Institute* - TPRI) imechambua sampuli 538 za viuatilifu ambapo sampuli 522 sawa na asilimia 97 zimekidhi viwango. Pia, TPRI imetoa vibali 1,456 kwa wafanyabiashara wa viuatilifu ambapo vibali 705 ni vya uagizaji, 176 vya uzaji, 97 vya usajili, 24 vya ufukizaji, 13 vya muingizaji na 441 vya uingizaji wa shehena za mimea na mazao yake. Vilevile, TPRI imekagua kampuni moja (1) na maduka 104 katika mikoa ya Mbeya, Katavi, Njombe, Songwe, Rukwa, Ruvuma, Mwanza, Shinyanga, Geita, Kagera, Mara, Arusha, Mtwara, Lindi, Dar es Salaam na Kilimanjaro. Ukaguzi huo umebaini maduka 25 yanauza viuatilifu visivyosajiliwa kwa mujibu wa sheria na hivyo wamiliki wa maduka hayo kufunguliwa mashauri mahakamani.

76. **Mheshimiwa Spika**, TPRI pia imetoa mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa wakulima, Maafisa Ugani na wauzaji wa viuatilifu 285 katika mikoa ya Mbeya, Morogoro na Arusha. Aidha, wakulima vijana 501 kutoka katika Wilaya za Bariadi, Itilima, Busega, Maswa, Meatu, Igunga, Geita, Shinyanga na Mbeya wamepatiwa mafunzo kuhusu utoaji wa huduma ya unyunyiziaji wa viuatilifu kwenye mazao ya bustani, pamba na nafaka na kuwezesha vijana hao kupata ajira. Vilevile, TPRI imefanya kaguzi za kimaabara kuhusu ubora wa viuatilifu ambapo mashauri 15 kwa waliokamatwa kwa makosa ya kutozingatia viwango vya ubora yamefunguliwa

mahakamani. Wizara itaendelea kuchukua hatua kwa wafanyabiashara wa viuatilifu wanaokiuka masharti ya leseni zao ili kuepuka kuwasababishia wakulima hasara.

## **Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea na Mazao Nzige wa Jangwani**

**77. Mheshimiwa Spika,** mwezi Januari, Februari na Machi 2021 nchi yetu ilivamiwa na nzige wa jangwani katika Wilaya za Siha (Kilimanjaro); , Monduli na Longido (Arusha) na Simanjiro (Manyara). Aidha, nchi zingine zilizovamiwa na nzige wa jangwani ni Kenya, Eritrea, Sudan, Ethiopia na Somalia.

**78. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Aprili, 2021 Wizara kwa kushirikiana na Ofisi za Mkoa na Halmashauri zilizovamiwa na nzige hao imefanikiwa kudhibiti makundi yote ya nzige wa jangwani yaliyoingia nchini pamoja na tunutu walioanguliwa na hakuna uharibifu uliofanywa na nzige hao kwenye mazao ya kilimo. Wizara kwa kushirikiana na uongozi wa mkoa, Halmashauri na Wananchi inaendelea kufuatilia taarifa za utabiri wa nzige wa jangwani na kuchukua hatua za kuwadhibiti pindi makundi mapya yatakavyojitokeza.

**79. Mheshimiwa Spika,** naomba nitumie Bunge lako Tukufu kuwashukuru Mhe. Dkt. Anna Mgwira aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mhe. Idd Kimanta aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha na Mhe. Joseph Mkirikiti aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara, wakuu wa Wilaya za Simanjiro, Siha, Longido na Monduli, Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa Wilaya husika kwa ushirikiano wao katika kupambana na nzige. Aidha, nitoe shukrani za dhati kwa Jeshi la Polisi, Mamlaka ya Anga na hasa Meneja wa Kiwanja cha Ndege Arusha, Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA) na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) kwa ushirikiano wao katika zoezi la kudhibiti nzige hao.



*Waziri Mkuu Mhe. Kassim M. Majaliwa akishuhudia Nzige wa Jangwani waliongamizwa kwa sumu katika Kijiji cha Engaruka Wilaya ya Monduli alipotembelea maeneo yaliyovamiwa na nzige.*

## **Nzige Wekundu**

80. ***Mheshimiwa Spika***, katika msimu wa 2021, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Kudhibiti Nzige Wekundu la Kati na Kusini mwa Afrika (*International Red Locust Control Organization for Central and Southern Africa – IRLCOCSA*) ilifanya savei katika maeneo yote ya mazalia wa nzige wekundu. Maeneo hayo ni Bonde la Mto Malagarasi (Wilaya ya Kigoma na Kaliua), Mbuga za IKuu/ Katavi (Wilaya ya Mpanda), Mbuga za Wembere (Wilaya ya Igunga), Mbuga za Ziwa Rukwa (Wilaya ya Sumbawanga) na Mbuga ya Bahi (Wilaya ya Bahi). Matokeo ya savei hiyo yameonesha hakuna tishio lolote la uvamizi wa nzige wekundu.

## Kweleakwelea na Panya

81. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea na udhibiti wa milipuko ya ndege waharibifu wa mazao aina ya kweleakwelea na panya kwenye maeneo yote yanayobainika kuwa na visumbufu hivyo ili kusiwepo na upotevu wa mazao ya wakulima. Hadi Aprili, 2021 udhibiti wa kweleakwelea umefanyika katika Wilaya 22 kwenye mikoa 12 ya Kilimanjaro (Mwanga, Moshi), Arusha (Meru), Manyara (Simanjiro na Babati), Dodoma (Chamwino, Bahi, Kondoa, Dodoma Jiji), Singida (Singida Vijijini, Itigi, Mkalama), Morogoro (Kilosa na Mvomero), Iringa (Iringa Vijijini), Mbeya (Mbarali), Geita (Geita Vijijini), Mwanza (Sengerema na Kwimba) na Shinyanga (Kishapu na Shinyanga Vijijini) na Pwani (Chalinze). Wizara inaendelea kudhibiti kweleakwelea katika maeneo mapya yanayoripotiwa. Aidha, Wizara imedhibiti panya katika Wilaya za Busega, Iringa na Manispaa ya Morogoro.

82. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao, Wizara imetoa mafunzo kuhusu udhibiti wa Nzige wa Jangwani kwa wataalam 24 katika Wilaya za Lushoto, Handeni, Korogwe, Rombo, Mwanga na Moshi, washauri wa kilimo wawili (2) kutoka Tanga na Kilimanjaro, maafisa kilimo watano (5) kutoka TPRI, na maafisa ugani sita (6) kutoka wilaya za Arusha na Manyara. Wizara pia, imetoa mafunzo kuhusu udhibiti wa panya kwa wataalam 12 wa kilimo katika Halmashauri za Wilaya za Kilosa na Busega. Vilevile, Wizara imetoa elimu kwa viongozi 12 wa kata ya Mpunguzi (Dodoma) kuhusu kisumbufu aina ya kantangaze cha zao la nyanya.

83. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na hatua hizo za mafunzo na matumizi ya viuatilifu vya kudhibiti visumbufu vya mazao, udhibiti husishi (*Integrated Pest Management – IPM*) unatumika ikiwemo kilimo mseto, kuzingatia kanuni bora za kilimo na kulinda wadudu marafiki. Ninapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa aina tatu (3) za manyigu (*Cotesia icipe*, *Telonomus spp* na *Trichogramma spp*) ambao ni marafiki wa mkulima wanaodhibiti viwavijeshi

wamegunduliwa katika Mikoa ya Morogoro, Kilimanjaro na Arusha. Wadudu hao watazalishwa kwa wingi katika Kituo cha Udhhibiti wa Visumbufu Kibaiolojia - Kibaha na kusambazwa kwa wakulima.

**84. Mheshimiwa Spika**, wakulima 300 wa pamba wamepatiwa mafunzo ya kudhibiti visumbufu vya zao hilo, kuongeza tija na kutunza mazingira kwa kutumia mbinu za udhibiti husishi (*Integrated Pest Management – IPM*). Vilevile, Wakulima 350 wa zao la mahindi katika mikoa ya Ruvuma (Songea), Dodoma (Chemba) na Manyara (Babati) wamepatiwa mafunzo kuhusu sumukuvu. Aidha, Wizara imeimarisha vituo tisa (9) vya kudhibiti milipuko ya visumbufu vya mazao na mimea katika Kanda ya Magharibi/Ziwa kwa kuvipatia vitendea kazi.

#### 4.2.6 Kuimarisha Usimamizi wa Maendeleo ya Ushirika

**85. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika imefanya ukaguzi wa ndani wa Vyama vya Ushirika 4,494 kati ya 9,185. Ukaguzi huo umebaini mapungufu katika uongozi na usimamizi wa Vyama vya Ushirika. Aidha, kaguzi maalum zimefanyika kwa vyama 35 na hatua stahiki zimechukuliwa kwa Vyama vya Ushirika 17 vilivyojihusisha na wizi na ubadhirifu wa mali na fedha za Vyama vya Ushirika. Vilevile, Vyama vya Ushirika 18 vipo katika hatua mbalimbali za uchunguzi.

**86.** Aidha, Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*Cooperative Audit and Supervision Corporation – COASCO*) lenye jukumu la kufanya ukaguzi wa nje limekagua Vyama vya Ushirika 6,021 ambapo vyama 289 vimepata hati inayoridhisha, 3,114 hati yenye shaka, 948 hati isiyoridhisha na 1,670 hati chafu. Hati zisizoridhisha, zenye shaka na hati chafu zimetokana na uandishi mbovu wa vitabu vya hesabu na taarifa za fedha kwa watendaji wa vyama hivyo. Tume inaendelea kutoa mafunzo ya uandishi wa vitabu vya hesabu kwa watendaji hao.

**87. Mheshimiwa Spika,** Tume imefuatilia mali za Vyama vya Ushirika zilizochukuliwa kinyume na utaratibu ambapo mali zenye thamani ya Shilingi bilioni 68.9 zimerejeshwa. Aidha, Tume imetekeleza maagizo ya Serikali ambapo wakulima wa mazao ya choroko, pamba, ufuta, korosho na kakao wameunganishwa na benki na malipo yao yanafanyika kupitia akaunti zao.

**88.** Aidha, Tume imehamasisha uanzishwaji wa viwanda vya kuchakata mazao ambapo viwanda vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika vimeongezeka kutoka 374 mwaka 2019 hadi 452 mwaka 2020. Idadi hiyo inahusisha viwanda viwili vya kuchambua Pamba vya Chama cha Ushirika cha Kahama (KACU) na Chato ambavyo vilifufuliwa msimu wa mauzo ya pamba 2020/2021. Aidha, ajira katika Vyama vya Ushirika imeongezeka kutoka 90,090 mwaka 2019 hadi 100,100 mwaka 2020.

**89. Mheshimiwa Spika,** Tume imetoa mafunzo kuhusu Sheria ya Ushirika, uendeshaji wa miradi, uandishi na utoaji wa taarifa za hesabu, uongozi na utunzaji wa takwimu katika Vyama vya Ushirika kwa wanaushirika 2,800 katika Mikoa ya Morogoro, Ruvuma, Iringa, Songwe, Singida, Mbeya, Dodoma, Arusha na Pwani. Aidha, Wizara kupitia *SAGCOT Centre Limited* imewezesha uanzishwaji wa Vyama tisa (9) vya Ushirika katika mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe na Songwe na kuunganishwa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB).

#### **4.2.7 Kuongeza Matumizi ya Teknolojia Bora katika Uzalishaji wa Mazao**

##### **Zana za Kilimo**

**90. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2020/2021 matumizi ya trekta yameongezeka kutoka asilimia 20 mwaka 2019 hadi asilimia 23 mwaka 2020. Ongezeko hilo limepunguza matumizi ya jembe la mkono kutoka asilimia 53 mwaka 2019 hadi asilimia 50 mwaka 2020. Aidha, matumizi ya wanyamakazi yameendelea kubaki asilimia 27. Katika

kipindi hicho sekta binafsi imeingiza nchini matrekta makubwa 1,124 na matrekta madogo ya mkono 459 na hivyo kufanya idadi ya matrekta makubwa kuwa 19,212 na matrekta madogo ya mkono 9,342.



*Matumizi ya trekta katika maandalizi ya shamba la miwa - Kilombero*

91. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na *Agricom African Ltd* imetoa mafunzo kuhusu matumizi ya zana bora za kilimo kwa wakulima 6,199 na Maafisa Ushirika nane (8) katika Halmashauri za Wilaya ya Nkasi, Kalambo, Sumbawanga na Manispaa ya Sumbawanga Mkoa wa Rukwa.

92. Vilevile, Wizara imewatambua wabunifu na watengenezaji 12 wa zana za kilimo katika mikoa ya Manyara, Dodoma, Shinyanga, Mwanza, Arusha, Njombe na Tanga kwa lengo la kuwaunganisha na taasisi za teknolojia za CAMARTEC na SIDO ili kuboresha ufanisi wa zana hizo kuendana na soko. Zana zilizobuniwa ni pamoja na mashine ya kuchakata mkonge, mashine ya kupura mahindi, mashine ya kukata michembe, mashine ya kupanda ngano na ufuta inayokokotwa na wanyamakazi, mashine ya kubangua karanga, mashine ya kuchakata mkonge, pampu za

kumwagilia maji mashambani na trekta. Aidha, mafunzo ya mikopo ya zana za kilimo yametolewa kwa wakulima 245 kutoka Wilaya ya Igunga.

### **Mfuko wa Pembejeo**

**93. Mheshimiwa Spika**, hadi Aprili 2021, Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo (AGITF) imetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi 1,388,058,000 kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za kilimo kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 2**. Aidha, katika kipindi hicho Mfuko umekusanya Shilingi 2,096,465,589 sawa na asilimia 33.77 ya lengo la Shilingi 6,207,899,734 kwa mwaka ikiwa ni marejesho ya mikopo, riba na riba ya adhabu. Kutofikiwa kwa malengo hayo kumetokana na mabadiliko ya hali ya hewa, kukosekana kwa masoko ya uhakika ya mazao ya kilimo kulikotokana na janga la ugonjwa wa Corona na kuwakosesha wakopaji kipato, hivyo wakulima wengi wao kushindwa kulipa mikopo yao kwa wakati.

### **Jedwali Na. 2: Mikopo Iliyotolewa Hadi Aprili, 2021**

<b>Na.</b>	<b>Aina ya Mkopo</b>	<b>Idadi ya mikopo</b>	<b>Thamani</b>
1.	Matrekta	20	944,500,000.00
2	Mashine	1	11,100,000.00
3	Matrekta ya mkono ( <i>power tiller</i> )	2	22,400,000.00
4	Umwagiliaji	3	84,808,000.00
5	Ufugaji	2	75,000,000.00
6	Uvuvi	1	35,000,000.00
7	Fedha za kuendeshea shughuli za shamba	2	60,000,000.00
8	Pembejeo	5	155,250,000.00
<b>Jumla</b>		<b>36</b>	<b>1,388,058,000</b>

*Chanzo: Wizara ya Kilimo, 2021*

### **Huduma za Ugani**

**94. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/2021 Wizara imeendelea na jitihada za kuimarisha huduma za



ugani. Kupitia mradi wa *Rapid Response Implementation Support* - RARIS imetoa Vifaa vya TEHAMA na ujenzi wa kitalu nyumba katika Vituo vya Mafunzo vya Wakulima vya Ichenga (Njombe), Bihawana (Dodoma) na Mkindo (Morogoro). Pia, Wizara kupitia TARI imetoa mafunzo kwa wakulima 51,304 na maafisa ugani 982 kuhusu teknolojia bora za kilimo kupitia vituo 11 vya TARI na Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia (Nyakabindi AgriTech).

95. Vilevile, Wizara imeandaa rasimu ya Mwongozo wa Usimamizi na Uratibu wa Huduma za Ugani utakaotumiwa na sekta ya umma na binafsi ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma hizo. Aidha, kupitia TARI, Wizara imetoa matokeo ya utafiti kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kwa lengo la kuhamasisha matumizi ya teknolojia na ubunifu.

96. **Mheshimiwa Spika**, Wizara pia, imeratibu maonesho ya wakulima (Nanenane) yaliyofanyika Kitaifa katika kiwanja cha Nyakabindi - Simiyu na katika Kanda saba (7) ambapo teknolojia za kilimo zilioneshwa. Katika maonesho hayo, jumla ya wadau 2,253 na Wakulima 1,250 walihudhuria na kujifunza teknolojia za kilimo bora na fursa za masoko.

97. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la *Lutheran World Relief* (LWR) kupitia mradi wa *Investing in New Venture of Entrepreneurial Student in Tanzania* - INVEST imewezesha wanafunzi 48 wa Chuo cha Sukari Nchini (NSI) kujengewa umahiri wa kujiajiri wenyewe baada ya kuhitimu. Wanafunzi hao wamewezeshwa kuanzisha miradi ya uzalishaji wa sabuni (3), nyanya (4), matikiti maji (5), *crips* za viazi na ndizi (5), uyoga (5), kukausha samaki (3), ufugaji wa samaki aina ya kambale (4), Piliipili hoho (4), asali (4), jamu, achali na juisi ya matunda (5), vyakula vya mifugo (1), kuku wa nyama (4) na batiki (1).

98. Vilevile, wanafunzi 26 wa chuo cha KATRIN wamewezeshwa kuendesha miradi ya uzalishaji wa tikitimaji (5), ufugaji wa samaki (5), ufugaji wa ng'ombe wa maziwa

(5), ufugaji wa kuku wa kienyeji (5) na utotoleshaji wa vifaranga vya kuku (6).

## Uzalishaji wa Mazao

### a) Mazao Makuu Asilia ya Biashara

**99. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/2021, Wizara imeendelea kutekeleza mikakati ya uzalishaji wa mazao asilia ya biashara ya Tumbaku, Pamba, Kahawa, Chai, Pareto, Korosho, Mkonge na Miwa. Katika kipindi hicho mwenendo wa uzalishaji wa mazao hayo ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 3**.

### Jedwali Na. 3: Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao Makuu Asilia ya Biashara

Zao	2016/2017	2017/2018	2018/2019	2019/2020	2020/2021
Pamba	132,934	222,039	348,910	348,958	122,833
Kahawa	48,329	45,245	68,147	60,651	67,675.91
Chai	26,975	34,010	37,193	28,715	10,940*
Pareto	2,150	2,400	2,014	2,510	2,005*
Tumbaku	58,639	50,522	70,824	37,546	68,571
Korosho	265,238	313,826	225,053	232,681	206,718.880
Mkonge	36,533	40,635	33,271	36,379	36,292.67
Sukari	330,843	303,752	359,219	311,357.61	361,474.37
<b>Jumla</b>	<b>901,641</b>	<b>1,012,429</b>	<b>1,144,631</b>	<b>1,058,798</b>	<b>876,510.83</b>

Chanzo: Wizara ya Kilimo; 2021

\* Uzalishaji unaendelea

## Zao la Tumbaku

**100. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/2021 uzalishaji wa Tumbaku ulikuwa tani 68,571 ikilinganishwa na tani 37,546 mwaka 2019/2020. Ongezeko hilo limetokana na matumizi bora ya mbolea ambapo tani 23 za mbolea ya N.P.K 10:18:24 zimesambazwa kwa wakulima 25,957 ambao wameingia mikataba ya uzalishaji na kampuni za ununuzi wa tumbaku kupitia Vyama vya Ushirika 377.



*Shamba la tumbaku - Tabora*

101. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hicho, ekari 123,131 zimepandwa tumbaku sawa na asilimia 113.5 ya lengo la ekari 108,482. Pia, miche ya miti 20,362,656 ya kukaushia tumbaku ya wakulima imeoteshwa ikilinganishwa na lengo la miti 24,321,795. Aidha, Bodi ya Tumbaku imekagua mabani ya kisasa 94,663 ya kukaushia tumbaku kati ya mabani 134,881 na kubainika kuwa yanakidhi vigezo.

### **Zao la Pamba**

102. **Mheshimiwa Spika**, katika msimu wa ununuzi 2020/2021 tani 122,833 za pamba zilizalishwa na kuuzwa ikilinganishwa na tani 348,958 katika msimu wa ununuzi wa 2019/2020. Upungufu huo, umetokana na mvua nyingi pamoja na kushuka kwa bei katika soko la dunia kwa msimu wa ununuzi wa 2019/2020 ambapo baadhi ya wakulima waliacha kulima pamba.

**103.** Aidha, katika msimu wa ununuzi wa 2020/2021, Wizara kupitia Bodi ya Pamba imetoa leseni za ununuzi wa pamba kwa Kampuni 24 kwa ajili ya kununua pamba katika mikoa ya Kanda ya Magharibi na kampuni moja katika Kanda ya Mashariki. Vilevile, viwanda viwili vya kuchambua pamba vilivyo chini ya Chama Kikuu cha Ushirika Chato (Geita) na Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (Shinyanga) vilifufuliwa na kuanza kufanya kazi msimu wa ununuzi 2020/2021.

**104.** *Mheshimiwa Spika*, katika msimu wa kilimo 2020/2021, Bodi imesambaza tani 15,495 za mbegu bora na Ekapaki 2,711,728 za viuatilifu kwa wakulima. Kati ya mbegu hizo, tani 261 zimeondolewa nyuzi (*delinted*) na tani 15,234 zisizoondolewa nyuzi (*fuzzy*). Mbegu hizo zimepandwa katika eneo la ekari 1,587,650 katika mikoa yote inayozalisha pamba nchini. Vilevile, mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha pamba yametolewa kwa Maafisa Ugani 72 na wakulima 1,000 kutoka Mikoa ya Mara, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Geita.

## Zao la Kahawa

**105.** *Mheshimiwa Spika*, hadi Aprili 2021, uzalishaji wa kahawa umefikia tani 67,675.91. Kahawa hiyo yote imeuzwa na kuliingizia Taifa Dola za Marekani milioni 133. Kati ya tani hizo, Arabika laini ni tani 27,822.75, Arabika ngumu ni tani 1,936.89 na Robusta ni tani 37,916.27. Wastani wa bei kwa wakulima wa kahawa kavu ya Arabika (*parchment*) imeongezeka kutoka shilingi 3,500 mwaka 2019/2020 hadi Shilingi 4,000 mwaka 2020/2021 kwa kilo na bei ya kahawa ya maganda ya Robusta (*Dry Cherry*) imeongezeka kutoka Shilingi 1,100 mwaka 2019/2020 hadi Shilingi 1,200 mwaka 2020/2021 kwa kilo. Ongezeko hilo limetokana na uhitaji mkubwa wa kahawa katika soko la dunia na kuongezeka kwa ubora wa kahawa.



*Kahawa bora aina ya Arabika katika Wilaya ya Hai – Kilimanjaro*

**106.** Aidha, katika msimu wa 2020/2021 *Alliance for Coffee Excellence (ACE)* kwa kushirikiana na *Portland Global Initiative* na wawekezaji wenye mashamba makubwa wilayani Karatu (Ngorongoro Coffee Group) waliandaa na kuendesha mashindano ya kupata kahawa bora. Mashindano hayo yalikusisha wazalishaji wa mashamba makubwa sita ambao waliwasilisha sampuli kutoka kwenye lot 40 zilizoandaliwa kwa njia sita tofauti ambapo lot 26 zilipata alama zaidi ya 80. Kahawa hizo ziliuzwa kwa njia ya mnada (*online auction*) na katika mnada huo kahawa yenye ubora wa juu zaidi kutoka shamba la Acacia ilishindaniwa na kununuliwa kwa bei ya juu zaidi ya Dola za Marekani 143.3 kwa kilo. Aidha, katika mnada huo makampuni zaidi ya 28 yalishiriki kununua kahawa iliyozalishwa Tanzania kutoka kwenye mataifa ya Marekani (USA), South Korea, Canada, Hong Kong, Thailand, Falme za Kiarabu, Belgium, Taiwan, Greece, Japan na Kuwait. Mnada huo uliuzwa kahawa yenye uzito wa kilogramu 6,380.475 na kuingiza Dola za Marekani 120,500.46.

107. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/2021, Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (TaCRI) imezalisha miche 3,244,709 na kusambaza bure kwa wakulima 231. Aidha, TaCRI kwa kushirikiana na Wilaya ya Tarime imetenga ekari 10 za kuzalisha mbegu chotara zinazostahimili ukame pamoja na matumizi kidogo ya mbolea; imetafiti na kutoa aina mpya za mbegu bora za Arabika na Robusta zenye tija kubwa na ukinzani dhidi ya magonjwa na ubora wa viwango vya kimataifa.

108. Vilevile, TaCRI imezalisha na kusambaza kilo 2,600 za mbegu chotara aina ya *compact* na kilo 30 aina ya Robusta *composite* kwa wakulima na kutoa mafunzo kwa Maafisa Ugani 168 na wakulima viungo 53 kuhusu kanuni bora za kilimo cha Kahawa.

## Zao la Chai

109. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/2021 uzalishaji wa Chai kavu umefikia tani 10,940 ikilinganishwa na tani 11,185.8 za kipindi kama hicho mwaka 2019/2020. Uzalishaji huo umeshuka kutokana na mabadiliko ya tabianchi na baadhi ya wawekezaji kusitisha uzalishaji kutokana na mlipuko wa homa kali ya mapafu (Covid-19). Aidha, Bodi ya Chai imefufua shamba la Chama cha Ushirika cha MUVYULU lenye hekta 215 na shamba la Mlangali linalomilikiwa na Kampuni ya *Dhow Mercantile (EA) Ltd* lenye hekta 200 limeanza kutumia kilimo cha umwagiliaji.

110. **Mheshimiwa Spika**, miche bora 6,120,000 ya chai imepandwa na miche 5,500,000 inaendelea kutunzwa kwenye vitalu katika Wilaya za Mufindi na Njombe. Kwa upande wa Wilaya ya Njombe, Kampuni ya *Njombe Outgrower Service Company* (NOSC) imepanda miche 6,000,000 na Mufindi *Outgrower Project* (MOG) imepanda miche 120,000. Kwa miche inayotunzwa vitaluni, Mradi wa MOG unatunza miche 800,000 na NOSC miche 4,700,000. Miche hiyo itapandwa katika msimu wa 2020/2021.

111. **Mheshimiwa Spika**, Bodi imetoa mafunzo kuhusu uongozi bora na umuhimu wa mikataba ya uuzaji chai kwa viongozi 69 wa Vyama vya Ushirika ili kupata uhakika wa bei na soko. Aidha, Bodi imetoa mafunzo kwa wakulima wadogo 390 kuhusu kanuni za kilimo bora cha chai ambao watatumika kama wakufunzi katika maeneo yao kwa lengo la kuongeza tija, ubora na ushindani wa chai ya Tanzania kwenye masoko ya kimataifa. Kwa mfano katika Wilaya ya Rungwe ubora wa majani mabichi ya chai umeongezeka kutoka asilimia 70 hadi 85 na Tarafa ya Lupembe ubora umeongezeka kutoka asilimia 45 hadi kufikia 65.

112. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Chai Tanzania (*Tea Research Institute of Tanzania - TRIT*) inaendelea kutekeleza mpango kabambe wa kuhaulisha teknolojia za uvunaji chai kwa njia ya mashine ili kukabiliana na uhaba wa nguvukazi unaoanza kujitokeza kwenye kilimo cha chai. Mpango huo ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa *Agri-connect* unaofadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya (EU). Utafiti wa mashine hizo unaendelea katika Wilaya ya Rungwe ambapo mashine 30 za uchumaji wa chai (*motorized hand plucking machines*) zimenunuliwa na kusambazwa katika vikundi vya wachumaji kwa lengo la kuangalia ufanisi wake.



*Uvunaji wa Majani ya Zao la Chai*

## Zao la Pareto

113. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/2021 uzalishaji wa maua ya pareto ulikuwa tani 2,005. Aidha, ubora wa maua ya pareto umefikia asilimia 1.24 ikilinganishwa na lengo la asilimia 1.3. Vilevile, Bodi imetoa mafunzo ya uzalishaji wa mbegu bora za pareto kwa wakulima 75 kutoka katika maeneo ya uzalishaji; imekagua vituo 40 vya ununuzi wa pareto kati ya vituo 53 vilivyopo katika Halmashauri za Mbeya, Ileje, Arusha na Mbulu Mji kwa lengo la kuhakiki uhifadhi wa pareto, ubora wa mizani, usafi na usalama wa ghala na vitabu vya stakabadhi za malipo.

## Zao la Miwa na Uzalishaji wa Sukari

114. *Mheshimiwa Spika*, hadi Aprili 2021, uzalishaji wa sukari ulikuwa tani 361,474.37 sawa na asilimia 95.74 ya lengo la kuzalisha tani 377,527. Uzalishaji huo umeongezeka kwa asilimia 16 ikilinganishwa na tani 311,357.61 zilizozalishwa mwaka 2019/2020. Kati ya mwezi Julai 2020 na Januari 2021 bei ya sukari ya jumla ilishuka kutoka Shilingi 2,526 hadi Shilingi 2,388 kwa kilo na bei ya rejareja kutoka Shilingi 2,847 hadi Shilingi 2,687 kwa kilo.



*Shamba la miwa - Mtibwa*



115. **Mheshimiwa Spika**, ili kuendeleza tasnia ya Sukari nchini, Bodi ya Sukari inaendelea kutoa mafunzo ya mbinu bora za kilimo cha miwa. Hadi Aprili, 2021, wakulima 533 kutoka maeneo ya Kilombero, Mtibwa, Kagera na Manyara wamepata mafunzo ya kilimo bora. Aidha, mafunzo kuhusu ununuzi wa mbolea kwa mfumo wa pamoja yalitolewa kwa Vyama nane vya Ushirika vilivyopo Mtibwa (2), Manyara (3) na Kagera (3). Vilevile, Bodi kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Mfuko wa Maendeleo ya Tasnia ya Sukari imetoa mafunzo kwa wajumbe 267 wa Bodi za Vyama vya Ushirika wa miwa katika nyanja za uongozi, maadili, uandaaji wa taarifa na hesabu za vyama.

116. **Mheshimiwa Spika**, ili kuhudumia wateja kwa wakati, kutunza takwimu pamoja na kudhibiti uhalali wa leseni na vibali, Bodi imeunganisha mfumo wa *SBT mobile application* na mfumo wa utoaji vibali wa ATMIS. Pia, Bodi imeunganisha mfumo wa ATMIS na mfumo wa makusanyo ya fedha za Serikali (*Government Electronic Payment Gateway – GePG*) ili kurahisisha utoaji wa namba za malipo (*Payment Control Numbers*) na kuboresha huduma kwa wateja. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*Tanzania Revenue Authority - TRA*) imedhibiti sukari iendayo nje ya nchi "*On Transit Sugar*" kwa kutumia mfumo wa *Cargo Tracking System* ambao umesaidia sukari hiyo isibaki nchini na kuharibu soko la sukari.

117. **Mheshimiwa Spika**, ili kuongeza uzalishaji wa sukari na kupunguza nakisi iliyopo, Bodi imefuatilia matayarisho ya ujenzi wa kiwanda cha Bagamoyo yanayoendelea ambapo hadi sasa hekta 800 zimelimwa kwa ajili ya kupanda miwa, majaribio ya mbegu 22 za miwa zinazotoa mavuno ya tani 160 kwa hekta zimepandwa katika eneo la hekta 30. Mbegu hizo zitatoa kupanda eneo la hekta 2,000.

118. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na kiwanda cha Bagamoyo, Bodi imeratibu uanzishwaji wa mashamba ya Kampuni ya Mkulazi yenye ukubwa wa hekta 2,482 ambapo

hekta 1,948 zimepandwa miwa. Pia mashamba ya wakulima wadogo yenye hekta 1,480 zimelimwa na kati yake hekta 850 zimepandwa miwa. Miwa hiyo ilitegemewa kuuzwa kwenye kiwanda ambacho kimechelewa kusimikwa. Ili kupata soko la miwa iliyokwisha pandwa, Uongozi wa kiwanda cha Mkulazi na wakulima wadogo wameingia mkataba wa kuuza miwa na kiwanda cha Mtibwa kwa makubaliano ya bei ya Shilingi 63,000 kwa tani moja. Uchakataji wa miwa katika kiwanda kitakachosimikwa Mkulazi unatarajia kuanza mwezi Desemba, 2022.

### ***Zao la Korosho***

119. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021 uzalishaji wa korosho umefikia tani 206,718.880 ikilinganishwa na tani 232,631 mwaka 2019/2020. Kushuka kwa uzalishaji kumetokana na mabadiliko ya hali ya hewa yaliyosabisha kuzuka kwa magonjwa na visumbufu vya mimea na matumizi madogo ya pembejeo. Kufuatia hali hiyo, Bodi ya Korosho inasimamia mpango wa ununuzi wa pembejeo kwa pamoja kupitia Vyama vikuu vya Ushirika ili wakulima waweze kupata pembejeo kwa wakati na kwa bei nafuu.

120. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendeleza zao la korosho, Wizara kupitia Bodi ya Korosho imeratibu ununuzi na usambazaji wa tani 60 za mbegu bora ambazo zitazalisha miche 9,000,000. Mbegu hizo zimesambazwa katika Halmashauri za Sumbawanga, Mafia, Songwe, Mpanda, Tanganyika, Nsimbo, Tabora, Mlele, Mpimbwe na Kyela. Vilevile, Bodi kwa kushirikiana na Vyama Vikuu vya Ushirika imesambaza tani 8,730 za salfa na lita 82,438 za viuatilifu vya maji kwa wakulima. Bodi pia, imetoa mafunzo kwa wakulima 845, Maafisa Ugani 1,396 na viongozi wa AMCOS 1,000 kutoka Wilaya 27 kuhusu kilimo bora cha korosho.

### ***Zao la Mkonge***

121. ***Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili 2021, uzalishaji wa mkonge umefikia tani 36,292.67 na uzalishaji unaendelea. Hivyo, ni mategemeo ya Wizara kuwa hadi mwisho wa msimu uzalishaji utazidi tani 36,379 zilizozalishwa mwaka 2019/2020.

122. **Mheshimiwa Spika**, mauzo ya bidhaa za mkonge nje ya nchi ikiwemo mazulia, kamba, vikapu, mapambo na magunia yameshuka kutoka tani 3,682.54 mwaka 2019/2020 hadi tani 2,107.32 mwaka 2020/2021. Pia, mauzo ya ndani kwa bidhaa hizo yameshuka kutoka tani 2,908.91 mwaka 2019/2020 hadi tani 1,826.73. Kushuka kwa mauzo kumechangiwa na mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu (*Covid-19*) ulioathiri uuzaji wa bidhaa hizo kwenye masoko ya China, India, Iraq, Saudi Arabia, Nigeria na Morocco. Pamoja na kushuka kwa mauzo, bei ya mkonge kwa wakulima wadogo waliojiunga na AMCOS imeendelea kuimarika ambapo mkonge unaouzwa kwa zabuni daraja la UG umefikia shilingi 3,600,000 kwa tani ukilinganisha na shilingi 3,500,000 kwa tani mwaka 2019/2020.

123. **Mheshimiwa Spika**, ili kuongeza uzalishaji wa zao la mkonge, Wizara kupitia TARI imepanda hekta 35.4 za vitalu vya miche ya mkonge katika kituo cha TARI Mlingano (hekta 33.8), Halmashauri ya Wilaya ya Muheza (hekta 1.2) na Gairo hekta 0.4. Eneo hilo litawezesha upatikanaji wa miche 2,896,000 ya mkonge ambayo itatosheleza kupanda hekta 579.2. Vilevile, Wizara kupitia Bodi ya Mkonge imeanzisha kitalu cha hekta 3.75 katika shamba la Hale na shamba darasa katika Wilaya ya Butiama.



*Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akizindua zoezi la kugawa miche bora ya mkonge kwa wakulima wa Mkoa wa Tanga ikiwa ni mkakati wa Serikali kukuza zao hilo alipotembelea TARI Mlingano Januari, 2021.*

124. *Mheshimiwa Spika*, TARI kwa kushirikiana na Bodi ya Mkonge imetoa mafunzo ya kanuni bora za kilimo cha Mkonge kwa Maafisa Ugani 867 katika Mikoa ya Tanga, Mara, Morogoro, Kilimanjaro, Shinyanga, Simiyu, Pwani na Lindi ambapo vitabu 650 vya kanuni bora za uzalishaji wa mkonge vimesambazwa kwa wakulima. Vilevile, wakulima 543 wamepatiwa mafunzo katika Wilaya za Mvomero, Gairo, Kilosa, Mkuranga, Kisarawe, Kibaha, Mtama, Ruangwa na Liwale.

### Mazao ya Mafuta

125. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/2020 uzalishaji wa mazao ya mafuta (alizeti, karanga, ufuta, chikichi na soya) umefikia tani 1,583,669.28 ikilinganishwa na tani 1,230,767 mwaka 2018/2019. Uzalishaji wa alizeti umefikia tani 649,437.3 ikilinganishwa na tani 561,297 za mwaka 2018/2019 (**Jedwali Na. 4**). Vilevile, katika kipindi hicho uzalishaji wa zao la ufuta umeongezeka kutoka tani 227,821 hadi tani 228,919.8 na uzalishaji wa zao la chikichi umeongezeka kutoka tani 42,176 hadi tani 42,386.88. Ongezeko hilo limetokana na matumizi ya teknolojia na kanuni za kilimo bora.

### Jedwali Na 4: Uzalishaji wa Mazao ya Mafuta (Tani)

Zao	2016/2017	2017/2018	2018/2019	2019/2020
Alizeti	352,902	543,261	561,297	649,437.3
Karanga	216,167	370,356	376,520	631,465.3
Ufuta	56,846	133,704	227,821	228,919.8
Chikichi	42,277	40,500	42,176	42,386.88
Soya	6,135	21,321	22,953	31,460
<b>Jumla</b>	<b>674,327</b>	<b>1,109,142</b>	<b>1,230,767</b>	<b>1,583,669.28</b>

Chanzo: Wizara ya Kilimo, 2021

126. *Mheshimiwa Spika*, ili kuongeza uzalishaji hatua mbalimbali zimechukuliwa zikihusisha kutoa mafunzo kwa wakulima 26,665 wa alizeti kuhusu kanuni za kilimo bora katika Wilaya za Kilosa, Kilombero, Gairo, Kondoa, Kilindi, Chamwino, Singida, Sikonge, Babati, Kibaha, Handeni,

Iramba, Manyoni, Ifakara, Sengerema, Kahama, Masasi, Mbozi, Nachingwea, Ruangwa, Momba na Kalambo; kutoa mafunzo ya kilimo bora cha michikichi kwa Maafisa Ugani 133 kutoka Wilaya nane (8) za Mikoa ya Kigoma, Mbeya na Ruvuma, wakulima 1,905, wanafunzi 16 wa Vyuo Vikuu, 50 wa sekondari na vijana 1,100 wa JKT Bulombora katika Mkoa wa Kigoma; na TARI kusambaza teknolojia ya matumizi ya mbegu bora za ufuta kwa wakulima na Maafisa Ugani 4,353 katika Mikoa ya Manyara, Dodoma, Morogoro, Katavi, Kigoma, Ruvuma, Mbeya, Pwani, Lindi, Mtwara na Singida. Matumizi ya mbegu bora za ufuta na kanuni za kilimo bora katika maeneo yaliyofikiwa, yamewezesha tija kuongezeka kutoka tani 0.3 kwa hekta hadi tani 1.0 kwa hekta.

127. **Mheshimiwa Spika**, upatikanaji wa mbegu bora za alizeti na ufuta umefikia tani 441.42 na 90.51 mtawalia. Aidha, Wizara kupitia TARI imezalisha mbegu 3,824,508 za chikichi na kusambaza miche 10,200 katika Mikoa ya Kigoma, Katavi, Kagera, Rukwa, Mbeya, Pwani na Ruvuma. Vilevile, TARI imenunua viotesheo vya asili 80 (*local germinators*) vyenye uwezo wa kuotesha mbegu 800,000 za chikichi kwa wakati mmoja na kuongeza upatikanaji wa mbegu kwa wakulima. TARI pia imenunua matrekta mawili (2) na zana unganishi kwa ajili ya vituo vya utafiti vya Tumbi na Kihinga.



Waziri wa Kilimo Mhe. Prof. Adolf F. Mkenda akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Gereza la Kwitanga - Kigoma kuhusu uzalishaji wa miche bora ya chikichi

## c) Mazao ya Bustani

128. *Mheshimiwa Spika*, uzalishaji wa mazao ya bustani umeongezeka kutoka tani 6,597,863.2 mwaka 2018/2019 hadi kufikia tani 7,560,010 mwaka 2019/2020 (**Jedwali Na. 5**). Ongezeko hilo limetokana na kuhamasika kwa vijana kuzalisha mazao ya bustani na mafunzo kuhusu teknolojia za kisasa za uzalishaji wa mazao hayo. Aidha, Wizara imetoa mafunzo kwa wakulima 135 mkoani Tanga kuhusu uhibitaji wa ugonjwa wa unyauifu kwenye zao la pilipili manga.

**Jedwali Na 5: Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao ya Bustani (Tani)**

Zao	2016/2017	2017/2018	2018/2019	2019/2020
Matunda	5,243,343	3,703,124	4,576,948	5,582,117.3
Mboga	1,298,388	1,595,489	1,926,927	1,852,676
Maua	11,615	12,622	13,240	1,709.5
Viungo	22,062	22,062	80,748.2	123,507.9
<b>Jumla</b>	<b>6,575,408</b>	<b>5,333,297</b>	<b>6,597,863.2</b>	<b>7,560,010</b>

*Chanzo: Wizara ya Kilimo, 2021*

129. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha sekta ndogo ya mazao ya bustani, Wizara imeandaa Rasimu ya Mkakati wa Uendelezaji wa Mazao ya Bustani wa miaka 10 (2021-2030) na kuuwasilisha kwa wadau kwa ajili ya maoni na maboresho. Mkakati huo utakuwa ni dira ya uwekezaji katika mnyororo wa thamani wa mazao ya bustani ili kuongeza uzalishaji na kuimarisha upatikanaji wa masoko ya ndani na nje ya nchi.

130. Pia, Wizara kupitia Mradi wa Lishe Endelevu unaotekelezwa na Shirika la *Save the Children* imezindua miongozo minane (8) ya uzalishaji na usimamizi wa mazao ya bustani baada ya kuvuna ambapo nakala 4,000 za miongozo hiyo imechapishwa. Aidha, Maafisa Ugani 791 na wakulima 31,460 kutoka Mikoa ya Rukwa, Iringa, Morogoro na Dodoma wamepatiwa mafunzo kuhusu uzalishaji wa

mazao ya bustani na kuwezesha kuanzishwa kwa mashamba darasa 980 katika Mikoa hiyo.

131. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Mradi wa Kuimarisha Uzalishaji wa Mazao ya Bustani kwa Wakulima Wadogo (*Tanzania Smallholder Horticulture Empowerment Project-TANSHEP*) wenye kaulimbiu ya “*Anzia Sokoni Malizia Shambani kwa Kipato Zaidi*” unaotekelezwa katika Halmashauri za Karatu, Meru, Lushoto, Bumbuli, Hai na Moshi imetoa mafunzo ya kilimo bora cha mazao ya bustani kwa Maafisa Ugani 156 na wakulima 1,610. Mafunzo hayo yamehusisha utafutaji wa masoko, utunzaji wa kumbukumbu, mbinu bora za kilimo cha kisasa cha mazao ya bustani na ukokotoaji wa gharama za uzalishaji.

132. Aidha, TARI imetoa mafunzo ya kanuni bora za kilimo na matumizi ya mbolea kwa zao la migomba kwa Maafisa Ugani 11 na wakulima 85 wa Wilaya za Rombo na Moshi Vijijini. TARI pia, imezalisha mbegu bora za mchicha tani 1.376 zikiwemo za awali tani 0.25 na za msingi 1.126.

133. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia SAGCOT imehamasisha wawekezaji wawili (Tanzanice Agrofoods Ltd & Olivado Tanzania Ltd) katika mikoa ya Iringa na Njombe ambao wamewezesha kuongezeka kwa mauzo ya parachichi kutoka tani 3,696 mwaka 2015 hadi tani 7,190 mwaka 2019 kwa wakulima wadogo. Aidha, bei ya parachichi imeongezeka kutoka Shilingi 1,200,000 kwa tani mwaka 2015 hadi Shilingi 1,800,000 kwa tani mwaka 2020. Uwepo wa kampuni hizi zinazowahakikishia wakulima soko imekuwa ni chachu ya kuongezeka kwa uzalishaji wa matunda.

### c) Mazao ya Chakula

134. **Mheshimiwa Spika**, uzalishaji wa mazao ya hakula unaojumuisha mahindi, mpunga, mtama/uwele, ngano, mikunde, ndizi, muhogo na viazi umeendelea kuongezeka kutokana na matumizi ya kanuni bora za kilimo, teknolojia bora za uzalishaji, usimamizi wa mazao baada ya

kuvuna, kuongeza thamani ya mazao na elimu inayotolewa kwa wadau katika mnyororo wa thamani wa mazao ya chakula na kuwaunganisha wakulima na masoko.

## Zao la Mahindi

**135. *Mheshimiwa Spika***, uzalishaji wa mahindi umeongezeka kutoka tani 5,652,005 mwaka 2018/2019 hadi tani 6,711,002 mwaka 2019/2020 Ongezeko hilo limetokana na matumizi ya mbegu bora, mbolea na viuatilifu pamoja na hali nzuri ya hewa katika maeneo ya uzalishaji. Aidha, upatikanaji wa mbegu bora za mahindi umefikia tani 38,071 ambapo tani 23,445.50 zilizalishwa nchini, tani 7,343 zilingizwa kutoka nje ya nchi na tani 7,282 ni bakaa ya msimu wa 2018/2019.

Zao la Mpunga

**136. *Mheshimiwa Spika***, uzalishaji wa mpunga umeongezeka kutoka tani 3,174,766.153 mwaka 2018/2019 hadi tani 4,673,969.231 mwaka 2019/2020. Ongezeko hilo limetokana na uhamasishaji wa matumizi ya kanuni bora za kilimo, teknolojia bora za uzalishaji, usimamizi baada ya kuvuna pamoja na uimarishwaji wa miundombinu ya umwagiliaji.



*Uvunaji wa zao la mpunga kwa kutumia zana bora*



**137. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (*Food and Agriculture Organisation – FAO*) kupitia Mradi wa Kupunguza Upotevu na Kuimarisha Mnyororo wa Thamani wa Zao la Mpunga imetoa mafunzo ya usimamizi wa mpunga baada ya kuvuna kwa Maafisa Ugani 563 kutoka Mikoa ya Mbeya, Songwe, Iringa, Morogoro, Shinyanga, Tabora, Manyara, Kilimanjaro, Mwanza, Rukwa na Dodoma. Aidha, nakala 1,750 za Mwongozo wa Uzalishaji na Usimamizi wa Zao la Mpunga Baada ya Kuvuna zimesambazwa katika Mikoa hiyo. Vilevile, ujenzi wa ghala lenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,200 za mpunga umekamilika na kukabidhiwa kwa wakulima katika Wilaya ya Iringa.

### **Zao la Ngano**

**138. Mheshimiwa Spika**, uzalishaji wa ngano umeongezeka kutoka tani 63,388 mwaka 2018/2019 hadi tani 77,276 mwaka 2019/2020. Uzalishaji huo ni pungufu ikilinganishwa na mahitaji ya tani 1,000,000 za majumbani na viwandani kwa mwaka. Ili kukabiliana na upungufu huo, Wizara imeandaa mkakati unaolenga kuongeza uzalishaji wa zao la ngano nchini kwa kufufua mashamba ya ngano, kuongeza matumizi ya mbegu bora. Kuhamasisha kilimo cha mkataba na matumizi ya zana bora kwa kufufua mashine zilizokuwa zinatumika kwenye mashamba ya ngano na kuhamisha uzalishaji wa ngano katika skimu za umwagiliaji baada ya kuvuna mpunga. Majaribio ya uzalishaji wa ngano katika skimu za umwagiliaji yamefanyika katika Skimu ya Bahi (Dodoma) na kuonesha mafanikio makubwa. **139.** Aidha, upatikanaji wa mbegu bora za ngano umeongezeka kutoka tani 63.7 mwaka 2019/2020 hadi tani 1,363.32 mwaka 2020/2021. Vilevile, TARI imeanzisha mashamba nane (8) ya mfano katika skimu za umwagiliaji za Kapunga, Mbarali, Kifyulilo, Ifwani, Nguvumali, Ganila, Liodi na West Kilimanjaro ili kuongeza maeneo ya uzalishaji wa ngano nchini.

**140. Mheshimiwa Spika**, katika kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa masoko, Wizara kupitia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (*Cereals and other Produce Board*

- CPB) imeingia mkataba na wakulima 264 wa Siha, Karatu, Monduli na Hanang' ambao wamelima ekari 2,937. Bodi hiyo imewakopesha wakulima mbegu bora za ngano tani 210 na kuwaunganisha na mabenki ambayo yamewapatia mikopo ya kununulia mbolea na viuatilifu.

141. Aidha, Bodi imeanzisha mashamba Darasa katika maeneo hayo kwa ajili ya kuwafundisha wakulima mbinu bora za Kilimo. Ngano itakayozalishwa itanunuliwa na CPB kwa bei ya mkataba ya Shilingi 800 kwa kilo.

## Zao la Muhogo

142. *Mheshimiwa Spika*, uzalishaji wa muhogo mkavu umeshuka kutoka tani 2,728,031 mwaka 2018/2019 hadi tani 2,427,190 mwaka 2019/2020 kutokana na mvua nyingi ambazo ziliathiri ukuaji wa zao hilo. Aidha, hadi Aprili 2021, upatikanaji wa vipando bora vya muhogo umefikia pingili 40,960,500 ikilinganishwa na pingili 30,492,830 za mwaka 2019/2020.



*Waziri wa kilimo Mhe. Prof. Adolf Mkenda akipata maelezo ya mbegu bora za muhogo katika Mkutano wa Wadau wa Kilimo cha Muhogo Tanzania uliofanyika tarehe 7 Mei, 2021 Jijini Dodoma*

143. Katika kuimarisha, uzalishaji, tija na upatikanaji wa masoko endelevu ya zao la muhogo, Wizara imezindua Mkakati wa Miaka Kumi (10) wa Uendelezaji wa zao la Muhogo (2020-2030). Mkakati huo unawaunganisha wadau wote wa zao la muhogo na umelenga kuongeza uzalishaji kutoka wastani wa tani milioni 8.2 mwaka 2019 hadi tani milioni 24 mwaka 2030 na tija kutoka tani 8.3 kwa hekta hadi tani 16 kwa hekta ifikapo 2030.

144. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia TARI imetoa mafunzo kwa wakulima 238 kuhusu uhibitaji wa magonjwa ya batobato na michirizi ya kahawia katika Wilaya za Mkuranga, Muheza, Bagamoyo, Mkinga, Sengerema, Bunda, Mtwara vijijini na Nyasa. Kadhalika, hadi Aprili 2021, tani 320 za muhogo mkavu zimenunuliwa ili kusafirishwa kwenda China.

### **Uongezaji wa Thamani ya Mazao ya Kilimo**

145. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuimarisha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (*Cereals and other Produce Board – CPB*) ili kununua na kuongeza thamani ya mazao ya chakula. Hadi Aprili 2021, tani 2,695.24 za mahindi zilisagishwa na kuzalisha unga tani 2,156.192 na pumba tani 539.048. Katika kipindi hicho jumla ya tani 719.46 za alizeti zilikamuliwa katika kiwanda cha Kizota Dodoma na kuzalisha lita 215,838 za mafuta ya alizeti na tani 503.622 za mashudu. Aidha, Wizara kupitia TARI, imezalisha bidhaa zitokanazo na korosho (*Roasted cashew kernels, White cashew kernels na Cashew apple wine*). Bidhaa hizo zimekidhi viwango vya kimataifa kwa kupata alama ya Shirika la Viwango Tanzania (*Tanzania Bureau of Standards – TBS*) na hivyo zitazalishwa kibiashara.

### **Masoko ya Mazao**

146. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/2021, Wizara imeendelea kufuatilia masoko ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi. Aidha, Wizara kupitia Bodi ya Korosho imeratibu minada 70 ya uuzaji wa korosho ambapo tani 206,718.880 za korosho ghafi zenye thamani ya Shilingi

473,178,774,764 zimeuzwa. Kati ya hizo, daraja la kwanza, bei ya juu ya korosho ilikuwa Shilingi 2,707 na bei ya chini ilikuwa Shilingi 1,685, kwa daraja la pili bei ya juu ilikuwa Shilingi 2,300 na bei ya chini ilikuwa Shilingi 1,300. Vilevile, Wizara kupitia Bodi ya Tumbaku imekagua tani 20,381.4362 za tumbaku viwandani zenye thamani ya Dola za Marekani 74,850,850 na kutoa vibali vya kusafirisha tumbaku hiyo nje ya nchi.

**147. Mheshimiwa Spika**, kwa msimu wa mauzo wa mwaka 2020, tani 8,517 za chai zenye thamani ya Dola za Marekani 11,697,720 zimeuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 7,743 zilizoingiza Dola za Marekani 11,124,716 katika kipindi hicho mwaka 2019 (**Jedwali Na. 6**). Aidha, tani 1,795 za chai zenye thamani ya Shilingi 16,198,395.077 zimeuzwa katika soko la ndani ikilinganishwa na tani 1,505 zilizoingiza Shilingi 12,116,207,210.00 msimu wa mwaka 2019 (**Jedwali Na. 7**). Mauzo ya chai yanaendelea katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

**Jedwali Na. 6: Mauzo ya Chai Soko la Nje**

Msimu	Mauzo (Tani)	Mapato (USD)
Julai-Novemba 2020	8,517.986	11,697,720
Julai-Novemba 2019	7,743.237	11,124,716
Tofauti (tani)	774.749	573,004
Tofauti (%)	1.78	2.56

Chanzo: Wizara ya Kilimo, 2021

**Jedwali Na. 7: Mauzo ya Chai Soko la Ndani**

Msimu	Mauzo (Tani)	Mapato (USD)
Julai- Novemba 2020	1,795.308	16,198,395,077
Julai- Novemba 2019	1,505.445	12,116,207,210
Tofauti (tani)	289.863	4,082,187,868
Tofauti (%)	19.25	33.69

Chanzo: Wizara ya Kilimo, 2021

148. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Bodi ya Pareto imesimamia ununuzi wa zao la Pareto ambapo maua ya pareto yamenunuliwa kwa bei elekezi ya Shilingi 2,500 kwa kilo ikilinganishwa na Shilingi 2,400 ya msimu wa 2019/2020. Aidha, bei ya maua imeongezeka kulingana na ubora ambapo bei ya juu imefikia Shilingi 4,000 kwa kilo.

149. Vilevile, CPB imenunua tani 85.06 za alizeti na tani 23,283.97 za mazao ya nafaka (mahindi tani 21,300.17, mpunga tani 755.94, mtama tani 1,001.08, maharage tani 31.64 na mchele tani 110.08) kutoka kwa wakulima. Aidha, hadi Aprili 2021 tani 61,306 za kahawa zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 123.8 na tani 1,346.7 za choroko zenye thamani ya Shilingi bilioni 2.4 zimeuzwa kwa msimu wa mauzo 2020/2021.

150. **Mheshimiwa Spika**, katika kufungua masoko mapya ya mazao, Wizara ilifanya Mkutano wa wafanyabiashara wa mazao ya nafaka ulioshirikisha Mabalazi wa Nchi za Rwanda, Misri, Burundi, DRC, Zambia, Sudan Kusini, Malawi, Kenya, Uganda na Msumbiji ili waweze kuunganishwa na masoko katika nchi hizo. Vilevile, Wizara imefungua masoko ya mazao mapya ya parachichi katika nchi za India, Marekani na inakamilisha taratibu za kufungua soko la zao hilo katika nchi ya China. Vilevile itafungua soko la maharage ya soya katika nchi ya China ambapo hadi Aprili, 2021 jumla ya wafanyabiashara 49 wamesajiliwa kwenye Mamlaka ya Forodha ya China kwa ajili ya kuuza soya.

151. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inashirikiana na sekta binafsi kuendeleza eneo la ukanda maalum wa uwekezaji Kurasini ili kujengea kituo cha pamoja (Agri hub) cha kutoa huduma za usafirishaji wa mazao kwenda nje ya nchi. Imeratibu na kuwezesha upatikanaji wa vibali kwa wafanyabiashara waliouza tani za mazao.

## ***Kuimarisha Vituo vya Utafiti, Vyuo vya Mafunzo na Vituo vya Wakulima***

### **Vituo vya Utafiti**

**152. *Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TARI imekarabati Ofisi ya Kituo cha TARI Bwanga na kujenga nyumba tatu (3) ambapo ukarabati na ujenzi umefikia asilimia 85. Aidha, TARI imenunua matrekta matano (5) kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu katika Vituo vya Utafiti vya Ilonga, Uyole, Makutupora, Selian na Mlingano. Vilevile, TARI imechimba visima vitatu (3) katika vituo vya TARI Kihinga, Selian na Uyole kwa ajili ya umwagiliaji wa mashamba ya mbegu ambapo hadi Aprili 2021 utekelezaji umefikia asilimia 80. Pia, TARI kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imeendelea kuwajengea uwezo watafiti 50 ambapo watafiti 22 wanasomea shahada ya uzamivu, 19 shahada ya uzamili, saba (7) shahada ya kwanza na wawili (2) stashahada.

### **Vyuo na Vituo vya Mafunzo ya Kilimo**

**153. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021, Wizara imedahili wanafunzi 2,491 wa ngazi ya Astashahada na Stashahada katika vyuo vyake 14 vya Mafunzo ya Kilimo kwa ufadhili wa Serikali. Kati ya hao, wanafunzi 1,345 ni wa mwaka wa kwanza na wanafunzi 1,146 ni wa mwaka wa pili. Vilevile, Wizara imedahili wanafunzi 297 ambao wanajigharamia wenyewe.

**154.** Katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vya mafunzo ya kilimo, Wizara imeendelea kukarabati miundombinu ya vyuo nane (8) vya mafunzo ya kilimo vya KATC, Mlingano, HORTI-Tengeru, Ukiriguru, Maruku, Tumbi, Ilonga na Mtwara.

**155. *Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kilimo Endelevu Tanzania (*Sustainable Agriculture Tanzania – SAT*) na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (*Tanzania Private Sector Foundation-TPSF*) kupitia Mradi wa Kuwezesha

Utekelezaji wa Mitaala Katika Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo (*Curriculum Implementation Support for Training Institute – CISTI*) imehuisha Mitaala sita (6) ya mafunzo ya kilimo ya *Horticulture, Agromechanization, Irrigation Engineering, Agricultural Land Use Planning and Management, Crop Production, Food Technology and Human Nutrition* ili iendane na mahitaji ya soko la ajira.

**156. Mheshimiwa Spika,** Wizara pia kupitia mradi wa CISTI imetoa mafunzo ya stadi za mawasiliano na ushirika kwa wakufunzi 56; mafunzo ya bustani za kilimo hai kwa wakufunzi 28 na mbinu za kufundishia kwa wakufunzi 121. Pia vitini viwili (2) vya kufundishia stadi za mawasiliano na ushirika vimeandaliwa. Vilevile, Wizara kupitia mradi huo imeanzisha bustani za mfano zenye kitalu nyumba, bustani za uani (*backyard gardens*) na bustani za wazi (*open gardens*) katika vyuo tisa (9) vya mafunzo ya kilimo.

**157.** Aidha, vifaa vya mafunzo kwa njia ya mtandao (*e-learning*) vimetolewa katika vyuo 14 vya Serikali na vyuo 15 binafsi. Ili kuhakikisha vyuo vinatoa wataalam wenye weledi wa kutosha katika masuala ya afya ya udongo, Wizara kwa kushirikiana na SAT imetoa vifaa vya kupima udongo (*soil test kits*) kwa vyuo 14 vya Serikali na vyuo 15 binafsi na kituo kimoja cha mafunzo kwa wakulima. Vilevile, Wizara imetoa ufadhili wa mafunzo kwa watumishi sita (6) ngazi ya shahada na watumishi 12 ngazi ya shahada ya uzamili ili kuongeza ufanisi wa ufundishaji.

#### **4.2.8 Kuimarisha Huduma za Upimaji wa Matabaka na Ubora wa Udongo**

**158. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2020/2021 Wizara imetoa mafunzo kuhusu matumizi ya chokaa (*lime*) na teknolojia za uhifadhi wa udongo na maji mashambani kwa Wakurugenzi watendaji watano (5), Wakuu wa Idara 95 na wataalam wa matumizi bora ya ardhi watano (5) kutoka Halmashauri za Wilaya za Momba, Ileje, Mbozi, Mbeya na Kyela katika Mikoa ya Songwe na Mbeya.

159. Ili kuleta ufanisi katika matumizi ya chokaa kama virutubishi vya udongo katika ardhi ya kilimo, Wizara imeandaa Mwongozo wa Matumizi ya Chokaa katika Kilimo. Mwongozo huo utatumiwa na Maafisa Ugani kufundishia wakulima namna ya kuitambua afya ya udongo kwenye mashamba yao na namna ya kukadiria na kutumia chokaa kwenye mashamba ambayo udongo wake una tindikali inayoathiri ukuaji wa mazao na tija.

160. **Mheshimiwa Spika**, TARI imepima sampuli 1,580 za udongo katika Wilaya za Bariadi (Simiyu), Igunga (Tabora) na Bunda (Mara) na kubaini kuwa kiwango cha Naitrojeni kiko chini (kati ya 0.18 – 0.2 mg/l ikilinganishwa na kiwango kinachohitajika cha 2-6 mg/l) na kushauri kuongeza matumzi ya mbolea zenye Naitrojeni ili kurutubisha udongo na kuongeza tija.

#### **4.2.9 Kuimarisha Masuala Mtambuka katika Kilimo**

##### **Ushiriki wa Vijana katika kilimo**

161. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kushirikisha Vijana katika Kilimo (*National Strategy for Youth Involvement in Agriculture* –NSYIA 20162021) ambapo Halmashauri 48 zimetenga hekta 217,882.36 kwa ajili ya kuwezesha vijana kushiriki katika shughuli za kilimo. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na SUGECO imetoa mafunzo kuhusu mpango wa biashara, uzalishaji mazao ya bustani kibiashara na uongezaji thamani, uchakataji wa mazao na mbinu bora za Kilimo kwa vijana 350 katika Kambi ya Mkongo. Vilevile, vijana 188 wamewezeshwa kupata mafunzo ya kilimo katika nchi za Israel (36) na Marekani (152).

162. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na SAT kupitia miradi yake imetoa mafunzo ya uongezaji thamani wa mazao ya kilimo, uanzishaji wa Vyama vya Ushirika, kuanzisha mashamba darasa na matumizi ya TEHAMA kwa vijana 3,153 (Me-753 na Ke 2,400) katika Wilaya za Mpwapwa, Chamwino, Mvomero, Kilosa, Ifakara, Mlimba, Ulanga na Morogoro Vijijini.





*Kikundi cha wasichana “Malkia wa Nguvu” Mang’ula – Morogoro wanaojishughulisha na kilimo cha mpunga*

**163. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la *Heifer* imetoa mafunzo kuhusu kilimo biashara cha mbogamboga na matunda, minyororo ya thamani ya mazao ya kilimo, akiba na mikopo, uongozi kwa viongozi wa Vyama vya Ushirika vya vijana; matumizi ya teknolojia za kielektroniki kwenye kupata taarifa za masoko, na programu ya uanagenzi (*Apprenticeship*) kwa vijana 3,807 (Me 1,905 na Ke 1,902) katika Mikoa ya Mbeya, Songwe, Njombe na Iringa. Aidha, vituo atamizi (*incubation centers*) vinne (4) vimeanzishwa katika mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe na Songwe kwa lengo la kuwajengea vijana ujuzi wa kilimo cha mazao ya bustani ambapo kituo kimoja cha Mbeya kimeanza kufanya kazi.

**164. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na *Heifer* imewajengea uwezo vijana 448 (Me 244 na Ke 204) kuhusu taratibu za kunufaika na mfuko wa maendeleo ya vijana. Aidha, mikopo yenye masharti nafuu ya Shilingi

136,406,100 kwa vijana 117 (Me 64 na Ke 53) imetolewa kupitia mfuko maalum wa mikopo unaosimamiwa kwa ushirikiano wa *Heifer International*, Benki ya FINCA na MUCOBA.

**165.** Vilevile, vikundi 21 vya vijana vimepata mikopo yenye thamani ya Shilingi 89,500,000 kutoka katika Mfuko wa Maendeleo ya Vijana uliopo chini ya Halmashauri za Mbeya, Songwe, Busokelo, Mbozi, Njombe, Njombe Mji, Wanging'ombe, Kilolo, Mufindi, Mafinga na Iringa. Kutokana na mafunzo na mikopo iliyotolewa, vijana 7,012 (Me 3,605 na Ke 3,407) wameweza kujajiri kwenye minyororo ya thamani ya mazao ya kilimo.

## Lishe

**166.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango Jumuishi wa Kitaifa wa Lishe (*National Multisectoral Nutrition Action Plan – NMNAP*) ambapo katika mwaka 2020/2021 kwa kushirikiana na wadau imeandaa Mpango wa kutekeleza masuala ya lishe katika kilimo (*Nutrition Sensitive Agriculture Action Plan – NSAAP*). Mpango huo unaelekeza kuhusu afua mbalimbali za lishe zitakazotekelezwa katika sekta ya kilimo ambazo utekelezaji wake utachangia kupunguza matatizo ya lishe nchini hususan watoto chini ya miaka 5, kina mama wajawazito na wanao nyonyesha.

**167.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara pia, imeendelea kusambaza Mwongozo wa Uongezaji Virutubishi Kibaolojia Katika Mazao ya Chakula na kuhakikisha mazao hayo yanazalishwa na kutumika nchini. Katika mwaka 2020/2021 Wizara kwa kushirikiana na Shirika la GAIN na *Nutrition International* - NI imetoa mafunzo kuhusu mwongozo huo kwa wadau 185 wa kilimo na lishe katika Mikoa ya Singida, Shinyanga na Manyara. Aidha, nakala 450 zimesambazwa kwa wadau hao na mwongozo huo umewekwa kwenye tovuti ya Wizara ([www.kilimo.go.tz](http://www.kilimo.go.tz)) kwa rejea.

**168.** Vilevile, Wizara imetoa mafunzo kuhusu uzalishaji, uhifadhi na matumizi ya mazao yaliyoongezewa virutubishi kibaiolojia katika Halmashauri za Ludewa, Wanging'ombe, Njombe na Makete kwa wakulima viongozi 200 na Maafisa 32 ngazi ya kata wakiwemo Maafisa Ugani, Maafisa maendeleo ya jamii, Watendaji wa Kata na Madiwani. Aidha, mashamba darasa 16 yameanzishwa katika kata 8 za Halmashauri hizo kwa lengo la kutoa mafunzo kwa vitendo kuhusu uzalishaji wa mazao hayo.

**169. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea kuratibu maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani ambayo katika mwaka 2020/2021 yalifanyika kitaifa Mkoani Njombe. Katika maadhimisho hayo, vyakula vya asili vinavyopatikana katika mkoa huo viliandaliwa ikiwemo chakula cha wanafamilia wote, chakula maalumu kwa mama anayenyonyesha (*mfyele*), chakula cha mtoto mwenye umri wa miezi sita (6) hadi 12 na chakula cha mtoto mwenye miezi 12 na kuendelea. Lengo la maonesho ya vyakula ni kuelimisha jamii umuhimu wa kutumia vyakula vinavyopatikana katika mazingira yetu na pia umuhimu wa mlo kamili katika kuimarisha afya ya mwili.

**170.** Aidha, kupitia bustani za mfano, wakulima walihamasishwa kuanzisha bustani za mboga na matunda katika kaya na kuhifadhi vyakula kwa kufuata kanuni na taratibu zinazotakiwa katika uhifadhi wa chakula.

**171. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara kwa kushirikiana na FAO na Ofisi ya Mkoa wa Kagera inatekeleza Mradi wa Kuboresha lishe- Kagera (*Strengthening Nutrition Sensitive Value Chain in Kagera Region*). Lengo la Mradi ni kupunguza utapiamlo hususan kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano na kina mama wenye umri wa kuzaa katika Mkoa wa Kagera kupitia uzalishaji na ulaji wa vyakula mchanganyiko vyenye virutubishi kwa wingi. Vilevile, TARI Maruku imesambaza vipando 140,000 vya muhogo, 175,000 vya viazi lishe na kilo 1,700 za maharage kwa vikundi 81 vya wakulima.

## Jinsia

172. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuzingatia masuala ya jinsia katika utekelezaji wa majukumu yake. Katika mwaka 2020/2021, Wizara imeratibu utekelezaji wa miradi na programu zinazotekelezwa na UN-Women, SAT, SUGECO na Rikolto ili kuhakikisha masuala ya jinsia yanazingatiwa katika mipango, bajeti, mikakati na miradi yao.

## Mazingira

173. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira inatekeleza Mradi wa Kutunza Mazingira ya Bonde la Ziwa Nyasa unaolenga kupunguza shughuli za kibinadamu zinazoathiri mazingira. Kupitia mradi huo, Wizara imeibua shughuli mbadala zikiwemo ufugaji wa nyuki, ujenzi wa kitalu nyumba kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya mboga, uvuvi wa kisasa, kuhamasisha uzalishaji wa kakao na michikichi kwa kutoa miche ya kisasa na uzalishaji wa zao la korosho kwenye vijiji 15 vya Wilaya za Makete, Kyela, Nyasa, Mbinga na Ludewa.

174. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI imesambaza nakala 145 za Mwongozo wa Kilimo Kinachokabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi. Aidha, mafunzo kuhusu kilimo kinachokabiliana na mabadiliko ya Tabianchi yametolewa kwa Maafisa Kilimo, Mazingira, Mipango, Ugani, na Wahandisi wa umwagiliaji 130 kutoka katika Halmashauri za Wilaya za Kwimba, Magu, Ukerewe, Mlele, Tanganyika, Nsimbo, Mpimbwe, Bukoba Mji, Ngara, Geita Mji, Mbogwe, Kyela na Busekelo.

175. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa, imeandaa Mwongozo kwa Maafisa Ugani na Wakufunzi Kuhusu Tafsiri na Matumizi ya Huduma na Taarifa za Hali ya Hewa kwa lengo la kuelimisha wakulima namna ya kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Chakula Duniani imetoa mafunzo kuhusu Kilimo Hifadhi kwa Mhandisi wa

kilimo mmoja (1), Maafisa Ugani wanne (4) na wakulima 150 kutoka Wilaya za Dodoma, Chamwino na Kondoa.

## VVU na Ukimwi

176. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu VVU na UKIMWI pamoja na magonjwa sugu yasiyoambukiza ili kupunguza na kuzuia maambukizi mapya kwa watumishi 1,009 wa Wizara. Pia, imeendelea kuwahudumia watumishi saba (7) wanaoishi na VVU kwa kuwapatia dawa pamoja na chakula lishe kila mwezi. Vilevile, Wizara imeendelea kutoa vifaa kinga ambapo hadi Aprili 2021, kondomu 6,000 zimesambazwa kwenye ofisi za Wizara.

## 5. MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2021/2022

### Masuala Muhimu Yaliyozingatia

177. **Mheshimiwa Spika**, Mpango na Bajeti ya mwaka 2021/2022 ya Wizara imezingatia; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu (2021/2022 – 2025/2026); Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2020-2025; na Program ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II). Aidha, mpango umezingatia masuala mtambuka ya jinsia, mazingira, lishe, vijana, kutokomeza ajira kwa watoto katika sekta ya kilimo, VVU na UKIMWI.

178. **Mheshimiwa Spika**, Miongozo yote iliyoainishwa imesisitizwa katika Hotuba ya Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, alipolihutubia Bunge lako Tukufu tarehe 22 Aprili, 2021. Hotuba hiyo imeweka dira kwa kuanisha vipaumbele vikubwa na vya kimkakati. Katika kupanga mipango ya mwaka 2021/2022 tumezingatia vipaumbele hivyo kama vilivyosisitizwa kwenye maelekezo ya Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Daniel Chongolo, tarehe 20 Mei, 2021.

179. **Mheshimiwa Spika**, katika hotuba yake, Rais alianisha tija ndogo kama tatizo kubwa linaloikabili sekta

ya kilimo. Hilo linaonekana wazi kwenye takwimu zinazohusu mchango wa Sekta ya Kilimo katika Pato la Taifa ambao umefikia asilimia 26.9 kwa mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 58.1 ya ajira. Hii ina maana kwamba takriban theluthi mbili ya nguvukazi hapa nchini inachangia takriban theluthi moja ya Pato la Taifa, hiki ni kielelezo tosha kwamba tija ni ndogo.

### **VIPAUMBELE VYA KIMKAKATI KWA MWAKA 2021/2022**

**180. Mheshimiwa Spika**, mpango mkubwa wa kimkakati ni kuongeza tija katika uzalishaji. Hivyo, **kipaumbele cha kwanza** kikubwa cha kimkakati katika kuongeza tija ni kuweka mkazo katika utafiti utakaozingatia ugunduzi wa aina za mbegu bora na mbinu bora za kilimo. Ili kufikia malengo hayo tutafanya yafuatayo:-

i. Kufanya utafiti wa mbegu bora zenye tija kubwa kwa mfano tafiti zinaonesha kuwa TARI wamefanikiwa kugundua aina za mbegu za muhogo zinayozalisha wastani wa tani 22-50 kwa hekta ikilinganishwa na wastani wa tani 8 kwa hekta zinazozalishwa sasa na wakulima wengi. Kwa upande wa pamba tija ya sasa ni kilo 250300 kwa ekari ikilinganishwa na uwezo wa kufikia wastani wa kilo 1000-2000 kwa ekari,

ii. kuongeza bajeti ya TARI kutoka Shilingi bilioni 7.35 mwaka 2020/2021 hadi Shilingi bilioni 11.63 mwaka 2021/2022, na

iii. kuimarisha upatikanaji wa fedha za maendeleo ya utafiti wa kilimo kwa kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Utafiti kwa mujibu wa Kifungu 26(1) cha Sheria Na. 10 ya mwaka 2016 iliyoanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI Act No. 10, 2016).

**181. Mheshimiwa Spika**, **kipaumbele cha pili** cha kimkakati cha kuongeza tija ni kuongeza uzalishaji wa mbegu bora. Sote tunafahamu nchi yetu bado hatujajitosheleza kwa mahitaji ya mbegu, hivyo kulazimika kuagiza kutoka nje ya nchi.

**182. Mheshimiwa Spika**, ili kuongeza uzalishaji wa mbegu bora nchi, Wizara imepanga kuendeleza mashamba 13 ya mbegu ya ASA kwa kuweka miundombinu ya umwagiliaji kwa kutumia fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji; kuongeza bajeti ya uzalishaji wa mbegu bora kutoka Shilingi bilioni 5.42 mwaka 2020/2021 hadi Shilingi bilioni 10.58 mwaka 2021/2022; na kuendelea kushirikiana na Sekta Binafsi katika kuzalisha mbegu bora nchini.

**183. Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha tatu** cha kimkakati ni kuimarisha huduma za ugani. Idadi ya Maafisa Ugani wanaotoa huduma za ugani nchini katika ngazi ya Kata na Vijiji ni 6,704. Idadi hiyo, ni ndogo ikilinganishwa na mahitaji ya 20,538. Pamoja na idadi hiyo kuwa ndogo, Maafisa ugani hao wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ukosefu wa vitendea kazi pamoja na mafunzo rejea.

**184. Mheshimiwa Spika**, upungufu huo wa maafisa ugani pamoja na changamoto wanazokabiliana nazo huchangia wakulima wengi kukosa huduma za ugani ikiwemo matumizi ya mbegu bora, matumizi sahihi ya viuatilifu, zana bora, mbinu bora za kilimo na taarifa za masoko.

**185. Mheshimiwa Spika**, ili kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imeongeza bajeti ya eneo hilo kutoka Shilingi milioni 603 mwaka 2020/2021 hadi Shilingi bilioni 11.5 mwaka 2021/2022. Fedha hizo zitatumika katika kuimarisha huduma za ugani nchini ikiwa ni pamoja na kununua pikipiki 1,500, vifaa vya kupima afya ya udongo, visanduku vya ufundi (*Extension Kit*), simu janja, kuwezesha uanzishwaji wa mashamba ya mfano kwa kila Afisa Ugani na kutoa mafunzo rejea. Vilevile, maafisa ugani watasimamiwa katika kuanzisha mashamba darasa kulingana na mahitaji ya wakulima kwa ajili ya kuendeleza kilimo katika eneo husika.

**186. Mheshimiwa Spika**, tutaianza safari yetu ya kuboresha huduma za ugani katika mikoa mitatu ya kielelezo

ambayo ni Dodoma, Singida na Simiyu. Mikoa hiyo ina fursa kubwa ya kuzalisha mazao ya mafuta hususan alizeti na pamba. Katika Mikoa hiyo maafisa ugani wote watapewa pikipiki, vifaa vya kupima afya ya udongo, visanduku vya ufundi (*Extension Kits*), simu janja, kuwezesha uanzishwaji wa mashamba ya mfano kwa kila Afisa Ugani na kutoa mafunzo rejea yatakayozingatia mazao yote yanayolimwa katika maeneo hayo. Pia maafisa ugani hao, watawezesha kuanzisha mashamba darasa.

**187. *Mheshimiwa Spika***, kwa kuwawezesha maafisa ugani hao, tunatarajia utoaji wa huduma za ugani utaimarika, wakulima wengi watafikiwa kwa wakati na tija itaongezeka. Kwa mfano, matumizi ya simu janja yatawezesha wakulima kupata utatuzi wa changamoto wanazokabiliana nazo ikiwemo taarifa za masoko ya mazao ya kilimo wanayozalisha. Mafanikio yatakayopatikana katika mikoa hiyo ya kielelezo, yataenezwa katika mikoa mingine nchini.

**188. *Mheshimiwa Spika***, Wizara pia itaendelea kushirikiana na Sekta Binafsi katika kuimarisha huduma za ugani kwa kutumia mbinu zilizoonesha mafanikio katika kuongeza tija. Kwa mfano, TAHA inatoa mafunzo ya kilimo bora cha mazao ya bustani na kuwaunganisha wakulima na watoa huduma za pembejeo na masoko. Vilevile, Kampuni ya kutoa huduma kwa wakulima wadogo wa chai Njombe (*Njombe Outgrowers Services Company*) imeajiri maafisa ugani, na inatoa huduma za uvunaji na uuzaji wa majani mabichi ya chai kwenye kiwanda cha Uniliver. Pia, Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU) kimeajiri maafisa ugani kwa ajili ya kutoa huduma kwenye mazao ya tumbaku na pamba.

**189. *Mheshimiwa Spika***, kwa kutambua mtawanyiko wa mazao ya kilimo yanayozalishwa nchini na mahitaji ya soko, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI na wadau wengine wa kilimo itasimamia utoaji wa huduma za ugani katika mikoa yote ili kuongeza tija katika mazao kulingana na viwango vya uzalishaji vinavyohitajika.



**190. Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha nne** cha kimkakati ni kuimarisha kilimo cha umwagiliaji. Kama tunavyofahamu, kilimo chetu nchini kinategemea mvua kwa asilimia kubwa ambazo hazitabiriki kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, kilimo cha umwagiliaji kinakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo ubovu wa miundombinu, kutokamilika kwa baadhi ya miradi ya umwagiliaji, kukosekana kwa miundombinu ya umwagiliaji kwenye maeneo yenye fursa za umwagiliaji, mitaji ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na elimu ndogo ya matumizi ya teknolojia za umwagiliaji.

**191. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha kilimo cha umwagiliaji nchini, Wizara imepanga kuongeza eneo la umwagiliaji kwa kuhamasisha wadau kuwekeza katika ujenzi miundombinu, uvunaji wa maji na uchimbaji wa visima kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Aidha, Wizara kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji (IDF) ulioanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 52 cha Sheria ya Umwagiliaji Na. 4 ya mwaka 2013 itakamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ikiwemo mashamba 13 ya mbegu ya ASA, kukarabati miundombinu ya umwagiliaji, kukamilisha miradi ya umwagiliaji, kujenga mabwawa na kufanya upembuzi yakinifu kwenye miradi mipya.

**192. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeanza kufanya tathmini ya skimu zote za umwagiliaji na maeneo yanayofaa kwa umwagiliaji. Lengo ni kuhakiki eneo linalomwagiliwa, kubaini mahitaji halisi ya rasilimali za kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kwa ajili ya kuboresha Mpango Kamambe wa Uendelezaji wa Kilimo cha Umwagiliaji Nchini.

**193. Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha tano** cha kimkakati ni kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo. Changamoto ya masoko nchini ina sura kuu mbili; kwanza ni uzalishaji mdogo usiokidhi mahitaji ya soko na pili ni kuwepo kwa uzalishaji mkubwa ikilinganishwa na upatikanaji wa masoko. Kwa mfano, viwanda vya kukamua mafuta ya alizeti vinafanya kazi takribani miezi minne kwa mwaka kutokana na ukosefu wa malighafi. Kwa upande wa

mazao ya nafaka ikiwemo mahindi na mpunga, uzalishaji wake ni mkubwa na ziada inakosa soko.

**194. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha upatikanaji wa masoko ndani na nje ya nchi, Wizara itaimarisha utekelezaji wa kilimo cha mkataba katika mazao ya shayiri, ngano, alizeti, zabibu, maharage ya soya na mazao mengine kwa kutoa mwongozo wa mikataba baina ya wakulima na wenye viwanda vya kusindika mazao.

**195.** Aidha, Wizara itaratibu ubia wa kibiashara baina ya wafanyabiashara wa mazao hapa nchini na nchi za nje zenye fursa kubwa ya masoko ikiwemo Sudani Kusini, DRC, Saudi Arabia, Falme za Kiarabu, Msumbiji, Kenya, Vietnam na China. Uratibu huo, utahusisha safari za wafanyabiashara kwenda katika nchi hizo na kuanzisha vituo vya kuonesha bidhaa za mazao ya kilimo kutoka Tanzania.

**196. Mheshimiwa Spika,** Wizara itawezesha upatikanaji wa masoko ya uhakika wa zao la shayiri na hivyo kuongeza uzalishaji wa ndani; inaendelea kuratibu uwekezaji wa kampuni za bia ili kuwekeza Dola za Marekani milioni 42 katika kiwanda cha kutengeneza kimea kitakachojengwa Jijini Dodoma chenye uwezo wa kusindika shayiri tani 35,000 kwa mwaka kutoka kwa wakulima. Wizara kupitia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko imeingia mkataba na wakulima kwa lengo la kununua tani 21,600 za ngano.

**197. Mheshimiwa Spika,** Wizara pia, itaendelea kuratibu makubaliano kati ya wasindikaji na wakulima ambapo wasindikaji watanunua kwanza ngano inayozalishwa ndani kabla ya kuagiza kutoka nje. Aidha, katika kuimarisha kilimo cha mkataba cha zao la alizeti, Wizara itaendelea kuwaunganisha wakulima na wasindikaji na kuandaa mazingira bora ya uwekezaji katika viwanda vya kusindika alizeti.

**198. Mheshimiwa Spika,** Wizara itaendelea kufungua mipaka ya kuuza mazao nje ya nchi na kutoa elimu ya utumiaji wa mfumo wa utoaji vibali kwa njia ya

kielektroniki (ATIMS) kwa ajili ya kusafirisha mazao nje ya nchi. Ninapenda kutoa wito kwa wafanyabiashara wa mazao kutumia mfumo huo. Aidha, ninaviomba vyombo vya usalama wa raia tushirikiane kuwezesha biashara ya mazao ya kilimo.

**199. Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha sita** cha kimkakati ni kuimarisha KILIMO ANGA kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya milipuko na vihamavyo kama vile nzige, kwelea kwelea na viwavijeshi vamizi. Kutokana na mabadiliko ya tabianchi, kumekuwa na ongezeko la visumbufu vigeni vinavyoathiri uzalishaji wa mazao na kusababisha upotevu wa mazao hadi asilimia mia moja endapo havitadhibitiwa kikamilifu na kwa wakati. Aidha, baadhi ya visumbufu kama vile nzige na kwelea kwelea udhibiti wake unahitaji vifaa maalum kama vile ndege kwa ajili ya savei na unyunyuziaji wa viuatilifu.

**200. Mheshimiwa Spika,** ili kutekeleza kipaumbele hicho, Wizara imeongeza bajeti ya KILIMO ANGA kutoka Shilingi milioni 150 mwaka 2020/2021 hadi bilioni tatu (3) mwaka 2021/2022. Fedha hizo, zitatumika kununua ndege moja mpya kwa ajili ya udhibiti wa visumbufu hivyo.

**201. Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha saba** cha kimkakati ni kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa mitaji. Upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya shughuli za kilimo umekuwa na changamoto kutokana na riba kubwa zinazotozwa, masharti ya kupata mikopo kutoka taasisi za fedha na vihatarishi katika sekta ya kilimo. Taarifa zilizopo zinaonesha kuwa ni asilimia 30 tu ya wakulima wanaofikiwa na huduma za mikopo. Aidha, ni asilimia kati ya 7 na 9 ya mikopo iliyotolewa na mabenki ya biashara katika kipindi cha miaka mitano iliyopita imeelekezwa kwenye sekta ya kilimo.

**202. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022, Wizara itafanya tathmini ya mifumo ya upatikanaji wa mitaji kwa wakulima wadogo na wawekezaji wengine kwenye sekta ya kilimo ili kuibua vizuizi na kuvitafutia majawabu kwa ajili ya kuimarisha ugharamiaji wa mazao katika mnyororo

wa thamani. Aidha, Wizara imeunda jopo maalum linalohusisha watendaji wakuu wa taasisi za fedha, ambalo litaongozwa na Naibu Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Bashe (Mb), kwa ajili ya kupitia minyororo ya thamani ya mazao na kushauri namna bora ya upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya uendelezaji wa kilimo nchini.

**203. Mheshimiwa Spika**, vilevile Wizara imeunda Timu ya Wataalam inayopitia na kuchambua mifumo ya kikodi katika sekta ya kilimo kwa lengo la kuvutia uwekezaji katika mnyororo wa thamani ya mazao ya kilimo. Katika hatua za awali, timu imeanza kazi hiyo katika tasnia za mazao ya alizeti, shayiri na dhamana za mikopo.

**204. Mheshimiwa Spika**, maelezo ya kina ya mpango wa vipaumbele hivyo vikubwa vya kimkakati kwa mwaka 2021/2022 vimefafanuliwa zaidi katika maeneo makuu manne ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II). Maeneo hayo ni Usimamizi na Matumizi Endelevu ya Maji na Ardhi; Kuongeza Tija na Faida katika Uzalishaji; Biashara na Kuongeza Thamani ya Mazao; na Kuiwezesha Wizara Katika Uratibu, Kufuatilia na Kutathmini.

## **5.1 Usimamizi na Matumizi Endelevu ya Maji na Ardhi**

### **5.1.1 Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Umwagiliaji**

**205. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imelenga kuongeza eneo la umwagiliaji kwa kuhamasisha wadau kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji. Aidha, Wizara kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji (IDF) ulioanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 52 cha Sheria ya Umwagiliaji Na. 4 ya mwaka 2013 itakamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu nne (4) ambazo ni Mgambalenga (Kilolo), Mbaka (Busekelo), Idudumo (Nzega), Muhukuru (Songea) na kufanya upembuzi yakinifu na kujenga mabwawa na skimu za umwagiliaji katika mashamba ASA ili kuhakikisha uzalishaji endelevu wa mbegu bora.

**206. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hicho, Tume itajenga skimu mpya ya Luiche yenye ukubwa wa hekta 3,000 iliyopo mkoa wa Kigoma; itajenga na kukarabati skimu nane (8) za umwagiliaji zenye ukubwa wa hekta 5,356; itakamilisha ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu za Kirya (hekta 800) Mwanga na Endagaw (hekta 276) Hanang'; itafanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina kwa mabwawa ya Nyisanzi (Chato), Ilemba (Sumbawanga), Makwale (Kyela), Ibanda (Geita), Mkombozi (Iringa), Ngomai (Kongwa) na Idudumo (Nzega). Aidha, Tume, itahakiki eneo linalomwagiliwa kwa kutumia miundombinu ili kuboresha mpango mkakati wa uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji nchini.

**207. Mheshimiwa Spika**, kazi nyingine zitakazotekelezwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wakulima na viongozi 50,000 kuhusu usimamizi na uendeshaji wa skimu 1,000; kutoa mafunzo kwa Vyama vya Umwagiliaji 1,300 kuhusu uandaaji wa kanuni ndogo kulingana na Sheria Na. 4 ya Umwagiliaji ya mwaka 2013 na Kanuni za Umwagiliaji za mwaka 2015 na kutoa mafunzo na kusambaza miongozo ya ukusanyaji wa ada za huduma za umwagiliaji katika skimu 1,000.

### ***5.1.2 Kuimarisha Huduma za Upimaji wa Matabaka ya Udongo na Uhifadhi wa Rasilimali Ardhi na Maji***

**208. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/2022, Wizara itakamilisha upimaji wa sampuli za udongo na kutoa ramani zitakazoonesha rutuba/afya ya udongo kwa Mikoa 26 ya Tanzania Bara. Ramani hizo zitatumika kushauri matumizi sahihi ya mbolea na utunzaji wa ardhi kwa ajili ya kilimo chenye tija. Vilevile, uchunguzi wa afya ya udongo utafanyika katika Wilaya ya Nzega kwenye skimu 5 za Idudumo (1,000 ha), Lusu (1,200 ha), Budushi (250 ha), Kanolo (1,200 ha) na Kahamaharanga (1,200 ha) kwa kilimo cha mpunga chenye tija na endelevu. Matokeo ya utafiti yatachapishwa na kusambazwa kwa wadau.

**209.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara itatoa mafunzo ya teknolojia za kuhifadhi ardhi na maji kwa maafisa ugani 150 katika Mikoa ya Songwe, Mbeya, Iringa, Morogoro, Pwani na Ruvuma ili kuwezesha usimamizi endelevu wa ardhi ya kilimo. Aidha, itapima afya ya udongo na kuhamasisha matumizi ya chokaa kwenye mashamba 20 yaliyoathiriwa na tindikali katika Mikoa ya Songwe, Mbeya, Ruvuma, Iringa, Rukwa na Katavi.

### **5.1.3 Kuwezesha Uanzishwaji wa Mashamba ya Wakulima Wakubwa**

**210.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2021/2022 Wizara itafanya tathmini ya mashamba ya ngano ya West Kilimanjaro (Kanamodo, Harlington, Matadi, Journey's end na Fosters) na Hanang' (Setchet, Murjanda na Gidagamowd, Mulbadaw na Bassotu) ili kubaini changamoto na kuzitatua kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa zao la ngano. Aidha, Wizara itahamasisha kilimo cha pamoja (*block farming*) kwenye maeneo ya uzalishaji wa mazao ya ngano, alizeti, muhogo na parachichi; itahamasisha ufufuaji wa mashamba makubwa ya zao la chai yaliyopo Njombe, Lushoto, Bukoba, Muleba na Kilolo na kuandaa Mikakati ya Uendelezaji wa Mazao ya kakao, parachichi na mazao ya mafuta.

**211.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara pia, itafanya savei ili kubaini mashamba makubwa na kutoa mwongozo wa mazao yatakayofaa kwa ajili ya kuboresha uzalishaji wa mazao katika Mikoa ya Dodoma, Rukwa, Mbeya, Arusha na Mtwara. Vilevile itahakiki, itapima na kuchora ramani za mashamba yenye ukubwa wa zaidi ya hekta 20 ambayo hayajaendelezwa na yana hatimiliki katika Mikoa mitano (5) ya Pwani, Morogoro, Kilimanjaro, Arusha na Manyara.

**212.** Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na OR - TAMISEMI itawezesha upimaji wa mashamba ya wakulima wadogo 400 wanaozunguka mashamba matano (5) ya uwekezaji katika mikoa ya Pwani na Morogoro na pia mashamba ya vikundi 20 vya vijana ili waweze kuzalisha kibiashara na kuongeza kipato.

#### **5.1.4 Kuongeza Matumizi ya Teknolojia na Mbinu za Kilimo Kinachohimili Mabadiliko ya Tabianchi**

213. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/2022, Wizara itatoa mafunzo na kusambaza Mwongozo wa Kilimo Kinachohimili Mabadiliko ya Tabianchi na Kuhifadhi Mazingira kwa wakulima 1,000 kutoka vijiji 15 vya Halmashauri za Wilaya za Kyela, Ludewa, Makete, Mbinga na Nyasa pamoja na vijiji 15 vinavyozunguka ziwa Manyara.

214. **Mheshimiwa Spika**, Wizara pia, itafanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa mabwawa manne (4) ya Nyisanzi (Chato), Kisesa (Kondoa), Ngomai (Kongwa) na Idudumo (Nzega) ili kuhamasisha kilimo cha umwagiliaji kwa ajili ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

215. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Mradi wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mfumo wa Ikolojia Vijijini (*Ecosystem Based Adaptation for Rural Resilience* – EBARR) itaanzisha mashamba darasa 11 kwa ajili ya kutoa mafunzo ya kilimo kinachohimili athari za mabadiliko ya tabianchi; itajenga vitalu nyumba 13 na kuchimba visima virefu nane (8) kwa ajili ya umwagiliaji katika Halmashauri za Wilaya za Mvomero, Mpwapwa, Simanjiro pamoja na Kaskazini A - Zanzibar. Vilevile, Wizara kupitia mradi wa EBARR itajenga malambo mawili (2) katika Halmashauri za Wilaya ya Kishapu kwa ajili ya kuvuna maji ya mvua.

## **5.2 Kuongeza Tija na Faida katika Uzalishaji**

### **5.2.1 Matumizi ya Teknolojia Bora Katika Kilimo**

#### **5.2.1.1 Utafiti wa Mbegu Bora**

216. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha utafiti wa mbegu bora, Wizara imeongeza bajeti kutoka Shilingi bilioni 7.5 mwaka 2020/2021 hadi Shilingi bilioni 9.9 mwaka 2021/2022. Aidha, Wizara kupitia TARI itafanya utafiti wa mbegu bora 15 za mazao ya nafaka, jamii ya mikunde na mafuta zenye sifa ya kutoa mavuno mengi, zinazostahimili ukame, wadudu na magonjwa na zenye viinilishe vingi.

Vilevile, TARI itazalisha mbegu mama tani 200, mbegu za awali tani 1,500 na mbegu za msingi tani 1,000 za mazao ya nafaka, mikunde, mafuta na mboga. Taasisi hiyo pia itakusanya na kuhifadhi vinasaba 10,000 vya mbegu bora za asili katika vituo vyake vya utafiti ili kuzuia upotevu.

#### **5.2.1.2 Uzalishaji na Upatikanaji wa Mbegu na Miche bora**

**217. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi itaendelea kuongeza uzalishaji wa mbegu bora kwa kutumia mashamba ya mbegu ya ASA, TARI, Kampuni za mbegu na kupata maeneo mapya ya uzalishaji wa mbegu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, mikakati hiyo itaenda sambamba na kufanya stadi za kisera na kisheria katika sekta ya mbegu kwa kufanya ulinganifu na nchi nyingine ili kuwezesha kuwa na mpango wa kitaifa wa uwekezaji katika sekta hii.

**218. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/2022, upatikanaji wa mbegu bora nchini unatarajiwa kufikia tani 107,780 zikiwemo tani 35,000 za mbegu za pamba. Kati ya mbegu zinazotarajiwa kupatikana, tani 2,300 zitazalishwa na TARI, tani 5,480 ASA na tani 65,000 mchango wa sekta binafsi. Vilevile, upatikanaji wa vipando vikiwemo miche, pingili na vikonyo utafikia 59,550,000 ambapo TARI itazalisha vipando 25,000,000, ASA 10,800,000 na Sekta Binafsi 23,750,000.

#### ***Jedwali Na. 8: Upatikanaji wa Vipando***



**219. Mheshimiwa Spika**, katika kufikia malengo ya uzalishaji wa mbegu bora, Wizara imeongeza bajeti ya ASA kutoka Shilingi 5,425,202,000 mwaka 2020/2021 hadi Shilingi 10,583,474,000 mwaka 2021/2022. Fedha hizo zitatumika kuongeza eneo la uzalishaji wa mbegu za alizeti kwa kufungua hekta 2,980 za mashamba ya ASA ya Msimba - Kilosa (hekta 2000), Mwele - Mkinga (hekta 500), Bugaga – Kasulu (hekta 100), Kilimi - Nzega (200), Tanganyika - Tanganyika (hekta 100) na Msungura – Chalinze (hekta 80).

**220. Mheshimiwa Spika**, ASA pia itajenga miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba yake yenye ukubwa wa hekta 220 yaliyopo Msimba (hekta 100), Arusha (hekta 80) na Mwele (hekta 40); itajenga ofisi, nyumba za wafanyakazi na ghala tatu (3) katika mashamba ya Msungura-Chalinze (1), Kilimi-Nzega (1) na Tanganyika-Katavi (1). Aidha, ASA itaweka mtambo wenye uwezo wa kuchakata tani 1,000 za mbegu kwa msimu katika shamba la Msimba.

**221. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia TARI itaongeza mashamba ya uzalishaji wa mbegu kutoka hekta 500 hadi hekta 1,000 katika vituo 16 vya TARI; itajenga na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji katika vituo vya Ilonga, Selian na Ifakara, ghala mbili (2) katika vituo vya Ilonga na Tumbi, chumba cha ubaridi (*cold room unit*) cha kuhifadhi mbegu katika kituo cha Tumbi na vitalu nyumba kwa ajili ya kuzalisha mbegu katika vituo vya Mlingano na Uyole.

### 5.2.1.3 Udhibiti wa mbegu

**222. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/2022 Wizara kupitia TOSCI itaendelea kudhibiti ubora wa mbegu zinazozalishwa nchini na zinazoingizwa kutoka nje ya nchi. Aidha, TOSCI itakagua hekta 70,000 za mashamba ya mbegu; itachukua sampuli 3,000 za mbegu kwa ajili ya kupima kwenye maabara; na itakagua maduka 1,000 na ghala 100 za mbegu.

**223.** Vilevile, TOSCI itafanya majaribio 60 ya sampuli za viazi na muhogo ili kubaini uwepo wa magonjwa; itafanya majaribio ya utambuzi (DUS test) kwa aina mpya 100 za mbegu; itafanya majaribio ya umahiri (*National Performance Trial*– NPT) ya aina mpya 55 za mbegu; na itafanya majaribio ya uhakiki wa uhalisia wa mbegu zilizopo katika uzalishaji (*Control Plot Test*) kwa sampuli 220.

**224.** *Mheshimiwa Spika*, TOSCI itatoa mafunzo ya udhibiti na uthibiti wa ubora wa mbegu kwa wakaguzi 25 wa Kitengo cha Afya ya Mimea kutoka katika mipaka ya nchi, wakaguzi wa Wilaya 25, maafisa kilimo 15 na maafisa wa Polisi 15 kutoka Wilaya zinazopakana na nchi jirani. Aidha, TOSCI itatoa vibali 3,000 vya kuingiza mbegu tani 20,000 na 25 vya kuuza mbegu nje ya nchi; itaimarisha ushiriki wa Tanzania katika ithibati ya ISTA na skimu za mbegu za OECD kwa kuongeza mazao ya nyanya, vitunguu na alizeti. Vilevile, TOSCI itajenga maabara za kupima ubora wa mbegu katika ofisi za kanda ya Ziwa (Mwanza), Nyanda za Juu Kusini (Rukwa) na Magharibi (Kigoma).

#### 5.2.1.4 Upatikanaji na udhibiti wa Mbolea

**225.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia TFRA itaratibu uingizwaji wa tani 600,000 za mbolea na kusafirisha tani 150,000 nje ya nchi. Aidha, TFRA itasajili mbolea mpya na visaidizi vyake (*fertilizer and fertilizer suppliments*) 30 na kutoa leseni 2,000 za biashara ya mbolea. Vilevile, itakarabati jengo na kununua vifaa kwa ajili ya maabara ya uchunguzi wa ubora wa mbolea na kukagua makampuni 23 yanayozalisha mbolea na wafanyabiashara 2,918 wa mbolea.

**226.** Kadhalika, TFRA itatoa mafunzo ya ukaguzi wa mbolea kwa maafisa kilimo 20 ili wawe wakaguzi wa mbolea na kuwajengea uwezo wakaguzi wa mbolea 35 wa Halmashauri za Wilaya 35. Vilevile, Wizara itahamasisha matumizi ya mbolea katika Halmashauri 185 na chokaa (*lime*) katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ambayo imeathiriwa na tindikali.

### 5.2.1.5 Upatikanaji wa Viuatilifu na Udhhibiti wa Visumbufu vya mazao

227. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/2022, upatikanaji wa viuatilifu vya kudhibiti visumbufu vya mazao na mimea utafikia lita 1,419,000 na kilo 26,000. Ili kudhibiti visumbufu hivyo, Wizara kupitia TPRI itasambaza mitego 300 ya kudhibiti viwavijeshi vamizi katika Halmashauri zote nchini; itatoa mafunzo ya matumizi bora ya viuatilifu na utambuzi wa visumbufu kwa maafisa ugani 2,000; na itachambua mabaki ya viuatilifu kwenye mazao ya chakula katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, Dar es Salaam, Iringa, Arusha, Mbeya, Lindi na Mtwara. Hatua hiyo itawezesha kulinda afya ya mlaji na kukuza biashara ya mazao nje ya nchi.

228. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia nchi yetu kuvamiwa na visumbufu vya mimea na mazao mara kwa mara wakiwemo nziye na kwelea kwelea, Wizara imeongeza bajeti ya kuimarisha udhibiti wa visumbufu kutoka Shilingi milioni 150 mwaka 2020/2021 hadi bilioni tatu (3) mwaka 2021/2022. Fedha hizo, zitatumika kuimarisha kituo cha KILIMO ANGA kwa kununua ndege moja mpya kwa ajili ya udhibiti wa kwelea kwelea na nziye ikiwa ni pamoja na kuwezesha mafunzo kwa marubani wawili (2). Hatua hii inalenga kuwezesha nchi kuwa tayari muda wote kupambana na visumbufu hivyo mara vinapojitokeza kuliko kusubiria ndege za mashirika ya kimataifa. 229. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na uhamasishaji wa Sekta Binafsi kuwekeza katika viwanda vya kuzalisha viuatilifu nchini ili kumpunguzia mkulima gharama za viuatilifu kutokana na uagizaji wake nje ya nchi, mwekezaji (*BAJUTA International*) atafungua kiwanda kwa ajili ya uzalishaji wa viuatilifu mkoani Arusha. Kiwanda hicho chenye uwezo kuzalisha lita milioni 26 kwa mwaka kipo kwenye hatua za mwisho za kufunga mitambo na mashine na kinatarajiwa kuanza uzalishaji mwaka 2021/2022.

### 5.2.2 Uzalishaji wa Mazao

a) Mazao ya Kimkakati yenye Mahitaji Makubwa ya Ndani

**229. Mheshimiwa Spika**, Wizara itaendelea kuhamasisha uzalishaji wa mazao yenye mahitaji makubwa nchini yakiwemo ngano, mazao ya mafuta na miwa ili kupunguza uingizaji wa bidhaa zitokanazo na mazao hayo kutoka nje ya nchi hivyo kuokoa fedha za kigeni.

### 5.2.2.1 Zao la Ngano

**231. Mheshimiwa Spika**, Wizara itaendelea kutekeleza mkakati wa kuendeleza zao la ngano kwa kipindi cha miaka mitano 2020/2021 – 2025/2026. Mkakati huo unalenga kuongeza uzalishaji wa ngano kutoka tani 77,000 hadi 1,000,000 ifikapo mwaka 2025/2026, kuimarisha vyama vya ushirika na masoko ya zao la ngano na kuweka mazingira wezeshi ya bishara ya ngano.

**232. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/2022 Wizara itahamasisha uzalishaji wa ngano kufikia tani 375,000. Ili kufikia lengo hilo, Wizara kupitia TARI, ASA kwa kushirikiana na Sekta Binafsi itazalisha na kusambaza kwa wakulima tani 18,000 za mbegu bora za ngano ambazo zitasheleza hekta 150,000.

**233.** Aidha, Wizara itasimamia ufufuaji wa mashamba ya Bassotu (hekta 5,437) na West Kilimanjaro (hekta 2,415) kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa ngano. Wizara pia, itawahamasisha wakulima kuongeza eneo la uzalishaji wa ngano katika mashamba yaliyokuwa ya NAFCO kutoka hekta 17,811 zinazolimwa sasa hadi kufikia hekta 43,538. Vilevile, Wizara itahamasisha uzalishaji wa ngano baada ya kuvuna mpunga katika skimu za umwagiliaji za Nguvumali, Ganila na Liodi - (Bahi) na Kapunga – (Mbarali) zenye zaidi ya hekta 280.

**234. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia TARI itakarabati maabara mbili (2) za TARI Selian (Arusha) na Uyole (Mbeya) kwa ajili ya kupima ubora wa ngano (*mill quality, gulten content and protein*) na kukarabati maabara mbili (2) za TOSCI zilizopo Njombe na Arusha kwa ajili ya kupima ubora wa mbegu za ngano.

### 5.2.2.2 Zao la Miwa na Uzalishaji wa Sukari

235. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/2022 Wizara kupitia Bodi ya Sukari itahamasisha uzalishaji wa sukari kufikia tani 450,000. Ili kufikia lengo hilo Bodi itafunga mitambo miwili (2) ya maji moto (*Hot Water Treatment Plants*) itakayotumika kuzalisha mbegu bora za miwa katika mashamba ya pamoja ya wakulima wadogo yenye ukubwa wa hekta 200 katika Wilaya ya Kilombero.

236. Vilevile, Bodi itahamasisha matumizi ya mbolea na kutoa mafunzo kuhusu Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja wa Mbolea (*Fertilizer Bulk Procurement System*) kwa Vyama 28 vya Ushirika vya wakulima wa miwa. Aidha, Bodi itajenga miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba mawili (2) ya pamoja yenye ukubwa wa hekta 100 yaliyopo Kilombero; itaanzisha mashamba matatu (3) ya mfano ya miwa katika maeneo yanayolimwa miwa ya Mtibwa, Kagera na Manyara.

### 5.2.2.3 Mazao ya Mafuta

237. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/2022 Wizara itahamasisha uzalishaji wa chikichi kufikia tani 50,000 na alizeti kufikia tani 1,000,000. Ili kufikia malengo hayo Wizara kupitia TARI na ASA itazalisha na kusambaza kwa wakulima tani 3,140 za mbegu bora za alizeti. Aidha, TARI itazalisha mbegu bora 5,000,000 za chikichi aina ya Tenara. Mbegu hizo zitatumiwa na TARI, ASA, Magereza ya Kwitanga na Ilagara, JKT – Bulombora, Mkoa wa Kigoma pamoja na kampuni binafsi kuzalisha miche 3,500,000 ya chikichi. Miche hiyo itasambazwa kwa wakulima na itatosha kupandwa katika eneo la hekta 28,000.

238. **Mheshimiwa Spika**, Wizara pia imepanga kuimarisha huduma za ugani katika mikoa ya Dodoma na Singida ili kuzalisha zao la alizeti kwa tija. Katika mikoa hiyo, maafisa ugani watawezesha kwa kupewa usafiri (pikipiki) kwa ajili kufuatilia na kutoa ushauri, pembejeo za kuanzisha

mashamba ya mfano na kuanzisha mashamba darasa. Pikipiki hizo ni sehemu ya pikipiki 1,500 ambazo Wizara imepanga kununua ikiwa ni mkakati wa kuimarisha huduma za ugani nchini. Aidha, watawezesha kuanzisha mashamba ya mfano 340 ambayo wakulima wengine wataweza kujifunza njia bora ya uzalishaji.

**239.** Vilevile, Wizara itatoa mafunzo ya kilimo bora cha zao la alizeti kwa maafisa ugani 340 katika mkoa hiyo kwa lengo la kuongeza ujuzi na maarifa ya kutoa elimu hiyo kwa wakulima. Aidha, TARI pia, itatoa mafunzo ya kilimo bora cha chikichi kwa wakulima 5,000, vijana 1,100 wa JKT Bulumbora na Maafisa Ugani 120 katika Halmashauri za Wilaya za Kigoma, Kilosa (Morogoro), Mbarali (Mbeya), Urambo na Uyui (Tabora) na Tanganyika (Katavi) ili kuongeza tija na uzalishaji katika zao hilo.

**240.** *Mheshimiwa Spika*, katika kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula, Wizara itaendelea kueneza mbinu ya kilimo cha mkataba iliyoanza kutumiwa na baadhi ya wenye viwanda kama vile Pyxus ili kuchochea uzalishaji na uhakika wa soko kwa mkulima.

#### ***b) Mazao mengine ya kimkakati***

##### **5.2.2.4 Zao la Mkonge**

**241.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Bodi ya Mkonge itahamasisha uzalishaji wa mkonge kufikia tani 120,000. Lengo hilo litafikiwa kwa kusambaza miche ya mkonge 48,000,000 kwa ajili ya kupanda katika mashamba yenye hekta 12,000 yaliyopo katika Wilaya 10 za Shinyanga, Kishapu, Bunda, Tarime, Bariadi, Meatu, Serengeti, Mkuranga, Kisarawe na Kongwa. Aidha, Bodi itawezesha uundwaji wa *prototype* ya korona na kuwapatia mitambo ya kuchakata mkonge vikundi 10 vya kilimo. Vilevile, itaendelea na ukarabati wa jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Bodi ya Mkonge – Tanga.

### 5.2.2.5 Zao la Tumbaku

242. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Bodi ya Tumbaku itahamasisha uzalishaji wa tumbaku kufikia tani 75,000 kwa kuhimiza matumizi sahihi ya mbolea na kuimarisha huduma za ugani. Aidha, Bodi itaunganisha vituo 1,500 vya kuchambua tumbaku na vituo 300 vya kuuzia tumbaku kwenye mfumo wa ATMS ili kudhibiti ubora wa tumbaku na kutathmini uzalishaji na ubora wa tumbaku.

### 5.2.2.6 Zao la Pareto

243. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Bodi ya Pareto itahamasisha uzalishaji wa pareto kufikia tani 2,600. Lengo hilo litafikiwa kwa kuanzisha mashamba darasa 16 ya kilimo cha pareto na kutoa mafunzo ya kanuni za kilimo bora cha pareto kinachohimili mabadiliko ya tabianchi katika Halmashauri za Wilaya 16 katika mikoa ya Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa, Arusha na Manyara.

244. Aidha, Bodi itahamasisha uzalishaji na usambazaji wa miche ya pareto kwa wakulima; itatoa mafunzo ya uzalishaji wa mbegu za pareto kwa vikundi vya wakulima; na itanunua na kusambaza vikaushio vya maua ya pareto katika Halmashauri 18 zinazolima pareto na kuhamasisha uanzishwaji wa mashamba ya pamoja (*block farming*) katika Halmashauri za Wilaya ya Mbulu, Mbeya na Mufindi.

### 5.2.2.7 Zao la Chai

245. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Bodi ya Chai itahamasisha uzalishaji wa chai kavu kufikia tani 40,000 na tija kutoka wastani wa kilo 1,000 hadi kilo 1,150 na kilo 2,000 hadi kilo 2,200 za chai kavu kwa hekta kwa wakulima wadogo na wakubwa mtawalia. Lengo hilo litafikiwa kwa kufufua mashamba yaliyotelekezwa katika Wilaya ya Lushoto (hekta 1,840) na Bukoba (hekta 400) ambapo kwa sasa eneo linalozalisha chai kwenye mashamba hayo ni asilimia 40.

**246.** Vilevile, Bodi kupitia Mradi wa NOSC itaongeza eneo la kilimo cha chai kwa hekta 230 katika Wilaya ya Njombe na hekta 100 katika ya Wilaya ya Mufindi kupitia Mradi wa MOG. Bodi pia itahamasisha ufunguaji wa kiwanda cha chai Mponde chenye uwezo wa kusindika kilo 70,000 za majani mabichi ya chai kwa siku. Aidha, itahamasisha matumizi ya pembejeo kwa wakulima wadogo wa chai.

**247. Mheshimiwa Spika,** Bodi pia, itaanzisha mashamba mama sita (6) ya aina mpya nne (4) za miche ya chai katika Wilaya za Rungwe (Mbeya), Mufindi (Iringa), Ludewa na Lupembe (Njombe), Lushoto (Tanga) na Tarime (Mara); na itazalisha miche bora 5,000,000 ya chai na kusambazwa kwa wakulima.

#### 5.2.2.8 Zao la Korosho

**248. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Bodi ya Korosho itahamasisha uzalishaji wa korosho kufikia tani 280,000 kwa kutoa mafunzo ya kilimo bora cha korosho na matumizi sahihi ya pembejeo kwa wakulima na wagani 1,500 na kusimamia uagizaji na usambazaji wa tani 21,000 za salfa ya unga na lita 1,298,000 za viuatilifu vya maji.

**249.** Aidha, Bodi itasambaza miche bora ya korosho 15,000,000 katika Halmashauri 91 nchini; itaratibu uanzishwaji wa mashamba makubwa ya pamoja (*cashew block farms*) mawili (2) katika maeneo mapya yanayolima korosho na itafanya ukarabati (*top working*) wa mikorosho 50,000 kwenye Wilaya tatu (3).

**250.** Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Mkoa wa Singida itaimarisha uendeshaji wa mashamba ya Korosho ya Manyoni kwa kuwaunganisha wakulima katika mashamba hayo na watoa huduma za pembejeo, huduma za ugani na masoko.



**251. Mheshimiwa Spika,** Bodi itatoa mafunzo kwa wataalamu, maafisa ugani na makarani wa AMCOS 2,700 kuhusu udhibiti wa ubora wa korosho. Aidha, itaweka vifaa vya kupima ubora kwenye kila AMCOS na kununua seti tatu (3) za vifaa vya kupima ubora wa korosho kwa ajili ya Matawi ya Bodi na kupanga madaraja ya korosho katika ngazi ya AMCOS. Vilevile, Bodi itaendeleza ujenzi wa ghala tatu (3) za kisasa za kuhifadhi korosho katika Wilaya za Tunduru, Mkuranga na Mkinga.

#### **5.2.2.9 Zao la Kahawa**

**252. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Bodi itahamasisha uzalishaji wa kahawa kufikia tani 70,000. Ili kufikia lengo hilo, Bodi itazalisha na kusambaza miche bora ya kahawa milioni 20 katika Halmashauri za Wilaya 30 zinazolima kahawa; itatoa mafunzo ya kanuni za kilimo bora cha kahawa na ukarabati wa mashamba kwa wakulima 50,000.

**253.** Aidha, Bodi itaanzisha mashamba darasa 40 katika Halmashauri za Wilaya 20 na kuratibu upatikanaji na uanzishwaji wa mashamba 10 makubwa ya pamoja katika Halmashauri za Wilaya 10. Bodi pia, itajenga miundombinu ya kuhifadhi kahawa katika eneo la EPZA- Kurasini Dar es Salaam kwa ajili ya soko la nje ya nchi na kujenga uwezo wa kufanya biashara kwa Vyama 250 vya Ushirika.

**254. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia TaCRI itakarabati miundombinu ya umwagiliaji Lyamungo; itajenga vituo vidogo viwili (2) vya utafiti wa kahawa katika mikoa ya Kigoma na Mara; itafanya tathmini ya aina 23 ya miche bora ya kahawa; itanunua vifaa vya maabara na vifaa vya nishati jua ya kuzalisha miche ya kahawa kwa njia ya chupa (*Tissue culture*); itafanya tafiti kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi, tabia za udongo na udhibiti husishi wa visumbufu vya kahawa; na kutoa mafunzo ya kanuni bora za kilimo cha kahawa, uhifadhi na utunzaji wa kahawa baada ya kuvuna kwa maafisa ugani 689, wakulima viungo 276 na wakulima 8,000 katika Halmashauri 69.

### 5.2.2.10 Zao la Pamba

255. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Bodi ya Pamba itahamasisha uzalishaji wa pamba kufikia tani 500,000 kwa kuimarisha mfumo wa uzalishaji, uchakataji na usambazaji wa mbegu bora tani 25,000. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na ASA itazalisha tani 10,000 za mbegu zilizoondolewa manyoya. Bodi pia, itaratibu ununuzi wa chupa 7,000,000 (*acrepacks*) za viudadudu na vinyunyizi 20,000 na kuvisambaza kwa wakulima.

256. Vilevile, Bodi itahamasisha matumizi ya mbolea ya samadi pamoja na kufanya majaribio ya matumizi ya mbolea za maji (*foliar fertilizers*). Bodi pia, itanunua mashine 200 za kupandia na 200 za kupalilia na kusambaza kwa wakulima na itanunua baiskeli 5,200 kwa ajili ya wakulima wawezeshaji pamoja na pikipiki 300 kwa maafisa kilimo ili kusaidia utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima.

257. **Mheshimiwa Spika**, Bodi pia itahamasisha uanzishwaji wa kiwanda cha kuchambua na kuchakata mbegu (*Ginning & Delinting Plant*) katika Wilaya ya Igunga-Tabora na kujenga bwawa moja (1) katika shamba la utafiti la Ukiriguru lililoko Nkanziga-Mwanza lenye ukubwa wa ekari 450.

258. **Mheshimiwa Spika**, Bodi itaratibu ukarabati na ujenzi wa ghala 400 katika wilaya 54 zinazolima pamba; itasimika viwanda vidogo vinne (4) vya kuchakata pamba katika ngazi ya AMCOS ili kuhamasisha uongezaji wa thamani wa zao la pamba kwa wakulima; itafunga mitambo kumi (10) ya kusokota nyuzi za pamba katika AMCOS kumi (10) za Mikoa ya Mwanza, Simiyu na Tabora kwa lengo la kuhamasisha uongezaji wa thamani wa zao la pamba; na kusimika mitambo miwili (2) ya kukamua mafuta ya kula yanayotokana na mbegu za pamba katika Mkoa wa Simiyu. Bodi pia, itasajili wakulima 600,000 wa pamba kwa mfumo wa baometriki ili kurahisisha utoaji wa huduma.

### 5.2.3 Kuimarisha Vituo vya Utafiti, Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo na Vituo vya Mafunzo kwa Wakulima

#### 5.2.3.1 Vituo vya Utafiti

259. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2021/2022 Wizara kupitia TARI itaimarisha miundombinu ya maabara ya TARI Mlingano ili kupata ithibati (*accreditation*) kwa ajili ya kupima afya ya udongo; itakarabati Maabara mbili (2) – TARI Mlingano kwa ajili ya kuzalisha miche ya mkonge na Mikocheni kwa ajili ya kupima mbegu za GMO.

260. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itaendelea kujenga kituo cha TARI Kihinga Kigoma kwa ajili ya utafiti na kuendeleza zao la michikichi kwa kujenga miundombinu ya utafiti na uzalishaji wa miche na vitendea kazi; kujenga Makao Makuu ya TARI Chamwino Dodoma; kuwajengea uwezo wataalamu 85 (Shahada 15, Shahada ya uzamili 10, Shahada ya uzamivu watano (5), Stashahada watano (5) na 50 mafunzo ya muda mfupi) kwa kupewa mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika vyuo vya ndani na nje ya nchi.

#### 5.2.3.2 Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo na Vituo vya Mafunzo kwa Wakulima

261. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2021/2022, Wizara itadahili Wanafunzi 2,450 katika vyuo 14 vya Mafunzo ya Kilimo ngazi ya Astashahada na Stashahada; itavipatia vifaa vya TEHAMA vyuo vya mafunzo ya kilimo vya Uyole, Ilonga, Tumbi na Ukiriguru; itawezesha ukarabati wa miundombinu ya vyuo vya kilimo vya Uyole, Maruku, KATC, KATRIN, Inyala, vituo vya mafunzo kwa wakulima vya Ichenga, Themi, Bihawana pamoja na kituo atamizi cha vijana Mkongo; itavipatia vifaa vya kufundishia, kujifunzia na uzalishaji vyuo vya kilimo Uyole, Mubondo, Tumbi, Maruku, Ukiriguru, Ilonga, Mlingano, KATC na Mtwara.

262. Vilevile, Wizara itawajengea uwezo watumishi 12 katika mafunzo ya Shahada ya Uzamili, tisa (9) Shahada, 30 mafunzo ya mbinu za kufundishia na wanne (4) mafunzo

ya muda mfupi. Aidha, Wizara itawezesha vituo vitano (5) vya wakulima vya Ichenga (Njombe), Bihawana (Dodoma), Mkindo (Morogoro), Themis (Arusha) na Nyakabindi (Simiyu) kutoa mafunzo kwa Wakulima 900 na Maafisa Ugani 100 na kuboresha kituo cha vijana cha Mkongo Rufiji.

**263. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na SAT kupitia mradi wa CISTI itaandaa Mwongozo wa Kuanzisha na Kuendesha Vyuo vya Kati vya Mafunzo ya Kilimo; itachapisha na kusambaza nakala 1,450 za vitini vitano (5) vya kufundishia; itaandaa kitini cha kufundishia moduli ya ujasiriamali na vitini vingine vya kufundishia moduli mpya za mitaala sita (6) iliyoishwa.

**264.** Aidha, Wizara itatoa mafunzo ya ujasiriamali, kilimo hai, jinsia katika kilimo, utunzaji wa mazingira, Ushirika, Stadi za mawasiliano na stadi za kuandaa mpango biashara (*Business plan writing skills*) na mpango mkakati (*Strategic Plan*) kwa wakufunzi 29. Vilevile, itatoa mafunzo kwa wasimamizi 70 wa bustani za kilimo hai zilizoanzishwa katika vyuo vya mafunzo ya kilimo, mafunzo ya stadi za uwezesaji (*Facilitation skills*) kwa wakufunzi 29 wa vyuo vya mafunzo ya kilimo na wataalamu wanne (4) wa makao makuu.

**265. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia mradi wa CIST itatoa mafunzo ya mbinu za kufundishia (*Competence Based Education and Training-CBET*) kwa wakufunzi 120 wa vyuo vya mafunzo ya kilimo na wataalamu wanne (4) wa Makao Makuu; itaboresha maktaba za vyuo vya mafunzo ya kilimo kwa kuanzisha mfumo wa maktaba mtandao (*e – Library*); itasambazwa vifaa vya kupima afya ya udongo (*Soil testing kit*) kwa ajili ya maabara za udongo za vyuo 29 vya mafunzo ya kilimo; itaandaa kanzidata ya vyuo vya mafunzo ya kilimo na kutoa mafunzo kwa wakufunzi 58 wa vyuo vya kilimo na wataalamu wanne (4) wa makao makuu kuhusu usimamizi na utumiaji wa kanzidata hiyo.

#### **5.2.4 Huduma za Ugani**

**266. Mheshimiwa Spika,** idadi ya maafisa ugani wanaotoa huduma za ugani nchini katika ngazi ya Kata na

Vijiji ni 6,704. Idadi hiyo, ni ndogo ikilinganishwa na mahitaji ya 20,538. Pamoja na idadi hiyo kuwa ndogo, maafisa ugani hao wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ukosefu wa vitendea kazi pamoja na mafunzo rejea.

**267. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/2022 Wizara imepanga kuimarisha huduma za ugani kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma kwa wakulima. Bajeti ya eneo hili imeongezwa kutoka Shilingi milioni 603 mwaka 2020/2021 hadi Shilingi bilioni 11.5 mwaka 2021/2022. Fedha hizo zitatumika katika kuimarisha huduma za ugani kwa kununua vifaa mbalimbali pamoja na pikipiki 1,500.

**268. Mheshimiwa Spika**, Wizara imepanga kuanza na mikoa ya Dodoma, Singida na Simiyu kama kielelezo ili kuimarisha mazao ya alizeti na pamba. Wizara itawapatia maafisa ugani wa mikoa hiyo pikipiki, vifaa vya kupima afya ya udongo na visanduku vya ufundi (*Extension Kit*), simu janja na mafunzo rejea. Wizara pia, itawawezesha maafisa ugani wa mikoa hiyo kuanzisha mashamba ya mfano na mashamba darasa kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wakulima na kukarabati Vituo vya Rasilimali za Kilimo vya Kata (*Ward Resource Centres-WARCs*) 34.

**269.** Aidha, TARI itatoa mafunzo kuhusu teknolojia mpya bora za mazao mbalimbali kwa wakulima 1,500,000.

### **5.2.5 Mifumo ya Upatikanaji wa Zana za Kilimo na Pembejeo**

**270. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa pembejeo na zana za kilimo kwa kuhamasisha Vyama vya Ushirika 29 kuingiza mbolea kwa mfumo wa BPS. Aidha, ASA itaimarisha usambazaji wa mbegu bora kupitia mawakala na *Tanzania Farmers Association* (TFA) ambao wana vituo 16 na kuongeza vituo vya kusambaza mbegu kwa Wilaya ya Nzega, Kilosa na Kiteto. ASA pia, itaingia makubaliano na Shirika la Reli Tanzania ili kupunguza gharama za usafirishaji wa mbegu bora katika Mikoa ya Kanda ya Kati na Kanda ya Ziwa ambayo itasaidia kupunguza bei ya mbegu bora.

271. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/2022, Wizara itaboresha upatikanaji wa zana za kilimo kwa kuviwezesha vituo viwili (2) vya zana za kilimo katika mikoa miwili inayozalisha mazao ya kimkakati ya ngano, alizeti na pamba. Vituo hivyo vitapatiwa matrekta mawili (2) na zana zake, mashine mbili (2) za kuvunia na mashine nne (4) za kunyunyizia dawa (*boom sprayers*) ambazo zitatumika kuhudumia maeneo yenye muunganiko wa mashamba makubwa (*block farms*) yanayozalisha mazao hayo.

272. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) itatoa mikopo 100 yenye thamani ya Shilingi 3,775,000,000 kwa ajili ya shughuli za kilimo (**Jedwali Na. 8**); itaanzisha utaratibu wa kuwakatia bima ya maisha kwa wakopaji wapya na ambao muda wao wa mikopo haujaisha; na itakusanya mikopo itakayokuwa imeiva.

**Jedwali Na. 9: Mikopo itakayotolewa mwaka 2021/2022**

S/N	Aina ya Mkopo	Idadi	Thamani
1.	Mitambo ya mashambani	21	1,050,000,000
2.	Ukarabati	7	70,000,000
3.	Fedha za kuendesha shughuli za shamba	21	630,000,000
4.	Pembejeo za kilimo	19	950,000,000
5.	Matrekta ya mikono	6	90,000,000
6.	Zana unganishi	6	180,000,000
7.	Zana za usindikaji na vifungashio vya mazao ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi	7	175,000,000
8.	Miundombinu ya kilimo, mifugo na uvuvi	9	450,000,000
9.	Kununua ardhi kwa ajili ya kilimo, mifugo na uvuvi	6	180,000,000
	<b>JUMLA</b>		<b>3,775,000,000</b>

Chanzo: Wizara ya Kilimo 2021

## 5.3 Biashara na Kuongeza Thamani ya Mazao

### 5.3.1 Kuimarisha Miundombinu ya Kuhifadhi Mazao ya Kilimo

273. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/2022, Wizara imelenga kujenga ghala mbili (2) za kimkakati katika mipaka ya Namanga na Mtukula kwa lengo la kuimarisha uhifadhi wa nafaka na kuboresha biashara ya mazao hayo nje ya nchi. Aidha, Wizara itakamilisha ujenzi na ukarabati wa ghala 15 katika Wilaya za Mlele na Songea ili kupunguza upotevu wa mazao.

274. Vilevile, Wizara itaendelea kufanya tathmini ya upotevu wa mazao ya chakula nchini kwa lengo la kupata takwimu sahihi zitakazowezesha kufanya maamuzi sahihi ya kisera na uwekezaji. Wizara pia, itaendelea kuimarisha akiba ya chakula katika Hifadhi ya Taifa kwa kununua na kuhifadhi tani 231,000.

275. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia CPB itajenga vihenge vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 85,000 katika mikoa ya Dodoma (tani 30,000) na Mwanza (tani 55,000) na ghala zenye uwezo wa kuhifadhi tani 40,000 katika mikoa ya Dodoma (tani 5,000), Katavi (tani 10,000), Mtwara (tani 20,000) na Kigoma (tani 5,000) kwa ajili ya kuhifadhi bidhaa na mazao ya mpunga, mahindi, alizeti na muhogo.

276. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia TANIPAC itajenga ghala 14 zenye uwezo wa kuhifadhi tani 34,000 za nafaka katika Wilaya za Chemba, Kiteto, Babati, Gairo, Namtumbo, Namyumbu, Itilima, Kasulu, Kibondo, Buchosa, Bukombe na Kilosa pamoja na Zanzibar. TANIPAC pia, itawapatia vifaa vijana 400 katika mikoa ya Dodoma, Mwanza, Manyara, Kigoma, Tabora, Ruvuma, Mtwara, Morogoro na Geita kwa ajili ya kutengeneza vihenge vya chuma visivyoruhusu hewa (*metal silo*) vya kuhifadhi nafaka katika ngazi ya kaya na hivyo kuongeza ajira kwa vijana na kuongeza kipato cha wakulima kwa kupunguza upotevu.

**277. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia NFRA itakamilisha ujenzi wa vihenge 56 vya kisasa na ghala nane (8) zenye uwezo wa kuhifadhi tani 250,000 zinazojengwa kupitia Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi (*Expansion of Storage Capacity*). Aidha, NFRA itakarabati ghala la Kipawa (tani 10,000) na ghala la Musoma (tani 4,500).

### **5.3.2 Uongezaji wa Thamani wa Mazao ya Kilimo**

**278. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia TARI itafanya utafiti wa teknolojia tano (5) za usindikaji; tano (5) za uhifadhi na 10 za uongezaji thamani wa mazao ya korosho, muhogo, viazi vitamu, zabibu, mtama, viazi lishe, soya, maharage na uyoga.

**1. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia CPB itasindika tani 32,400 za mahindi zitakazozalisha tani 25,920 za unga na tani 6,480 za pumba; itakamua tani 7,200 za alizeti na kuzalisha lita 2,160 za mafuta na tani 5,040 za mashudu; itakoboa tani 34,560 za mpunga zitakazozalisha tani 22,464 za mchele na tani 12,096 za pumba; itasindika tani 18,000 za ngano zitakazozalisha tani 12,600 za unga na tani 5,400 za pumba na itachakata tani 100 za korosho kwa ajili ya kuzalisha jibini (*cashewnut butter*).

**279. Mheshimiwa Spika**, CPB itanunua mashine ya kusafishia nafaka itakayofungwa Dodoma; itajenga jengo la utawala la kiwanda cha kukoboa mpunga katika Mkoa wa Mwanza; itatengeneza vinu vinne (4) vilivyopo katika mikoa ya Arusha (2), Iringa (1), na Shinyanga (Isaka - 1); itakarabati kiwanda cha mpunga cha Isaka, ghala sita (6) na vihenge vitatu (3) katika mikoa ya Dodoma (ghala 2), Arusha (ghala 2 na kihenge 1), Iringa (ghala 1 na vihenge 2) na Manyara (ghala 1); itajenga vihenge vinne (4) katika mikoa ya Dodoma (2) na Mwanza (2) na ghala sita (6) katika mikoa ya Dodoma (1), Katavi (2), Mwanza (1), Kigoma (1) na Iringa (1).

**280. Vilevile**, CPB itasavei kubaini uwezekano wa kufungua kiwanda cha kutengeneza unga wenye



mchanganyiko wa mahindi na muhogo katika Mkoa wa Mwanza, kiwanda cha kuchakata muhogo Kigoma na kiwanda cha vifungashio katika Mkoa wa Dodoma.

**281. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia TARI itafanya utafiti wa teknolojia za kuhifadhi nyanya ya unga na juisi ya miwa kwa muda mrefu ili kuwezesha upatikanaji wake kwa mwaka mzima.

### **5.3.3 Upatikanaji wa masoko ya ndani na nje ya nchi**

**282. Mheshimiwa Spika**, Wizara itaendelea kuhamasisha na kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya wakulima ambapo katika mwaka 2021/2022, itawezesha upatikanaji wa eneo kwa ajili ya maonesho ya bidhaa za kilimo katika nchi za Saudi Arabia na China. Aidha, Serikali ipo kwenye majadiliano na kampuni za bia ili kuwekeza katika kiwanda cha kimea chenye uwezo wa kusindika shayiri tani 35,000 kwa mwaka kutoka kwa wakulima. Hatua hiyo itawezesha upatikanaji wa soko la uhakika wa zao la shayiri na hivyo kuongeza uzalishaji wa ndani.

**283.** Vilevile, katika kuimarisha kilimo cha mkataba cha zao la alizeti, Wizara itaendelea kuwaunganisha wakulima na wasindikaji na kuandaa mazingira bora ya uwekezaji katika viwanda vya kusindika alizeti.

**284. Mheshimiwa Spika**, Wizara itajenga soko moja (1) katika Wilaya ya Longido; itaimarisha mfumo wa utoaji taarifa za masoko ya mazao ya kilimo; itatoa mafunzo kuhusu kilimo biashara na mifumo ya masoko kwa maafisa ugani 2,000 na Wakulima 4,000 kutoka Mikoa 26 na kukagua mazao yanayoingizwa na kutolewa nje ya nchi.

**285. Mheshimiwa Spika**, Wizara itaendelea kuimarisha CPB na NFRA ili kuongeza ununuzi wa mazao ya wakulima. NFRA itanunua tani 165,000 za nafaka ambazo zinajumuisha tani 150,000 za mahindi, tani 11,000 za mpunga na tani 4,000 za mtama kutoka kwa wakulima, vikundi vya

wakulima na Vyama vya Ushirika. CPB itanunua tani 32,400 za mahindi; tani 21,600 za ngano, tani 7,200 za mbegu za alizeti, tani 4,608 za muhogo, tani 34,560 za mpunga na tani 1,440 za korosho kutoka kwa wakulima kwa ajili ya viwanda vyake vilivyopo katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Iringa, Mwanza na Dar es Saalaam. Vilevile, CPB itanunua kwa wakulima mazao ghafi ya mahindi, alizeti, mpunga, maharage ya soya, ngano, korosho, maharage, mtama mweupe, ufuta, mbaazi na *green mugs*.

**286.** Vilevile, Wizara kupitia TANIPAC itajenga kituo mahiri cha mafunzo kwa wakulima na usimamizi wa mazao baada ya kuvuna (*Post Harvest Center of Excellency*) kwa ajili ya kuwezesha masoko na kusambaza teknolojia za usimamizi na uchakataji wa mazao ya kilimo baada ya kuvuna.

#### **5.3.4 Usalama wa Chakula na Lishe**

**287.** *Mheshimiwa Spika*, kupitia mradi wa TANIPAC, Wizara itajenga Maabara Kuu ya Kitaifa ya Kilimo (Dodoma) na kukarabati Maabara ya Udhhibiti Visumbufu Kibailoija (Pwani) kwa lengo la kusimamia ubora na usalama wa mazao ya chakula, kulinda afya za walaji na kuimarisha biashara ya mazao ya kilimo kimataifa.

**288.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara itaendelea kutekeleza Mpango Jumuishi wa Kitaifa wa Lishe kupitia ASDP II kwa kuwajengea uwezo wadau 484 kuhusu uongezaji thamani na matumizi ya mazao yenye virutubishi kwa wingi na yale yaliyoongezewa virutubishi kibaioloija ili kupunguza matatizo ya lishe nchini. Aidha, itaratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Masuala ya Lishe katika Kilimo.

**289.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia TARI itazalisha na kusambaza vipando na mbegu bora za mazao yenye virutubishi kwa wingi ikiwemo vikonyo 500,000 vya viazi lishe, tani tano (5) za mahindi yenye protini kwa wingi na tani tano (5) za maharage aina ya Jesca yenye zinki na madini chuma kwa wingi kwa lengo la kupunguza utapiamlo.

## 5.4 Kuiwezesha Sekta Katika Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini

### 5.4.1 Kuimarisha Mifumo ya Upatikanaji wa Mitaji

290. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2021/2022, Wizara itafanya tathmini ya mifumo ya upatikanaji wa mitaji kwa wakulima wadogo na wawekezaji wengine kwenye sekta ya kilimo ili kuibua vizuizi na kuvitafutia majawabu kwa ajili ya kuimarisha ugharamiaji wa mazao katika mnyororo wa thamani. Hatua hiyo, itahusisha kuendelea kufanya uchambuzi wa mfumo wa kiseru, kisheria na kikodi ili kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kujihusisha na shughuli za kilimo. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na TIRA itaanda Mpango Kabambe wa kutekeleza bima ya mazao nchini; itaratibu masuala ya utoaji wa huduma za bima ya mazao.

291. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeunda kamati maalum inayohusisha viongozi mbalimbali kutoka Wizara ya Kilimo, taasisi za fedha, Mfuko wa PASS na Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa ajili ya kupitia na kushauri namna bora ya upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya maendeleo ya kilimo.

### 5.4.2 Ufuatiliaji na Tathmini

292. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itafanya ufuatiliaji wa kina wa mashirika, mashamba na mali za umma zilizobinafsishwa kwa lengo la kutathmini utekelezaji wa maelekezo ya Serikali yanayohusu ubinafsishaji wa mashirika, mashamba na mali hizo. Kwa kuzingatia uchambuzi wa taarifa za hali halisi zitakazokusanywa, Wizara itaandaa mapendekezo mahsusi kuhusu mali na mashamba yanayohusika na kuwasilisha Serikalini kwa ajili ya kufanyiwa maamuzi stahiki.

### 5.4.3 Kuboresha Mifumo ya Kitaasisi, Bodi na Sheria

293. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka, 2021/2022, Wizara itakamilisha tathmini ya kina ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2013 ili kubaini maeneo ya kiseru

yenye upungufu na kuchambua mapungufu hayo iwapo yanatosheleza kutunga Sera mpya au kufanya marekebisho ya Sera iliyopo.

**294. *Mheshimiwa Spika***, Wizara itaendelea kukamilisha utekelezaji wa maelekezo ya Serikali yanayohusu Andiko lenye mapendekezo ya Kutunga Sheria ya Kilimo. Kadhalika, Wizara itaendelea na usajili wa wakulima na kuhakiki taarifa zao katika kanzidata; itapitia sheria zilizozanzisha taasisi za kilimo ili kuzirekebisha au kutunga mpya; itawezesha Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (TPHPA) kutekeleza majukumu yake.

**295.** Aidha, Wizara itafanya marekebisho ya Sheria ya Sukari; Sheria ya Mbegu, mapitio ya Sheria za Tasnia za Mazao na kuimarisha Mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za kilimo (ARDS) kwa kuwajengea uwezo Maafisa Ugani katika Halmashauri 185 kuhusu ukusanyaji wa takwimu za kilimo nchini.

#### ***5.4.4 Kuimarisha Usimamizi wa Maendeleo ya Ushirika.***

**296. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Tume ya Maendeleo ya Ushirika itavijengea uwezo Vyama vya Ushirika kutumia mfumo wa ununuzi wa pamoja wa pembejeo (BPS); itasimamia uendeshaji wa Vyama vya Ushirika ikiwemo ukaguzi wa mahesabu na mali za ushirika pamoja na kufanya ukaguzi wa nje wa Vyama vya Ushirika 6,500.

**297.** Aidha, Tume itahamasisha wakulima wadogo wa miwa kujiunga katika Vyama vya Ushirika ili kupata fursa ya kuzalisha na kuuza miwa kwa viwanda vya uzalishaji wa sukari kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria ya Sukari ya mwaka 2001. Vilevile, Tume itahamasisha wakulima wa zao la chikichi katika Mkoa wa Kigoma kujiunga kwenye Vyama vya Ushirika ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za kilimo ikiwemo pembejeo na mikopo.

#### 5.4.5 Kuimarisha Masuala Mtambuka katika Kilimo

##### 5.4.5.1 Vijana

298. **Mheshimiwa Spika**, Wizara itakamilisha Mkakati wa Taifa wa Kushirikisha Vijana kwenye Kilimo Awamu ya Pili (*National Strategy for Youth Involvement in Agriculture – NSYIA II 2021- 2026*). Wizara kwa kushirikiana na SUGECO itatekeleza mfumo wa kilimo biashara (*Kizimba Business Model*) unaolenga kushirikisha vijana katika uzalishaji wa miche ya maembe na mbegu za soya, maharage na alizeti kwenye mashamba ya pamoja (*block farms*) katika Mikoa ya Simiyu, Tabora, Singida na Morogoro. Aidha, mfumo huo utawezesha vijana 2,400 kupata ajira kwa kuzalisha zao la maembe, maharage na soya kwenye eneo la ekari 1,500 lililopo Dakawa Mkoa wa Morogoro.

299. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Shirika la Kimataifa la Heifer itahamasisha na kuwezesha vijana 1,550 kupata mikopo kupitia mfuko maalum wa Mikopo ya Heifer; kupata mafunzo ya kilimo biashara kwa vitendo kwa vijana 1,750; kuanzisha SACCOS sita (6) za vijana; kuwezesha Vyama vitano (5) vya Ushirika vya vijana kupata masoko ya uhakika; na kuwezesha vijana 500 kunufaika na fedha za mfuko za Maendeleo ya Vijana za Halmashauri.

##### 5.4.5.2 Jinsia

300. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/2022, Wizara itaendelea kujumuisha masuala ya jinsia katika miradi, mikakati na program za kilimo kwa kuandaa Mwongozo wa Ujumuishwaji wa Masuala ya Kijinsia katika Sekta ya Kilimo (*Guideline for Gender Mainstreaming in Agriculture Sector*). Aidha, itafuatilia utekelezaji wa maeneo ya Jinsia katika miradi ya TANIPAC na Agri-Connect ili kuhakikisha utekelezaji wa masuala ya jinsia unazingatiwa.

##### 5.4.5.3 VVU na UKIMWI

301. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/2022, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Afya itaendelea kutoa

elimu ya VVU na UKIMWI kwa wafanyakazi wa Wizara ili kuzuia na kupunguza maambukizi mapya. Vilevile, Wizara itaendelea kuwahudumia watumishi 12 walioathirika na kuhamasisha watumishi kupima ili kujua afya. Pia Wizara itatoa na kusambaza vifaa kinga katika maeneo yanayofikiwa na watumishi.

## 6. SHUKRANI

**302. Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kuzishukuru Nchi na Mashirika ya Kimataifa ambayo yamesaidia Wizara katika kuendeleza kilimo. Naomba kutaja baadhi ya Nchi na Mashirika ya Kimataifa kama ifuatavyo: Serikali za Japan, Marekani, Uingereza, Ireland, Malaysia, China, Indonesia, Korea ya Kusini, India, Misri, Israel, Ubelgiji, Ujerumani, Finland, Norway, Brazil, Uholanzi, Vietnam, Canada na Poland.

Ninayashukuru pia Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, AU, IFAD, DFID, UNDP, FAO, JICA, EU, ENABEL, GIZ, UNICEF, WFP, CIMMYT, ICRISAT, ASARECA, USAID, KOICA, ICRAF, IITA, IRRI, ILRI na CABI. Nyingine ni EAC, SADC, AVRDC, AGRA, KILIMO TRUST, CIP, CIAT/PABRA, UNEP, WARDA, Shirika la Kudhibiti Nzige wa Jangwani (DLCO-EA), Shirika la Kudhibiti Nzige Wekundu (IRLCO-CSA) na HELVETAS. Wadau wengine ni, *Bill and Melinda Gates Foundation, Gatsby Trust, Rockefeller Foundation, Clinton Foundation, Aga Khan Foundation, TAHA* na Asasi zisizo za kiserikali nyingi ambazo hatuwezi kuzitaja zote hapa.

**303. Mheshimiwa Spika**, natoa shukrani kwa wakulima wote kwa kazi kubwa wanazofanya kuendeleza kilimo nchini. Ni wazi kuwa mafanikio ya kilimo yanatokana na juhudi na ushirikiano mkubwa na Serikali. Kipekee nirudie kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Rombo kwa namna wanavyoniunga mkono na kunipa ushirikiano. Naomba wote watambue kuwa kilimo ni maisha, uchumi, biashara, viwanda na ajira.

## 7. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2021/2022

### 7.1 Makusanyo ya Maduhuli

304. Mheshimiwa Spika, *katika mwaka 2021/2022, Wizara inatarajia kukusanya Shilingi 34,495,000,000 kutokana na ada za ukaguzi wa mazao yanayouzwa nje ya nchi au kuingizwa nchini, uuzaji wa nyaraka za zabuni, ukodishaji wa mitambo ya Tume ya Umwagiliaji. Kati ya fedha hizo, Shilingi 4,480,000,000 zitakusanywa katika Fungu 43 na Shilingi 30,015,000,000 zitakusanywa kwenye Fungu Na.05.*

### 7.2 Fedha kwa Mafungu yote (43, 24 na 05)

304. *Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Wizara ya Kilimo inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 294,162,071,000 kupitia Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24 kama ifuatavyo;*

#### 7.2.1 Fedha kwa Fungu 43

305. *Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 228,871,243,000 kupitia Fungu 43 kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi 164,748,000,000 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Maendeleo ambapo Shilingi 82,180,000,000 ni fedha za ndani na Shilingi 82,568,000,000 ni fedha za nje. Aidha, Shilingi 64,123,243,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo Shilingi 42,492,457,000 ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi 21,630,786,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.*

#### 7.2.2 Fedha kwa Fungu 05

306. *Mheshimiwa Spika, jumla ya Shilingi 51,487,450,000 zinaombwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi 46,500,000,000 ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ambapo Shilingi 35,000,000,000 ni fedha za Ndani na Shilingi 11,500,000,000 ni fedha za Nje. Aidha, kati ya fedha zinazoombwa, Shilingi 4,987,450,000 ni kwa ajili ya Matumizi*

**ya Kawaida ambapo Shilingi 3,349,266,000 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Tume na Shilingi 1,638,184,000 ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo.**

### **7.2.3 Fedha kwa Fungu 24**

**308. Mheshimiwa Spika**, jumla ya Shilingi **13,803,378,000** zinaombwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **6,549,009,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Tume na Shilingi **4,654,984,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Tume. Aidha, Shilingi **1,000,000,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya kawaida ya COASCO na Shilingi **1,599,385,000** ni kwa ajili ya mishahara ya COASCO.

**309. Mheshimiwa Spika**, hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara: [www.kilimo.go.tz](http://www.kilimo.go.tz)

## **8. HITIMISHO**

### **310. Mheshimiwa Spika**, NAOMBA KUTOA HOJA

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana kwa uwasilishaji mzuri sana wa hotuba yako.

Waheshimiwa Wabunge, kwenye visumbuzi vyetu tunayo hotuba nzima na viambatanisho vyake vyote. Tupitie tuweze kuona mambo kemkem yaliyopo katika hotuba hii ya Wizara muhimu sana ya Kilimo.

Baadhi ya wageni ambao pia ningependa kuwatambulisha ni Baraza la Madiwani wa Nzega. Pale mlipo naomba msimame. Ooh, karibuni sana, sana wana-Nzega hapa Dodoma. Pia nimeambiwa Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Nzega amefuatana nanyi, Ndugu Kanuda, karibu sana, karibu Mwenyekiti, karibu Dodoma. Mwangalie



tu, magari mengi, Jiji kubwa Dodoma hili. Maana Wanyamwezi mmezoea baiskeli tu kwenu kule. Karibuni sana watani zangu. *(Makofi/Kicheko)*

Katibu wa CCMNzega, Ndugu Goha Saidi, karibu sana, popote pale ulipo, karibu sana, karibu Goha. *(Makofi)*

Katibu wa CCM Mkoa wa Tabora, Ndugu Solomon, nimeambiwa upo. Upo wapi Katibu wa CCM Mkoa? Karibu sana Solomon, mtu mwema sana huyu, karibu sana. *(Makofi)*

Sasa tuendeleo, nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo. Ninapomwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, basi Mheshimiwa Joseph Mhagama, Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Njalu Silanga, mtakuwa katika wachangiaji wa mwanzo kabisa.

Mwenyekiti! Ahsante, anakuja Mheshimiwa Almas Maige, kwa niaba ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. Karibuni tusikilize hotuba ya Kamati hii muhimu. *(Makofi)*

**MHE. ALMASI A. MAIGE (K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa muda, naomba taarifa hii yote iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji na kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa mwaka wa fedha 2020/2021, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati yameelezwa kwenye Kanuni za Bunge Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane pamoja na masharti ya Kanuni ya 118(4). Kwa mujibu wa kanuni hizo, kabla ya Taarifa ya Utekelezaji wa Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo kujadiliwa Bungeni, zilipaswa

kuchambuliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa uchambuzi huo ulifanyika baada ya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotekelezwa chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, ili kuonyesha mawanda ya uchambuzi, nilikumbushe Bunge lako kuwa, Bajeti ya Wizara ya Kilimo inajumuisha Mafungu matatu, Fungu 43 - Wizara ya Kilimo; Fungu 24 - Tume ya Ushirika; na Fungu Namba 5 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo Iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) inayozitaka Kamati za Bunge kukagua miradi ya maendeleo na kufanya ziara katika Mkoa wa Morogoro. Katika ziara hiyo, Kamati ilitembelea:-

(a) Wakala wa Taifa wa Uzalishaji na Uendelezaji wa Mbegu za Kilimo (ASA);

(b) Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI);  
na

(c) Skimu ya Umwagiliaji za Kigugu - Mvomero na Mvumi - Kilosa.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha, 2020/2021, Wizara ya Kilimo ilitengewa jumla ya shilingi 150,073,324,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya kupitia mafungu mawili. Fungu la 43 - Wizara ya Kilimo na shilingi 137,273,144,000/=; Fungu 05 - Tume ya Taifa ya Umwagiliaji shilingi 12,801,180,000/=.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ilibaini kwamba, matumizi ya teknolojia ya umwagiliaji yamesaidia sana kuongeza uzalishaji wa mazao. Kuongezwa kwa bajeti ya uzalishaji mbegu kumesaidia kuongeza uzalishaji wa mbegu nchini na hivyo wakulima kupata mbegu bora kwa wakati na kwa gharama

nafuu. Bajeti ndogo inayotengwa kwa Wakala wa Taifa wa Uzalishaji na Uendelezaji wa Mbegu (ASA), haitoshi kujenga maghala ya kuhifadha mbegu na hivyo mbegu zinazozalishwa kuharibika kabla ya matumizi yake.

Mheshimiwa Spika, ili kujiridhisha na utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Kilimo na Taasisi zake, Kamati ilifanya uchambuzi wa mambo makuu mawili:-

(a) Uzingatiaji wa maoni na ushauri uliotolewa Bungeni;

(b) Utekelezaji wa bajeti ikilinganishwa na upatikanaji wa fedha;

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi wa Kamati yalisaidia katika majadiliano ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha, 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa mapato wa bajeti wa Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha, 2020/2021, ulilenga kulinganisha upatikanaji wa fedha na idhini ya Bunge kuhusu bajeti. Matokeo ya uchambuzi yanaonyesha kuwa jumla ya kiasi cha fedha kilichopokelewa hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 ni asilimia 55.88 ya bajeti iliyoidhinishwa, ambao ni mwenendo usioridhisha katika upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Aprili, 2021 fedha za matumizi ya maendeleo ya ndani zilizotoka ni shilingi 48,595,760,000/= sawa na asilimia 70.7 na fedha za nje zilizotoka zilikuwa ni shilingi 20,111,135,120/= sawa na asilimia 29.3 ya fedha zilizoidhinishwa.

(c) fedha za ndani za maendeleo na fedha za matumizi ya kawaida zimekuwa zikitoka kwa wakati. Uchambuzi umeonyesha Serikali inawezesha Watendaji wa Wizara kutekeleza majukumu yao kikamilifu kwa kuwapatia fedha za matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha, 2020/2021, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo tisa. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara ya Kilimo, imezingatia baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati na inaendelea kuzingatia sehemu ya ushauri iliyotolewa.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kwa Wizara ya Kilimo, unajumuisha mafungu matatu kama nilivyoeleza hapo juu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; Wizara ya Kilimo kupitia mafungu yake matatu, imepanga kutekeleza vipaumbele mbalimbali, ambavyo maelezo yake yamefafanuliwa kwa kina kwenye Taarifa ya Waziri.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza malengo yaliyokusudiwa, Wizara ya Kilimo inaomba kuidhinishwa jumla ya shilingi 294,162,071,000/=. Katika fedha hizo, shilingi 82,914,071,000/= sawa na asilimia 28.2 ya bajeti inayoombwa, ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 211,248,000,000/= sawa na asilimia 71.8 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulifanya ulinganisho wa bajeti ya Wizara ya Kilimo na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha, 2021/2022. Katika uchambuzi huo, mambo yafuatayo yalibainika.

Mheshimiwa Spika, moja, Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, ambayo ni shilingi 294,162,071,000/= ni sawa na asilimia 0.08 ya bajeti ya Serikali, ambayo kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa 2021/2022 shilingi trilioni 36.26.

Mheshimiwa Spika, mbili Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka wa Fedha 2021/2022, unaonesha ongezeko la bajeti kwa asilimia 26 ikilinganishwa na Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2020/2021. Wakati bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa

Mwaka wa Fedha 2021/2022 imeongezeka kwa asilimia 22 ikilinganishwa na ile bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021.

Mheshimiwa Spika, tatu, Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaonesha ongezeko la asilimia 2.76 katika fedha za maendeleo ambazo ni sawa na asilimia 36.68 ya Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Wakati bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Kilimo ambayo ni sawa na asilimia 07 ya bajeti ya Taifa ikilinganishwa na bajeti ya mwaka jana au Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambayo ni asilimia 011.

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu ya kuzingatia katika maombi ya fedha kwa mwaka wa 2021/2022; Sekta ya Kilimo inachangia takriban asilimia 27.7 ya pato la Taifa na asilimia 25 ya fedha ya kigeni na inaajiri karibu takriban asilimia 65 ya Watanzania wote. Vile vile, sekta hii ni chanzo kikuu cha malighafi kwa ajili ya viwanda ambavyo huchangia asilimia 60 ya malighafi ya viwandani. Ni chanzo kikuu cha chakula cha wananchi, mapato kwa wakulima, lakini lishe na afya kwa wananchi wetu. Licha ya umuhimu wa Sekta ya Kilimo iliyoelezwa hapo juu, Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alipokuwa analihutubia Bunge tarehe 22 Aprili, 2021 alionesha umuhimu ulioko kwenye sekta hii.

Mheshimiwa Spika, kuongeza uzalishaji wa upatikanaji wa mbegu bora za kilimo; usalama wa mbegu ni usalama wa chakula na usalama wa chakula ni usalama wa nchi. Jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora kwa mujibu wa sheria liko chini ya Wakala wa Mbegu (ASA). Pamoja na umuhimu wa ASA, inakabiliwa na changamoto mbalimbali, baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na fedha kidogo zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo; mbili, fedha zinazoidhinishwa na Bunge kutopatikana kwa wakati; tatu, upungufu wa maghala ya kuhifadhia mbegu; na nne ukosefu wa hifadhia ya mbegu za kimkakati kwa Taifa (*strategic seed reserve*)

Mheshimiwa Spika, utafiti umeonesha kuwa zao la mpunga pekee kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji umeonesha tija inayoweza kupatikana endapo hekta milioni

22 zikilimwa misimu miwili kwa wakati mmoja, zinaweza kuzalisha kisio la chini kabisa tani milioni 220. Thamani ya kila gunia la mpunga la kilo 100 ni shilingi 65, mpunga utakaozalishwa kwa mwaka utakuwa na thamani ya shilingi trilioni 143 ambayo ni sawa na bajeti ya Tanzania kwa takriban miaka minne. Hii ni kabla ya kuongeza thamani ya kuuza kwenye masoko ya ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha upatikanaji wa huduma za ugani kwa wakulima; huduma za ugani ni huduma za msingi ambazo zinapaswa kutolewa na wataalam wa kilimo kwa wakulima kuhusu kanuni bora za kilimo kwa lengo la kuinua uzalishaji na tija kwa mazao ya kilimo kwa kuongeza tija kwenye kilimo. Takwimu zinaonesha mahitaji halisi ya Maafisa Ugani nchini ni 21,258 ambapo walioko hivi sasa ni 7,307 sawa na asilimia 34 ya mahitaji. Aidha, takwimu hizi zinaelezea uwiano wa sasa ni sawa na Afisa Ugani mmoja kwa wakulima 600.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya riba kubwa zinazotolewa na taasisi za fedha kwa ajili ya mikopo ya wakulima wadogo wadogo; Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ni taasisi ya kifedha ambayo husimamiwa na Benki Kuu. Kazi ya msingi ya Taasisi ya Fedha yoyote ni kutengeneza faida ili kuweza kurudisha pesa za wawekezaji kwenye kuhakikisha benki hizi hazitoi mikopo kwa biashara ambazo hazina uhakika wa kurudisha mikopo kama vile kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo *TADB* haiwezi kuendesha shughuli zozote kwa kutoa mikopo pasipo uhakika wa namna mikopo hiyo itakavyorudishwa. Kwa sababu hiyo, haishangazi kuona Benki ya Maendeleo ya Kilimo inatoa riba sawa na benki zingine za biashara ambayo ni kati ya asilimia 10 mpaka 20. Pia, mkulima anatakiwa kuwa na dhamana ya pamoja na kukata bima ya mkopo.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya upotevu wa mazao baada ya kuvunwa; pamoja na jitihada za Serikali za kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvunwa kwa kujenga miundombinu ya kuhifadhia mazao kama maghala

na vihenge, bado kuna changamoto ya upotevu wa mazao unaotokana na ubovu wa barabara za vijijini ambazo hutumika kusafirishia mazao kutoka shambani hadi sokoni.

Mheshimiwa Spika, kuongeza uzalishaji wa zao la korosho. Korosho ni moja ya mazao makubwa makuu ya biashara hapa nchini na inaingizia Tanzania fedha za kigeni kiasi cha dola za Kimarekani milioni 585.1 sawa na shilingi za Tanzania trilioni 1.3. Licha ya mchango wa zao la korosho kwenye uchumi, uzalishaji wa zao hili umekuwa unashuka kwa asilimia 34 kutoka tani 313,826 kwa uzalishaji wa msimu wa mwaka 2017/2018 na kufikia tani 206,719 kwa msimu wa mwaka 2020/2021. Pamoja na sababu nyingine, sababu kubwa iliyosababisha kushuka kwa uzalishaji wa korosho ni marekebisho yaliyofanywa kwenye Sheria ya Fedha ya Mwaka 2018, *Finance Bill Act, 2018* na kusitishwa kwa shughuli za Mfuko wa Wakfu wa Kuendeleza Tania ya Korosho (*CADTF*).

Mheshimiwa Spika, jedwali namba tatu lililoko kwenye Taarifa yangu hii ya Kamati inaonesha takwimu ya kushuka kwa uzalishaji wa zao la korosho nchini.

Mheshimiwa Spika, changamoto za ushirika; ushirika ni imani ambayo huunganisha wanachama katika kufikia malengo ya pamoja waliyojiwekea. Kufuatia imani hii ya kufikia malengo kwa pamoja, manufaa ya ushirika yamedhihirika mahali kwingi katika maeneo kwa nyakati mbalimbali. Baadhi ya Vyama vya Ushirika vilivyowahi kufanya vizuri ni pamoja na Chama Kikuu cha Ushirika Shinyanga (*SHIRECU*), Chama Kikuu cha Ushirika Mwanza (*NCU*), Chama Kikuu cha Ushirika Kilimanjaro (*KNCU*) na Chama Kikuu cha Ushirika Kagera (*KCU*), lakini vile vile, Mamlaka ya Mkonge.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua na kupongeza juhudi mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali katika kuimarisha ushirika. Pamoja na pongezi hizo, Kamati ina imani kuwa ili kuongeza ufanisi wa usimamizi katika vyama vya ushirika, Serikali ina wajibu wa kuhakikisha Vyama Vikuu vya Ushirika vinatekeleza majukumu yake kwa kuvihudumia

vyama vya wanachama wake kwa kusimamia uzalishaji, upatikanaji wa pembejeo, huduma za ugani, masoko na kuajiri watendaji wenye sifa kwa kuzingatia ukubwa wa chama.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya kupitia Taarifa za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti inayomalizikia na Maoni ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

**SPIKA:** Changamka changamka mtani. Ongeza sauti.

**MHE. ALMASI A. MAIGE (K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Mheshimiwa Spika, kuimarisha bajeti kwa ajili ya Sekta ya Kilimo; pamoja na mchango mkubwa wa Sekta ya Kilimo katika nchi yetu, bado Serikali haijajiwekeza ipasavyo kuimarisha ukuaji wa Sekta hii. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Sekta ya Kilimo imetengewa bajeti chini ya asilimia moja ambayo ni sawa na asilimia 0.08 tu.

Mheshimiwa Spika, kuwezesha Maafisa Ugani kutekeleza majukumu yao kikamilifu; kufuatia upungufu wa maafisa ugani uliopo na kwa kutambua umuhimu wa Maafisa Ugani katika kuongeza uzalishaji kwenye kilimo Kamati inashauri Serikali kuajiri Maafisa Ugani ili kukidhi mahitaji ikiwa ni pamoja na kuwatengea rasilimali fedha, kuwapatia vitendea kazi na kuwapa mafunzo ya mara kwa mara kwa kuimarisha kufanya kilimo chenye tija.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha utafiti na uzalishaji mbegu. Kamati inatambua na inapongeza juhudi zinazochukuliwa na Serikali kujenga uwezo wa Wakala wa Mbegu (ASA) kuzalisha kulingana na mahitaji. Pamoja na juhudi hizo, fedha zinazotengwa ni kidogo na hazitoki kwa wakati. Kamati inashauri Serikali kuiongezea ASA bajeti na ni muhimu fedha zinazotengwa kupelekwa kwa wakati.



Mheshimiwa Spika, kurejeshwa kwa Mfuko wa Kuendeleza Tasnia ya Korosho; ili kuongeza uzalishaji wa zao la korosho ambao umekuwa ukishuka kwa miaka mitatu mfululizo, Kamati inaishauri Serikali kuona uwezekano wa kurejesha tena Mfuko wa Kuendeleza Tasnia ya Korosho. Aidha, Kamati inasisitiza kwamba ili Mfuko huo uweze kuleta tija ni vyema kasoro zilizosababisha kufutwa kwa Mfuko huu kwanza zirekebishwe.

Mheshimiwa Spika, kukabiliana na changamoto ya upotevu wa mazao baada ya kuvunwa; Kamati inatambua juhudi kubwa inayofanywa na Serikali katika kupunguza kiasi cha upotevu wa mazao baada ya kuvunwa kwa kujenga vihenge na maghala ya kuhifadha mazao. Ili kukabiliana na changamoto hii, Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha *TARURA* kwa kupewa fedha zaidi za kutosha kwa ajili ya kuboresha miundombinu na hasa barabara za kutoka vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha utendaji Bajeti ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji; kwa kuwa, hakuna shaka na tija inayoweza kupatikana kutokana na uwekezaji kwenye kilimo cha umwagiliaji, ni vyema Serikali ikatambua fursa iliyopo na kutenga bajeti ya kutosha itakayosaidia kuongeza ufanisi wa kuimarisha uratibu wa shughuli za umwagiliaji nchini.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha ushirika nchini. Ili kuhakikisha ushirika wa hiari ambao ndiyo msingi wa imani yenyewe, Kamati inaishauri Serikali: Moja, kuisimamia na kuwaelimisha wakulima umuhimu wa kujiunga kwenye vyama vya ushirika; Mbili, kuboresha uongozi, kudhibiti wizi na ubadhilifu ndani ya Vyama vya Ushirika; Tatu, kuhakikisha vyama vya ushirika vinasimamiwa na sheria inayowalinda na kuwanufaisha wanaushirika na hivyo kuchangia ipasavyo katika ustawi wa wanachama na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi kwa vile ambavyo mmekuwa mkituongoza kwa kipindi chote cha Mkutano wa Bunge la Bajeti na kuliwezesha Bunge kutimiza wajibu wake wa kuisimamia Serikali kwa niaba ya wananchi

kwa mujibu wa Katiba. Aidha, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa katika kipindi chote cha Kamati ilipokuwa ikitekeleza wajibu wake. Kwa dhati kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao waliyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara pamoja na kuandaa Taarifa hii hadi kukamilika kwake. Kutokana na kazi kubwa waliyoifanya, natamani kuwataja kwa majina yao...

**SPIKA:** Ruka.

**MHE. ALMASI A. MAIGE (K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** ...lakini kwa sababu ya muda, naomba majina yao yaingizwe kwenye kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda; Naibu Waziri, Mheshimiwa Hussein Bashe; Katibu Mkuu, ndugu Andrew Massawe; Naibu Katibu Mkuu, Profesa Siza Tumbo; pamoja na wataalam wa Wizara kwa ushirikiano wao walioipa Kamati ilipokuwa ikitekeleza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumpongeza Katibu wa Bunge ndugu Nenelewa Mwihambi kwa kuteuliwa kuwa mwanamke wa kwanza kuongoza mhimili wa Bunge. Namshukuru pia Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge ndugu Athuman Hussein; Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Fedha ndugu Michael Chikokoto kwa kuisaidia na kuwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kwa namna ya kipekee, nashukuru Sekretarieti yangu ya Kamati ambayo ni ndugu Rachel Nyega na ndugu Vigil Mtui...

**SPIKA:** Ahsante. Unaweza ukahitimisha tu Mheshimiwa.

**MHE. ALMASI A. MAIGE (K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Mheshimiwa Spika, baada ya

maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGONA MAJI  
KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA KILIMO KWA  
MWAKA WA FEDHA 2020/2021 PAMOJA NA MAONI YA  
KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA  
WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, majukumu ya Kamati yaelezwa kwenye Kanuni za Bunge Kifungu cha 7 (1)(a) cha Nyogeza ya Nane pamoja na masharti ya Kanuni ya 118 (4). Kwa mujibu wa Kanuni hizo, kabla ya Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo, kujadiliwa Bungeni, zilipaswa kuchambuliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa uchambuzi huo ulifanyika baada ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuonesha mawanda ya uchambuzi, nilikumbushe Bunge lako kuwa, Bajeti ya Wizara ya Kilimo inajumuisha mafungu (3) matatu ambayo ni **Fungu 43** – Wizara ya Kilimo; **Fungu 24** - Tume ya Ushirika; na **Fungu 05** - Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ninayoiwasilisha inafafanua kuhusu maeneo manne (04) ambayo yanahusu: -

- a) Matokeo ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
- b) Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;
- c) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; na
- d) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## **2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

**2.1 Mheshimiwa Spika**, ukaguzi wa miradi yamaendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ulitokana na masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inayotaka Kamati kufanya ziara kwa siku zisizozidi saba kwa ajili ya kukagua miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni hiyo kwa kufanya ziara katika Mkoa wa Morogoro na katika ziara hiyo, Kamati ilitembelea: -

- a) Wakala wa Taifa wa Uzalishaji na Uendelezaji wa Mbegu za Kilimo (ASA) kwa lengo la kutathimini shughuli za uzalishaji mbegu bora na uhakika wa kuwafikia wananchi kwa wakati na kwa bei nafuu;
- b) Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) kwa lengo la kutembelea Maabara na kukagua shughuli za udhibiti ubora unavyofanyika ili kuhakikisha usalama wa mbegu; na
- c) Skimu za Umwagiliaji za Kigugu-Mvomero na Mvumi - Kilosa kwa ajili ya kutathimini utekelezaji wa

Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP -II) yenye lengo la kuongeza uzalishaji wenye tija kwa maendeleo ya viwanda na chakula nchini.

## **2.2 Ufafanuzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha na kukaguliwa;**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ya Kilimo, ilitengewa jumla ya **Tsh 150,073,324,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kupitia mafungu mawili (2) kama ifuatavyo: -

a) **Fungu 43:** Wizara ya Kilimo – **Tshs. 137,273,144,000/=**

b) **Fungu 05:** Tume ya Taifa ya Umwagiliaji – **Tsh. 12,801,180,000/=**

## **2.3 Yaliyobainika**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati imebaini kwamba:

a) Matumizi ya tekinolojia ya umwagiliaji yamesaidia kuongeza uzalishaji wa mazao kwani wananchi wameweza kulima kipindi cha mwaka mzima;

b) Kuongezwa kwa bajeti ya Uzalishaji Mbegu kumesaidia kuongeza uzalishaji wa mbegu nchini na hivyo wakulima kupata mbegu bora kwa wakati na kwa gharama nafuu;

c) Bajeti ndogo inayotengwa kwa Wakala wa Taifa wa Uzalishaji na Uendelezaji wa Mbegu (ASA) haitoshi kujenga maghala ya kuhifadhia mbegu na kupelekea mbegu zinazozalishwa kuharibika kabla ya matumizi yake; na

d) Ukosefu wa Takwimu sahihi kuhusu mahitaji halisi ya mbegu zinakwamisha mipango ya kibajeti na utekelezaji wake.

### 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI

**Mheshimiwa Spika**, ili kujiridhisha na utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Kilimo na Taasisi zake, Kamati ilifanya uchambuzi wa mambo makuu mawili: -

a) Uzingatiaji wa maoni na ushauri uliotolewa Bungeni wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; na

b) Utekelezaji wa bajeti ikilinganishwa na upatikanaji wa fedha.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi huo, naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa matokeo ya uchambuzi wa Kamati yalisaidia katika majadiliano ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

### 3.1 Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ulilenga kulinganisha upatikanaji wa fedha na idhini ya Bunge kuhusu Bajeti kwa kuzingatia malengo ya bajeti yaliyowekwa. Njia zilizotumiwa kufanya uchambuzi ni pamoja na kuangalia hali halisi, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa vikao vya Kamati. Kwa mantiki hiyo, muhtasari wa matokeo yaliyobainika ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 01** hapa chini.

**Jedwali 1: Ulinganisho wa Bajeti iliyoidhinishwa na kiasi cha fedha kilichotolewa hadi Aprili, 2021;**

BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2020/2021			UPATIKANAJI WA FEDHA HADI APRILI,2021		
Mchanganuo	Kiasi	%	Mchanganuo	Kiasi	%
Kawaida	79,765,484,450	37.7	Kawaida	59,717,135,529	74.8
Maendeleo	150,074,324,000	62.3	Maendeleo	68,706,896,035.23	45.8
<b>Jumla</b>	<b>229,839,808,000</b>	<b>100</b>	<b>Jumla</b>	<b>128,424,031,564.23</b>	<b>55.88</b>

*Chanzo: Uchambuzi wa Randama zilizowasilishwa.*

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa:

a) Jumla ya kiasi cha fedha kilichopokelewa hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 ni **asilimia 55.88** ya bajeti iliyoidhinishwa, ambao ni mwenendo usioridhisha katika upatikanaji wa fedha;

b) Hadi mwezi Aprili, 2021 Fedha za Matumizi ya Maendeleo za Ndani zilizotoka ni shilingi **48,595,760,915.07** sawa na **asilimia 70.7** na Fedha za Nje zilizotoka zilikuwa shilingi **20,111,135,120.16** sawa na **asilimia 29.3** ya fedha zilizoidhinishwa;

c) Fedha za Ndani za Maendeleo na Fedha za Matumizi ya Kawaida zimekuwa zikitoka kwa wakati na hivyo kutokuathiri utekelezaji kwa malengo ya bajeti ya maendeleo; na

d) Uchambuzi umeonyesha Serikali inawawezesha Watendaji wa Wizara kutekeleza majukumu yao kikamilifu kwa kuwapatia fedha za Matumizi ya Kawaida kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa ujumla wa Kamati umebaini kwamba, mtiririko wa fedha kutoka Hazina ni wa

kuridhisha ikilinganishwa na miaka mingine iliyopita. Kwa mfano;

a) Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia Matumizi ya Kawaida hadi kufikia mwezi **Februari, 2020** ilikuwa ni **asilimia 55** wakati kwa mwezi Aprili, 2021 ilikuwa ni **asilimia 74.87**;

b) Upatikanaji wa fedha za kugharamia Miradi ya Maendeleo mwezi **Aprili, 2020** ulikuwa ni **asilimia 29.52** wakati hadi kufikia **mwezi Aprili, 2021** ilikuwa ni **asilimia 70.7**.

### **3.2 Uchambuzi wa Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo tisa (9). Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ya Kilimo, imezingatia kiasi baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati na inaendelea kuzingatia sehemu ya ushauri uliotolewa. Mfano wa ushauri uliozingatiwa unahusu utekelezaji wa Sheria Na. 5 ya Mwaka 2013 Kifungu cha 52 ambacho kinaitaka Serikali kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Umwagiliaji. Kuanzishwa kwa Mfuko huu kutasaidia kufidia ufinyu wa Bajeti ya Maendeleo kwa ajili ya kugharamia miradi ya kilimo hususan eneo la umwagiliaji.

Aidha, mfano wa ushauri ambao unaendelea kuzingatiwa ni ule wa Wizara kuwa na Mkakati wa kutafuta masoko ya mazao mbalimbali nje ya nchi. Utekelezaji wa ushauri huu umezingatiwa ambapo juhudi za Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Wizara ya Viwanda na Masoko na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa zimeonekana baada ya kupata soko la mazao ya *Soya Bean* nchini China, Mahindi nchini DRC, Kenya, Burundi na Rwanda na Sudan ya Kusini. Aidha, Mazao ya mboga mboga na matunda kama parachichi nayo yalipata soko nchi za Ulaya ikiwemo Ufaransa na Uingereza.



**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa ushauri ambao haukuzingatiwa kabisa, mfano wake ni ushauri kuhusu jitihada za makusudi kufanyika ili kuinua zao la korosho ambapo kwa miaka mitatu mfululizo uzalishaji wa zao la korosho katika mikoa ya Kusini umeendelea kushuka. Taarifa ilionesha kuwa uzalishaji wa zao la korosho umeshuka kutoka **tani 313,826** zilizoalishwa mwaka **2017/2018** hadi kufikia tani **206,718** Mwaka **2020/2021**.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwa, kwa kiasi kikubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri uliotolewa, Kamati ina maoni kuwa bado kuna umuhimu wa kuendelea kuzingatia ushauri ambao haujafanyiwa kazi na hakuna sababu za msingi za kutouzingatia.

**Kwa mfano**; ushauri kuhusu umuhimu wa Serikali kulipa madeni ya muda mrefu ya mawakala waliotoa huduma ya kusambaza pembejeo kwa wakulima haujatekelezwa kwa maelezo kwamba suala hili bado liko kwenye vyombo vya dola kwa uchunguzi. Kamati inaamini uchunguzi huo umechukua muda mrefu na hivyo kuchelewesha malipo ya mawakala.

Vilevile Kamati iliishauri Serikali kulipa fedha za korosho zilionunuliwa na Serikali kwa msimu wa Mwaka 2018/2019 kwa wakulima ambao walikuwa hawajalipwa. Ushauri huo haujatekelezwa kwa maelezo kwamba, wakulima hao hawajalipwa kwa sababu akaunti namba za benki walizowasilisha zilikuwa hazijatumika muda mrefu (*Dormant Account*). Kamati inaamini sababu hii haina msingi wowote kwani benki zinao utaratibu wa kuihisha akaunti ambazo hazijatumika muda mrefu (*Activate Dormant Accounts*).

#### **4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIPIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge lako tukufu kufanya uamuzi sahihi kuhusu hoja ya Serikali kuliomba Bunge kuidhinisha matumizi ya Wizara ya Kilimo na Taasisi zilizo chini yake, Kamati imefanya Uchambuzi wa Mpango na Makadirio

ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Naomba kutoa Taarifa kuhusu matokeo ya uchambuzi huo kama ifuatavyo: -

#### **4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;**

**Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, kwa Wizara ya Kilimo, unajumuisha Mafungu Matatu ambayo ni (Fungu 43) – Wizara ya Kilimo, (Fungu 24)– Tume ya Maendeleo ya Ushirika, na (Fungu 05) – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Mpango huu umeandaliwa kwa kuzingatia: -

a) Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano Awamu ya Tatu (2021/22 - 2025/26);

b) Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya Mwaka 2020;

c) Mwongozo wa Taifa wa kuandaa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

d) Malengo Endelevu ya Maendeleo (SDGs);

e) Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2013 pamoja na

f) Maeneo muhimu ya kuzingatia kama yalivyoanishwa na Serikali ya Awamu ya Tano na ya Sita.

#### **4.2 Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika**,Wizara ya Kilimo kupitia mafungu yake matatu imepanga kutekeleza vipaumbele mbalimbali ambavyo maelezo yake yamefafanuliwa kwa kina kwenye taarifa ya Waziri.

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza malengo yaliyokusudiwa, Wizara ya Kilimo inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 294,162,071,000/=**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 82,914,071,000/=** sawa na **asilimia 28.2** ya bajeti inayoombwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 211,248,000,000/=** sawa na **asilimia 71.8** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, bajeti inayoombwa kuidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 imeongezeka kwa **Shilingi 64,322,263,000/=** sawa na **asilimia 22** ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambayo ilikuwa **Shilingi 229,839,808,000/=**.

Aidha, kwa upande wa Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 kuna ongezeko la **Shilingi 6,148,587,000/=** sawa na **asilimia 7.4** ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambapo Matumizi ya Kawaida yalikuwa **Shilingi 76,765,484,000/=**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeendelea kubaini kwamba kiasi cha Fedha za Maendeleo kinachoombwa kimeongezeka kwa **Shilingi 61,173,676,000/=** sawa na **asilimia 29** ikilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 ambacho kilikuwa **Shilingi 150,074,324,000/=**.

Ongezeko hili linatarajiwa kwenda kuboresha, kukarabati na kujenga skimu za umwagiliaji ili kuongeza tija kwenye kilimo kwa kupunguza utegemezi wa kilimo cha kutegemea mvua.

#### **4.3 Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara kwa kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulifanya ulinganisho wa bajeti ya Wizara ya Kilimo na Mpango wa Maendeleo wa Taifa, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Ulinganisho huo ulilenga kubaini ni kwa kiasi gani ongezeko la bajeti ya Taifa lina athari chanya kwenye ukuaji wa sekta ya Kilimo. Ufafanuzi wa uchambuzi huo umetekelezwa kwa

kutumia jedwali, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji. Katika uchambuzi huo mambo yafuatayo yalibainika: -

a) Bajeti ya Wizara ya Kilimo, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ambayo ni **Shilingi Bilioni 294,162,071,000** sawa na **asilimia 0.08** ya Bajeti yote ya Serikali ambayo kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa 2021/2022 ni **Shilingi Trilioni 36.260/=**.

b) Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 unaonesha ongezeko la bajeti kwa **asilimia 26** ikilinganishwa na Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; wakati Bajeti ya Wizara ya Kilimo, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 imeongezeka kwa **asilimia 22** ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2020/2021; na

c) Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaonesha ongezeko la **asilimia 2.76** katika fedha za maendeleo ambazo ni sawa na **asilimia 36.68** ya Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; wakati bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Kilimo ambayo ni sawa na **asilimia 0.71** ya Bajeti ya Taifa, ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambayo ni **asilimia 0.11**.

## Jedwali 2: Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo dhidi ya Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

BAJETI KUU YA TAIFA 2021/2022			BAJETI YA WIZARA YA KILIMO 2021/2022		
Mgawanyo	Bajeti Kuu (Tsh, Trilioni)	% ya Jumla ya BajetiKuu	Mgawanyo	Bajeti ya Wizara (Tsh. Bilioni)	% ya Jumla ya Bajeti ya Wizara
OC	3,944,164,	10.98	OC	30,817,	0.78
Malipo ya deni la Taifa	10,663,278	29.66	-	-	-
Mshahara	8,150,509	22.68	Mishahara	52,096	0.64
Maendeleo	13,255,855	36.68	Maendeleo	94,068	0.71
<b>Jumla</b>	<b>36,258,806</b>	<b>100</b>	<b>Jumla</b>	<b>294,167</b>	<b>0.81</b>

*Chanzo: Uchambuzi wa randama zilizowasilishwa kwenye Kamati*

#### 4.4 Mambo muhimu ya kuzingatia katika Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2021/2022;

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Kilimo inachangia takribani **asilimia 27.7 ya Pato la Taifa, asilimia 25 ya fedha za kigeni** na inajiri takribani **asilimia 65 ya Watanzania wote**. Vilevile, sekta hii ni chanzo kikuu cha malighafi kwa ajili ya viwanda ambapo huchangia **asilimia 60 ya malighafi ya viwanda**, ni chanzo kikuu cha chakula, mapato kwa wakulima, lise na afya. Licha ya umuhimu wa Sekta ya Kilimo ulioelezwa hapo juu, Rais Samia Suluhu Hassan alipokuwa analihutubia Bunge tarehe 22 Aprili, 2021 alionesha umuhimu ulioko kwenye sekta hii. Aidha Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (*Africa Development Bank*) Akinwumi Andesina, mara kadhaa amenukuliwa akisema;

*"The future Millionnaires and Billionnaires of Africa will not be coming from Oil and Gas Sector, they will be coming from the Agriculture Sector. But I want African countries to be looking at agriculture as a business, not as a way of life"*. Kwa tafsiri isiyo rasmi maana yake ni kuwa ipo fursa kubwa kwenye kilimo endapo nchi za Afrika zitafanya uwekezaji wa kutosha kwenye Sekta ya Kilimo.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na umuhimu huo wa kilimo katika nchi yetu na Bara la Afrika kwa ujumla, Kamati ilifanya tathimini kwa bajeti iliyotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ili kubaini kama umuhimu unaoelezwa wa sekta hii una uwiano na bajeti inayotengwa kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na tija. Tathimini ya Kamati imebaini pamoja na kwamba kuna ongezeko la bajeti kwa **asilimia 22**, bado kilimo hakijapewa uzito unaostahili kutokana na mchango wake kwenye Pato la Taifa. Takwimu zinazoelezea mchango wa Sekta ya Kilimo kwa Pato La Taifa, ajira kwa Watanzania, malighafi kwa ajili ya viwanda na kipato kwa wakulima umetokana na kilimo kinachofanywa na wakulima wadogo na kinajulikana kama kilimo cha kujikimu.

**Mheshimiwa Spika**, naliomba Bunge lako tukufu litafakari endapo Serikali itawekeza vya kutosha kwenye kilimo cha biashara ni manufaa kiasi gani yanaweza

kupatikana kwa Taifa na kwa wakulima? Kwa muktadha huu, Kamati inapendekeza kuanzia Mwaka wa Fedha 2022/2023 Sekta ya Kilimo itengewe bajeti inayoendana na mchango wake kwa Taifa. Pamoja na ushauri huo wa jumla, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua kwa kushughulikia na kuimarisha maeneo yafuatayo: -

#### 4.4.1 Kuongeza Uzalishaji na Upatikanaji wa Mbegu Bora za Kilimo

**Mheshimiwa Spika**, usalama wa mbegu ni usalama wa chakula na usalama wa chakula ni usalama wa nchi. Nchini Tanzania jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora kwa mujibu wa sheria, liko chini ya Wakala wa Mbegu wa Taifa (ASA). ASA ina wajibu wa kuhakikisha mbegu zilizogunduliwa katika vituo vya utafiti zinamfikia mkulima mahali popote nchini kwa wakati, ubora, wingi na kwa bei nafuu. Kwa maana rahisi, ASA ina wajibu wa kuhakikisha usalama wa mbegu unakuwepo nchini. Hivyo, ASA ni Taasisi inayohusika moja kwa moja katika usalama wa chakula wa Nchi.

**Mheshimiwa Spika**, vile vile upatikanaji wa uhakika wa malighafi za viwandani ni lazima uende sambamba na kukuza kilimo na kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali. Uzalishaji wa mazao hayo unategemea upatikanaji endelevu wa mbegu bora. Pamoja na umuhimu huo, ASA inakabiliwa na changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na: -

a) Fedha kidogo zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo;

b) Fedha zilizoidhinishwa na Bunge kutopatikana kwa wakati;

c) Upungufu wa maghala ya kuhifadhi mbegu;

d) Ukosefu wa Hifadhi ya Mbegu ya Kimkakati kwa Taifa (*Strategic Seed Reserve*).

e) Mfumo wa Manunuzi wa Serikali unaongeza changamoto ya upatikanaji wa mbegu kwa wakati hasa kipindi ambacho mbegu huitajika kwa dharura.

#### 4.4.2 Kukuza Kilimo kupitia ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji

**Mheshimiwa Spika**, wakati Rais wa Awamu ya Sita Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akihutubia Bunge, alieleza kuwa " sekta ya kilimo inachangia **asilimia100** ya chakula nchini, **asilimia 60** ya Malighafi ya viwandani, **asilimia 27.7** ya Pato la Taifa na **asilimia 25** ya fedha za kigeni" pamoja na mchango huo mkubwa bado sekta ya kilimo inazalisha kwa tija ndogo kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kilimo cha kutegemea mvua".

**Mheshimiwa Spika**, kilimo cha umwagiliaji ndio njia pekee inayoweza kututoa kwenye tija ndogo ya kilimo na kukifanya kilimo chetu kuwa kilimo cha biashara na kwa kufanya hivyo, uzalishaji na tija katika kilimo vikiongezeka makusanyo ya kodi yataongezeka na hivyo kuongeza Pato la Taifa na mapato ya wakulima yataongezeka. Pia bei ya vyakula itapungua, fursa za ajira katika maeneo ya vijijini na mijini zitaongezeka na upatikanaji wa malighafi za viwanda nao utaongezeka.

**Mheshimiwa Spika**, tafiti zinaonyesha kuna **hekta milioni 29.4** zinazofaa kwa umwagiliaji. Ikiwa mkazo utawekwa kwenye kilimo cha umwagiliaji tunaweza kuongeza uzalishaji na tija kwenye kilimo. Hivi sasa eneo linalotumika kwa umwagiliaji ni sawa na **asilimia 2** ya eneo linalofaa kwa umwagiliaji. Tangu Serikali ilipoongeza bajeti ya umwagiliaji, uzalishaji wa tija kwenye kilimo umeongezeka kwa mazao yafuatayo: -

a) Mpunga kutoka tani 1.8 – 2.0 kwa hekta hadi kufikia wastani wa tani 5.0 – 8.0 kwa hekta;

b) Mahindi kutoka tani 1.5 hadi tani 3.7- 5.0 kwa hekta;

- c) Vitunguu kutoka tani 13 hadi 26 kwa hekta;  
na
- d) Nyanya kutoka tani 5 hadi 18 kwa hekta.

**Mheshimiwa Spika**, utafiti uliofanywa kwa zao la mpunga pekee kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji, umeonyesha tija inayoweza kupatikana endapo **hekta milioni 22** zikilimwa misimu miwili kwa mwaka zinaweza kuzalisha kisio la chini **tani milioni 220**. Thamani ya kila gunia la mpunga la kilo 100 inakadiriwa kuwa **shilingi 65,000/=**, mpunga utakaozalishwa kwa mwaka utakuwa na thamani ya **shilingi Trilioni 143** ambayo ni sawa na Bajeti ya Tanzania kwa takribani miaka 4, na hii ni kabla ya kuongeza thamani na kuuzwa kwenye masoko ya ndani na nje.

#### 4.4.3 Kuimarisha Upatikanaji wa Huduma za Ugani kwa Wakulima

**Mheshimiwa Spika**, huduma za ugani ni huduma ya msingi ambayo inapaswa kutolewa na wataalam wa kilimo kwa wakulima kuhusu kanuni bora za kilimo kwa lengo la kuinua uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa kuongeza thamani kwenye kilimo. Aidha, Maafisa Ugani wanaowajibu wa kutoa elimu na mafunzo kwa wakulima ili kuwajengea uwezo na ujuzi wa kulima kibiashara ili kuongeza tija na uzalishaji kwenye kilimo.

Hata hivyo, huduma za ugani hapa nchini hazijaweza kuleta mafamikia tarajiwa kutokana na wakulima wengi kulima kilimo cha kujikimu kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo upungufu wa Maafisa Ugani. Mahitaji halisi ya Maafisa Ugani nchini ni **21,258** ambapo waliopo sasa ni **7,307** sawa na **asilimia 34** tu ya mahitaji. Takwimu zinaonyesha uwiano wa sasa ni sawa na Afisa Ugani Mmoja kwa wakulima zaidi ya mia sita (1: 600).

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na upungufu huo uliopo, bado Maafisa Ugani hawapati mafunzo ya mara kwa mara, hawana vitendea kazi, hawatumii takinolojia za kisasa,



hawawatembelei wakulima ipasavyo na wengi hawafanyi kazi za ugani kutokana na kupangiwa kazi zingine na Wakurugenzi wa Halmashauri.

Kamati inaamini hali hii imetokana kwa kiasi kikubwa kukosekana tamko la kisheria ambalo linawataka Wakurugenzi kutenga kiasi cha **asilimia 20** ya fedha zinazotokana na tozo ya ushuru wa mazao kurudi kwenye kilimo ili kusaidia kuendeleza shughuli za kilimo hususan huduma za ugani. Tofauti na hali ilivyo sasa ambapo kiasi cha fedha zitokanazo na mapato ya Halmashauri zinazorudi kwenye kilimo zinategemea utashi wa Mkurugenzi wa Halmashauri husika.

#### **4.4.4 Changamoto ya Riba Kubwa zinazotolewa na Taasisi za Fedha kwa ajili ya mikopo kwa wakulima wadogo**

**Mheshimiwa Spika**, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) ilianzishwa chini ya Sheria ya Makampuni Na. 212 ya Mwaka 2012 kwa lengo la kusaidia kuongeza mnyororo wa thamani kwa kutoa mikopo kwa wakulima wadogo kupitia vyama vya ushirika vya msingi. Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ni taasisi ya kifedha na taasisi zote za kifedha zinaongozwa na kusimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania ambapo kazi ya msingi ya taasisi za fedha ni kutengeneza faida ili kuweza kurudisha pesa za wawekezaji kwa kuhakikisha benki hizi hazitoi mikopo kwa biashara ambazo hatarishi (*risk*) yake ni kubwa kama kilimo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha huu, TADB haiwezi kuendesha shughuli zake kwa kutoa mikopo pasipo uhakika wa namna mikopo hiyo itakavyorejeshwa. Pamoja na angalizo hilo mikopo itakayotolewa ni lazima iwe na riba ili benki iweze kujiendesha kwa faida na kurudisha pesa ya wawekezaji. Kwa sababu hiyo haishangazi kuona Benki ya Maendeleo ya Kilimo inatoza riba sawa na benki zingine za biashara ambayo ni kati ya **asilimia 10-20**, lakini pia mkulima anatakiwa kuwa na dhamana pamoja na kukata bima ya mkopo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua changamoto hiyo, Serikali ilianzisha Mfuko wa SAGCOT CATALYTIC TRUST FUND ambao ulianza kufanya kazi rasmi mwezi Mei, 2011 chini ya Sheria ya Mifuko (*Trustee Incorporation Act, Cap 318 R.E 2002*). Malengo ya msingi ya mfuko ni pamoja na: -

**Kwanza**, kutoa mitaji ya upatikanaji wa masoko kwa mazao ya wakulima wadogo, mitaji ambayo hutolewa kama mikopo yenye masharti nafuu au mikopo isiyo na riba, ili irudishwe pindi tu bishara hizo zinapopata mitaji kutoka sekta binafsi au kupitia soko la hisa.

**Pili**, kutoa dhamana za mikopo kwa makampuni mbalimbali ili kuyawezesha makampuni hayo kupata mikopo katika taasisi mbalimbali za fedha ili kuboresha uzalishaji katika mashamba ya wakulima wadogo kupitia "*Loan Guarantee Fund*";

**Tatu**, kutoa mikopo isiyo na riba kwa miradi inayolenga kupunguza gharama za ufanyaji biashara zilizoko nje ya uwezo wa wawekezaji au wakulima wadogo hususan miundombinu wezeshi ya kilimo shambani ikiwemo barabara za ndani, madaraja madogo, skimu za umwagiliaji; na

**Nne**, kutoa ruzuku kwa wakulima wadogo kupitia vyama vya ushirika vya msingi ili kusaidia wakulima wadogo kushiriki kikamamilifu katika minyororo ya thamani ya kilimo na kupata tija na faida kupitia dirisha la "*Matching Grant Fund*" ili kutatua changamoto za upatikanaji wa huduma na uwekezaji unaolenga kumuwezesha mkulima mdogo kufikia mahitaji ya masoko kwa viwango pamoja na ubora wa mazao yake.

**Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha huu, SAGCOT CATALYTIC TRUST FUND, sio mbadala wala mshindani wa mabenki na taasisi zingine za fedha katika utoaji mikopo katika kilimo, bali inatumika kama chombo maalumu kinacho-chochea taasisi zingine za fedha /mabenki kutoa

mikopo kwa wakulima wadogo kwa riba isiyozidi **asilimia 6** na urejeshaji wa muda mrefu bila kuvunja taratibu za Benki Kuu. Kwa kutambua umuhimu wa chombo hiki, Serikali iliingiza SAGCOT CATALYTIC TRUST FUND katika Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2015/16 - 2020/22) kama mradi wa kimkakati na kuitengea bajeti ya **Shilingi bilion 894** ambazo hazijawahi kutoka hadi hivi leo ninapowasilisha taarifa hii.

#### **4.4.5 Changamoto ya Upotevu wa Mazao baada ya kuvunwa**

**Mheshimiwa Spika**, Sera ya Taifa ya Kilimo (2013) inatambua kuwa, mojawapo ya changamoto za sekta ya kilimo ni upotevu wa mazao kabla na baada ya kuvuna unaokadiriwa kuwa kati ya **asilimia 30-40** kwa mwaka kwa mazao ya nafaka. Aidha, upotevu mkubwa unatokea kwenye mazao yanayoharibika haraka kama mazao ya matunda, mboga na mazao jamii ya mizizi. Pamoja na jitihada za Serikali za kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna kwa kujenga miundombinu ya kuhifadha mazao kama maghala na vihenge, bado kuna changamoto ya upotevu wa mazao unaotokana na ubovu wa barabara za vijijini ambazo hutumika kusafirisha mazao kutoka shambani hadi sokoni na hivyo kuathiri mnyororo mzima kuanzia ngazi ya uzalishaji hadi mlaji.

Upotevu wa mazao baada ya kuvuna ni mkubwa wakati wa msimu wa mavuno ambapo barabara nyingi kwa sehemu kubwa ya Tanzania huwa hazipitiki na hivyo kupelekea mazao mengi kuharibikia njiani. Hasara za moja kwa moja zitokanazo na upotevu wa mazao ni pamoja na: -

a) Wakulima kulazimika kuuza bidhaa zao kwa bei ambayo hailingani na bei ya soko na hivyo kupunguza pato la wakulima na kuchangia kuongezeka kwa umaskini;

b) Kupunguza ubora wa bidhaa na kusababisha bei ya mazao kushuka katika soko na hivyo kuongezeka kwa bei ya vyakula; na

c) Mwenendo wa upotevu wa mazao baada ya kuvuna huwakatisha tamaa wakulima na taasisi za fedha kuwekeza kwenye sekta ya kilimo kwa sababu hakuna uhakika wa kupata mapato yanayolingana na uwekezaji uliofanywa.

#### 4.4.6 Kuongeza Uzalishaji wa Zao la Korosho,

**Mheshimiwa Spika**, korosho ni moja ya mazao makuu ya biashara hapa nchini na inayolingizia Taifa fedha za kigeni kiasi cha **Dola za Marekani milioni 585.1** sawa na shilingi za Tanzania **trilioni 1.3**. Licha ya mchango wa zao la korosho kwenye uchumi, uzalishaji wa zao hili umeshuka kwa **asilimia 34** kutoka **tani 313,826** kwa uzalishaji wa msimu wa mwaka **2017/2018** na kufikia **tani 206,719** kwa msimu wa mwaka **2020/2021**.

Pamoja na sababu nyingine, sababu kubwa iliyopelekea kushuka kwa uzalishaji wa korosho ni **marekebisho yaliyofanywa kwenye Sheria ya Fedha ya Mwaka 2018. (Finance Bill Act, 2018)** na kusitishwa kwa Shughuli za Mfuko wa Wakfu wa Kuendeleza Tasnia ya Korosho (CIDTF).

**Mheshimiwa Spika**, baada ya marekebisho ya Sheria ya Fedha (**Finance Bill Act, 2018**) wakulima wamekuwa wakijigharamia pembejeo kwa **asilimia 100** ambapo hulazimika kununua pembejeo kwa pesa taslimu au mkopo. Utaratibu huu umeonekana kutoleta matokeo mazuri kwani kumekuwepo na matumizi madogo ya pembejeo kunakosababishwa na wakulima kushindwa kumudu gharama za pembejeo, kudorora kwa huduma za ugani katika maeneo yanayolima korosho, kuchelewa kukamilika kwa ujenzi wa maghala ya kuhifadhia korosho yaliyokuwa yanagharamiwa na mfuko katika wilaya za Mkinga, Tunduru

na Mkuranga na hivyo kupelekea uzalishaji wa korosho kushuka kutoka **tani 313,826** zilizozalishwa mwaka **2017/2018** hadi kufikia tani **206,718** Mwaka **2020/2021**.


**Mheshimiwa Spika**, vile vile kusitishwa kwa Shughuli za Mfuko wa Wakfu wa kuendeleza Tasnia ya Korosho kumepelekea kutotekelezwa kwa majukumu ya Mfuko wa Wakfu ambayo yalikuwa kugharamia shughuli za pamoja za uendelezaji wa tasnia ya korosho (*Shared functions*) kwa kugharamia huduma za ugani na pembejeo kwa wakulima wa korosho nchini, kugharamia utafutaji wa masoko ya korosho ghafi na zilizobanguliwa nchini, kuhamasisha na kuwezesha ubanguaji wa korosho ndani ya nchi, na kugharamia utafiti wa mnyororo wa thamani wa zao la korosho. Aidha, fedha za *Export Levy* kupitia mfuko wa wakfu zilisaidia wakulima kupatiwa ruzuku ya **asilimia 50**. Vilevile, wakati wa msimu wa 2017/2018 ruzuku hiyo iliongezeka na kufikia **asilimia 100** na kupelekea uzalishaji wa zao la korosho kuongezeka kutoka **tani 127,947** mwaka **2012/2013** hadi kufikia kiasi cha **tani 313,826** mwaka **2017/2018**.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuelewa vyema dhana ya kushuka kwa uzalishaji wa zao la korosho nchini, ufafanuzi wa takwimu unaonyesha hapa chini kupitia Jedwali namba 3.

**Jedwali 3: Mwenendo wa matumizi ya pembejeo (Salfa) na uzalishaji wa korosho ghafi kuanzia msimu wa 2012/2013 hadi msimu wa 2020/2021**

Msimu	Sulphur ya Unga (Tani)	Viuatilifu vya Maji (Lita)	Uzalishaji wa Korosho Ghafi (Tani)
2012/2013	5,000	182,230	127,947
2013/2014	5,000	346,300	129,823
2014/2015	8,000	300,000	198,114
2015/2016	10,000	160,000	155,245
2016/2017	15,000	255,000	265,238
2017/2018	18,000	310,000	313,826
2018/2019	12,352	339,009	225,154
2019/2020	8,610	448,258	232,682
2020/2021	8,731	182,438	206,719

Mchoro 1: Mwenendo wa Matumizi ya Pembejeo na Uzalishaji wa Korosho Ghafi kuanzia Msimu wa 2012/2013 hadi Msimu wa 2020/2021;



*Chanzo: Taarifa ya Bodi ya Korosho iliyowasilishwa kwenye Mkutano wa Wadau wa Korosho tarehe 23 Aprili, 2021*

#### 4.4.7 Changamoto za Ushirika Nchini;

**Mheshimiwa Spika**, ushirika ni imani ambayo uunganisha wanachama katika kufikia malengo ya pamoja waliojiwekea. Ushirika ni njia ya uhakika ya kuwawezesha wanachama kuwa na uwezo mkubwa wa kutatua matatizo yao ya kiuchumi na kijamii kwa kutumia juhudi zao za pamoja katika kufikia malengo ambayo yasingefikiwa kwa juhudi za mtu mmoja mmoja.

Kufuatia imani hii ya kufikia malengo kwa pamoja, nchini Tanzania manufaa ya ushirika yamejidhihirisha mahala pengi nchini katika maeneo na nyakati tofauti. Baathi ya vyama vya ushirika vilivyowahi kufanya vizuri ni pamoja na Chama Kikuu cha Ushirika Shinyanga, (SHIRECU), Chama Kikuu cha Ushirika Mwanza (NCU-1984), Chama Kikuu cha Ushirika Kilimanjaro (KNCU- 1984), Chama Kikuu cha Ushirika Kagera (KCU- 1990) na Mamlaka ya Mkonge.

Vyama hivi vimewahi kufikia mafanikio makubwa yakiwemo kuinuia kipato cha wanaushirika, kufadhili masomo katika ngazi mbalimbali kwa familia za wanaushirika, kuanzisha viwanda vya kuchakata mazao ya wanaushirika na kujenga maghala ya kuhifadhia mazao baada ya kuvunwa. Pamoja na mafanikio hayo, katika miaka ya hivi karibuni ushirika umepoteza imani kutokana na kukithiri kwa vitendo vya ubadhirifu, wizi na uporaji wa mali za vyama vya ushirika. Ili kukabiliana na hali hiyo, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ili kurejesha imani kwa wanaushirika kwa kurejesha mali za vyama vya ushirika zilizokuwa zimeuzwa kiholela na nyingine kuporwa. Kamati inatambua na kupongeza juhudi zinazochukuliwa na Serikali, hata hivyo Kamati ina maoni kuwa, ili kuongeza ufanisi na usimamizi katika Vyama vya Ushirika Serikali ina wajibu wa kuhakikisha vyama vikuu vya ushirika vinatekeleza majukumu yake kwa kuvihudumia vyama na wanachama wake kwa kusimamia uzalishaji, upatikanaji wa pembejeo, huduma za ugani, masoko na kuajiri watendaji wenye sifa kwa kuzingatia ukubwa wa chama na miamala inayofanywa.

## **5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupitia Taarifa za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Taarifa za Utekelezaji wa bajeti inayomalizika na Maombi ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo: -

## 5.1 Kuimarisha bajeti kwa ajili ya sekta ya Kilimo

Pamoja na mchango wa Sekta ya kilimo katika Pato la Taifa, ajira kwa wananchi na malighafi kwa ajili ya viwanda, bado Serikali haijawekeza ipasavyo kuimarisha ukuaji wa sekta ya kilimo. Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 sekta ya kilimo imetengewa bajeti **chini ya asilimia 1** ambayo ni sawa na **asilimia 0.08** ya bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/2022 pungufu ya makubaliano ya Azimio la Maputo na badae Malabo linalotaka nchi wanachama kutenga angalau **asilimia 10** ya Bajeti ya Taifa. Kamati inashauri Serikali kutenga bajeti ya kukidhi kutekeleza programu mbalimbali za kuimarisha sekta ya kilimo.

## 5.2 Kuwawezesha Maafisa Ugani kutekeleza majukumu yao;

Kufuatia upungufu wa Maafisa Ugani uliopo na kwa kutambua umuhimu wa Maafisa Ugani katika kuongeza uzalishaji kwenye kilimo. Kamati inaishauri Serikali kuajiri Maafisa Ugani ili kukidhi mahitaji ikiwa ni pamoja na kuwatengea rasilimali fedha, kuwapata vitendea kazi, na kuwapa mafunzo ya mara kwa mara ya kuwaimarisha kufanya kilimo cha kisasa; Ili kuwawezesha Maafisa Ugani, Kamati inashauri Serikali iangalie uwezekano wa kutunga sheria itakayozitaka Halmashauri za Mikoa na Wilaya kurudisha sehemu ya tozo zitokanazo na mazao ya kilimo kwa ajili ya kuendeleza shughuli za kilimo tofauti na hali ilivyo sasa ambapo maamuzi hayo hayajawekewa masharti ya kisheria na yanategemea utashi wa Mkurugenzi na Baraza la Madiwani.

## 5.3 Kuimarisha Utafiti na Uzalishaji Mbegu

Kamati inatambua na kupongeza juhudi zinazochukuliwa na Serikali kujengea uwezo Wakala wa Mbegu (ASA), pamoja na juhudi hizo ni muhimu kwa Serikali kutambua kuwa kazi ya uzalishaji wa mbegu bora lazima iendane na utafiti. Pamoja na majukumu haya kuhitaji fedha za kutosha, bado fedha zinazotengwa hazitoshelezi kukudhi



mahitaji. Hivyo Kamati inashauri ASA kuongezewa bajeti na fedha zinazotengwa kutolewa kwa wakati ili kuiongezea ASA uwezo wa kuzalisha mbegu bora za mazao.

Aidha, ni maoni ya Kamati kuwa nguvu kubwa ielekkezwe kwenye uzalishaji wa mbegu za mafuta ya alizeti, mchikichi na ngano ili kupunguza gharama kubwa ya fedha za kigeni inayotumika kuagiza bidhaa hizo nje ya nchi.

#### **5.4 Kurejesha Mfuko wa Kuendeleza Tasnia ya Korosho;**

Ili kuimarisha uzalishaji wa zao la korosho ambao umekuwa ukishuka kwa miaka mitatu mfululizo, Kamati inashauri Serikali kuona uwezekano wa kurejesha Mfuko wa kuendeleza tasnia ya korosho. Aidha, Kamati inasisitiza kwamba ili Mfuko huo uweze kuleta tija ni vyema kasoro zilizopelekea kufutwa kwa mfuko huu kurekebisha.

#### **5.5 Kukabiliana na changamoto ya upotevu wa mazao baada ya kuvunwa;**

Kamati inatambua juhudi kubwa inayofanywa na Serikali katika kupunguza kiasi cha upotevu wa mazao baada ya kuvunwa kwa kujenga vihenge na maghala ya kuhifadha mazao. Hata hivyo upotevu mwingi wa mazao baada ya kuvunwa husababishwa na miundombinu mibovu ya barabra. Ili kukabiliana na changamoto hii, Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha kifedha Mamlaka ya Barabara Vijijini (TARURA) kwa kupewa fedha za kutosha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya barabara zitakazosaidia kutoa mazao ya wakulima shambani.

#### **5.6 Namna Bora ya kuwezesha wakulima wadogo kupata mikopo yenye riba nafuu;**

Kwa kuwa imekuwa ni vigumu kwa taasisi za fedha na benki kukopesha wakulima wadogo kwa riba chini ya **asilimia 10** ambayo kitaalamu inaelezwa kuwa na tija katika kilimo.

Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu mahusus wa kuuwezesha upatikanaji wa mikopo rafiki kwa sekta ya kilimo. Aidha, kwa kuanzia Kamati inaishauri Serikali kutathimini na kuona uwezekano wa utekelezwaji wa SAGCOT CATALYTIC TRUST FUND kama ilivyoelezwa katika Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2015/16/2020/22).

Vilevile, Kamati ina maoni kuwa kwa kuwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo ni benki ya biashara na hivyo imeshindwa kukidhi mahitaji ya wakulima wadogo, Kamati inaishauri Serikali kuona uwezekano wa kuifanyamarekebisha Benki ya Maendeleo ya kilimo kwa kuongeza kitengo mahususi kwa ajili ya kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa wakulima.

#### **5.7 Kuimarisha Utengaji Bajeti ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji;**

Kwa kuwa eneo la Umwagiliaji linalofaa kwa kilimo ni **hekta milioni 29.4** na kwa kuwa ufinyu wa bajeti umepekelea kuweza kutumia eneo linalofaa kwa umwagiliaji kwa **asilimia 2 tu**. Kamati ina maoni kuwa kwa tahimini iliyofanywa inayoonyesha tija itakayopatikana kutokana na kilimo cha umwagiliaji ni vyema Serikali ikatambua fursa iliyopo na kutenga bajeti ya kutosha itakayosaidia kuongeza ufanisi na kuimarisha uratibu wa shughuli za umwagiliaji kwa kuipatia vitendea kazi Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa ajili ya kuongeza matumizi ya eneo linalofaa kwa umwagiliaji, kukamilisha ujenzi wa skimu za umwagiliaji pamoja na kukarabati skimu chakavu.

#### **5.8 Kuimarisha Ushirika Nchini;**

Ili kuhakikisha ushirika wa hiari ambao ndio msingi wa Imani yenyewe Kamati inaishauri Serikali: -

a) Kuhamasisha na kuelimisha wakulima umuhimu wa kujiunga kwenye vyama vya ushirika;

b) Kuboresha uongozi, kudhibiti wizi na ubadhirifu ndani ya vyama vya ushirika;

c) Kuhakikisha vyama vya ushirika vinasimamiwa na sheria itakayowalinda na kuwanufaisha wanaushirika na hivyo kuchangia ipasavyo katika ustawi wa wanachama na Taifa kwa ujumla.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika kwa jinsi ambavyo mmekuwa mkituongoza kwa kipindi chote cha Mkutano wa Bunge la Bajeti na kuliwezesha Bunge letu kutimiza wajibu wake wa kuisimamia Serikali kwa niaba ya Wananchi kwa mujibu wa Katiba. Aidha, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa katika kipindi chote Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao walioyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara pamoja na kuandaa taarifa hii hadi kukamilika kwake. Kutokana na kazi kubwa walioifanya natamani kuwatambua kwa kuwataja majina yao. Hata hivyo, kutokana na utaratibu tuliojiwekea hapa Bungeni naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*). Majina ya Wajumbe hao ni kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Athuman Almas Maige, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo - Mjumbe
4. Mhe. Prof. Patrick Aloysi Ndakidemi, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Balozi. Dkt. Bashiru Ally Kakurwa, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Charles John Mwijage, Mb - Mjumbe
9. Mhe. January Yusuf Makamba, Mb - Mjumbe

10. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Christopher O. Ole Sendeka, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Munde Tambwe Abdallah, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Benaya Liuka Kapinga, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Maryam Azan Mwinyi, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Jackson Gideon Kiswaga, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Janejelly James Ntate, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Mohamed Suleman Omari - Mjumbe
22. Mhe. Tumain Bryceson Magessa, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Michael Mwita Kembaki, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Furaha Ntengo Matondo, Mb - Mjumbe
25. Mhe. Yahya Ali Khamisi, Mb - Mjumbe
26. Mhe. Yustina Arcadius Rahhi, Mb - Mjumbe
27. Mhe. Mrisho Mashaka Gambo, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Kilimo Mhe. Profesa Aldolf F. Mkenda (Mb), Naibu Waziri Mhe. Hussein M. Bashe, (Mb), Katibu Mkuu Ndg. Andrew W. Massawe, Naibu Katibu Mkuu Profesa Siza D. Tumbo pamoja na Wataalamu wote wa Wizara kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini si kwa umuhimu napenda kumpongeza Katibu wa Bunge, Ndg. Nanelwa Mwihambi kwa kuteuliwa kuwa mwanamke wa kwanza kuongoza muhimili wa Bunge, namshukuru pia Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Kamati za Fedha Ndg. Michael Chikokoto kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kwa namna ya kipekee naishukuru Sekreterietu ya Kamati ambao ni Ndg. Rachel Nyega na Ndg. Virgil Mtui wakisaidiwa na Ndg. Waziri Kizingiti, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, ninaunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

DK. Christine G. Ishengoma, Mb  
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA  
BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI**

24 ME1, 2021

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Almas Maige kwa niaba ya Kamati.

Kabla hatujaendelea na uchangiaji niwatambue pia Wadau muhimu sana wa Maendeleo katika Wizara ya Kilimo na wageni pia wa Mheshimiwa Waziri, wafuatao: Ndugu Jacqueline Machangu, huyu ni wa *IFAD*. Karibu sana. Hawa wametoa fedha nyingi sana kusaidia masuala ya mbegu. Karibuni sana *IFAD*. (*Makofi*)

Dkt. Jacqueline Mkindi, huyu kutoka *TAHA*. Karibu sana popote pale ulipo. Ndugu CK Richard wa *European Business Group*. Ndugu Gilman Kasiga wa *General Electric* na Ndugu Francis Nanai wa *TPSF*, karibuni sana. (*Makofi*)

Sasa wakati Mheshimiwa Waziri wa Kilimo anatoa hoja yake alisoma *figure* ya Wizara hii anayoiomba na bilioni 2,094,162,071. Alikosea, atarekebisha vizuri zaidi wakati wa kuhitimisha hoja, *exact figure* yake. Kwenye vitabu vyetu ni bilioni 294,162,071,000, lakini Mheshimiwa Waziri wakati wa kuhitimisha utaiweka vizuri zaidi kwa ajili ya kumbukumbu zetu za *Hansard*.

Sasa wachangiaji ni wengi sana, kwa hiyo dakika unazozipata jitahidi moja kwa moja uende kwenye

unachotaka kukisema, tujitahidi kwa dakika saba, saba endapo zitatoshwa. Jipange tu vizuri dakika saba ni nyingi. Zaidi wewe jipange kwa dakika tano, ukiweza saba basi inakuwa vizuri. Tunaanza sasa.

Mheshimiwa Joseph Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Shally Raymond kama nilivyosema. Karibu sana utufungulie.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuwa mchangiaji wa kwanza kwenye hotuba hii muhimu inayawahusu asilimia 80 ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameweka vipaumbele vya majukumu ya Wizara katika bajeti ya mwaka huu na kipaumbele namba tano (5) ni soko la mazao ya kilimo. Ningepata fursa, ningeweza kurekebisha hotuba yake na kusema kipaumbele namba moja (1) kiwe soko la mazao ya mkulima. Nasema hivi kwa nini? Kwa sababu mwarobaini wa Sekta ya Kilimo ni soko. Msingi wa kilimo ni soko. Katika mnyororo wa kilimo kuna shughuli mbalimbali ikiwemo uzalishaji, usafirishaji, usindikaji, masoko, lakini soko ndiyo dereva anayeendesha Sekta ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale ambapo mkulima ana uhakika wa soko, pale ambapo mkulima atakuwa anauza zao lake kwa faida, hatahitaji kukusubiri wewe umletee Afisa Ugani, atamtafuta yeye mwenyewe, atamwajiri yeye mwenyewe kwa sababu kuna faida kwenye kilimo. Ili kilimo kiwe na faida lazima tuwekeze kwenye masoko. Ukishawekeza kwenye soko una-*create incentive* ya mkulima kuzalisha, akiona inamlipa atatafuta Maafisa Ugani, huko ndiko tupeleke fedha.

Mheshimiwa Spika, ili kilimo kiwe na faida lazima tuwekeze kwenye masoko. Ukishawekeza kwenye soko una-*create incentive* ya mkulima kuzalisha akiona inamlipa atatafuta maafisa ugani, huko ndiko tupeleke fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakupa mfano, kwenye Bunge lako kwa miaka yangu yote sita sijawahi kumuona Mbunge anayehamasisha vijana wakanunue bodaboda, lakini vijana wanaenda kununua bodaboda kwa sababu, bodaboda zinawalipa, hiyo ndiyo *essence* ya kuwekeza kwenye kitu kinacholipa. Hatujafanya *promotion* ya bodaboda nchi hii, lakini Watanzania vijana wetu wanawekeza kwenye bodaboda na sio kwenye kilimo cha mahindi; hawawekezi kwenye maharage kwa sababu, maharage hayalipi kwa sababu hatujawekeza kwenye soko. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe Mheshimiwa Waziri abadilishe vipaumbele vyake kipaumbele namba moja kufanya mapinduzi ya kilimo nenda kaweke kwenye soko. Soko ndio lita-*create demand* ya maafisa ugani, lita-*create demand* ya *processing*, n.k. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, changamoto ya kwenye soko ni nini? Moja changamoto Mheshimiwa Waziri vitu ambavyo anatakiwa kuvijua ni vitatu; changamoto ya kwanza kwenye soko ni upatikanaji wa masoko yenyewe ya mazao. Mwaka jana wakulima wa Mkoa wa Ruvuma wameibiwa sana fedha zao, wamedhulumiwa sana mahindi kwa sababu, hatuna soko la uhakika la mazao ya mahindi. Wameenda kuuza kwa msanii mmoja pale Mkako mamilioni ya fedha yamepotea. Mheshimiwa Waziri ajue changamoto ya kwanza ni upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, changamoto ya pili kuhusu masoko ya mazao ya kilimo ni miundombinu ya masoko ya mazao ya kilimo. Na tunapoongea miundombinu ni dhana pana na sitaweza kuifafanua kwa kina, lakini Profesa Mkenda na Ndugu yangu Mheshimiwa Bashe ni wabobezi kwenye eneo hili. Tukisema miundombinu ya kilimo tuangalie maghala na maeneo ya kuhifadhia mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, soko lina *specifications* zake. Soko la mahindi ya Kenya wanataka mahindi ambayo hayana sumu kuvu, ili uweze kukidhi hitaji hilo lazima uwe na uhifadhi ambao utasaidia mahindi yako yanapokwenda Kenya yawe

hayana sumu kuvu. Hiyo ndio miundombinu ya masoko, tuwekeze kwenye maghala na vifaa vya kuhifadhi ubora wa mazao yetu ili yawe shindani kwenye masoko tunayoyataka. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini eneo la pili kuhusu miundombinu ni miundombinu ya barabara. Hii imefafanuliwa na Mwenyekiti wa Bajeti amesema. Kwa maslahi ya muda nitaruka eneo moja muhimu sana la miundombinu ya masoko naomba niende kwenye mfumo wa masoko.

Mheshimiwa Spika, mifumo ambayo tunaitumia kuuza mazao yetu ipo mingi, lakini hapa nitaitaja mitatu; tuna mfumo wa kilimo mkataba, tuna mfumo wa stakabadhi za ghala (*warehouse receipt system*), tuna mfumo wa *TMX* ambao nadhani tutakuwa tumeuchukua Ethiopia. Hii mifumo mitatu ningepeta nafasi ningefafanua kwa kina faida na hasara zake. Lakini namuomba Mheshimiwa Waziri, Profesa Mkenda, naomba nenda kafanye *assignment* kuhusu kilimo mkataba, faida zake ni zipi. Moja ya faida muhimu ya kilimo cha mkataba kinakusaidia ku-*meet demand* za soko *in terms of quality* na *quantity*. Lakini pia kinakusaidia kupata ku-*raise capital* ya kuzalisha. Wakulima wengi hawana mitaji na hatuna namna ya kuwasaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini mfumo wa soko la stakabadhi ghalani hautekelezwi kwa mujibu wa kanuni na sheria zilizowekwa kuhusu soko la stakabadhi ghalani. Stakabadhi ghalani ya Tanzania imekuwa soko la kukusanyia mazao, hakuna stakabadhi ya ghala pale. Mkulima hapati pembejeo, mkulima hapati mbegu bora, hapati mbolea, hapati mtaji wa kwenda kulima, tunaita stakabadhi za ghala sio stakabadhi ya ghala hiyo, hiyo ni *aggregation center*, hiyoni *collection center* ya mazao sio stakabadhi ya ghala kwa sababu, ai-*add value* ya kutosha kwa mkulima. Mheshimiwa Waziri naomba ukafanyie *assignment* kwenye eneo hilo.



Mheshimiwa Spika, lakini tatu kafanyie *assignment* kwenye suala la *TMX*. Je, tunatumia *modal* gani ya *TMX*? Je, *TMX* ni *complimentary* ya *warehouse receipt system* au ni kitu kinachosimama peke yake? Unawezaje ku-*implement TMX* katika mazingira yetu kama huna maghala yenye ubora? Kama huna mifumo ya teknolojia inayoweza kukusaidia kuweza kuingia kwenye masoko shidani?

Mheshimiwa Spika, muda ni mchache sana, *agenda* hii ni pana. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Makofi hayo hayatoshi Waheshimiwa Wabunge. Hongera sana Mheshimiwa Mhagama, umetufungulia vizuri mjadala wa kilimo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri, ni mkulima Mheshimiwa, ni vizuri mnavyotembelea mikoani mkatembelea na Waheshimiwa wakulima mkaona wanavyojitahidi. Mkulima mwingine kule ni Mheshimiwa Jenista Mhagama pia namfahamu ni mkulima mzuri sana wa mahindi na ni mfugaji pia wa ng'ombe, eeh, na samaki pia Mheshimiwa Mhagama yule wa kule, Mheshimiwa Joseph anafuga kwa hiyo, kilimo kinaendelea.

Mheshimiwa Shally Raymond, utafuatiwa na Mheshimiwa Njalu Silanga.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

**SPIKA:** Kengele itakuwa moja tu baada ya dakika saba.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, sawa, ahsante. kipekee namshukuru Mungu kwa siku ya leo na zaidi sana niseme nafurahi na ninawashukuru wageni kutoka Kilimanjaro kwenye Jimbo la Mheshimiwa Profesa ambao wale kwa kweli ni mabosi wangu kazini. Na leo wataniona nikichangia *live* mubashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nipongeze sana Profesa kwa hotuba ya kurasa 143 ambayo imesheheni kila jambo la kilimo. Na niseme kwamba, yote ni mazuri, lakini sasa sisi tunafanya nyongeza na maombi. Naona kabla sijasahau nianze na maombi, wametaja vitu vizuri, mbegu za maparachichi, wametaja mbegu za alizeti, wametaja mbegu za maharage, yote hayo yametajwa hapa ndani, lakini hayajafikia hata kule Rombo hayajafika.

Mheshimiwa Spika, sasa niombe kupitia kwako tuweze kupatiwa mbegu hizo. Maparachichi yale nikayasambaze haraka sana na mbegu zote ambazo ni nzuri, lakini zaidi sana watupatie mbegu ya kahawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TACR*/iko Kilimanjaro unaifahamu, lakini tunaambiwa kwenye hotuba waliosambaziwa mbegu za bure ni wakulima 220 tu; ni wachache ni tone tu la maji kwenye bahari. Naomba sasa ikiwapendeza watusambazie mbegu hizo, wamekua wakiitisha sana semina hapa za wakulima, lakini wakulima wa Kaskazini wa kahawa hatujafikiwa. Kwa hiyo, tunaomba elimu hiyo, ili tuweze kwendanayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina kila sababu ya kumshukuru Mungu kwamba, sisi Tanzania tumekuwa na baraka miaka mitano iliyopita hatukuwa na njaa na mpaka tumegawa chakula na tulizalisha zaidi asilimia 126, hiyo ni neema pekee. Kwa hiyo, tulipata shida ya mafuta na kama tulipata shida ya mafuta mwanamke hawezi kutofautishwa na mafuta ya kupika, pale ambapo huna chochote cha kupika unatupa kitunguu kwenye mafuta unafunga mlango, watoto wanasikia kikiungua wanadhani unapika pilau kumbe hamna kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninawaomba hii mbegu ya alizeti waliyozungumzia isambazwe kote kwenye kaya zote Tanzania, kila mwanamke akizalisha debe moja la alizeti tumejikomboa, hatutangoja mafuta kutoka bandarini yanayoshushwa ambayo ni ya kiwango cha chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ametueleza katika vipaumbele vyake, ameeleza Mheshimiwa Waziri kwamba, anatamani kuona alizeti inazalishwa kwa wingi na hapa Dodoma kutakuwepo na mashamba ya mfano. Na nawaombea Wabunge wote wapate eka mbili-mbili hapa Dodoma, hapa kwako, ipitishwe kwenye halmashauri yako tukalime hiyo alizeti yawe mfano. kila Mbunge awe na shamba, asiwe tu Mbunge wa kuongea kwenye karatasi, haitusaidii sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa vile wewe ni diwani wa huku nakuomba sana utufikirie Wabunge wenzio tuweze kwenda kulima. Kwa sababu, amesema mbegu hiyo nzuri ya *RECORD* ya alizeti mpaka sasa imesambazwa kwenye mikoa mitano tu ikiwepo Mbeya na hiyo iko kwenye ule ukurasa wa 31, Kigoma, Dodoma mpo, Morogoro na Singida, huko kwingine je?

Mheshimiwa Spika, natamani kuona kila kaya. Na haya mafuta yaitwe, ikimpendeza sana Mheshimiwa Waziri, amuombe mama Rais Samia Suluhu Hassan, Jemadari wa nchi hii, aweze kuitwa mafuta yake yaitwe Samia. Tumechoka kula mafuta ya Korie na ya nini hayana viwango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninalotaka kumuomba tu Waziri wetu wa Kilimo, Profesa Mkenda, ni kuhusu kilimo hai (*Organic Agriculture*). *Organic agriculture* au mazao yanayozalishwa kwa kilimo hai yamekuwa na bei kubwa sana nchi za nje. Kahawa inayozalishwa katika viwango hivyo inafika hata kilo moja shilingi 10,000 ambapo bei ya kawaida *Arabika Coffee* ambayo ni nzuri kabisa ni shilingi 4,000. Na ninazungumzia *Arabika Coffee* kwa sababu, Kahawa ya Arabika Kilimanjaro sisi tunalima Arabika na tunalima katika tambarare ya Mlima Kilimanjaro ambayo ardhi yake imepata *volcano* kidogo. Ndio kahawa ambayo ina-*blend* kahawa zote duniani ili kuipa *aroma* nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini sasa kahawa hii watu baada ya kuona ni shida sana kulima wameamua kung'oa ile kahawa na sasahivi watu wanalima ndizi badala ya kahawa.

Nimuombe sana Profesa atusaidie na ana Katibu mzuri tu, Katibu Mkuu mzuri ambaye anayajua hayo maeneo, tuweze kurudisha tena hili zao la kahawa katika njia yake nzuri kwa sababu, wengi wa miaka hiyo wamesomeshwa na zao la kahawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini bahati ya kahawa ya arabika unaweza kuotesha mazao mengine, ni *inter-cropping*. Kwa hiyo, haizuwii ndizi kuoteshwa, haizuwii maharage kuoteshwa, haizuwii mahindi kuoteshwa. Kwa hiyo, kwenye kahawa hizo unaweza ukalima mazao mengi na ikawa ni faida kwa familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazungumzia hivyo kwa sababu, natoka eneo ambalo watu mashamba yao ni kidogo na yanaitwa vihamba. Kihamba kikubwa kabisa tena cha tajiri ni eka saba, sasa wengine wote ni eka tatu, mbili na moja na nusu na wote wanategemea hayohayo. Nimewaona wadau wa kilimo hapa, nimemsikia Jaqueline yupo, tunaomba basi afike na watusaidie tulime kahawa hizo pamoja na haya mazao ya *horticulture*. Zao mojawapo ambalo naliomba sana ni zao la parachichi, lakini pia tunaomba hata hii migomba yetu iweze kuboreshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakubaliana na mimi kwamba, zao la mgomba linavunwa mwaka wote mzima, yani vijana wanakwambia *24/7 annually*. Kila siku ndizi inakatwa na ndizi itaota, lakini unakuta sasa wasipopelekwa vizuri katika kulea migomba hii inatoa mikungu midogo sana ambayo haina tija. Nilikuwa naomba sasa ili kilimo hiki kiweze kuwa cha tija, tuweze kupatiwa mbegu ambazo zinatoa mikungu mikubwa, lakini pia tuweze kupatiwa maafisa ugani ambao watakuwa kama wale wa zamani; maafisa ugani wa zamani walikuwa wanajua kaya fulani ina migomba mingapi, kaya fulani ina kahawa ngapi, kaya fulani inazalisha kiasi gani na kwa pamoja sasa ndio inaweza kuleta *summation*, yaani junla ya mavuno yote ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuna mazao ambayo yapo tu siku zote, ni kama mazao ya mtama yanalimwa kidogo sana

kwenye tambarare, lakini muhogo umekuja na sisi wachaga tunaogopa mihogo kwa sababu, mihogo tunaogopa ina sumu, lakini nasikia kuna mihogo mizuri imekuja ambayo ni salama.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ah sante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Shally Raymond. Amemalizia vizuri kwamba, bwana Mchaga muhogo, ayaaa, wanaogopa kwelikweli. Mheshimiwa Njalu Silanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Aloyce Kwezi.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba hii muhimu sana ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo. Na kwa maelezo yake mazuri sana tunaanza kupata matumaini sisi wakulima wa pamba na wakulima wa mazao mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia kwenye suala la uzalishaji, uzalishaji wetu unaenda sambamba na masoko, kama mchangiaji mwenzangu alivyozungumza. 2019/2020 soko lilipokuwa zuri tulizalisha tani 348, mwaka 2021 tukashuka tukazalisha tani 122, sasa ndio utanza kujiuliza kwamba, katika Mpango wa Bajeti ya Serikali wanapopanga mambo ya kiuchumi na Mheshimiwa Waziri ametuelezea vizuri sana kwamba, tunategemea kupata fedha za kigeni, tunategemea kupata ajira kwa vijana wetu, ni vitu vingi vinavyojumishwa kwenye suala la kilimo na kuwa na fedha nyingi kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa nilitaka Serikali watusaidie fedha hizi tunazozitenga kila mwaka kwa ajili ya kilimo, lakini fedha hizi hazifiki kwa muda unaotarajiwa, matokeo yake fedha hizi na taasisi kama bodi hizi na nimpongeze tu Mheshimiwa Waziri Bashe jinsi walivyohangaika kupata fedha kwa ajili ya kusaidia wakulima. Na inasababisha taasisi tunazozipa mamlaka hizi zinakuwa na changamoto kubwa

sana kwenye suala la kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya kimkakati, hususan zao la pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukisimamia vizuri kwenye kilimo, pamba, alizeti, korosho, hasa mazao mawili hapa, tunakuwa na changamoto ya kulalamika mafuta. Alizeti ikizalishwa kwa wingi na pamba tukizalisha kwa ekari ambazo kwenye takwimu zao wameziorodhesha kilo milioni moja laki tano na hamsini na sita, ukifanya tu wapate kila ekari moja kilo mia nane-mia nane au mia tano-mia tano tutazalisha mwaka mzima. Tutakuwa na mzunguko wa mwaka mzima wa fedha, tutakuwa na mzunguko wa mwaka mzima wa ajira, lakini na *train* zetu nazozijenga zitasafirisha mzigo kutoka Mwanza kuja Dar-es-Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yote hii Mheshimiwa Waziri wa Kilimo tunakutegemea na Ofisi yako na Bodi zako. Na ikienda mbali tunapozungumzia maafisa ugani hawa wanapoendelea kubaki kwenye halmashauri zetu, ni diwani kwenye halmashauri yangu na wote Wabunge ni madiwani, bila kuwa na mkakati mahususi hawa maafisa ugani tunaowatarajia kuwaajiri wakawajibika moja kwa moja kwenye mabodi yetu na ukawapa mikakati na takwimu, tutapiga hatua na tutafika mbali sana, lakini ngonjera hizi za kuzungumza kila siku hatutafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini suala la pili kuhusiana na dawa. Dawa zetu hizi mnazozileta wataalamu wetu watafiti, umeelezea hawa *TARI*, n.k., hayauwi wadudu. Hadi mkulima ambaye yuko kijijini kule hajui mambo ya utafiti anakwambia nimepulizia, nimechanganya hiki na hiki, lakini yule funza hafi. Matokeo yake tunarudi kwenye uzalishaji wa chini. Lakini yote haya mukiyawekea utaratibu mzuri naamini kabisa tunaweza tukapiga hatua na Taifa letu likaeendelea kupata mapato ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la mbegu, ningeeendelea kuishauri tu Serikali kwamba, tunayo mabwawa ambayo yamechimbwa, tuisubiri sana kila mwaka mpaka msimu wa

mvua uanze, lakini huku tuna mabwawa. Bora tuwekeze kwenye mabwawa haya, kwangu jimboni kwangu nina mabwawa karibu manne, Bwawa la Habia, Mwamapalala, Nobola, Sawida na Mwasuguya kule Bariadi, mabwawa makubwa kabisa. Mkiwekeza kwenye suala la mbegu hususan kwenye upande wa pamba na pamba inakamilika kwa miezi minne; ukilima mwezi wa sita mwezi wa kumi na moja unavuna, tayari utakuwa umepata mbegu iliyo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hivi sasa tunakwenda kwenye uzalishaji unaokuwa chini na sababu zinakuwa ni nyingi, unaweza ukakuta mbegu zilishapitwa na wakati. Sisi kule kwenye pamba tuna mbegu UK91 ya mwaka 91, leo tuko mwaka 2021 ni miaka 20, jambo hili wataalamu mnalifahamu, lakini kwa sababu tunakaa hapa kutimiza wajibu tunabaki kusimama hivyo bila kuzisimamia taratibu na kanuni za uzalishaji bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukiendelea kusimamia hivyo viwanda vyetu tunavyovizungumzia tayari tutapata malighafi ya kuviendesha vile viwanda, lakini tumewekeza sana kwenye miundombinu na mengine, lakini ningeshauri sana Serikali kwa ujumla fedha hizi kwenye suala la kilimo zitoke ili ziweze kufanya kazi nzuri zaidi. Ikishindikana Serikali mwaka uliopita ilikuja na sera, tulikuwa na bodi na taasisi zetu mifuko hii ya kuendesha mazao mbalimbali ikazichukua, changamoto ikaanzia hapo tukashuka kwenye uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeomba kama Serikali kama kuna changamoto humo basi, taasisi hizi za wadau ziruhusiwe kulingana na mifumo iliyokuwa ikiendesha ili tuondokane na matatizo haya ambayo yunayapata. Kwa sababu, unakuta dawa inaenda mwezi wa tatu, sasa mwezi wa tatu unaenda kupulizia nini? Tayari na Serikali inaingia kwenye madeni ambayo hayalipiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaiomba sana Serikali chini ya Mheshimiwa Waziri na umesema umeunda timu inayoshughulikiwa na Mheshimiwa Bashe, nina imani inaweza ikaleta majibu yakutosha, lakini kubwa zaidi tunalohangaikanalo sisi ni uzalishaji kuwa wenye tija, lakini na masoko yakiwa yenye tija, naamini tunaweza tukazalisha uzalishaji mkubwa tukapata mafuta yakutosha, lakini tukapata ajira za kutosha na tukapata fedha za kigeni za kutosha kwenye maeneo yetu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mzunguko wa kilimo, pale ambapo kilimo kinapokuwa kimezalisha kwa wingi zaidi mzunguko unakuwa ni mkubwa wa fedha kwenye maeneo mbalimbali. Bila kuwa na mzunguko wa kuwasaidia wakulima hatuwezi kupiga hatua hata tufanyaje kwa sababu, hata hizi ndege tunazozinunua watu wanahitaji kupanda, *train* za mwendo kazi tunazozijenga hizi zinahitaji watu wapande. Nani atapanda hizo *train* kama watu hawana vyanzo kwenye maeneo yao mbalimbali kwa ajili ya kupata nanilii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendele tu kusisitiza kwamba, ninaendelea kuiunga Serikali mkono kwa maana ya Wizara kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kufanya chini ya bodi zetu hizi. Naamini tutafanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Njalu Silanga, mdau mkubwa wa suala la pamba, tunakushukuru sana kwa mchango wako, kutoka Itilima. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Aloyce Kwezi atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Sanga.

**MHE. ALOYCE A. KWEZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Binafsi nakushukuru wewe kwa hekima na busara zako za kuongoza Bunge letu. Pia nichukue nafasi hii



kuwapongeza sana Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya watendaji kwenye Wizara ya Kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Kaliua hususani Mkoa wetu mzima wa Tabora kuhusiana na zao la tumbaku. Naomba Wizara hii itusaidie, kwanza kabisa kwenye zao la tumbaku kumejitokeza changamoto kwenye soko. Bei elekezi ya zao la tumbaku Serikali imetoa ni dola 1.61 lakini pia gharama ya mkulima kuzalisha anatumia dola 1.4, wanunuzi walipokuja wamenunua chini hata ya gharama ya wakulima; wamenunua chini ya dola 1.2. Haya yametokea siyo kwenye Jimbo la Kaliua peke yake pia yametokea kwenye maeneo ya Usimba, Kasungu, Kaliua *Rural*, Kamsekwa, Igwisi na maeneo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, zao hili la tumbaku limekuwa na changamoto, ambaye ananunua vizuri kabisa ni kampuni ya *GTI*, lakini kampuni ya *Alliance One* wamenunua tofauti kabisa wakati wale ma-valuer wa Serikali wamefika wakatathmini bei ikaonekana ni nzuri walipofika *GTI* wakanunua kwa bei nzuri lakini walipokuja kununua hawa *Alliance One* wamenunua kwa bei ya chini sana ambayo inaumiza wakulima. Naomba Wizara iingilie kati kuhakikisha masoko ambayo yamefanyika katika kipindi cha mwezi mmoja uliopita bei ya wakulima iweze kupanda kama tathmini ya Serikali ilivyokuwa imesema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niongelee *CSR* kwenye kampuni hizi, kampuni ya *GTI* hii imetusaidia sana inatoa *CSR*, tunajua madhara pia ya tumbaku, wanatu-*support* madarasa, zahanati, vituo vya afya, hata mimi kwangu Usinge wameleta milioni 500. Huyu *Allowance One* ambaye ananunua sana tumbaku kule hata *CSR* kwa maana ya huduma za jamii ha-*support*. Sasa kwa nini yeye anakuwa tofauti na wanunuzi wengine? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna kampuni ya *Grand Tobacco Limited* pamoja na *Majestic*, wamenunua tumbaku msimu wa 2019/2020 mpaka sasa hawajalipa wakulima wa

tumbaku. Pale kwangu kuna chama kinaitwa Mwamko kinadai shilingi milioni mia moja na moja mpaka sasa hawajawalipa. Kibaya zaidi wamerudi kwenda kufunga mkataba yaani unamdai, hajalipa, halafu umefunga mikataba na vyama vya msingi. Naibu Waziri alikuja akatuahidi kulishughulikia lakini muafaka bado, naomba Bunge litusaidie kwenye zao hili la tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye zao hili hili la tumbaku nashangaa sana tumewekewa ukomo wa kulima yaani wewe unaambiwa zalisha kilo mia mbili wakati wewe una uwezo wa kuzalisha zaidi ya kilo mia mbili, hii *limit* kwa nini wanaiweka? Ni kwa nini Wizara isiingilie kati na kuhakikisha tunapata masoko? Lazima tusimame pamoja kupata masoko ya kutosha. Naomba hii *limit* iondolewe kwa wakulima wazalishe kadri ya pembejeo wanazopata na uwezo walionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia Wizara itusaidie kuhusiana na kilimo cha alizeti katika Mkoa wa Tabora. Tabora alizeti inakubali, Singida na Tabora unaitofautishaje, hali ya hewa ya Kaliua, Urambo, Igalula, Nzega na Igunga inafanana na alizeti tunalima. Hizi mbegu ambazo zimesambaza kwenye mikoa mitano kama alivyokuwa analia wa Kilimanjaro tunaomba zifike Tabora. Kwa heshima zote nawaomba waingilie kati watusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niwapongeze kwa jambo kubwa sana, jiografia ya Kigoma inafanana na ya Tabora, mmetusaidia kwenye Jimbo la Kaliua mmetuletea michikichi miche karibu laki moja na nusu. Naomba sambazeni miche ile katika mkoa wote wa Tabora kwa sababu haya mazao yanakubali kwenye Mkoa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la pembejeo na nina ushauri; *CRDB Bank* na mabenki mengine yanatusaidia lakini Benki yetu ya Kilimo kwa nini isitusaidie kwa sababu riba ya pembejeo ikitoka kwenye *TADB* itakuwa ni ya chini kuliko ambavyo ipo kwenye mabenki mengine. Asilimia nane ni kubwa, naamini hata kule wanako-*support*

kama *TADB* akisimama vizuri tutakuwa na mchango mzuri sana na wananchi watanufaika sana kwa sababu asilimia 80 ni wakulima na sisi tumesimama hapa leo tumesomeshwa na wakulima, kama siyo alizeti basi ni kahawa, kama siyo tumbaku basi ni zao lingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa mwisho uende kwenye kilimo cha umwagiliaji. Yapo maeneo tunapoteza maji, mafuriko yanatokea hivi tumeshindwa ku-*design* mabwawa ya kutosha ili kila kiangazi tuzalishe nyanya, vitunguu na mazao mengine ya umwagiliaji. Hatuna sababu ya kudharau kilimo cha umwagiliaji. Nawaomba Kata ya Zugimlote tuwekeeni bwawa pale, Igwisi tumesha *design* bwawa tunaomba mtuletee fedha, lakini Igagala Namba Tano tume-*design* bwawa, tunaomba mtuletee fedha hizo ili ziweze kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwapongeza Wizara hii kwa umakini, unapowapa taarifa wanakuja haraka na wanatusaidia kutatua migogoro mbalimbali. Kwa hiyo, mimi nikuombe Mheshimiwa Waziri Profesa wangu na Naibu wako makini kabisa Mheshimiwa Bashe, msilale, hiki kilimo ndiyo kinatufanya sisi tuonekane tumetekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa siyo kwa umuhimu *CSR* nyingi sisi tunazipata kupitia mazao ambayo yanapatikana kwetu na hususani tumbaku. Halmashauri zetu mapato ya ndani zinategemea kwenye tumbaku, naomba hawa watu muwabane walipe, wanapolipa Halmashauri zikapata mapato ndiyo tunaweza kusaidia Serikali Kuu kwenye ujenzi wa vituo vya afya, barabara, kununua mitambo ya barabara na mambo mengine ya msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nashukuru kwa hekima na upendeleo ambao umenipatia mimi. Nakushukuru sana, Mungu akubariki, naunga mkono hoja asilimia mia moja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Aloyce Kwezi kwa mchango wako hasa kuhusu tumbaku. Mheshimiwa Kwezi wakati unachangia Mwenyekiti wako wa Mkoa anataka kuruka kabisa, maana Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tabora ni mmoja wa wakulima wakubwa wa tumbaku. Hoja kubwa hapa jamani iondoke *limit* mtu unaambiwa uzalishe tu tani fulani basi, labda kuna sababu za msingi watatuambia. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Deo Sanga atafuatiwa na Mheshimiwa Miraji Mtaturu, Mheshimiwa Esther Malleko ajiandae.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niwe miongoni mwa wachangiaji katika Wizara hii ya Kilimo. Kwanza, nianze kwa kumpongeza Waziri na Naibu Waziri, Katibu wake na watumishi wote wa Wizara hii. Wizara hii imepata mtu ambaye tunamtegemea sana Waziri pamoja kijana wetu Naibu Waziri, kwa kweli tunawapongeza kwa kazi nzuri ambayo mmekuwa mkiifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi, naunga mkono ushauri wa Kamati ya Kilimo na nadhani muifanyie kazi. Kamati ya Kilimo wameshauri vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie changamoto ambazo zipo nchi nzima au kwenye Mkoa wetu wa Njombe na hususani Jimbo langu la Makambako. Tuna changamoto kwenye zao la mahindi, mahindi katika Mkoa wetu inawezekana na Mikoa mingine ni tatizo kubwa. Mpaka sasa mahindi hayajapata soko, mahindi ya mwaka jana mpaka sasa yapo. Nashauri Wizara ijipange kutafuta masoko ili wananchi wetu waweze kuuza mahindi haya. Wamekuwa wakitupigia simu sana, mahindi yapo kwenye maghala yao mpaka sasa hayajauzwa na hivi sasa kwetu Njombe wameanza kuvuna tena ya msimu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda Njombe kule mahindi yanauzwa debe Sh.3,000 au Sh.3,500, plastiki ya lita kumi na

tisa au ishirini. Kwa hiyo, unakuta sasa uuzaji wa mahindi wa debe hili au gunia hauendani na ununuzi wa pembejeo. Kwa mfano, mbolea ya *DAP* ndiyo tunatumia sana sisi na mbolea hii ya *Urea*, mfuko mmoja unauzwa kati ya Sh. 55,000 hadi Sh.60,000, ukijumlisha mifuko miwili unapata Sh.110,000. Katika Sh.110,000 mpaka uuze gunia karibu nne ndiyo ununuzue mifuko miwili. Kwa hiyo, tunaiomba sana Wizara ione namna ya kukomboa wakulima wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashauri ili mbolea hii iwe bei chini, Mheshimiwa Waziri tunaimani sana na wewe, Serikali tafuteni wawekezaji ili vijengwe viwanda vya mbolea ya kuzalisha *DAP* na *Urea* katika nchi hii hii. Tukipata wawekezaji wa kujenga viwanda vya mbolea, tunaimani mbolea itashuka itaendana angalau na bei ya soko la mazao ambayo wananchi wetu wamekuwa wakiuza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine tuna maghala ambayo mlianza kujenga Dodoma, Makambako na mahala pengine, maghala haya hayajaisha. Ombi letu muhakikishe maghala haya maghala haya yanaisha.

Mheshimiwa Spika, tuna Benki ya Kilimo (*TADB*), benki hii ipo Dar es Salaam na wakulima wetu kutoka mikoani kule kwenda Dar es Salaam ni mbali. Kwa hiyo, haiwasaidii kabisa vinginevyo inawasaidia watu wenye uwezo mkubwa. Ombi langu ni kwamba benki hii iende katika maeneo husika angalau muite Dar es Salaam muweke Dodoma hapa ndiyo katikati. Vilevile mshushe huko kwenye mikoa yetu hasa kwenye mikoa ile ambayo ndiyo inayozalisha mazao ya kimkakati na mazao mengi zaidi ikiwepo Mkoa wa Njombe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile ipo changamoto ya wakulima wetu wa chai, amezungumza sana ndugu yangu hapa Mheshimiwa Swalle ambapo kule Njombe kuna majimbo matatu yanayozalisha chai kwa wingi likiwepo Jimbo la Mheshimiwa Mwanyika, Jimbo la Mheshimiwa Swale la Lupembe na Jimbo la Ludewa. Tatizo kubwa wakulima hawa wameanza kukata tamaa kwa sababu

wanacheleweshewa kulipwa fedha zao wanapouza chai, inachukua mpaka miezi minne/mitano hawajalipwa. Kwa hiyo, ombi langu Wizara msimamie kuhakikisha wananchi wanalipwa chai yao wanapouza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Njombe tuna zao kubwa vilevile la parachichi. Parachichi soko lake ni kubwa lakini parachichi hizi zinapozalishwa kule Njombe vifungashio, sitaki nionyeshe vinaonyesha vinatoka nchi gani, vifungashio vile wakifunga inaonekana maparachichi haya hayatoki Tanzania yanatoka nchi jirani. Ombi langu kwa Wizara hebu mfuatilie nchi ambazo zinanunua sana maparachichi na ninyi mjipange kuona moja kwa moja parachichi zinavyotoka Tanzania zinaandikwa parachichi za Tanzania, hii itatusaidia sana katika suala zima la masoko. Sasa hivi watu wanalima kwa wingi sana parachichi, itapendeza kujua soko hili litadumu kwa miaka mingapi na ni nchi gani ambazo zitanunua? *(Makofi)*

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa, ndiyo nimekuona Mheshimiwa.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba nchi ya Mexico wanatumia ekari 260,000 kuzalisha zao la parachichi sawa na asilimia 5 ya eneo zima la Mkoa wa Njombe na wanauza parachichi duniani wanapata trilioni 5. Hii maana yake sisi hatujakifanya kilimo hiki cha parachichi kama kilimo biashara. Ahsante.

**SPIKA:** Unapokea taarifa hiyo Mheshimiwa Deo Sanga kwamba bado msisitizo kwenye parachichi unatakiwa.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, mimi nadhani anasisitiza kwenye suala la kilimo cha parachichi. Kwa hiyo, Waziri amesikia.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante na kengele tayari.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, dakika amenimalizia huyo. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Hapana, hayajatumia dakika zako, ahsante sana Mheshimiwa Deo Sanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Miraji Mtaturu, Mheshimiwa Esther Malleko atafuatia Mheshimiwa Nape Nnauye na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla ajiandae. Mheshimiwa Mtaturu kwa sasa.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti hii muhimu iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, wote tunakubaliana hapa kwamba kilimo ndiyo kimebeba uchumi wa nchi yetu. Asilimia 80 ya Watanzania wanafanya kilimo na kumekuwa na juhudi mbalimbali zinafanyika, naipongeza Serikali na katika hili juhudi inatakiwa kuongezeka na tumeendelea kushauri mara nyingi, nataka nishauri kwenye eneo moja kubwa sana la mbegu.

Mheshimiwa Spika, tusipokuwa na mbegu zenye tija hatuwezi kubadilisha kilimo chetu. Wananchi wataweka juhudi zao, muda wao, rasilimali zao lakini bado tutajikuta tunarudi nyuma, hatuwezi kwenda mbele. Kama hivi tunavyoambiwa wenzetu nchi nyingine wanalima eneo dogo lakini wanapata uzalishaji mkubwa ni kwa sababu ya utafiti mkubwa walioufanya kwenye mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kama hiyo haitoshi kumekuwa na ruzuku inayotolewa kwa ajili ya mbegu. Nitajitika kwenye eneo la zao la alizeti. Leo hii tunalia wote hapa kwamba tuna tatizo kubwa la mafuta ya kula, Serikali

inatumia fedha nyingi kwa ajili ya kuagiza mafuta ya kula wakati tuna ardhi ya kutosha na mazao mengi yanayoweza kutoa mbegu za mafuta. Mfano zao la alizeti, tumekuwa na mawazo mengi ya kuhakikisha kwamba tunaongeza uzalishaji, kuna baadhi ya mbegu zile za kienyeji unatoa magunia matatu kwenye heka, unapoteza muda mrefu sana kufanya kazi ambayo haina tija.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na mawazo ya mbegu mbalimbali ambao zimeendelea kufanyiwa utafiti kwenye maeneo yetu. Kwenye eneo hili nimeona kuna fedha zimetengwa kwa ajili ya kuongeza utafiti. Nimuombe Waziri tuongeze nguvu kwenye eneo hili, watafiti wetu wapo, vituo vyetu vipo viongezewe fedha za kutosha kwa ajili ya kuja na mbegu zenye uzalishaji wa kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mfano mdogo kumekuwa na mawazo ya kuwa na *GMO*, tunatakiwa kuwa makini sana kwenye kuingiza mbegu hizi. Kuna baadhi ya nchi ambazo ni ushahidi leo wanapata mbegu hizo za *GMO* asilimia 100 hawana mbegu zao za asili katika nchi yao. Niombe sana Serikali inapoamua kufanya haya iwe na uhakika na tunachoenda kukifanya.

Mheshimiwa Spika, lakini kama hiyo haitoshi kilimo cha umwagiliaji kipewe nafasi kubwa. Hekta hizi ambazo zinatengwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji hazitoshi, hatuwezi kujitegemea kwa chakula. Katika eneo hili pia tuongeze wataalam wa kutosha kwenye Halmashauri zetu. Leo hii unaweza kusema unaweka skimu ya umwagiliaji unawakabidhi wakulima ambao wao wenyewe hawana uwezo wa kuendesha mradi ule, tunapoteza fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumesikia Tume ya Umwagiliaji inaboreshwa, niombe sana nguvu ziongezewe tuwaweke wataalam wale mpaka kwenye Halmashauri zetu ili waweze kusimamia kweli kilimo cha umwagiliaji. Kilimo cha umwagiliaji tukikifanya vizuri, maeneo mengine wamefanya vizuri kwenye eneo dogo tunapata uzalishaji mkubwa. Leo nchi yetu inapata mvua nyingi sana kila mwaka, tuna baadhi



ya maeneo mpaka zinaharibu miundombinu, tumekuwa tunalalamika hapa barabara zetu zinaharibika ni kwa sababu ya mvua nyingi. Yale maji yanapotea yanakwenda baharini. Naombe sana Serikali iweke nguvu kwenye kuvuna maji ya mvua na tuwe na mabwawa ya kutosha kwenye maeneo yetu ambayo yatumika kwenda kuwasaidia wakulima wetu wawe na kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni masoko ya mazao yanayopatikana, lazima tuwe na uwezo wa kuhakikisha kwamba mkulima anapolima ana uhakika anakwenda kuuza wapi. Mfano mdogo kwenye eneo la kilimo cha alizeti kuna baadhi ya maeneo kama Singida kule imeshuka kwa sababu kuna baadhi ya maeneo wakulima wanakopwa bado wapo shambani, watu wanakwenda kununua shambani bado mtu hajavuna. Maana yake ni kwamba anauza kwa bei ya kutupa, mkulima huyu mwakani hawezi kurudi kulima. Naomba Maafisa Biashara, Maafisa Mipango na Maafisa Kilimo kwenye Halmashauri zetu wasimamie vizuri suala la masoko ili kumfanya mkulima huyu afaidike na kilimo chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Maafisa Biashara, Maafisa Mipango kwenye Halmashauri zetu na Maafisa Kilimo wasimamie vizuri suala la masoko ili kumfanya mkulima huyu afaidike na kilimo chake. Tunaposema tuwe na usalama wa chakula kweli chakula, tutaendelea kuwa na uwezo wa kuhifadhi, lakini kuna mazao ya biashara tumesema hapa tuwe na kilimo biashara. Eneo dogo, tuweze kuwa na uzalishaji wa kutosha na mwisho wa siku mwananchi huyu tuweze kumkomboa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hili nilikuwa nataka niongee kidogo sana kwenye eneo la Benki yetu ya Kilimo. Leo tunaipigia chapuo, ni benki imepewa fedha isimamie, lakini masharti yale siyo rafiki kwa wakulima walioko vijijini. Mfano, mimi ninayo *AMCOS* moja pale kwangu Misughaa pale Ikungi, leo hii ile *AMCOS* wamekopeshwa shilingi milioni 85 tu. Leo ninavyoongea mimi na wewe, wale *AMCOS* kwa sababu tu msimu uliopita haukuwa na mvua ya kutosha,

wamepelekwa TAKUKURU, wamepelekwa Mahakamani, ni kama vile ambavyo hapakuwa na mkataba. Usitegemee wakulima hao mwakani wakaenda tena kwenye Benki ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana, nitakukabidhi *document* hiyo Mheshimiwa Waziri ili uweze kufuatilia. Haiwezekani watu waliokuwa na mkataba wa makubaliano ya mkopo na walikubaliana kwamba watu wa bima wapo, wameshachukua ile nafasi ya bima halafu mwisho wa siku kwenye msimu wasipovuna vizuri wanapelekwa TAKUKURU, wanapelekwa Mahakamani, hakuna sababu. Huyu mkulima unamfanya aogope hata kwenda kukopa kwenye hiyo Benki ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na juhudi zinazofanyika za kuongeza fedha, lakini kuna *treatment* siyo nzuri inafanywa na baadhi ya maeneo kwenye Benki yetu ya Kilimo, kwa sababu haimsaidii mkulima, inaenda kumnyonya zaidi na kumwondoa kwenye mawazo mazuri ya kukopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo tunaposema kwamba kuna baadhi ya benki hazina urafiki na wananchi wa kawaida. Basi hata hii Benki ya Kilimo ambayo Serikali imeweka fedha, tuwawekee mazingira mazuri wakulima wetu waweze kuwa na uwezo mkubwa wa kulima eneo kubwa, wawe na pembejeo za kutosha, wawe na vifaa ikiwemo matrekta ili kubadilisha kilimo chao kutoka kwenye kilimo kile cha kawaida. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Miraji.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, nawatakia kila la heri Wizara hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunashukuru kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, kuna fomu ambayo inatembea, mtagawiwa huko, inatoka Tume ya Taifa ya Umwagiliaji; ni dodoso la aina fulani ambalo mtaombwa mjaze; litasaidia sana Tume katika kuweka mipango yake vizuri ikiwemo mipango ya umwagiliaji katika jimbo lako.

Mheshimiwa Spika, tunao wageni wa *NMB* bahati mbaya sikupata majina yao mapema. Meneja wetu wa *NMB* wa Tawi la Bunge, Grace karibu sana, sana. Amefuatana na Mkuu wa Kitengo cha Kilimo, Ndugu Isack Masusu, ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia yuko Afisa Mkuu, Masuala ya Wateja, Ndugu Filbert Mponzi. Ahsanteni sana na karibuni sana *NMB*, ninyi ni wadau wetu wa karibu sana. Tunafurahi mnapokuwa karibu nasi. Inaelekea *NMB* nao wana *package* ya kuhusu masuala ya kilimo, tutapenda kujua baadaye kama hilo lipo, ahsante.

Mheshimiwa Ester Maleko, atafuatiwa na Mheshimiwa Nape Nnauye.

**MHE. ESTER E. MALEKO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana ya Kilimo. Kwanza naipongeza Wizara kwa hotuba nzuri, lakini nijikite moja kwa moja kwenda kuzungumzia changamoto zinazokabili sekta hii ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, sekta hii ya kilimo inaajiri zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania na pia inatoa pato la asilimia 29 kwenye pato la uchumi wa Taifa, lakini hii ndiyo sekta yenye changamoto kubwa kuliko sekta nyingine zozote. Tunategemea tutapata ajira kutoka kwenye sekta hii, lakini hatujaweka mkazo mkubwa kwenye hii sekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu gani? Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2022 katika ukurasa wake wa 33 imeeleza kwa kirefu mikakati ya kukifanya kilimo cha kisasa na cha kibiashara chenye tija na ambacho mazao

yake yatakuwa yameongezwa thamani, lakini shida kubwa pamoja na hayo, ni masoko. Wakulima wengi wanalima lakini hawajui mahali pa kuuza mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakumbuka Mheshimiwa Rais wetu Hayati John Pombe Magufuli alipokuwa anahutubia Bunge tarehe 13 Novemba, 2020 alisema anaomba Wizara ya Kilimo, Wizara ya Biashara na Wizara ya Mambo ya Nje ikishirikiana na Mabalazi waweze kukutana ili kuangalia ni namna gani wanaweza kutatua changamoto zinazokabili kilimo. Ninaamini kabisa Wizara hizi zikikutana zikaweza kuweka mawazo yao ya pamoja tutaenda kutatua changamoto kubwa ya kilimo inayowapata wananchi wa Tanzania. Wengi wanalima lakini hawajui watauzi wapi mazao yao.

Mheshimiwa Spika, inawezekana kutokana na uelewa mdogo au kutokujua namna gani ya kuongeza thamani ya mazao yao, wanakuja wafanyabiashara kutoka nje ya nchi; nchi za Jirani hapa, wananunua mazao yanayolimwa hapa Tanzania, wanakwenda wanayaongezea thamani, wanauza nchi za nje na wanapata fedha nyingi, lakini wakulima wanaolima ambao wanatoka Tanzania wanaendelea kubaki nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaiomba sana Wizara ya Kilimo inayoongozwa na kaka yangu Mheshimiwa Prof. Mkenda, ninajua wewe na ndugu yangu Mheshimiwa Bashe ni viongozi makini sana, muende mkaliangalie suala hili kwa makini, wakulima wetu wanapata changamoto kubwa sana, wanaishia kufanya kilimo ambacho hakina tija, wanaishia kulima lakini hawana faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo Benki ya Kilimo haiwasaidii wakulima wadogo. Inanufaisha wakulima wakubwa na wakulima hawa wadogo ndio tunaotegemea waende kuinua kipato chao na kuchangia kwenye pato la Taifa. Wanachangiaje sasa ikiwa hata hii benki ambayo imewekwa mahususi kwa ajili ya kuwasaidia, haiwasaidii?

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kubwa ambalo linakwaza kwenye kilimo ni upatikanaji wa mbegu bora. Wizara ya Kilimo, nimesikia kwenye hotuba yenu, mmetenga bajeti na mtasimamia kuhusu upatikanaji bora wa mbegu za kilimo, tunaomba mwahamasishe wakulima ni namna gani wanaweza kwenda kulima mbegu bora na sisi tukaweza kupata mbegu zinazohitajika hata tukaacha kulia kama tunavyolia leo nchi haina mafuta, tunaenda kuagiza nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, leo tukilima kilimo hiki cha alizeti, ninaamini suala hili la kulia mafuta, mafuta, litakwisha. Haiwezekani nchi kubwa kama Tanzania yenye zaidi ya asilimia 44 ya ardhi yake inafaa kwa kilimo, lakini bado sisi tunaendelea kuagiza mafuta nje ya nchi. Ni aibu kubwa sana. Naomba sana Wizara ya Kilimo iangalie namna ya kuwapatia wakulima mbegu bora na ziwafikie kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, pia suala la Maafisa Ugani, hili ni tatizo lingine. Leo hii Chuo cha Kilimo *SUA* kinatoa wataalam, lakini kwa sababu wanaona sekta hii haiwalipi, wanaenda kuajiriwa benki badala ya kwenda kusaidia wakulima hawa ambao ndiyo tunasema tutapata ajira, tutakomboa vijana, tutakomboa wanawake ambao wanateseka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, katika mazao saba ya kimkakati yaliyowekwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2025, kuna zao la mkonge. Zao hili linalimwa pia Kilimanjaro, lakini asilimia kubwa ya wananchi hawa wa Kilimanjaro hawajui vizuri juu ya suala hili. Naiomba basi Wizara iangalie namna ya kuwapatia akina mama na vijana fursa ya kuweza kulima zao hili. Zaidi ya yote, tunalima hili zao la kimkakati, lakini pia tunahitaji kufufua kiwanda cha magunia kilichoko Moshi, kwani kimekufa. Tunasemaje tunaenda kutafuta mazao ya kimkakati, tunaenda kuzalisha bidhaa, lakini kile kiwanda ambacho kinatumika kuzalisha bidhaa hizo, hakipo; lakini tuna malighafi na hatuna mahali pa kwenda kuzipeleka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiwanda cha Magunia cha Moshi ni tatizo. Kimechukuliwa na mwekezaji, lakini mpaka sasa hakijaendelezwa, lakini leo tunasema zao hili ni la kimkakati na pale Kilimanjaro tunataka wakulima wetu waende kulima zao hili. Wapolima, tunategemea wakauze pale na kiwanda kile kiweze kuboreshwa kisitengeneze tu magunia, kikatengeneze na vitu vingine ambavyo vinatokana na zao la mkonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naishukuru Serikali kwa kuona umuhimu wa kufufua kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tools*. Huko tutapata vipuri vya matrekta, ma-*Power Tiler*, lakini hivi hivi ndiyo vitakavyoenda kuwasaidia wakulima wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, Kilimanjaro tunalima ndizi na parachichi. Katika kulima ndizi, wakulima wetu mfano wanaotoka Jimbo la Hai wanauza mazao yao ya ndizi katika soko la Kwa Sadala, lakini soko hili limekwisha kabisa, hawawezi hata kuhifadhi vitu vyao. Mvua ikinyesha, ni shida hata mchuuzi kuingia kwenye lile soko kwenda kununua bidhaa. Ninaiomba Wizara iangalie kwa jicho la tofauti soko hili la Kwa Sadala ambalo linawasaidia akina mama wengi na vijana, kujikwamua kiuchumi waweze kupata...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ESTER E. MALEKO:** ahsante sana naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ester. Mheshimiwa Nape Nnauye, Mheshimiwa Hamisi Kigwangala atafuatia na Mheshimiwa Conchester Rwamlaza.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie kidogo kwenye Wizara hii ya Kilimo. Napongeza hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri na nipongeze kazi nzuri inayofanywa na

Wizara hii; Waziri na Naibu Waziri. Nadhani katika Wizara ambazo *combination* yake imekaa vizuri ni Wizara hii. Mawaziri wake ni wasikivu, lakini wana werevu mzuri, nami nina matumaini kwamba sekta ya kilimo itakwenda vizuri. Hongera sana Waziri na Naibu wako pamoja na Katibu Mkuu. Watu wapole na wasikivu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, nataka nizungumze jambo mahususi kwenye korosho. Mwaka 2018 tulibadilisha sheria hapa ya tasnia ya korosho. Tulipofanya yale mabadiliko yalisababisha kufutwa kwa mfuko wa kuendeleza zao la korosho ambao ulikuwa unaitwa Mfuko wa Pembejeo, ambapo chanzo chake cha fedha ilikuwa ni tozo ya mauzo ya nje *(Export Levy)*. Uamuzi ule ulipofanyika, wale waliokuwepo wanakumbuka, Serikali ilitoa ahadi hapa Bungeni kwamba inachukua zile fedha ambazo zilikuwa zikipatikana; na kwa sababu kile chanzo bado kipo, fedha zinapelekwa kwenye mfuko mkuu ili zikasimamiwe vizuri kwa hoja kwamba zilipokuwa kwenye huu mfuko zilikuwa hazisimamiwi vizuri.

Mheshimiwa Spika, makubaliano ilikuwa ni kwamba hizi fedha zikishaenda Mfuko Mkuu, zitarudi kuja kuendeleza zao la korosho kama ambavyo zilikuwa zikifanyika kwenye mfuko wa pembejeo. Kwa hiyo, kilichofanyika ilikuwa ni kubadili msimamizi. Sasa huu ni msimu wa tatu toka makubaliano hayo yafanyike na sheria hii ibadilishwe, bahati mbaya sana hii fedha haijarudi kwenye zao la korosho, haiendi kabisa. Hili ni la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, baada ya hii fedha kuchukuliwa, uzalishaji wa korosho ukashuka kutoka tani 320,000 ukaenda mpaka tani 200,000 na kitu, kwa maamuzi tu haya ya kuchukua huu mfuko. Baya kuliko yote, badala ya kurudisha hii fedha kwa wakulima, kilichofanyika, msimu uliofuata moja ya kazi iliyokuwa inafanywa na hii fedha ilikuwa ni kugharamia utafiti na kuendesha Bodi ya Korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ikaleta mapendekezo, ikaweka tozo kwa wakulima shilingi 25/= ya utafiti na shilingi 25/= ya kuendesha Bodi ya Korosho, badala ya kutumia ile fedha waliyoichukua, ile fedha haikurudi na ule mzigo akarudishiwa mkulima. Kwa hiyo, mkulima anakatwa shilingi 50/= kwa ajili ya utafiti na kwa ajili ya kuendesha Bodi ya Korosho. Huu ni udanganyifu. Tulipoahidiwa hapa Bungeni tuliambiwa hii fedha ingeenda, lakini sasa huu mzigo amebeshwa mkulima.

Mheshimiwa Spika, baya zaidi, sasa hivi yako mapendekezo mengine ya kugharamia pembejeo kwa kumkata mkulima shilingi 110/= kwa kilo. Ahadi iliyotolewa hapa ni kwamba hii fedha ya *Export Levy* ndiyo ambayo ingerudi kuja kugharamia. Sasa kwa mahesabu ya kawaida, mwaka 2018 iliingizwa shilingi bilioni 37, wakati huo mfuko haukufanya kazi kwenda kugharamia pembejeo. Serikali ilipata mapato shilingi trilioni moja na zaidi, kwa kuingiza shilingi bilioni 37 tu. Mwaka huu makisio ya uzalishaji ni tani 280,000 mpaka 350,000, tunahitaji shilingi bilioni 55 tu. Sasa kwa nini tunataka kwenda kumbebesha huu mzigo mkulima badala ya kuchukua ile fedha ambayo mlituhidi hapa kwamba itakwenda kutumika vizuri? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, shilingi bilioni 55, tunazalisha zaidi ya trilioni moja *plus!* Ni maombi yangu kwa Serikali, naomba sana; na bahati nzuri Naibu Waziri wakati ule tuna mgogoro huo wa *Export Levy* hapa, alikuwa Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Bajeti na alituunga mkono. Ni matumaini yangu kwamba kwenda kwake Serikalini hakujambadilisha kuliona hili jambo kwa mtazamo sahihi, tuchukue fedha ya *Export Levy* turudishe iende kugharamia korosho ili Serikali mpate.

Mheshimiwa Spika, kushuka kwa uzalishaji kumemuumiza mkulima kwa sababu uzalishaji umeshuka, lakini kumeiumiza Serikali. Sasa siyo vibaya kurekebisha. Ni ombi langu kwamba Serikali ifanye marekebisha badala ya kwenda kumkata mkulima, chukueni fedha, shilingi bilioni 55 kati ya shilingi bilioni 200 au shilingi bilioni 300, rejesheni huku tukomboe zao la korosho lisife. (*Makofi*)



Mheshimiwa Spika, la pili, mfuko huu ulipoondolewa na Bodi ya Korosho ilivunjwa, huu mwaka wa tatu. Zao ambalo ndiyo linaloongoza kwa kuiingizia fedha nyingi za kigeni nchi hii kuliko zao lolote, mwaka wa tatu hakuna bodi. Mkurugenzi wa Bodi, yuko anakaimu.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya mimi nadhani Mkurugenzi amepewa kazi kubwa kuliko uwezo wake. Hii kazi imemshinda, mtafutieni kazi nyingine, tuteeni Mkurugenzi mwingine. Kwa sababu huyu Mkurugenzi anakwenda kule, anafika mahali akibanwa na wakulima anaanza kutoa majibu ya kiburi kabisa. Sasa zao ambalo ndiyo linawaingizieni fedha; mwaka wa tatu huu kuunda bodi tu inashindikana; tuna lengo gani na zao hili? Hili zao likifa tunapata nini? Tuundieni bodi, tutafutieni Mkurugenzi mwenye uwezo, tutengenezeeni mambo.

Mheshimiwa Spika, la tatu, mwaka ule wakati tunaanza kuhamasisha kulipeleka hili zao mikoani, wako wananchi waliohamasishwa kutengeneza miche ya korosho; na kati yao kwanza wengi hawajalipwa, lakini kati yao walikuwepo Watumishi wa Umma. Mkoa wa Lindi wako saba, nchi nzima wako 24. Wameingia mkataba na Bodi ya Korosho.

Mheshimiwa Spika, maajabu kabisa, wameshazalisha miche imechukuliwa imesambazwa, wanaambiwa wao hawakutakiwa kuzalisha. Kwa nini mliingia nao mkataba? Kwa nini mmechukua miche yao? *Why don't you pay them today?* Uharamu unapatikana baada ya kuchukua miche na kusambaza. Eti ni Watumishi wa Umma! Kwani Mtumishi wa Umma akizalisha akapata hela ya ziada, dhambi iko wapi? Mimi nadhani hii ni roho mbaya tu ambayo haina sababu. Tengi fedha, walipeni hawa watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mapendekezo yangu, msimu huu ambao pengine muda wa kurekebisha sheria unaweza ukawa haujafikia na bahati nzuri Kamati imependekeza...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Malizia kwa sentensi moja.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Kamati kwa kupendekeza jambo hili, mfuko wa kuendeleza zao la korosho urudishwe. Kabla haujarudishwa, tupeni shilingi bilioni 55 mkalipie pembejeo, ile iliyobaki rekebisheni.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Nape Nnauye.

Mheshimiwa Waziri utakapokuja kuhitimisha hoja, kwa kweli mambo haya kimsingi yalivyokuwa tutapenda tusikie Serikali inasema nini? Kesho wakati wa mafungu, *inshallah* nitakuwa nimekaa hapa, wakikubana na mimi sina nanii; ni-*declare* bahati mbaya nami ni mkulima wa korosho. Kwa hiyo, kesho, tunataka kidogo ili tuende mbele kwenye suala la korosho. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Hamis Kigwangalla, atakuja Mheshimiwa Conchester Rwamlaza na Mheshimiwa Luhaga Mpima ajiandae.

**MHE. DKT. HAMIS A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa leo ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge lako Tukufu, toka tumalize miaka mitano iliyopita ambayo pia nilipata heshima ya kuwa Mbunge wa Jimbo la Nzega Vijijini, naomba nianze hotuba yangu kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai. Pili kwa kuwashukuru wanachama wenzangu wa Chama cha Mapinduzi wa Jimbo la Nzega Vijijini na wananchi wenzangu wote wa Jimbo la Nzega Vijijini

kwa kunipa heshima ya kuwa Mbunge wao kwa kipindi kingine cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, pili nikushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa fursa ya kuzungumza katika hoja hii ya Waziri wa Kilimo siku hii ya leo. Jambo la kwanza ambalo napenda kulizungumzia linahusiana moja kwa moja na uelekeo wa kilimo cha umwagiliaji kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania na Bara la Afrika kwa ujumla wake limejaliwa kuwa na bahati ya kuwa na maji mengi ya baridi, siyo maji ya chumvi. Ukienda katika nchi ya Israel utakuta kule wanafanya *treatment* ya maji ya chumvi kuyafanya yawe ya baridi ili waweze kumwagilia, lakini sisi hatuna haya ya kufanya hivyo katika mito mirefu na maziwa makubwa duniani, 10 bora duniani, Tanzania imeajliwa kuwa nayo sita. Kwa hiyo, katika vyanzo vya maji baridi Tanzania tuna mtaji mkubwa ukilinganisha na nchi zote ambazo zinatuzunguka na hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nalisema hili kwa sababu naamini tunapoelekea tutashuhudia zaidi vita nyingi zikisababishwa na ukosefu wa maji baridi kuliko vita hizi za mafuta na gesi ambazo tumezishuhudia katika kipindi tulichopita, wanaziita *water wars*. Sasa ili tusiende huko, lakini pia tuweze kuitumia *resource* ya maji ambayo tumejaliwa by *virtual of being Tanzanians* na kuwa na hii *land scape* nzuri ni lazima kwanza tujipange kuhifadhi vyanzo vya maji hususani maji baridi.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni lazima tupange kufanya matumizi endelevu na yenye faida kwa vizazi na vizazi vya nchi yetu. Sababu kubwa ni moja, leo hii tunawekeza kwenye kilimo, watu wetu tunawahamasisha walime ambao ni zaidi ya asilimia 70, lakini mwisho wa siku hatupati *yield* ya kutosha kwa ajili ya ku-*sustained* chakula cha ndani, lakini pia kwa ajili ya kuuza nje, wakati tuna vyanzo vya maji baridi vya kutosha kuliko nchi zote zinazotuzunguka hapa jirani.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo nataka niishauri Serikali kwamba katika Awamu hii ya Tano iliyopita na sasa tumeingia

ya Sita, bahati nzuri Rais aliyeko sasa alikuwa sehemu ya Awamu ya Tano, imefanyika miradi kabambe mikubwa ya kihistoria ambayo inaweka *legacy* ya Serikali ya Awamu ya Tano kwa kiasi kikubwa sana. Napenda kuishauri Serikali iwekeze kwenye kilimo cha umwagiliaji kama *legacy* ya Serikali ya Awamu ya Sita, tutoke kwenye kilimo cha kutegemea mvua, kwa sababu kilimo cha kutegemea mvua kimesha-*prove* kwamba hakiwezi kutupeleka popote.

Mheshimiwa Spika, wakati sisi tunazaliwa na kukua pale Nzega, kiwango cha mvua kilikuwa kinazidi milimita za ujazo 2,000. Leo hii kiwango cha mvua kipo kati ya milimita za ujazo 600 mpaka 900. Ni kiwango ambacho hakiwezi kuivisha mazao ya mahindi mpaka kufikia mwisho na kuvuna. Kwa maana hiyo wananchi wetu ambao walizoea kulima kilimo cha kutegemea mvua wanalima mahindi leo hii wakiendelea na utaratibu huo wa kulima mahindi, hawawezi kuvuna. kwa hiyo, ni lazima sasa tubadilishe utaratibu, twende kwenye kilimo cha umwagiliaji na cha uhakika Zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nazungumzia huu unapaswa kuwa ni mradi kabambe ambao utaweka *legacy* ya Serikali ya Mheshimiwa Mama Suluhu Hassan ya Awamu ya Sita ni kwa sababu, vyanzo vya maji tulivyonavyo; Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Ziwa Victoria na mito yote ambayo inatengeneza haya maziwa na inayoingia baharini, kama tukitumia ipasavyo na tukitumia mabonde tuliyojaaliwa na Mwenyezi Mungu tunaweza kuwa *godown* la chakula la Ukanda huu wa Afrika na hata kupeleka nchi nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wazo langu ni kwamba, leo hii tunajadili sana, kila Mbunge akisimama anazungumza naomba maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, kuna baadhi ya vijiji havina maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Kwa nini tusiwe hapa Bungeni Wabunge tunajadili kuletewa maji kwa ajili ya umwagiliaji, kwamba tujenge mabomba makubwa ambayo mtu mrefu kama mimi naweza nikatembea ndani yake kutoka Ziwa Victoria, kutoka Ziwa

Tanganyika, kutoka Ziwa Nyasa tuyatawanye mpaka huku Dodoma, Dodoma kuna ardhi nzuri, lakini hakuna maji, mvua ni chache. Kama tukileta maji kutoka Ziwa Victoria ama maji kutoka Ziwa Tanganyika maana yake yatapita mikoa yote ya huko Magharibi mpaka kufika hapa Dodoma na tutamwagilia na tutalima kwa uhakika, hata wale wafugaji wanaohamama hawatakuwa na haja ya kuhama kwenda maeneo mengine ambayo yana vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wazo hili linaweza kuonekana ni wazo gumu kutekelezeka, lakini ni wazo ambalo linawezekana. Kama Israel leo hii wana-*treat* maji chumvi kuyapeleka kuwa maji baridi ili wafanye kilimo cha umwagiliaji kwenye nchi ambayo ni kame, kwa nini sisi tushindwe kutumia maji baridi ambayo tayari tunayo, *arable land* ambayo tunayo, tunakwama wapi?

Mheshimiwa Spika, mfano kule kwetu, kuna bonde maarufu sana linaitwa Bonde la Isagee, nimeona Wizara wanatujengea pale *godown*, kijijini kwangu Puge, ulipita pale na lile godown likijengwa pale maana yake liko kwenye *catchment area* ya walimaji wazuri wa nafaka ikiwemo mpunga na mahindi. Hata hivyo, kilimo kinachofanyika pale kwa kiasi kikubwa kinatoka kwenye hili bonde la Isegenhe kwa nini bonde kama lile lisipate maji ya uhakika kutoka kwenye mito na maziwa ya maji baridi ambayo yanatuzunguka hakuna sababu kwa nini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. DKT. HAMIS A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana Dkt. Hamis Kigwangalla. Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, atafuatiwa na

Mheshimiwa Luhaga Mpina na Mheshimiwa Aida Khenani, ajiandae.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia machache juu ya hoja iliyopo mbele yetu ya bajeti ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye huduma za ugani katika nchi yetu. Tunapofikiria kilimo na hasa kwa wanakijiji huku ngazi ya chini, tunahitaji Maafisa Ugani ili wananchi, hawa wakulima waweze kufundishwa na ni tabia ya wanadamu kwamba kila wakati wanapenda kufundishwa kupewa utaalam. Kuna uhaba mkubwa wa Maafisa Ugani. Kwa mfano, nchi nzima mpaka sasa hivi imeajiri Maafisa Ugani 6,700. Kwa hiyo, kuna upungufu mkubwa wa zaidi ya 14,000 na ushee ya Maafisa Ugani katika nchi yetu. Kwa hiyo, ukija kuangalia waliopo ni kama asilimia 36 tu.

Mheshimiwa Spika, hatutegemei kilimo chetu kitakua hasa kwa ngazi ya chini kama hatuna wataalam wa kusaidia wakulima. Mambo ya zamani hayawezi kwenda wakati huu, lakini tunaweza kuchukua mambo mazuri ya zamani tukachanganya na mambo ya sasa hivi. Hebu tuchukue Awamu ya Kwanza ya Nchi yetu ilikuwa inapelekaje kilimo. Tuangalie miaka hiyo na sasa tuchukue yale mazuri. Kwa mfano, sisi ambao tuna umri wetu tulishuhudia ni namna gani Mabwana Shamba walikuwa wanafika katika mashamba ya wazazi wetu kufundisha kilimo cha migomba kwa mfano Mkoa wa Kagera, kilimo cha kahawa na mambo mbalimbali. Kwa hiyo, tuna haja ya kuhakikisha kwamba tunaajiri Maafisa Ugani ili waweze kusaidia wakulima wetu, tuone kama kilimo hiki kinaweza kuleta tija na wakulima wanaweza kuzalisha vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu tunajua mashamba tuliyonayo siyo mashamba makubwa na nchi hii imeweza kutunzwa na wale wakulima wadogo ambao wanaitwa *small scale farmers*, wamelima wemeweza kulisha nchi hii, kwa hiyo wanahitaji utaalam, wanahitaji Maafisa Ugani katika kila kijiji kama mwongozo wa ugani ulivyo

katika nchi yetu. Kwa hiyo, tunahitaji pia maafisa ugani hawa wafundishwe mbinu za kisasa. Kwa sababu kilimo tunachoendesha kipindi hiki ni *owner's risk*, kila mtu anafanya anavyoona. Haya mashamba darasa aliyoyataja Mheshimiwa Waziri hapa hayapo na kama yapo yanafanya kazi kwa wakati ule na yanatumia pesa nyingi.

Mheshimiwa Spika, mimi nalima migomba siyo mingi, lakini nina shamba la migomba sijawahi kabisa katika kijiji changu kuona Afisa Ugani hata mmoja. Kwa hiyo kila mtu anafanya anavyotaka na anavyoona inafaa. Kwa hiyo natoa ushauri kwamba, Serikali ijitahidi kuhakikisha kwamba tunapata ugani, tunapata wataalam, wapo vyo ni vingi, watoto wetu wanasoma, hata kule Bukoba ukienda kwenye Chuo cha Maruku pale watu wanamaliza kila mwaka, lakini hawana mahali pa kwenda na wale walio na kazi sasa hawana vitendea kazi. Hawana hata zile *kit* wanazosisema zile za kupima udongo hawana. Hawana usafiri, wamekaa maofisini, hata hawa 6,000 tunaowasema wapo maofisini kule kwenye kata, hawaendi vijijini kwa sababu hawana usafiri.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye ushirika; nimesoma ukurasa wa 11 ya hotuba ya Waziri, ametaja idadi ya watu walioingia kwenye ushirika kutoka milioni tano kwenda milioni sita. Hoja yangu ni kwamba, hapa tusingalie idadi ya wananchi ambao wanajiunga katika ushirika, tuangalie kazi ya ushirika ni nini na ufanisi wake.

Mheshimiwa Spika, ushirika wa sasa hivi kazi yake ni kununua mazao na kuuza, hawasaidii katika kuhakikisha wakulima wanapata *production*. Nategemea kwamba ushirika kama ulivyokuwa wa zamani ungeweza kuwa wa mashamba ya miti, ungeweza kuwa na Maafisa Ugani pia.

Mheshimiwa Spika, naangalia Chama cha Ushirika cha Kagera *by then BCU*, kilikuwa na Maafisa Ugani, kilikuwa na nyenzo zake, Serikali huku na ushirika huku. Kwa hiyo, ina maana kama ushirika wenyewe utafanya kazi ya kununua na kuuza, hawasaidii hata kidogo katika *production*

kwamba, je, wakulima hawa ambao wanatuuzia mazao wanalima na wanapata mazao mazuri? Kwa hiyo, naishauri Serikali kwamba ushirika pamoja na Wizara ya Kilimo wafanye kazi kwa pamoja ili watakaposhindwa kuajiri Maafisa Ugani, ushirika uajiri Maafisa Ugani wake. Pia ushirika utafute masoko, huko nyuma ushirika ulikuwa unatafuta masoko, masoko hatuwezi kuwaachia Serikali peke yake.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa natazama leo, kwa mfano, sisi Mkoa wa Kagera tunauza kahawa au tuseme wakulima wanauza kwa Sh.1,200 sasa hivi, lakini kwa bei ya leo ninapokwambia Uganda wanauza kahawa au wananunua kahawa ya kulima kwa Sh.1,500/= mpaka Sh.1,700/=. Je, nani anaangalia *everyday exchange*, kwa sababu ukiangalia wao sasa hivi kwa bei ya leo ni 0.67 dola, mpaka 0.7 dola. Sasa kama Serikali haiwezi kutafuta masoko, basi na ushirika na wenyewe wawajibike katika kuhakikisha kwamba wakulima wanapewa bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, leo Mheshimiwa Anatrofia aliuliza swali kuhusu masoko ya Mkoa wa Kagera, lakini walitambua kutokuwa na masoko katika mipaka kwa mfano, Mtukula pale, nani anawajibika, ni Serikali, ni Wizara ya Kilimo au ni Wizara ya biashara? Kwa hiyo, wote kwa pamoja wanaweza kuliangalia hilo. Kwa mfano, ukienda Mtukula tunavuka sisi watu watu wa Kagera kwenda kununua bidhaa Uganda, lakini hatuna Waganda wanaokuja kununua huku kwetu.

Mheshimiwa Spika, ina maana kungekuwa na soko pale mpakani ni kwamba tungekuwa tunapeleka michele pale pale, halafu Waganda wenyewe wanakuja kule kule kwetu wanakuja kununua, lakini tuna ndizi. Ukienda Uganda, ukienda Entebe *Airport* pale unakuta ndizi zinasafirishwa kwenda Arabuni, lakini sisi Mkoa wa Kagera hatuna soko kwa hiyo, tunaomba Wizara ya Kilimo isaidie katika kutafuta masoko, ushirika usaidie katika kutafuta masoko kuonyesha kwamba hata sisi katika mkoa wetu tuna uwezo wa kupeleka ndizi zikaenda kuuzwa katika nchi za Uarabuni, Oman, Saudi Arabia na nyinginezo.



Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema kingine ni kilimo chetu hiki katika nchi yetu kina mtazamo gani yaani *perception* yake. Je, kizazi hiki kilichopo kinaonaje kilimo, kizazi hiki kilichopo kinaona kilimo kama adhabu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsate sana Mheshimiwa Conchesta, ulikuwa umefikia *point* muhimu kweli, lakini muda hauko upande wako.

Mheshimiwa Luhaga Mpina na Mheshimiwa Aida, jiandae.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi. Naamini kabisa tunakubaliana kwamba Sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi ni sekta muhimu sana kwa Taifa letu na ndiyo maana tunasema tunachangia asilimia 25 ya fedha za kigeni, lakini zinachangia asilimia 30 ya pato la Taifa, zinachangia asilimia 65 ya ajira na zinachangia asilimia 100 ya chakula.

Mheshimiwa Spika, tunakubaliana pia kwamba kwa mwaka tuna wastani sasa hivi wa kuagiza chakula cha thamani ya trilioni 1.3. Sasa tu niseme nimesikia hapa wadau wazalishaji wa mbogamboga, matunda, maua na viungo wako kwenye Bunge lako hili. Nachukua nafasi hii kuwapongeza sana kwa sababu kati ya sekta ambazo zimefanya vizuri katika miaka mitano iliyopita 2015 - 2020 ni hiyo sekta ya wazalishaji hao ambao nimesikia wapo hapa pamoja na CEO wao Jacqueline Mkindi ambao uzalishaji ulikuwa milioni 400 tuliweza kuuza maouzo yetu ya nje milioni mia nne kumi na mbili mwaka 2015 ilipofika mwaka 2020 tayari wameshafika milioni 779, karibu mara mbili. Kwa hiyo, ni moja ya eneo linaenda vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, tunazungumza hiki kilimo chetu cha wananchi wetu hawa ambacho kimekumbwa na mzigo mkubwa wa matatizo, kimebeba mzigo mkubwa wa

matatizo. Hapa wenzangu wamezungumzia suala la watumishi, watumishi wamesema wako 6,000 na kitu hapa, lakini wengine wako wilayani, hawapo kwa wakulima kwa hiyo tuna vijiji karibu 7,000, havina Maafisa Ugani. Sasa kama huna Afisa Ugani, ni nani anawaongoza wananchi wako, nani anakagua magonjwa ya wananchi katika mimea yao, nani anayewaongoza wakulima kupata mbegu bora, nani anayetibu mimea yao na kama hakuna wa kutibu na sisi ndiyo tunasema hili eneo ndiyo uti wa mgongo, ni uti wa mgongo gani ambao hauangaliwi hata ukipata magonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tuna suala hili la mbegu bora. Mheshimiwa Waziri amezungumza mambo ya mbegu bora hapa. Kwanza mbegu zinazozalishwa ni chache na hazitoshi, lakini gharama yake ni kubwa sana, tatizo la gharama limetatulijawe? Mbona hatujaelezwa kwenye hotuba yake kwa sababu wananchi wengi wanashindwa kununua mbegu kwa sababu ya gharama kubwa sana, kilo moja unaambiwa Sh.6,000/=, Sh.7,000/= au Sh.8,000/=, nani atanunua? Kamfuko kamoja ka kilo mbili unauziwa Sh.10,000/ na zaidi nani atanunua?

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ni kubwa sana, Wabunge wenzangu wamezungumza hapa, ni suala la bei na suala la masoko. Wananchi wetu wana tatizo kubwa sana la masoko na tatizo linalotupeleka kwenye masoko hapa ni kwa sababu tunauza malighafi nje ya nchi. Tutaacha lini kuuza malighafi katika masoko ya Ulaya, tutaacha lini kuuza malighafi masoko ya China, India na sehemu zingine za AGOA na kwingine na kwanini tuendeleo kuuza malighafi? Ni lini tutajenga viwanda vyetu wenyewe na kwa nini tusiamue leo na kukataa kuuza malighafi nje ya nchi? Tukiua malighafi nje ya nchi wananchi wetu wananyonywa bei, wananchi wetu hawapati kipato kinachostahili, ajira tunaziua nje, Watanzania wanageuka kuwa manamba wa kufanyia kazi viwanda vya nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kujenga viwanda vya kimkakati shida kubwa ni mitaji kwa baadhi ya watu. Nani atakuja

akujengee kiwanda hapa cha pamba wakati pamba anaweza akaichukua kwa bei ya kutupa, akaipeleka China, aka-*process*, akakuletea nguo, pamba ya s Sh.3,000/= akaja kukuuzia shati la Sh.50,000/= au Sh.100,000/=, nani atakuja kujenga kiwanda hapa? Kwa nini tusifanye maamuzi kama tulivyofanya kwenye umeme au kama tunavyofanya kwenye miundombinu ya barabara? Tukajenga viwanda hapa, tunajenga kiwanda kikubwa cha nyuzi, tukajenga kiwanda cha nguo, tukajenga kikubwa kiwanda kikubwa cha korosho kwa kutenga fedha zetu wenyewe, hata kama sisi Serikali tusipoendesha Watanzania wako wa kuendesha./ Tunajenga kiwanda kama ni cha bilioni 100, tunawakabidhi Watanzania waendeshe.

Mheshimiwa Spika, pia tunaweza kuwapa mikopo ya masharti nafuu, hata ya miaka 30, tatizo liko wapi? Leo hii tungekuwa na viwanda vyetu tusingekuwa tunapata matatizo haya, wananchi wetu wangenufaika kwa bei nzuri, lakini Taifa lingepata kodi nzuri katika eneo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tu ya muda, niseme pia kwamba, viwanda hivi tunaweza kuvijenga, lakini tatizo tulilionalo lingine ni ulinzi wa viwanda vyenyewe, viwanda vingi vilikuwepo, vingine vimekufa, vingine vimefungwa na wawekezaji wengine hawatakuja. Moja linalofanya viwanda vyetu viwe na changamoto kubwa ni mfumo wa kodi mbaya, *unsupportive taxation regime* yetu haifanyiwi tathmini mara kwa mara. Unaweza kukuta wakati mwingine hata mazao ya kutoka nje ya nchi yanakuwa *exempted*, wazalishaji wa ndani wanapigwa kodi, wale wanaoingiza mazao hayo ndani ya nchi na bidhaa hizo ndani ya nchi wamesamehewa. Sasa atashindanaje mwenye kiwanda hapa ndani? Hawezi kushindana.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa huu mfumo nilitegemea Wizara ya Kilimo wangeleta tathmini hapa ya kodi ambazo zina changamoto kubwa, tuna changamoto kubwa sana kwa mfano kwenye maziwa, ngano na kadhalika. Wazalishaji wa ndani ya nchi wanapigwa kodi lakini wanaoingiza wanasamehewa kodi, sasa nani atawekeza

viwanda ndani ya nchi yako. Matokeo yake tuna mfumo wa ku-favour watu wanaoingiza bidhaa ndani kuliko wale wanaozalisha wakauze ndani. Huwezi kupiga hatua kwa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni ulinzi wa viwanda vyenyewe, viwanda hivi vinalindwaje wakati bado kuna *importation* kubwa ya mazao mengine kutoka nje ambayo sambamba na haya yanayozalishwa hapa nchini, mengine yanaingia holela bila kufuata utaratibu, hawalipi kodi wala hawafanyi chochote, wanaingiza na kuuza mazao hapa. Ulinzi unafanywaje na Wizara ya Viwanda na Biashara, ulinzi unafanywaje na Wizara ya Kilimo, ulinzi unafanywaje na vyombo vyetu vya dola, hapa kuna viwanda vinakufa kwa sababu ya kukosekana kwa ulinzi wa kulindwa viwanda hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hata mipango yetu mingine tunaanza tena, wananchi wanahangaika kuuza hiyo malighafi, tunaleta ushirika wa kuu wanunuzi wengine, unatengeneza ushirika wa kwenda kuu wanunuzi wengine, matokeo yake wananchi wanakopwa mazao yao hawalipwi, wengine wanapoteza kabisa fedha zao na wengine wanacheleweshwa fedha zao halafu kwenye Kijiji kimoja wanakuwepo wanunuzi wapo kumi unaenda kuamua awe mnunuzi mmoja; unaua ajira zote, Na Waziri hapa kwenye hotuba yake anazungumza ana... (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** ...anazungumza mambo ya ajira ya vijana wakati umeenda kuu ajira za vijana kwa kuthamini ushirika peke yake na kuwaondoa vijana waliokuwa wamejajiri; kwa nini usiweke ushirika wenye pesa na vijana wanaonunua kivyao wakanunua halafu wakashindwana kwenye bei, wananchi wakaenda kuuza kwenye bei nzuri iliyokubwa aidha ya ushirika au ya mtu wa kujitegemea, tatizo liko wapi? Sera zetu zinakinzana na tunachotaka kufanya. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Aida Khenani atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Lulida

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na pia namshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kunifikisha siku ya leo niweze kuchangia Wlizara muhimu si kwa wananchi wa Mkoa wa Rukwa peke yake bali Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, toka nimeingia kwenye Bunge hili, Wizara ya Kilimo kila ilipowasilisha bajeti yake nimechangia toka nikiwa Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuzungumza niwashukuru sana kwa sababu hotuba zao zote wanapowasilisha huwa zinakuwa nzuri ila shida inakuwa kwenye utekelezaji wa hizo hotuba zao ambazo wanazileta ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaanza na Mkoa wangu wa Rukwa, Mkoa wa Rukwa ni miongoni mwa Mikao inayozalisha zao la mahindi kwa kiasi kikubwa sana lakini leo Mkoa wa Rukwa tunaliona zao la mahindi ni kama zao la laana kwenye Mkoa wetu wa Rukwa. Pamoja na kwamba ni Mkoa wa Rukwa na mikoa mingine ya nyanda za juu kusini na mikoa mingine Tanzania inayozalisha mahindi ningependa kujua hapa kwenye hotuba yako umezungumza kidogo sana Mheshimiwa Waziri. Kama zao la mahindi ni zao ambalo kwa sasa mmekosa ufumbuzi wa soko njooni na zao mbadala wananchi waachane na mahindi; wanatumia gharama kubwa kununua pembejeo na haiendani na bei halisi ya mahindi tunayolima sisi watu wa nyanda za juu kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo mwananchi anakwenda tena kuvuna mahindi ya mwaka huu wakati msimu uliopita mahindi yapo ndani. Natambua kwamba Serikali haiwezi

kuwapangia bei lakini ni wajibu wa Serikali iliyopo madarakani kuhakikisha wananchi wake wanapata masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo ningependa Wizara mnapokuja mtuambie ile mbegu ya mahindi inayotoka Zambia kama mmeiona ndiyo mbegu bora waambieni Watanzania na wakulima wa zao la mahindi wajue kwamba mbegu ile ndiyo inayostahili kwa sababu leo kama kweli wanafanya tafiti Wizara ya Kilimo, mbegu inayotumika na inayopendwa Zaidi ya wakulima wa nyanda za juu kusini ni mbegu inayotoka Zambia. Leo wakiamua kufanya jambo lolote mkumbuke kwamba tupo kwenye ushindani wa masoko, mnategemea wakulima wa Tanzania watakuwa kwenye hali gani. Ni vizuri mkafanya tafiti na mje na mkakati wa ziada kwenye jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kibaya zaidi mbegu hizo zinapitishwa kwenye njia za panya. Serikali pamoja na kwamba Wizara ya Kilimo mnashirikiana na Wizara mbalimbali hapa kwenye majukumu yenu ni pamoja na kulinda hali ya wakulima pamoja na mbegu.

Mheshimiwa Spika, kwa hali ya kawaida kuna maazimio mbalimbali ambayo kama Watanzania tumeshiriki, Azimio la Maputo ya Nchi za Afrika la mwaka 2014 pamoja na nchi yetu ilishiriki ambapo maazimio yalifanyika kwenye kwa nchi zote za Bara la Afrika. Katika maazimio hayo ilikuwa ni pamoja na kuweka mahususi Sera za Kilimo ambazo zitaenda kuondoa umaskini kwenye Bara la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia kwenye utekelezaji wa bajeti zetu na hayo maazimio ilikuwa ni kufikia mwaka 2025, leo tupo 2021. Nitatoa mfano tu kwenye utekelezaji wa bajeti, miaka mitano mfululizo bajeti ya mwaka 2016/2017 ilitokelezwa kwa asilimia 2.22, 2017/2018 asilimia 11, 2019/2020 asilimia 15 na 2020/2021 asilimia 26.46. Kwa maana hiyo miaka mitano imetekelezwa kwa wastani wa asilimia 19.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana nyingine miaka mitano Wizara ya Kilimo utekelezaji wa bajeti pamoja na kwamba tunatenga lakini imeweza ina maana kwamba asilimia 80.7 bajeti hii utekelezaji wake imeshindikana kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wetu kutenga bajeti lakini ni wajibu wa Serikali kupeleka fedha kama Bunge lilivyotenga. Na hapa kumekuwa na changamoto, kutenga bajeti ni jambo moja na utekelezaji wa bajeti hiyo ni jambo lingine. Tumekuwa na kauli mbiu nyingi Kilimo ni Uti wa Mgongo, kilimo sijui ni kitu gani sisi hatuna shida na *slogan*, tuna shida na utekelezaji wa kilimo. Na kama kweli lengo ni kuwasaidia vijana wa nchi hii, tunawezaje kutekeleza suala hilo kwa kupeleka fedha kama hizi kwenye maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine, mbegu hiyo ambayo leo kaka yangu Mheshimiwa Mhagama alisema katika vipaumbele vyenu vya Wizara kwamba ni vizuri mnganza na masoko. Narudia tena katika michango yangu yote ya miaka yote pamoja na kutafuta masoko, lazima tuwekeze kwenye utafiti kwenye suala la kilimo. Hauwezi kutafuta masoko kama mbegu zako asilimia 60 ya Taifa hili ya mbegu tunaagiza kutoka nje, haiwezekani. Tunaingiaje kwenye ushindani wa masoko kama mbegu ndo hizi asilimia 60 unategemea kutoka nje, tunaaminije wale watu wa nje watafanya sisi tuongoze kwenye biashara kwenye mazao tunayolima wakati wao ndio wanatuletea sisi mbegu kwa asilimia 60. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba mnajitahidi, Waziri na Naibu wako lakini mtajitahidi kama mnapewa fedha kama tunavyokuwa tumetenga ndani ya Bunge. Haitawezekana kwa maneno matupu kufikia malengo ambayo tumejiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, kupitia Ripoti ya CAG kuna mambo kadhaa ambayo yamezungumzwa pale na katika mambo hayo ni pamoja na udhibiti mbovu

wa mbegu na pembejeo kutoka kwenye Wizara yako. Sasa kama malengo ni kusaidia Taifa letu, hatuwezi kushindwa kudhibiti tukategemea malengo/matokeo chanya kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali, ni vizuri kama kweli tunaamini kipaumbele kitakwenda kukomoa umaskini wa Taifa letu, tuweke kilimo kama kipaumbele kwa kuwapatia fedha, pembejeo lakini tukawekeze kwenye tafiti kwa kupima udongo kama nyanda za juu kusini imeshindikana mahindi, tujue ni zao gani ambalo tutapeleka iwe mbadala wa mahindi lengo tu ni kuondoa umaskini na kuwasaidia wakulima wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia pamoja na hayo, wakulima hawa wana hali ngumu sana. Tunapozungumzia mikopo ya kilimo, hiyo Benki ya Kilimo hebu mje siku moja mtuambie hapa mikoa hii ambayo inazalisha sana ni wakulima wangapi wamenufaika na mikopo inayotokana na Benki ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna danadana nyingi lakini ukiangalia maneno kwenye hotuba mbalimbali inaonesha kabisa fedha zinatoka, zinakwenda, zinakwenda kwa nani mbona hatuyaoni matokeo kwa wakulima wetu kama kweli wanapewa hiyo mikopo? Kuna mazingira ambayo lazima tubadilishe pamoja na kwamba vipaumbele vinakuwa vingi, tuje na kipaumbele kimoja ambacho lengo ni kumkomboa mkulima na Mtanzania, ahsante sana nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Aida Khenani, mmh hii bunduki hii ndiyo maana Mzee Keissy kumbe, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Riziki Lulida tafadhali.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana na nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyenijaalia kunipatia afya njema na kuwaombea Wabunge wenzangu Mwenyezi Mungu awabariki sana tusimame kwa



Pamoja tuweze kuwasaidia wakulima ambao wengi wanahangaika na wakiwa katika mazingira magumu ya mafanikio yao. Msimamo wa Wabunge kuwasaidia wakulima utainua uchumi na kumsaidia Rais wetu katika kuleta maendeleo yaliyokuwa ya kweli.

Mheshimiwa Spika, bado ni mtoto ambaye nimezaliwa katika zao la korosho, korosho ndio zao la kwanza toka tumepata uhuru ukichukulia madini tunaweza kupata fedha za kigeni. Kutoka mwaka 1961 tunapata uhuru mpaka mwaka 2017 zao la korosho lilichezewa danadana sana, tulikuwa tunapata haizidi bilioni 141. Lakini mwaka 2017 baada ya kusimamia mifumo na kuona hapa tunapigwa tuliweza kuuza korosho kwa dola milioni 530 tukapata trilioni 1.2 ikaitwa dhahabu ya kijani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii dhahabu ya kijani haikuja hivihivi, ilikuja kwa kusimamiwa; tujulize kwa nini tuliweza kuleta mafanikio ambayo yalichezewa kwa muda wote pana kundi hapa linacheza na wakulima ambao hawawataki mema wakulima.

Mheshimiwa Spika, wakulima hawa unaowaona wanapalilia mashamba yao kwa hela yao, wananunua pembejeo kwa hela yao lakini siku ya stakabadhi ghalani mabenki yote yapo pale na wafanyabiashara wote wapo pale wanataka kuhakikisha mkulima huyu kazi aliyoifanya wao wawe wanufaika zaidi kuliko wao, haikubaliki. Huu ni unyonge wametufanyia kwa miaka mingi hatukubali, nataka niwe mkweli na ni mzalendo wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna lugha wanazungumza wafanyabiashara wanaonewa, sikubali kama wafanyabiashara wanaonewa, wanaonewa katika kilimo ni wakulima sio mfanyabiashara. Kama tuliwezanyonywa kuhakikisha tunapata bilioni 141 zaidi *vis-a-vis* ya trilioni 1.2, nani alimuibia mwenzake hapa? Aliyeibiwa hapa ni mkulima. Watanzania tufunguke, hali ya uchumi wetu tunaweza kuusimamia na tukaweza kutoka hapa, tuache longolongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, viwanda, biashara na kilimo vinakwenda sambamba; leo enzi ya Mwalimu alitengeneza mifumo ambayo tungeenda nayo mpaka sasa hivi tungeruka. Mikoa yote inayolima korosho tulikuwa na viwanda, viwanda vyote vimefungwa mpaka leo hatujui mwisho wake ni nini. Tumemnyima ajira Mmakonde, Mngoni, Myao na mtu wa Liwale kwa ajili ya uhuni wa kibiashara halafu mnasema wanaonewa, nani anamuonea? Tuachane na lugha ambazo zinatufanya tuna- *paralyze* katika akili na mifumo yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tumeonewa sana katika kilimo halafu bado wameonewa, wameonewa; amemuonea nani, wao walizoea kutuonea. Korosho ilikuwa inauzwa shilingi 600 lakini ghafla mwaka 2017 korosho iluzwa 3200, nani alikuwa anamuonea mwenzake? Na hiyo 600 kuipata kamilifu haiwezekani, tukapata hela ya mfuko. Mfuko wa kwanza ilikuwa bilioni 97 macho yalianzia hapo, baada ya kuona bilioni 97 pakaleta siasa za uongo na vitu mbalimbali ambavyo vilifanya zile hela hazikumsaidia tena mkulima, korosho imeanguka chini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mikoa iligawanyika kwa ajili ya mazao yanayolima, kahawa Kilimanjaro, Kagera na Mbeya, korosho Lindi, Mtwara, Ruvuma na Pwani tuendeleze hapa kwanza na mikoa ya Tanga ya Pwani ambayo hali ya hewa yao inakwenda sambamba na korosho. Leo tumeitoa korosho tukapeleka sehemu ya baridi unafikiri korosho inastawi, haistawi, itaota lakini haitakuwa na *yield* ya kutosha. Sasa hela zikagawanyishwa peleka huku, peleka huku matokeo yake mkulima wa korosho aliyesafisha shamba na kutafuta pembejeo yeye mwenyewe inapatikana hela hana thamani tena, hela ya mfuko inapelekwa sehemu zingine mkulima wa korosho ameachwa anahangaika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nililizungumza viwanda vilifungwa makusudi na wawekezaji na wawekezaji wapo humu ndani ni wafanyabiashara, wamevifunga mpaka leo havifanyi kazi maana yake hakuna ajira kusini. Tuambieni kusini kuna

kiwanda gani, Mkoa wa Lindi, Mtwara na Ruvuma hakuna viwanda nenda Tunduru viwanda vimefungwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ili achukue ile korosho anaipeleka nje kama *as a raw material*, malighafi na kule anapopeleka anasimamia kwa viwanda vya kule vitafanya kazi na itatoa ajira kwa watu wa kule sio kwa ajili ya mtu wa kusini. Tujiulize tunafanya nini, Watanzania tunasomesha vijana wana *degree* mbalimbali za kilimo lakini unaona bado tunahangaika na kilimo.

Mheshimiwa Spika, tunaomba viwanda vya korosho vifunguliwe tupate ajira ili matatizo ya kutaka korosho ile kuipeleka nje wanaotufanyia baadhi ya wafanyabiashara korosho ya Tanzania italiwa na Mtanzania humuhumu ndani na *brand* itatoka Tanzania. Leo *brand* ya korosho inatoka Sri Lanka wewe hujawahi kusikia vitu kama hivi; kahawa ya Tanzania inakuwa *branded* Uganda, parachichi la Njombe linakuwa *branded* Kenya, tuko wapi? Unaletewa wataalam wa shamba *shape* kuja kutusaidia kutoka Kenya, hivi hatuna vijana tuliwasomesha wanaojua suala la kilimo, tume-*paralyze*. Na kama hatujifungui kwa hilo nakwambia tutaendelea kupiga kelele na siasa ambazo hazitamsaidia mkulima. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mkulima anahitaji akombolewe, tulijua kuanzia mwaka 2017 tumeshatatua tatizo la korosho tungekwenda kwenye kahawa lakini leo kahawa ya watu wa Bukoba inauzwa Rwanda na Rwanda wanapata uchumi kwa kupitia mazao ya Tanzania, sisi wenyewe tupo wapi? Tunasema tuna asilimia 29, haiwezekani, hii ni asilimia ndogo sana sio ya kuridhika na kufurahia nayo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ufuta; zao la ufuta la pili...

**SPIKA:** Mheshimiwa Riziki muda haupo upande wako.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru naunga mkono hoja. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Riziki Lulida, leo Wabunge wakali kwelikweli. Mheshimiwa Katani hebu malizia hizi dakika.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, niungane na Wabunge wenzangu wanaotoka mikoa ya kusini. Moja niunge mapendekezo ya Kamati ya Kilimo kuhusu Sheria ile ya Mfuko wa kuendeleza zao la korosho ambao mwaka 2018 Spika ukiwa kwenye Kiti hicho ililetwa sheria ile tukaibadilisha Sheria Na.17A. Kamati imependekeza vizuri kwamba sheria ile irejeshwe ili kumlinda mkulima huyu ambaye asilimia 65 ya fedha ile ilikuwa inakwenda moja kwa moja kwenye pembejeo, Bodi ya Korosho na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, mheshimiwa Nape amezungumza jambo mahususi hapa kwa sababu kwa matamko ya Serikali yenyewe ilisema fedha zile bilioni 200 ilizichukua baada ya kuona Bodi ya Korosho imeshindwa kuzisimamia vizuri. Sasa na Serikali nayo imeshindwa kuzisimamia vizuri mara tatu kuliko yale yaliyokuwa yanafanywa na Bodi kwa sababu kwa miaka minne au mitatu tumeishi hatuna Bodi ya Korosho, fedha zimechukuliwa na Serikali, wakulima hawana pembejeo na uzalishaji umepungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe sana kwa sababu fedha zilitunzwa, tunajua zimetumika mahali pengine lakini Serikali igharamie pembejeo hizi ambazo leo Wizara imefikiria jambo jema lakini *approach* yake inakwenda kumuongezea mzigo mkulima. Unaposema mkulima aendelee kuchangia 110 wakati Serikali imechukua bilioni 200 ya fedha za wakulima, nadhani Waziri mwenye dhamana Mheshimiwa Bashe ulikuwepo na ulikuwa unaunga mkono kwamba wakulima wanadhulumiwa, sasa ukae na Serikali hiyo hiyo umepewa dhamana ya unaibu Waziri, Profesa ufanye kazi hii muiombe Serikali itupe bilioni 55/60 iende kulipa pembejeo wakulima wapate pembejeo mtakuwa mmewasaidia sana wakulima wa korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali inachukua bilioni 200 ilisema ingelipa gharama zote yenyewe, mwaka jana

Serikali imechukua tena shilingi 25 kuchangia gunia za fedha ya korosho 2017/2018. Fedha ambayo wameikata kwenye mjengeko wa bei toka mwezi wa kumi lakini mpaka leo hao wenye magunia hawajalipwa hiyo fedha, fedha imechukuliwa wanaodai magunia hawajapewa lakini ni Serikali ilibeba mzigo wote kwamba tungeweza kulipa korosho hizi fedha, tungelipa magunia; wenye magunia wanadai, watu wa pembejeo wanadai na fedha zimechukuliwa.

Mheshimiwa Spika, niombe kwa sababu tuna Serikali Sikivu sana, na Mawaziri mpo makini kwelikweli lakini sijui shida mnaipata wapi, shida mnaipata wapi? Kaeni na Serikali muiambie kwamba tulikopa fedha za wakulima wa korosho maana zile mlisema matumizi sio mazuri, haya matumizi sio mazuri mmeshindwa kuunda Bodi ya Korosho, kwa miaka mitatu hakuna Bodi ya Korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkaja na ngonjera nyingine ambayo siifikiri kabisa eti uunganishe bodi za mazao haya ipatikane bodi moja, tuache bodi za kila zao libaki lenyewe litashughulika vizuri kuliko hayo mambo anayokuja nayo yaani Bodi ya Korosho, Bodi ya Pamba, Bodi ya Nini utengeneze dubwana moja Mheshimiwa Rais ndiyo maana alimuondoa Meya wa Jiji la Dar es Salaam kwa kuona kwamba unatengeneza mtu amekaa tu pale kama picha, acheni tupate Bodi ya Korosho ambayo itasimamia zao na Sekta ya Korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana, Mheshimiwa Nape kawakumbusha hapa miche ya korosho ambayo imekuja mpaka Dodoma watu wake hamjawalipa, fedha zilikuwepo za kutosha, zilikuwa zinaweza kugharamia Sekta ya Korosho, lakini hatuna cha kujifunza. Msumbiji ambao wamekuja Tanzania kujifunza mfumo wa stakabadhi ghalani wanatoa pembejeo kwa wakulima bure kwa miaka 13 sasa, wamekuja kujifunza Taifa hili nyinyi waliokuja kujifunza ndiyo kwanza mnawaza tupate 110 tumkate mkulima, tufanye hivi, tunajifunza kutoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbona Ethiopia tulikojifunza sisi wanampa mkulima pembejeo bure, magunia bure, mabomba ya kupuliza korosho bure kila kitu wanafanya bure Serikali, mnapokusanya asilimia 15 ya *export levy* kwenye tani zile ulizokusanya 2016/2017/2018 laki tatu mnakusanya zaidi ya bilioni 144 ambazo mkichukua bilioni 55 mnaweza kugawa mapembejeo hayo na bado Serikali mkabakiwa na bakaa, mkawa mnamnyonya ng'ombe maziwa huku unamlisha.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali hii unamnyonya mkulima humlishi, mkulima huyu ataendeleaje? Mnasema asilimia 65 ya watanzania ni wakulima, wakulima ambao hawapewi pembejeo, wakulima ambao hawapewi magunia, wakulima ambao wakati wa kilimo hakuna mafunzo mnawapa, wakulima ambao kila jambo wanafanya wenyewe (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana, Mheshimiwa Waziri *translate* sasa u-*professor* wako kwenda kwenye vitendo vya kumsaidia mkulima, tusiwe tunajisifia ma-*professor* mpo tunakata ma-*professor* mtafsiri elimu yenu ije kwenye manufaa *add value addition* kwa wakulima wa korosho tutakaa tutapongeza tunama-*professor* chungu nzima, tuna madaktari chungu nzima, tafsiri elimu yenu kwenda kwenye *value addition* ya wakulima wa korosho, kwenye *value addition* ya wakulima wa mahindi, wakulima wamekuwa wakilalamika kila wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Taifa hili linautajiri wa kutosha kutoka kwenye kilimo, korosho tunayoisema hata Marehemu Mheshimiwa Rais, Mungu amrehemu alishasema kwenye korosho kama leo mtaamua kuwekeza vizuri kwenye korosho mkaleta viwanda, maganda ya korosho yanatengeneza *brake pad* ya kwenye magari tena *Mercedes – Benz*, maganda. Mafuta yanayotokana na korosho unaenda kutibu mbao zile za Mufindi haingii na mchwa hata mmoja hawezi kuharibu mbao, mabibo ya kwenye korosho leo mkiamua kufanya yawe na thamani tunaweza kutengeneza juisi,

tunaweza kutengeneza pombe, Ulaya mkauza mapombe, mkulima wa Tanzania asingekuwa maskini hata dakika moja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Waziri kaeni mtafakari jambo hili, Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake amesema vizuri sana anataka kuona wakulima wakinufaika, Waziri onyesha mfano huo, tuanze na kwenye korosho huku, ombeni fedha, pembejeo hizi mtoe bure, lakini mkiangalia tathimini mliyoifanya natoa tani 8730 za *Sulphur*. Lakini nenda kwenye jedwali zenu 2017/2018 ambapo tumezalisha tani 313 *Sulphur* iliagizwa tani 18,000, nyinyi mmeagiza tani 8730 maana yake hatuendi kuongeza uzalishaji mnaoukusudia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwenye dawa za maji tuliagiza lita laki tatu na, leo mmeagiza lita 82,438 hamuendi kutoa majibu ya wakulima, hamuendi kutoa majibu na hiyo ipo kwenye hotuba zenu, mkae mfanye tafakari ya kina, tunahitaji mkusaidia mkulima huyu, mkulima ambaye anapata shida watu wamezungumza hapa adha ambazo mkulima anapata. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa, Katani.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, shukurani sana. (Makofi)

**SPIKA:** Watu wana moto kweli kweli leo, bajeti ya kilimo na kuna kila sababu. Hatuwalaumu Waheshimiwa Mawaziri sio kwamba nyinyi ndio mmeleta mambo hayo, lakini matarajio yetu ni kwamba mtajitahidi muwezavyo. Wizara hii ngumu, Wizara ya Kilimo ngumu. Kuna wakati huko nyuma paliwahi kufanyika maamuzi makusudi kwamba, aletwe Mzee mmoja ndio ataweza hii kilimo hii. Kama mnakumbuka Mzee Wasira, bado akatoka akarudi tena bado, yaani kilimo huwa ni mfupa mkavu sana na ni Wizara ambayo imejaa wasomi kwenye utafiti yaani wasomi watupu. Siku hizi *extension officers* kuanzia kijijii ana *degree* hao wachache mnaosema, *diploma, degree* lakini wapi! (Makofi/Kicheko)

Kwa hiyo, liko tatizo ni jambo ambalo linatakiwa Wabunge wote tuliangalie wala sio la kulaumu pale au pale, lakini ni *frustration* za watu, lakini ndio ukombozi wetu ulipo kwenye kilimo. Kwa hiyo, Profesa tuko na wewe, Naibu tuko na nyinyi, wataalamu wetu lakini safari bado ni ndefu moja ya tatizo kubwa ni *government intervention*. Yaani tukiona tu mambo yanaenda vizuri Serikali inaingia jambo linaharibika, Serikali inaingia jambo linaharibika. (Makofi)

Tuipe nafasi *private sector* pale inapoweza kufanya jambo vizuri, tuipe nafasi sisi tukae nyuma tusimamie tu. Tukubali hilo Dunia imebadilika hata Rusia imebadilika, hata China imebadilika sana. Wanafanya *reform and opening up* ndio sera hizo mbili tu wanafanya Wachina, zilizobadilisha *the whole of the China, reform and opening up*. (Makofi)

Sasa sisi *ku-open up* bado shida yetu kwenye *opening up*, kikweli kweli kwamba hapa sekta binafsi, hapa sisi *tu-monitor* tuangalie hapo *balance* hiyo, lakini ushauri ni kwamba tuzidi *ku-open up*. Ndio nilikuwa nawatania ndugu zangu wa mifugo ni kweli kabisa hizi *Ranch* za Taifa hazina maana za nini! Serikali inachunga ng'ombe ya kazi gani hakuna sababu ya *Ranch* za Taifa bakia na vieneo vidogo unavyofanya *research*, unavyofanya huduma za *extension* kwa wafugaji.

Lakini ufugaji halisi hata watanzania wanaweza kabisa hauna sababu, zimefeli zote *Ranch* miaka yote hii. Luhaga Mpina nani nani wameweka yaani tangu 1967 hakuna kitu, hata Naibu anasema mtakuja kuongeza bajeti hata mfanyeje *Ranch* hazifufuki. Twendeni *private* huo ndio ukweli, *open up*. Ng'ombe wa Serikali we bwana wee, ng'ombe wa mwananchi anaiangalia usiku na mchana. (Makofi)

Juzi ng'ombe wangu mmoja ni jike amepofuka sijui kwa sababu gani wamejitahidi wataalamu lakini amepofuka, sasa unaangalia akichinjwa haiwezekani kwa sababu, kwanza ana mimba. Kwa hiyo ukimsubiri akizaa ana ndama pia huwezi kumchinja kwa sababu, ana ndama. Lakini sasa



inabidi achungwe peke yake kwa sababu hawezi kwenda na kundi lile lingine, Lakini angekuwa wa Serikali nani atashughulika naye. *(Makofi)*

Ahsante sana tutaendelea jioni na uchangiaji wetu, ni uchangiaji mzuri tu wala hauna neno na Mheshimiwa Abdallah Chikota, Masache Kasaka, Tabasamu, Dkt. Pindi Chana, Mheshimiwa Cecilia Paresso na wengine, wote mtapata nafasi. Muendeleo tu kujiandaa vizuri ili tusirudie rudie sana lakini tuweke msisitizo kwenye masuala haya ya kilimo. Kwa sababu, nia yetu wote ni njema, Serikali yetu na sisi wenyewe kwa pamoja tuna nia njema sana kwa wakulima wetu wa nchi hii. *(Makofi)*

Basi, sasa nitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni ya leo.

*(Saa 7.08 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Majadiliano yanaendelea, Mheshimiwa Abdallah Chikota atafuatiwa na Mheshimiwa Masache Kasaka.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mjadala huu ambao upo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwapongeza viongozi wa Wizara hii, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara hii, Wakurugenzi wa Mashirika pamoja na Watendaji Wakuu wa Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii. Kwa kweli mmeandaa hotuba safi ambayo inaanza kujibu baadhi ya changamoto ambazo zipo kwenye sekta yetu ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuchangia kuhusiana na sekta ya korosho. Korosho ni zao pekee ambalo kwa sasa

tuna-*export levy* na *export levy* ipo Tanzania mpaka *Ivory Coast* wazalishaji wakubwa wa korosho duniani. Wenzetu wanatumia *export levy* siyo kama chanjo cha mapato kwanza ni katika kuhamasisha ubanguaji wa ndani na kutoa vivutio kwa wale wanaobangua korosho. Vilevile *policy* hii inatumika hadi Msumbiji kwamba wale ambao wanabangua korosho ndani wanapewa vivutio.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano *Ivory Coast* wanatumia kama senti sitini kwa kila mzalishaji wa ndani anayebangua korosho, uki-*convert* kwa fedha yetu ni kama ni Sh.1,500. Fedha hii inasaidia watu wengi kujiingiza kwenye sekta ya ubanguaji na hivyo viwanda vya ndani vinafanya kazi na hivyo kutoa ajira nyingi. Kwa hiyo, sisi tuliweka *export levy* na tukafanya hivyo hivyo tukapeleka asilimia 65 ya *export levy* kwenye Mfuko wa Kuendeleza zao la Korosho. Sitaki nikukumbushe kilichotokea maana unajua kabisa kwenye Sheria ya Fedha, 2018 tulitoa ile asilimia 65 ambayo ilikuwa inaenda kwenye Mfuko kuendeleza zao la korosho tukapeleka kwenye mfuko mkuu na tangu hapo sekta ya korosho ikaachwa bila kuwa na ugharamiaji mkubwa.

Mheshimiwa Spika, sekta ya korosho inahitaji fedha nyingi sana na sasa hivi tunahesabu miko 17 ambayo inalima korosho, kwa hiyo lazima tuwe na mpango wa kugharamia sekta hii ya korosho. Niungane na wenzangu ambao wanasema kwamba kwanza *export levy* itumike katika kuendeleza sekta ya korosho, tutoe motisha kwa wabanguaji wa wetu ndani.

Mheshimiwa Spika, niliuliza swali wiki iliyopita tunawapa motisha ipi wabanguaji wa ndani? Kwenye minada ya awali wakulima hawapeleki korosho kwa sababu bei ni ya chini, tukiwapa motisha kwa kutumia fedha hizi wanunuzi au wakulima watakubali kupeleka korosho kwenye minada ya awali na viwanda vyetu vitapata korosho za kutosha na hivyo kutoa ajira kwa wanawake na vijana wengi.

Mheshimiwa Spika, lakini si hivyo tu na mimi nichangie kwenye hoja ya pembejeo za msimu wa mwaka huu. Kwanza nianze kuipongeza Wizara kwa kazi kubwa ambayo wameifanya kwanza kuja na mfumo wa kuagiza pembejeo nyingi kwa wakati mmoja. Tunavyoongea sasa hivi kuna tani 21,000 za *sulphur* zimeshaigiza nchini, hili ni ongezeko kubwa sana lakini tuna viuatilifu vya maji kama lita 1,300,000 hatujawahi kuagiza *sulphur* na viuatilifu vya maji kwa kiasi kikubwa kama hiki. Kwa hiyo, naipongeza Wizara kwa hatua hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyopo ni ugharamiaji, tunagharamiaje pembejeo hizi. Naungana na wenzangu kusema kwamba lile wazo la kumtaka kila atakayeza korosho gulioni Sh.110, hizo ni fedha nyingi sana kwa sababu mkulima huyu tayari ameshakatwa Sh.50 kwa ajili ya Naliendele na Bodi ya Korosho, ameshakatwa fedha za *export levy* kwa sababu ile *export levy* mnunuzi anapokuja kwetu anapunguza bei ili aweze kulipa *export levy*, kwa hiyo, ile *export levy* anaibeba mkulima, sasa tukimchangisha tena Sh.110 anakuwa na mzigu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niungane na wenzangu waliokwisha changia kusema kwamba zitafutwe hizi shilingi bilioni 55 mpaka 60 tupeleke ili *sulphur* hiyo igawanywe kwa wakulima. Utafiti umeonesha wazi kwamba mwaka ambao *sulphur* na viuatilifu vya maji vimegawanywa kwa wingi na uzalishaji unaongezeka. Mwaka 2017/2018 ambapo tulifikisha tani 520,000 ndiyo mwaka ambao tuligawa bure *sulphur* kwa wakulima. Kwa hiyo, tukitoa *sulphur* hii tutafikisha lengo letu la kufikisha tani 280,000, tusipofanya hivyo basi uzalishaji utaendelea kuporomoka kama unavyoporomoka kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, vilevile nichangie kuhusu Bodi yetu ya Korosho. Kama nilivyosema kwamba fedha za *export levy* zipelekwe kwenye uendelezaji wa zao la korosho, kwa hiyo Mfuko wa Kuendeleza zao la Korosho lazima urejeshwe ili kuhakikisha fedha hizi zinatumika ipasavyo. Pia ili fedha hizi zitumike vizuri kwenye Mfuko lazima uwe na Bodi imara,

kilichopo sasa hivi kwenye sekta ya korosho ni kizungumkuti kwa sababu Bodi haijaundwa kwa miaka mitatu sasa, lakini hata Mtendaji aliyeko ni Kaimu na ile Bodi ni dudu lizito lazima tupate Mtendaji ambaye yuko imara na muda wote atakuwa anashughulikia korosho na pengine hata mzigo uliopo Wizarani utapungua kwa sababu mambo mengine watafanya kwenye ngazi ya Bodi ya Korosho.

Mheshimiwa Spika, Mfuko ule ulikuwa muhimu sana kwa sababu ulitoa fedha kwenye utafiti, wagani katika halmashauri yetu lakini kwa ajili ya usimamizi kwenye halmashauri, uligharamia ubanguaji mpaka usambazaji wa miche. Ile miche ambayo imefika Kongwa na Manyoni ni kwa sababu ya Mfuko huu lakini tukaridhika mapema kwamba korosho ina fedha za kutosha tukaziondoa zile fedha. Zile fedha tungeziacha kulekule sasa hivi tungekuwa tunahesabu tumeshazalisha tani 500,000 lakini tukazinyofoa mapema kabla ya muda wake. Turejeshe ule Mfuko ili hata mikoa mingine ambayo inalima korosho sasa hivi inufaike na sekta hii, tusipofanya hivyo itakuwa maumivu.

Mheshimiwa Spika, nichangie kuhusu ushirika. Watu wengi waliochangia kuhusu ushirika siyo kwenye korosho tu, kwenye pamba, mahindi mpaka maparachichi watu wanalalamika, kuna changamoto kwenye ushirika. Mwaka jana nilichangia hivi hivi kwamba hebu tuangalie kilichoko kwenye ushirika tatizo ni nini? Ni Sheria ya Ushirika, Tume au Ofisi ya Mrajisi wa Ushirika? Litafutwa tatizo liko wapi? Sasa hivi Wizara inataka kufanya marekebisho ya sheria, inawezekana hata tukibadilisha sheria matatizo yatabaki vilevile. Tuangalie mfumo wa uendeshaji wa ushirika, mfumo wa kitaasisi wa ushirika na uwezesaji wa ushirika, kuna changamoto kule. Haiwezekani Sheria ya Ushirika inasema kwamba mtendaji kwenye *AMCOS*kiwango chake cha elimu kisipungue kidato cha nne lakini anachukuliwa mtu ambaye hana kiwango hicho, Afisa Ushirika na Mrajisi wapo, hakuna hatua inayochukuliwa, fedha zikipotea tunaanza kulalamika. Kwa hiyo, ushirika uchunguzwe na yafanyike mabadiliko makubwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chikota, nakushuru sana. Nilishakutaja Mheshimiwa Masache Kasaka atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi niweze kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Kilimo. Kwanza nimpongeze Waziri pamoja na Naibu Waziri na Wizara kwa ujumla kwa wasilisho zuri lakini pia kwa mwelekeo mzuri kwamba sasa tunaanza kuona dira namna nzuri ya kilimo chetu tutakavyokwenda kukupeleka.

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia kwa kuongelea zao la tumbaku. Zao la tumbaku sasa hivi limekuwa halina tija tena kwa mkulima, wakulima wetu sasa wanalima kwa mazoea maana yake hawanufaiki nalo tena. Kama tunataka kuwakomba wakulima wetu hawa lazima tujielekeze kwenye masoko ya uhakika. Makampuni ya ununuzi yanapokuja huwa yanaweka makisio ya kununua na kulima. Kwa hiyo, huyu mkulima wetu hata alime vipi kama atakuwa amelima zaidi ya yale makisio aliyowekewa maana yake tumbaku yake haiwezi kununuliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi kwa wakulima wetu hawa wadogowadogo kwa mkulima mmoja wao wanaruhusiwa kulima heka mbili tu pekee lakini kwa gharama anayotumia kulima kwa heka mbili hana uwezo wa kulima heka tatu. Shida ni kwamba hata akilima kwa heka tatu maana yake ni kwamba tumbaku yake ambayo itanunuliwa ni ile ya heka mbili. Huyu mkulima ili kumsaidia maana yake lazima aweze kulima zaidi ya heka mbili kwa msimu ndiyo aweze kupata kipato cha kumtosheleza na aweze kupata faida. Namna pekee na tuishauri Serikali ili

kuwasaidia wakulima wetu hawa ni kutafuta masoko ya uhakika, makampuni yawepo mengi ili makisio ya hawa wakulima yaweze kuongeza. Hii ndiyo njia pekee ambapo tunaweza tukawasaidia hawa wakulima wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine kwenye suala hili la tumbaku ni haya madaraja yanayopangwa na makampuni kwa ajili ya wakulima wetu. Wakulima hawa wanapokuwa wamelima tumbaku yao wao wenyewe huwa wanai-*grade* sasa makampuni yanapokuja na yenyewe yanakuja tena kui-*grade* upya tumbaku ile. Kitengo hiki huwa kinapelekea sasa hapa katikati wale wanaokuja ku-*grade* kule kwetu wanaonekana kama Mungu amefika, akifika siku hiyo mkulima lazima umnyenyekee, umlishe kuku vizuri ili sasa aweze kui-*grade* tumbaku yako vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bila kufanya hivyo tumbaku yako inaweza ikawa kwenye *grade* nzuri lakini yeye akai-*under grade*. Bahati mbaya sana kwenye zao letu hili ukishindwa kuuza kwenye kampuni ile maana yake huwezi kuuza tena. Kwa hiyo, tunaishauri sana Serikali ione namna nzuri sana ya kukaa na makampuni haya au wanao-*grade* tumbaku wawe na watu wao lakini sisi kama Serikali pia tuwe na watu wetu waweze kuhakikisha kwamba hiki ndiyo kiwango ambacho kinatakiwa.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala hili la tumbaku pia wafanyakazi wa haya makampuni na wenyewe wanajiingiza kwenda kulangua tumbaku hii. Wanachofanya ni kwenda kununua tumbaku hii kwa wakulima kwa bei ndogo ili baadaye na wao waweze kuja kuuzia makampuni ambayo wanafanyia kazi. Hawa wakulima wasipowauzia tumbaku hii wale wafanyakazi ndiyo baadaye wanashindwa kupata *grade* bora zaidi na wengine hawapati kabisa masoko katika kununua. Kwa hiyo, naishauri Serikali iweze kuangalia jambo hili.

Mheshimiwa Spika, nizungumze kidogo kwa Wilaya Chunya, lilianzishwa zao mbadala la tumbaku la korosho. Zao hili lililetwa miche, kwa maana Serikali ilitoa ruzuku kuleta

miche hii, lakini ilikuja tu awamu ya kwanza baada ya hapo ile miche tena haikuja. Baadaye halmashauri na yenyewe ilijitahidi kutoa fedha zake kununua miche na kuwapatia wakulima wetu hawa lakini na wao wamefika hatua nao wameshindwa. Sisi wakulima wetu wa Wilaya ya Chunya wanashindwa kuipata hii miche mizuri zaidi ili wawekeze kwenye zao hili la korosho.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwenye zao hili la korosho kwa kuwa ni zao jipya Maafisa Ugani wetu ambao wapo kule Wilaya ya Chunya bado na wao hawajaweza kupata elimu ya kutosha kuhusu zao hili la korosho. Mimi niishauri Wizara kupitia TARI-Naliendele waweze kuleta wataalam wao mara kwa mara kwa Maafisa Ugani wetu hawa ili waweze kuwapa hii elimu na wao Maafisa Ugani wetu kwa kuwa ndiyo wanakaa kulekule na wakulima hawa waweze kuwapa hii elimu ya mara kwa mara. Hii itaweza kutusaidia sana na hili zao liweze kwenda vizuri zaidi. Sisi tunaamini zao mbadala la tumbaku ni korosho, kwa hiyo, lazima tuwekeze kwa kiasi kikubwa ili hili zao liweze kuwasaidia wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, pia nizungumizie suala la umwagiliaji. Wilaya yetu ya chunya tulipata bahati ya kuwa na skimu ya umwagiliaji katika Kata ya Ifumbo. Skimu hii ilianza zaidi ya miaka kumi iliyopita, ilianza kwa za ufadhili wa nje baadaye Serikali ikaja kutoa fedha zake lakini mara ya mwisho Serikali kutoa fedha mwaka 2013, fedha zilizowekezwa pale ni zaidi ya bilioni moja lakini mpaka leo tunasema zile fedha tulizitupa pale. Niiombe Serikali kupitia Wizara ya Kilimo iweze kupitia hii miradi ambayo ilisimama kwa muda mrefu, ione tatizo lilikwamia wapi ili baadaye waweze kuweka fedha na lile dhumuni kubwa ambalo lillikuwa limekusudiwa kwa ajili ya kujenga hizi skimu liweze kuwasaidia wananchi wa maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Ifumbo tunaitegemea sana kwa Wilaya ya Chunya kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Skimu ile ikiweza kupata fedha za kutosha na ikianza kufanya kazi maana yake mbogamboga na vyakula

vyote vinavyozalishwa kwenye skimu za umwagiliaji tutaweza kupata kutoka Kata hii ya Ifumbo. Wilaya ya Chunya ambayo tunaona kama kame nako tutaweza kupata mazao mengi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.  
(Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Masache Kasaka. Mheshimiwa Cecilia Paresso atafuatiwa na Mheshimiwa Tabasam Hamis.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Kilimo. Nianze kwa kumpongeza Waziri na Naibu Waziri kwa jinsi ambavyo mlipambana vya kutosha wakati tumepata baa la nzige. Kwa kweli hongereni mlifanya vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hakuna ambaye hatambui umuhimu wa kilimo hapa nchini na sote tunatambua jinsi gani ambavyo kilimo kinachangia kwenye uchumi wetu au kwenye pato la Taifa kwa maana asilimia 26 ya pato letu la Taifa linatokana na sekta ya kilimo, kinatoa ajira kwa asilimia 58 lakini mauzo ya bidhaa za nje kwa asilimia 30 na pia sekta ya kilimo inachangia asilimia 65 ya malighafi viwandani.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano uliweka kipimo kwamba kilimo kiweze kukua kwa asilimia 7.6 lakini hadi leo kilimo hiki kimekuwa kwa asilimia 4.9 Sasa tunaweza kujjuliza kwamba kama tunajiwekea mipango au vipimo fulani vya kutupima kama nchi na hatuvifikii maana yake kuna visababishi vingi ambavyo vinasababisha hicho ambacho tunakiweka tusikifikie.

Mheshimiwa Spika, mojawapo kwanza kilimo hakipati uwekezaji wa kutosha. Kama nchi sina hakika kama tumeona kilimo pamoja na haya nilioyataja huko juu namna gani kinachangia uchumi wa nchi lakini sina hakika kama Serikali mmeona umuhimu wa kuwekeza vya kutosha kwenye kilimo ambacho kinawasaidia Watanzania wengi sana karibia



asilimia 80. Hivyo basi ni muhimu sana mkaona umuhimu wa kuwekeza vya kutosha kwenye kilimo. Kama ambavyo tunafanya jitihada kubwa ya kuwekeza kwenye miundombinu kwa maana ya labda Wizara ya Ujenzi, barabara, *Siegler's*, *SGR*na kila kitu, vivyohivyo tufikirie namna gani ya kuwekeza vya kutosha kwenye sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiwekeza vya kutosha kwenye sekta ya kilimo maana yake hata hawa vijana wetu walio nje wengi huko hawana ajira wanamaliza vyo, tukifanya mazingira mazuri na watu wakapenda kilimo na watu wakaona kilimo si tu cha kupanda mahindi kwa maana ya mahitaji ya chakula lakini wakafikiri kwamba nitapanda mahindi lakini pia itakuwa ni sehemu ya biashara na kuniingizia kipato. Maana tunahitaji pia kubadilisha mitizamo ya watu kwa kuwawezesha kwamba ninalima kilimo kama biashara na akiba nitakayopata nyingine itakuwa kama chakula. Kwa hiyo, tunahitaji sana kuwa na mbinu hizo za kubadilisha mfumo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia mchawi mwingine mkubwa wa kilimo chetu ni fedha tunazoidhinisha hapa Bungeni za miradi ya maendeleo, haziendi kama inavyotakiwa. Tukitafuta uchawi ni nini? Nadhani uchawi mkubwa uko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano, mwaka 2017/2018, tuliidhinisha shilingi bilioni 150 kwenye fedha za maendeleo tu, zilizokwenda ni shilingi bilioni 27. Mwaka 2018/2019, tuliidhinisha shilingi bilioni 98, zilizoenda ni shilingi bilioni 46; mwaka 2019/2020 tuliidhinisha shilingi bilioni 143, zilizoenda ni shilingi bilioni 46. Mwaka huu ambao bado hatujaamaliza, lakini mpaka Aprili, tuliidhinisha shilingi bilioni 150 lakini mpaka Aprili zilizotoka ni shilingi bilioni 68. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tusitegemee muujiza wa kuikomboa sekta ya kilimo kama hata hiki kidogo tunachokitenga hakiendi. Ukiangalia hapa, maana yake hata asilimia 50 ya fedha tulizotenga kwenye miradi ya

maendeleo kwa maana ya kilimo, hazijawahi kutoka kwa miaka hii niliyoitaja. Ndiyo maana nasema upo umuhimu wa Serikali kuona kwamba tunawekeza vya kutosha kwenye kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hebu tuiombe na kuishauri Serikali kwamba safari hii hiki ambacho tutakipitisha hapa kiende kwa asilimia angalau 80. Halafu tujipime kwamba hicho tutakachokipeleka: Je, kweli kitakwenda kufanya yale tunayoyakusudia na kuleta mapinduzi ya kilimo?

Mheshimiwa Spika, huko nyuma tulikuwa na *slogans* nyingi za kilimo, wakati wa Serikali ya Awamu ya Nne pia kilimo kiliingia kwenye *Big Results Now*, Kilimo Kwanza, mambo mengi sana. Ni vyema hizo *slogans* tunazoziweka na hiyo mikakati tunayoiweka tuitekeleze kwa Serikali kutoa fedha zinazotakiwa, zilizoidhinishwa hapa Bungeni zitoke zote kama ambavyo inatakiwa. Hilo ni muhimu sana. Hapa tutakuwa tumeondokana na uchawi wa sekta ya kilimo kwa ujumla, angalau tutakuwa tumepunguza. Kwa hiyo, ni muhimu sana Serikali ikatazama hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi, kwa mujibu wa *report* ya CAG, ameonesha mambo mengi sana ambayo ni changamoto au ni madhaifu kwenye sekta ya kilimo. Ameonesha mfano mmojawapo, kwamba wakulima hawana ujuzi wa matumizi ya mbegu, mbolea na viuatilifu. Sasa haya ni mambo ambayo Wizara mnaweza kuyafanya yakatekelezeka, mkulima huyu akapata ujuzi, akajua matumizi ya mbegu bora, akajua matumizi ya mbolea sahihi kulingana na ardhi yake, anatakiwa atumie mbolea gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii itakwenda sambamba na kuangalia yale maabara ya kupima udongo, kwamba hapa udongo huu nikilima naweza kutumia mbolea ya aina gani? Ifike mpaka wilayani, tusiweke tu hivi vituo kwenye *centre* za mikoa, ni ngumu kwa mwananchi kufika, lakini tukiweka mpaka *centre* za halmashauri zetu kwa Maafisa Ugani kule chini, maana yake tutakuwa tumemsaidia mwananchi kwa

kumpa ujuzi kujua kwamba udongo wangu hapa ninapaswa kutumia mbolea ya aina gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo linguine, CAG ameonyesha kwamba, “kuna usambazaji wa pembejeo usiokuwa na ubora. Hii ni kutokana na kwamba Serikali mmeshindwa kudhibiti.” Haya siyo maneno yangu, ni maneno ya *report* ya CAG ameeleza. Sasa ni mambo ambayo yako chini ya uwezo wenu Wizara kuhakikisha mnadhibiti. Bila shaka hili hata kama linahitaji fedha, siyo nyingi sana. Ila tunaweza kuona namna gani tunadhibiti haya ili kuhakikisha kile tunachokusudia katika usambazaji wa pembejeo, basi ufanyike kwa kadri ambavyo inatakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo linguine, CAG amesema kwamba kwa mwaka 2016/2017 mpaka 2019/2020, ni asilimia 39 tu ya ugavi wa pembejeo ulifanyika kwenye mbegu, mbolea na viuatilifu. Sasa tuone kwamba kama tunaweza kununua kwa asilimia 39 tu; na inawezekana hii ni kwa sababu ya ufinyu wa bajeti, tusitegemee muujiza. Kama hatufiki hata asilimia 50 ya ununuzi wa hivi vitu ili viweze kumfikia mkulima, tusitegemee mkulima aweze kusaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishauri sana Serikali na Wizara, CAG ameeleza mambo mengi sana, mkifanyia kazi haya ambayo ameeleza kama ni changamoto, bila shaka tunaweza kuvuka hatua moja mbele kuhusiana na sekta ya kilimo kumkomboa mwananchi na mkulima wa Tanzania kuhakikisha kwamba kilimo chetu kinakuwa na faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba tunahitaji pia kufanya Watanzania wakipende kilimo. Vijana wetu wakimaliza shule wasifikirie tu kazi ni kwenda ofisini, waone pia kilimo ni kazi ambayo inaweza kumpatia kipato na kuendesha maisha yake kwa Serikali kujenga mazingira mazuri.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Cecilia Paresso.

Mheshimiwa Tabasam Hamis Hussein, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sengerema, naomba kushauri kama ifuatavyo katika hii bajeti ya Wizara ya Kilimo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, nashukuru Wizara ya Kilimo kwa kuwa na wataalam wengi sana katika Wizara yao. Katika nchi hii ukiondoa Wizara ya Elimu, Wizara ya Afya, Wizara ambayo ina watu ambao ni maprofesa na madaktari ni Wizara hii ya Kilimo, lakini mpaka sasa hivi, pamoja na kuwa na elimu kubwa kiasi hicho, hawajaweza kutatua kilio cha wananchi katika nchi hii. Nchi hii asilimia 75 wanategemea kilimo; na hiki kilimo kimeshindwa kumsaidia mwananchi toka nchi hii ipate uhuru. Sasa linakuwa ni tatizo kubwa sana. Hatujui tatizo liko wapi?

Mheshimiwa Spika, ili nchi hii iweze kupata maendeleo katika sekta ya kilimo, tunahitaji mjadala wa Kitaifa. Ufanyike mjadala wa Kitaifa tupate *solution* kwamba tufanyeje? Yaani tuwe tumeondoa matatizo. Bila kwenda na mjadala wa Kitaifa katika Wizara hii, watabadilishwa sana Mawaziri. Kwa sababu katika Wizara ya Kilimo kuna watu wana roho mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kukwambia, sijui tutafanyaje katika hii Wizara. Bahati nzuri wewe ni mtoto wa mkulima, unajua, umekaa huko Ushirombo, umeona ile hali iliyoko kule. Umekuja tena huku kwenu Ugogoni umeona hali iliyopo; lini wakulima wa nchi hii nao watakuwa matajiri? Sasa ujue kuna roho mbaya iko pale.

Mheshimiwa Spika, tunasomesha mtoto, anatoka huko kwetu kijijini na ameona hali ya wazazi wake ilivyo; anakwenda *SUA*. Akitoka *SUA* pale anaishi mjini, harudi tena kuja kumsaidia mzazi wake lima hivi, kama alivyosoma, haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa kwanza kabisa, naomba hii Bodi ya Kilimo ivunjwe. Bodi ya Pamba hii kwa sisi wakulima wa Mkoa wa Mwanza ivunjwe. lundwe Bodi ya Pamba ya watu ambao wanajua kilimo cha pamba ni nini?

Mheshimiwa Spika, mimi nataka kuzungumzia pamba tu. Tuna Chuo chetu pale cha Ukiriguru, kimekuwa hakina tija. Pale Ukiriguru kuna *TARI* wako pale. Kwa mfano, Mheshimiwa Bashe, hivi ninavyozungumza na wewe, bahati nzuri nawe ni mtoto wa mkulima, lakini utachoka, yaani utazeeka kabla ya muda wako, kwa sababu umezungukwa na watu wenye roho mbaya. Mimi ndicho ninachotaka kukwambia, utatembea sana, lakini mpaka utatoka kwenye hiyo Wizara bila kuwasaidia wakulima wa pamba. Umezaliwa Nzega wewe, unajua kabisa pamba inavyotusaidia sisi. Haya maneno gani haya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tuna tani 350,000, leo tunakuja kurudi kwenye tani 120, haya maneno gani? Tutafikaje kwenye Ilani ya Uchaguzi tunasema tuwe na tani milioni moja? Tunahitaji mjadala wa Kitaifa katika jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siyo mchezo, hili ni jambo ambalo ukisimamia nafasi yako hapa vizuri kabisa ndani ya hili Bunge, kutusaidia wakulima wa pamba, tukienda kwenye mjadala wa Kitaifa tutakuletea jibu sahihi tufanyeje ili tuweze kupata mapinduzi makubwa ya kilimo cha pamba? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Mheshimiwa Bashe, Mheshimiwa Waziri, Profesa pale, hebu wakulima wa kilimo cha pamba, wasajiliwe nchi nzima. Wakulima wako katika mikoa 17, wako katika wilaya 54; wapeni vitambulisho tujue kwamba katika kilimo cha pamba tuna ekari ngapi zinalimwa mwaka huu? Hawa wakulima wa pamba wanahitaji kitu gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe umekwenda kuona, bahati nzuri Mheshimiwa Bashe nilikuwa ofisini kwako juzi, nimekwambia kale kadawa kanaitwa *heka pack* peke

yake kanauzwa shilingi 9,000/=, leo umekwenda kusema waagize kwa jumla, kamekuja kuuzwa shilingi 4,500/=. Hiyo shilingi 4,500/= bado ni kubwa. Tunakuomba uendelee kuwa mzalendo hivyo hivyo japo watakuchukia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, leo wanakuja kuagiza mbolea kwenye *high season*, kitu ambacho ni cha ovyo kabisa. Sijui nisemeje? Wakati wa *low season* hamuagizi mbolea, mnakuja kuagiza mbolea mwezi Septemba, mwezi Agosti, kwenye *high season* wakati kila nchi inataka mbolea. Leo Serikali ya India inaagiza tani 1,100,000, wewe una tani zako 50,000, unasubirije mpaka mwezi Septemba huko? Kwa nini usinunune mwezi Februari?

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge humu ndani, jamani mnielewe. Ni habari gani hii? Ninyi badala ya kuagiza kwenye *low season* mkatoa *tender* hiyo mkaagiza kwa *bulk* mbolea ikaja hapa ya bei rahisi, mnakuja kuagiza mbolea ambayo inafika hapa kwa bei kubwa! Sasa ukiwasajili wakulima, hapo hapo una haki ya kwenda kuzungumza na watu wa Wizara ya Ardhi mwapimie vipande vyao hivyo vya ardhi, tupime mashamba yote tujue tatizo ni nini ili wananchi sasa waweze kuja kupata tija na hiki kilimo chao.

Mheshimiwa Spika, leo Misri ekari moja inatoa tani moja na nusu mpaka tani mbili. Wenzetu wa Chad wanatoa tani mbili na nusu. Leo hapa tuliko pamba inalimwa hapa chini Msumbiji, wanatoa tani moja na nusu. Sisi iweje ekari moja inatoa kilo 150, kilo 300? Nani atapenda kuilima pamba? Ardhi imechoka, inalimwa toka mwaka 1960 mpaka leo bila mbolea, unawezaje ukazalisha hizi tani? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hawa Maafisa Ugani wetu tulionao na wenyewe ni tatizo, wapelekeni pia kwenye semina. Sisi wakulima wa pamba tunajua pamba. Bila hata kumleta Afisa Kilimo, mimi nailima pamba tu; nimekuta nyumbani inalimwa, mimi mwenyewe nimeilima, tena tunailima kwa jumla. Hili najua ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine liko kwenye ushirika. Wamekuja kuunda hizi wanaziita *AMCOS*, majambazi wakubwa kabisa. Yaani hatujawahi kuona ujambazi kama huu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Bashe amepita mwenyewe ameziona hizi *AMCOS*; mnakuja kuleta matatizo kwa wananchi tu wanakuja kudhulumiwa pesa zao. Badala ya kuimarisha ushirika, mnaleta maneno ya *AMCOS*, wajanja fulani watatu, wanne wanakaa kwenye kijiji wanajiita *AMCOS*. Hebu mzipitie hizi *AMCOS* zote katika nchi hii mje mwone. Hawa watu wanatakiwa kupelekwa Mahakamani. Hata sasa hivi tunashangaa bado wako huru. Hii ni hatari sana katika nchi hii. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, ninachotaka kuwaambia ninyi watu wa Wizara,...

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam...

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, yaani nina kamchango kadogo, kaendeleo...

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam, muda hauko upande wako.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, ninachoomba tu ni kwamba...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Ameshamaliza. Malizia Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, lakini muda wangu umekuwa ni mdogo sana. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Katibu Mkuu na wataalam, ujumbe ni huo, anasema mna roho mbaya sana huko Kilimo. Acheni roho mbaya jamani. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana tafadhali, atafuatiwa na Mheshimiwa George Mwenisongole.

**MHE. DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza naunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanafanya sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, moja kwa moja nakwenda kwenye kilimo cha kisasa. Kilimo cha kisasa hatuwezi tukafanya kwa kutumia jembe la mkono. Sisi wengine tumesomeshwa kwa jembe la mkono na sasa siyo sawa kusomesha watoto wetu kwa jembe la mkono, tunahitaji vitendea kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, miaka 50 baada ya Uhuru Tanzania lazima tuulizane viwanda vya matrekta viko wapi? Wizara itusaidie, Serikali itusaidie tupate viwanda vya matrekta vya kutosha. Leo hii nina *invoice* hapa, nilikuwa na-*compare* trekta moja bila jembe siyo chini ya shilingi milioni 50; trekta aina ya Ford, Valmet na hizi zote zinatoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumetoa ushuru, lakini haiwezekani mkulima wa Makete, Njombe akanunua trekta kwa shilingi milioni 50 bila jembe na kadhalika. Tunahitaji viwanda vya *power tiller* vya kutosha. Pia Halmashauri zetu zisaidie kuona katika kila Halmashauri kuwepo na wawekezaji wa masuala haya ya kilimo cha kisasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana, wakati umefika; kama tulivyosema kwenye Ilani kwamba tunataka kwenda kwenye kilimo chenye tija, kilimo cha kisasa cha kuongeza kipato kwa mkulima, lakini leo hii kwa mkulima imekuwa ndiyo changamoto. Yaani mtu ukimwuliza



*profession*, katika kazi mbalimbali; wewe una taaluma gani? Ukisema mkulima, mtu anageuka pembeni. *You see!*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli lazima kilimo kiwe cha kuvutia, chenye tija. Watoto wanapokwenda kusoma *University* anaulizwa unataka *combination* gani? Yaani mtu akichagua *agriculture* wanamwangalia mara mbili; *why not business, why not finance? Agriculture, are you serious?* Kwa hiyo, lazima tubadilike kwa kweli kilimo hiki kiwe ni chenye tija. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ifuatilie takwimu kwa kila Halmashauri kuna matrekta mangapi? Mtashangaa kuna baadhi ya Halmashauri matrekta ya kuongeza tija kwenye kilimo cha kisasa hazipo; ziwe ni mbovu au mpya, hazipo. Hapa tunahitaji *Government intervention*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nimetumwa na wananchi wa Mkoa wa Njombe ni lumbesa katika mahindi na viazi. Unakuta magunia mawili yanashonwa linatafsiriwa ni gunia moja. Eneo hili pia imekuwa ni changamoto ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limezungumzwa hapa ni suala zima la masoko. Kwa kweli masoko ni changamoto. Naipongeza Wizara, imeshirikisha sana balozi zetu mbalimbali, kwa hiyo, katika balozi zetu tuwape takwimu za kutosha. Hizi balozi zetu, hususan zinazozunguka mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nchi zinazotuzunguka wanahitaji sana bidhaa za mazao; maharage, mbao, viazi, chai, alizeti na kadhalika. Mara nyingi wanauliza, mna tani ngapi ambazo tunaweza tuka-*import* kutoka Tanzania. Yaani Tanzania inakuwa ina-*export*.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, takwimu lazima ziwepo na ziwe zinapatikana mara moja. Unakuta hizi takwimu mpaka taarifa itoke ubalozini iende *Foreign*, ikitoka *Foreign* iende Kilimo, tena itoke Kilimo irudi *Foreign* ifike kule; huyu mwekezaji hawezi kusubiri, ataenda Brazil kuchukua

mahindi. Kwa hiyo, taarifa hizi za kutafuta masoko ziwepo na tushirikishe taasisi binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna taasisi kama *East Africa Grain Council*, wao wanachukua takwimu kwamba nafaka ziko wapi; mahindi, maharage, njegere na nani anahitaji? Wanachofanya ni kuwaunganisha kwenye mtandao, *you see!* Kwa hiyo, lazima sasa tushirikishe sekta binafsi katika suala zima la utafutaji wa masoko na uwekezaji katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, tuwe na masoko ya mipakani. Wakati mwingine wakulima wetu wakipeleka mazao nje ya nchi, wanasumbuliwa sana na madalali, hawapati haki zao kwa wakati. Kwa hiyo, tukiwa na masoko haya katika mipaka ya nchi zetu mbalimbali, wanaweza wakapata mazao haya kiurahisi zaidi. Kwa hiyo, nchi mbalimbali ambazo ni nchi jirani haziwezi kuhangaika kusafiri kwenda mpaka mikoa ya kusini; pale pale mpakani anapata anachohitaji.

Mheshimiwa Spika, parachichi ni zao muhimu sana. Mkoa wa Njombe wamenituma, iko changamoto ya madawa ya parachichi, iko changamoto ya *cold rooms* za kuhifadha parachichi. Pia hii parachichi inatakiwa iwe *certified*. Ili mkulima auze nje lazima u-*certify* zao la parachichi.

Mheshimiwa Spika, zile taasisi zinazo-*certify* zinatoka nje ya nchi...

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa, Mheshimiwa nimekuona.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, mzungumzaji anayezungumza, mimi Mbunge mwenzake wa Njombe, pia tumetumwa kwenye suala la pamba, kwa sababu miche ya michikichi inatolewa bure, mbegu za pamba zinatolewa bure na mbegu za mazao mengine tofautitofauti Serikali imekuwa ikitoa bure. Je, ni lini Serikali itaanza kutoa mbegu za parachichi bure?

Mheshimiwa Spika, hii ni taarifa ambayo wamenipa wananchi wa Njombe nije niulize Bungeni. Ahsante. *(Kicheko)*

**SPIKA:** *Chief Whip*, inabidi uandae semina, maana mambo haya ya Wabunge wako. *(Kicheko)*

Mheshimiwa mchangiaji, endelea.

**MHE. DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naendelea. Hiyo taarifa naikubali kwamba mbegu ya parachichi ni lazima itolewe bure. Kwa hiyo, eneo hili ni muhimu liangaliwe kinagaubaga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Makete kwa kweli tunalima viazi, lakini jembe la mkono linamtoa mkulima. Leo hii ukiangalia mikono yetu sisi wakulima wa Njombe tunatumia jembe la mkono. Wananchi wa Makete, akina mama wa Njombe wamenituma, wanasema haiwezekani tukapata vitendeakazi vya kulima viazi hizi kwa mashine? Miaka 50 baada ya Uhuru, kweli jembe la mkono! Kwa hiyo, tupate vitendeakazi. Kuwe na mashine maalum ya kuweka matuta tuachane na jembe la mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, akina mama, wananchi wa Lupembe kwa kweli wanafanya kazi kubwa sana ya kuzalisha chai, lakini msimu wa kiangazi kutokana na upungufu wa maji, unakuta mazao yanapatikana machache. Kwa hiyo, tunahitaji umwagiliaji katika chai na wakulima walipwe kwa wakati. Kuna wakati viwanda vya chai vinachelewa kuwalipa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilimo kinakwenda sambamba na miundombinu, barabara. Naungana na Taarifa ya Kamati ya Kilimo, imesema *TARURA* waongezewe fedha. Sisi pale Njombe pia tuna uwanja wa ndege, kuna wawekezaji wanatoka nchi za jirani wanakwenda Njombe, wanahitaji kusafiri kwa haraka...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana. Nilikutaja Mheshimiwa George Mwenisongole, utafuatiwa na Mheshimiwa Neema Lugangira na Mheshimiwa Vita Kawawa awe tayari.

Mheshimiwa George.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi. Nianze mchango wangu kwenye hii Wizara kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nimeingiwa na hofu sana baada ya kuisoma hii bajeti. Nimeingiwa na hofu kwa sababu hii ni bajeti ya kwanza tangu tutoke kuinadi Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2020 kwenye Uchaguzi ambao ulitupa ushindi wa kishindo sana kutoka kwa wananchi. Tuliwajaza matumaini makubwa sana wakulima na Watanzania masikini waishio vijijini kuhusu bei za mbolea na uhakika wa masoko; lakini katika hii bajeti ambayo nimeisoma zaidi ya mara tatu, sijaona hata mstari mmoja ambao unasisitiza kwamba Serikali itaweka mkazo kupunguza bei za mazao ya mahindi au kahawa. Sijaona mkazo wowote katika hii bajeti kuelezea uhakika wa soko la mahindi.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi kule kwetu Mbozi, debe la mahindi ni shilingi 3,000/=, gunia ni shilingi 18,000/= lakini mfuko wa mbolea ni shilingi 70,000/=. Sasa unategemea hawa wakulima ambao tumetoka tu kwenye uchaguzi wakatupa kura, watatuelewa vipi? Tunarudi tena mtaani hakuna *solution* ya bei za mbolea! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kati ya vitu ambavyo Bunge hili linaweza kufanya ni kuishinikiza Serikali *at least* kutoa bei elekezi za mbolea. Shilingi 70,000/= kwa mfuko wa mbolea ni kubwa mno, huwezi kulia eka. Tutakuwa hatuwatendei haki wakulima masikini ambao wametuumini wakatupa kura zao, lakini miezi sita baadaye, Bajeti ya Kilimo ambayo

walikuwa wakiisubiri, haina majibu ya matatizo yao. Kwa kweli hili ni suala ambalo ni lazima Mheshimiwa Waziri aliingilie na kulitilia mkazo sana kuhakikisha bei ya mbolea na uhakika wa haya masoko unakwenda kupatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kingine, nimpe pole Mheshimiwa Waziri, kwa sababu kama Wabunge wenzangu walivyoongea, uzoefu unaonyesha fedha za bajeti ya maendeleo zinatengwa nyingi, lakini zinazokuja ni chache. Sasa sijui kuna miujiza gani ya hizo baiskeli na pikipiki alizowaahidi Maafisa Ugani? Sijui atazipata vipi wakati fedha za maendeleo hazipati? Sijui atajigawa vipi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hili ni suala ambalo kama kuna kitu ambacho Bunge hili linaweza kufanya, shilingi bilioni 200 ambazo ni bajeti nzima ya hii Wizara, ni hela ndogo sana kwa Serikali ambayo inakusanya zaidi ya shilingi trilioni moja kwa mwezi. Sasa kuna ugumu gani kupeleka hizo hela zote? Kwa nini kila mwaka hii Wizara hela inazoomba kwa maendeleo huwa hazikidhi vigezo vyao? Kwa nini hawapelekewi hela zao zote wanazoomba? *What is* billioni 200 kwa hii Serikali ambayo inakusanya zaidi ya shilingi trilioni moja kwa mwezi? Kwa nini wasipelekewe zote? Ugumu uko wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lazima tuje na jawabu kuhakikisha hii bajeti, fedha zote walizoomba wanapelekewa kama kweli tuna nia ya kutaka kumsaidia mkulima masikini wa kule kijijini.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nataka niongelee hivi vyama vya msingi, *AMCOS*. Ni kweli kabisa kwamba vyama vya *AMCOS* ni Sera ya CCM na vilikuja kwa nia nzuri ya kutaka kumsaidia mkulima, *especially* wa kahawa kule kwetu Mbozi. Kwetu Mbozi hivi vyama vya ushirika vimegeuka kuwa kaburi kwa wakulima. Kwanza vinachukua mikopo benki bila wanachama wao kujua, unapofika wakati wa malipo, benki inakuja inakata hela zao na kuwafanya wakulima wale masikini kushindwa kupata malipo yao.

Mheshimiwa Spika, mpaka dakika hii ninapoongea hapa ndani ya Bunge lako Tukufu, kuna *AMCOS* zaidi ya tisa ndani ya Wilaya ya Mbozi hazijalipa wakulima wao. Watu wameshindwa kupeleka watoto wao shule, wameshindwa kulima, wametiwa umasikini wa ajabu na Serikali ipo, inaona.

*Mheshimiwa Spika, siku moja nilishangaa hapa, posho zetu sisi Wabunge zilichelewa kwa siku mbili tatu, kulikuwa hakukaliki humu ndani. (Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge)*

Mheshimiwa Spika, lakini wakulima wangu mimi Mbozi hawajalipwa mwaka sasa fedha zao za *AMCOS* na hakuna anayeshtuka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenisongole, hapo unamchokoza Spika. Unajaribu kuonesha kama kuna *inefficiency* hapa ndani, kitu ambacho siyo kweli. Futa hiyo kauli yako.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, *okay*, nafuta, lakini msisitizo wangu...

**SPIKA:** Hakuna cha lakini, unafuta halafu unaendelea kuchangia.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, *okay*, nafuta.

**SPIKA:** Eeh, endelea.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, *point* yangu ninayotaka kusema ni kwamba, suala hili la wakulima wa *AMCOS* kutokulipwa, nataka nitilie mkazo, kwa sababu hawa ni watu ambao wamepeleka mazao yao, wamepima, lakini mpaka leo hii hawajalipwa. Katika hali hiyo, suala hili hatuwezi kumsaidia yule mkulima.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo, ninachoomba ni kwamba utakapokuja kuhitimisha bajeti,

uje na majibu ya kuhakikisha kwa nini hawa *AMCOS* mpaka sasa hivi bado hawajalipa fedha zao?

Mheshimiwa Spika, kwa kusema hayo, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa George Mwenisongole, Mbunge kutoka Mbozi.

Mheshimiwa Neema Lugangira, atafuatiwa na Mheshimiwa Vita Kawawa.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika Wizara hii. Naomba nianze kwa kusema naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Sera yetu ya Kilimo hapa nchini inasema kwamba Mgani Mmoja, Kijiji Kimoja. Kama tunavyofahamu, tuna vijiji takribani 12,000 lakini hadi sasa tuna wagani 7,000; kwa hiyo, tuna upungufu wa wagani kama 5,000.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa napenda kuipongeza Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, hususan Mheshimiwa Waziri, Prof. Adolf Mkenda, pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Hussein Bashe, kwa jitihada kubwa walizoweka kuleta mageuzi kwenye huduma ya ugani, ikiwemo kutenga bajeti kwa ajili ya kuwanunulia hawa Maafisa Ugani vitendeakazi kama pikipiki. Nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bado kuna changamoto ambayo naiona. Hii changamoto ni kwamba tunategemea Afisa Ugani huyu awe mtaalam wa kila kitu; ajue mazao yote, ajue masuala ya mbolea, masuala ya wadudu, masuala ya madawa, *fungus*, ukungu na kadhalika. Jambo ambalo siyo rahisi.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka miaka ya nyuma Serikali ilishaliona hili na ilianzisha kitu kinachoitwa *Ward Agriculture Resources Centers*, yaani Vituo vya Rasilimali ya Kilimo ngazi ya Kata. Kama sikosei vituo hivi vilianzishwa kwenye kata 200 hapa nchini. Pamoja na kuanzisha vituo hivi Serikali iliweka watalaam kwenye vituo hivi na iliweka vitendea kazi kama kompyuta, *generator*, *screen* za kufundishia na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Wizara kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, wamesema wanaenda kuvifufua hivi vituo, lakini ningependa kushauri kwamba, ni lazima Wizara iangalie hivi vituo kweli vifanye kazi ambayo ilikusudiwa. Nasema hivi kwa sababu hivi sasa, kwa kuwa hivi vituo vipo chini ya halmashauri, kwenye halmashauri nyingi vituo hivi havifanyi kazi iliyokusudiwa ya kuendeleza kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano pale Chamwino, kituo hiki badala ya kufanya kazi ya kuendeleza kilimo kinatumika na *TARURA*. Kwa hiyo ningependa kuishauri Serikali ipitie upya vituo hivi na ione kama vinatumika kadri ambavyo inafaa na kama kuna changamoto basi vituo hivi virudishwe viwe chini ya Wizara ya Kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapo hapo kwa miaka mingi sasa halmashauri zimekuwa hazitengi bajeti ya huduma ya ugani, ambapo hii ni changamoto kubwa na hatuwezi kuendeleza kilimo wakati ni hizi halmashauri karibu asilimia 70 ya mapato yao ya ndani yanatokana na kilimo, lakini utengaji bajeti wa huduma ya ugani hawatengi. Kwa hiyo hili nalo ningependa katika kuhitimisha najua linahusu zaidi Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Mheshimiwa Waziri yupo hapa pengine atatuambia anapanga vipi kuhakikisha kwamba hizi halmashauri zinatenga bajeti ya huduma ya ugani. Naamini kwamba lengo zima la kuanzisha vituo hivi lilikuwa ni kuhakikisha tunaimarisha huduma ya ugani. Tukifanya hivyo tutaweza kuongeza tija na muhimu zaidi kuongeza pato la mkulima. (*Makofi*)



Mheshimiwa Spika, eneo langu la pili ambalo ningependa kuchangia ni pato la mkulima. Kwa muda mrefu sana tumekuwa tukiongelea bei ya mkulima na kabla sijaingia hapa Bungeni nilikuwa nafanya kazi kwenye Shirika ambalo lipo chini ya Wizara ya Kilimo *SAGCOT* yaani *Southern Agriculture Growth Corridor of Tanzania* kama Mkurugenzi wa Idara ya Sera na Wezeshi kwenye Biashara, nimefurahi nimekwona boshi wangu Mr. Geoffrey Kilenga yupo ndani ya ukumbi huu wa Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kipindi kirefu tunaongelea bei ya mkulima, lakini nadhani wakati umefika sasa tuongelea pato la mkulima, kwa sababu tunapooongelea pato la mkulima lina *variable* mbili. *Variable* moja ni *price*, *variable* ya pili ni *quantity and quality*. Sasa tumekuwa tukiweka jitihada kubwa sana kwenye bei, tunasahau hii *variable* ya pili ambayo ni muhimu ya *quantity and quality*.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu wengi wameongelea tija yetu ya kwenye kilimo, nitatoa mfano mdogo, wenzetu wa Zambia kilo moja ya mahindi wanauza Sh.250 mpaka Sh.300 ya Tanzania na wenyewe wakiuza kwa bei hiyo wanarudisha gharama zao zote yaani wana-*break even*, lakini kwetu sisi Tanzania ili kufikia hiyo *break even point* lazima kilo moja ya mahindi tuuze Sh.500.

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo ipo hata kwenye pamba, nchi ambazo tunashindana nazo India, Brazil, China, Egypt, wao wanazalisha kwa eka moja kilo 1,000 mpaka kilo 1,250. Kwa hiyo wao wakiingia sokoni wanaweza wakauza kwa bei ya Sh.500 na waka-*break even*, lakini sisi kwa sababu tija yetu ni ndogo tunazalisha wastani wa heka hiyo hiyo moja kilo 250 hatuwezi kuuza kwa ile bei ya Sh.500 mpaka ifike angalau bei ya Sh.1,000.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hilo, ndiyo maana napendekeza kwamba ifike mahali Wizara ya Kilimo ianze kuongelea pato la mkulima na siyo bei ya mkulima. Kwa kufanya hivyo, tutaweza kuongeza tija ambayo itaongeza

mchango katika pato la Taifa kwa sababu tunasema kila siku asilimia 65 ya Watanzania wapo kwenye kilimo, lakini bado tunachangia asilimia 27 tu kwenye pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo inatokana na kwamba tija yetu bado ni ndogo na hiyo inatokana kwamba kila siku wimbo wa Wizara ya Kilimo ni kwamba bei ya mkulima. Kwa hiyo naomba kusisitiza tutoke kwenye bei ya mkulima twende kwenye pato la mkulima. Na na... *(Makofi)*

**SPIKA:** Bei ya mkulima ndiyo nini?

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, bei ya mkulima ni ile ambayo inakuwa inapangwa, yaani unakuta mkulima akishakuwa amepata mavuno, Wizara ya Kilimo inaitisha wadau, wanakaa halafu wanapanga bei ya mkulima. Kama wanaweza wakaitisha wakulima wazao wa pamba wanakaa wanapanga kwamba bei ya kilo moja ni Sh.1000 au wanaenda kwenye mnada. Sasa ninachojaribu kusema kwa kufanya hivyo hatukuzi tija inakuwa kama vile tunafidia ule upungufu wa tija ambao tulionao. Tukijikita katika pato la mkulima ina maana zile *variable* zote mbili, bei maana ya *price, quantity* na *quality* tutakuwa tumezifikia

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa fursa hii na naunga mkono tena hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Hili la idadi ya Wagani linahitaji kuliangalia, naona watu wengi wanachangia sijui Wagani ni wachache sijui, hebu tuangalie tija ya hawa waliopo kwanza. Jamani, jamani hata wajaze kila kijiji, sasa umeshaambiwa Njombe huko debe la mahindi Sh.3000 tatizo Mgani au tatizo nini? Kwa hiyo, kuna mahali pa kuanzia halafu hawa wengine watafuata tu, hata hao Wagani ambao wameshasomeshwa na Serikali, hawana ajira na nini, mambo yakishakuwa mazuri, wote hao watapata kazi, maana siyo lazima Serikali iajiri Wagani wote, lakini wakiwa ndani ya nchi na mambo yanakwenda vizuri watakuwa *busy* wote, walioajiriwa na wasioajiriwa watakuwa *busy*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Vita Kawawa, utafuatiwa na Mheshimiwa Philipo Mulugo.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia katika Wizara yetu hii ya Kilimo. Nawapongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu na watalaam wote wa kilimo wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nijielekeze katika malengo ya kimkakati ya Wizara ya Kilimo ambayo yapo tisa. Moja ya lengo la Wizara ni ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji, masoko na miundombinu ya uhifadhi wa mazao. Naomba nianze kuzungumzia hili la ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, miradi ya umwagiliaji iliyofanyika ilikuwa ni kukusudia kuongeza uzalishaji kwa wananchi na kwa Taifa zima, lakini ilikuwa haijafanyika tathmini ya miradi hiyo ipoje kwa sasa na je, miradi hiyo ilikamilika? Je, iliyokamilika ina-*perform* vipi? Uzalishaji wake ukoje? Naona hii tathimini ilikuwa haijafanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunapopeleka fedha za maendeleo katika maeneo kama haya ya kilimo kwenye umwagiliaji tunaenda kujenga *fixed asset* na *fixed asset* yoyote lazima tupime wakati inajengwa na inapokamilika, utekelezaji wake baada ya kukamilika, je, kile tulichotarajia kinaleta tija au la?

Mheshimiwa Spika, leo tunawashukuru Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imetuletea dodoso, Wabunge wote tumesambaziwa humu ndani, lakini dodoso hili tulilosambaziwa katika ukurasa wa pili, *paragraph* ya mwisho, mstari wa tatu kutoka mwanzo, *paragraph* ya mwisho, inasema:

*“Aidha, Tume imeambatanisha orodha ya skimu za umwagiliaji zilizopo katika jimbo lako kutoka katika kanzidata kwa ajili ya rejea yako.”*

Mheshimiwa Spika, ukimuuliza Mbunge yoyote humu hakuna *list* hiyo ya kanzidata humu. Sasa sisi tutajuaje hiyo miradi iliyopo katika kanzidata ambazo wamesema humu. Sasa hata tukijaza humu, tunajaza ile tunayoifahamu, kama mimi nimejaza ile ambayo haifanyi kazi na fedha nyingi zimeingia. Tuna Mradi wa Liyuni umeingia zaidi ya bilioni moja, lakini mradi haujakamilika mpaka leo. Nimekaa katika Ubunge miaka kumi, nikaenda likizo bila malipo miaka mitano ya ubunge, lakini ule mradi nimeukuta vilevile, haujakamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna Mradi wa Likonde, nao umeingia zaidi ya milioni 900, haujakamilika. Kuna Miradi ya Mwangaza, Mbecha na Mahoka, miradi hii haijakamilika, maana yake ilikuwa haijafanyika tathmini miradi ile imekamilika na inafanyaje, ina-*perform* au hai-*perform*. Kwa hiyo naomba sana tunapoelekeza fedha hizi lazima kweli tuwe tunaenda kufanya tathmini na ufuatiliaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nawashukuru sana Tume leo wametuletea, lakini tunaomba, naomba na mwongozo wako kwamba tupatiwe hiyo *list* ya miradi ya kanzidata za Serikali walizonazo ili tuweze ku-*compare* na tuone hiyo ni miradi ipi iliyokuwepo kule na sisi tuliyonayo ni ipi ambayo fedha nyingi za Serikali zimeingia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kuna jambo lingine sisi kwetu kule Namtumbo tuna kituo...

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa, endelea.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELE:** Mheshimiwa Spika, nataka nimtaarifu msemaji kwamba kiambatanisho hicho kipo katika hiyo bajeti iliyopo sasa hivi kipo, kinaonekana. Ahsante.

**SPIKA:** Ukurasa wa ngapi?

**MBUNGE FULANI:** Kipo Ukurasa wa ngapi?

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELE:** Mheshimiwa Spika, kipo *separate* yaani kimekuwa kiko peke yake.

**MBUNGE FULANI:** Wapi?

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELE:** Kwenye sehemu ya bajeti, kwenye kishikwambi pale..

**SPIKA:** Wanasema kwenye kishikwambi, hiyo orodha inapatikana.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELE:** Ndiyo kwenye kishikwambi pale, zipo *attachment* tatu.

**SPIKA:** Ahsante sana. Endelea Mheshimiwa Vita.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nashukuru kwa taarifa, nitaangalia kwenye kwishikwambi kwa sababu hotuba tumewekewa leo, ila humu hamna. Hili dodoso hili hatuwezi kulifanya leo tukalimaliza leo, kwa sababu kuna ekari humu zinatakiwa tuandike kuna ekari ngapi, maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, kijiji, kata na ekari za maeneo hayo. Kwa hiyo, lazima tupeleke kwa wataalam wetu wa kilimo katika halmashauri zetu, kwa hiyo lazima watupe muda na hili pia na hiyo tutaangalia kwenye vishikwambi vyetu hiyo taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuendelea. Sisi kule Namtumbo tuna Kituo kilichokuwa kinaitwa Shirika la Kilimo Uyole, Suluti au SKU Suluti, Namtumbo. Kituo hicho kilikuwa ni kwa ajili ya uzalishaji na utafiti wa mbegu ambazo zinafaa kwa ajili ya mazingira ya Nyanda za Juu Kusini na hususani Mkoa wa Ruvuma. Kilifanya kazi yake vizuri sana kituo kile, kilikuwa kinazalisha na mbegu za mahindi na mazao mengine mchanganyiko, lakini kituo kile kimekufa. Toka nilipopumzika Ubunge miaka mitano na nimerudi sasa hivi kimekufa kabisa. Majengo yake ni magofu, sisi kwetu kule tunaita mang'oa

au mang'oani. Mang'oani ni mahali ambapo waliishi mababu zetu halafu wakahamishwa kwenda kwenye vijiji au kwa jina lingine mahameni.

Mheshimiwa Spika, ukitaka kupajua hapa waliishi watu utakuta miembe mikubwa na yale magofu, mahameni. Sasa hicho kituo ni kama mahame tu, kule kwetu tunaita ling'oa na ni kituo cha Serikali kilichofanya kazi vizuri sana mpaka Mkoa wa Ruvuma ukawa unaonekana ni moja ya *big five* katika nchi hii kwa kuzalisha mazao ya mahindi, lakini kituo kile kimekufa... (*Makofi*)

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa, toa taarifa

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Nataka nimpe taarifa Mbunge anayezungumza sasa kwamba na ni suala la mang'oa ni eneo ambalo walikuwa wanaishi watu na watu wale wameshaondoka, inakuwa kama ni eneo ambao ni zama zamadamu, zile kumbukumbu za kale ndivyo ilivyo, ndiyo tafsiri yake. Ahsante sana.

**SPIKA:** Wote mnaongea lugha moja wote.

**MHE. VITA S. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, Ndiyo, tunaongea lugha moja na nashukuru.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Vita. Wote Wangoni hawa. (*Kicheko*)

**MHE. VITA S. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, sasa kile kituo kimekuwa kama kumbukumbu tu ya watu wa kale na wakati kilikuwa kinatusaidia na kipo pale na ni ardhi ambayo imehodhiwa na Serikali, lakini ipo ndani ya Mji wa Namtumbo, Kijiji cha Suluti. Tunaiomba Serikali ituambie inapokuja kujibu,

kituo kile watakifufua au waturudishie Suluti tuendelee kuifanyia shughuli zingine za kilimo au pale tujenge shule. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la pili, tuna shamba kubwa lililokuwa linaitwa *NAFCO*, nalo vilevile limekufa miaka mingi kabisa na hakuna chochote kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wamenikatiza, lakini naunga mkono hoja. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Vita kawawa, tunakushukuru sana. Mashamba ya Serikali yaliyokufa ni mengi sana, ndiyo hayo nilikuwa nasema tangu asubuhi kwamba ipo haja ya kuangalia namna gani ya kusonga mbele na jambo hili.

Mheshimiwa Philipo Mulugo atafuatiwa na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

**MHE. PHILOPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nimwombe sana Mwenyezi Mungu niweze kuzungumza katika hali ya kawaida nisi-*panic* kwa sababu Wizara hii ilitaka kusababisha mimi nipoteze uhai kwa sababu ya suala la stakabadhi ghalani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naongea hapa kwa niaba ya wananchi wa Songwe, Wilaya ya Songwe ambayo takribani miezi miwili sasa tulipata kidogo mgogoro juu ya suala la stakabadhi ghalani. Cha kwanza, nataka nielezee Wizara ya Kilimo sijui kama wanafanya utafiti. Suala la stakabadhi ghalani Wizara ya Kilimo au Serikali kwa ujumla wanasema ni suala la mpango wa kumkomboa mkulima, si sawa kila suala hili ni zao la kumchanganya mkulima. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mkulima hana amani kabisa na suala la stakabadhi ghalani. Ni kweli jambo hili lipo kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi na naomba ikiwezekana kama tunaweza hata tukalirekebisha tulitoe kabisa kwa sababu

kule vijijini haliji katika mfumo wa kubembelezana, ni jambo la lazima kwa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, haiwezekani! Mkulima huyu wakati anaandaa shamba Serikali haipo wala haimwoni, mkulima huyu anapopalilia Serikali haipo wala haimwoni, anakopa fedha kwa wachuuzi wa zao la ufuta au alizeti Serikali haipo, halafu baadaye mwezi Machi au Aprili, ufuta umeshang'aa sasa umekomaa, Serikali ndiyo inakuja inasema, sasa ufuta wote huu tunaomba msiuze kwa huko mlikokuwa mmekopa hela ila mpeleke stakabadhi ghalani. Haiwezekani katika hali ya kawaida. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nilihama Bungeni hapa sikuwepo takribani mwezi mzima, nilikuwa Jimboni nashughulikia wakulima wangu hapa. Ni kero kubwa, nimshukuru sana Mheshimiwa Bashe nilimpigia simu, Mheshimiwa Waziri nilimpigia simu alipokea baadaye akasema atanipigia na hakunipokea, nina jambo naye, lakini namshukuru sana Mheshimiwa Bashe kwa sababu alipokea simu na kesho yake aliwatumia Mrajisi na Mr. Bangu, Mkurugenzi wa Stakabadhi Ghalani, akaja mpaka Songwe Jimboni. Nimewaona wale pale wamekaa, waseme wenyewe waliona nini kule jimboni. Haiwezekani mambo kama haya Serikali tunaangalia tu! (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba Wabunge wenzangu kesho waniunge mkono, kesho nitavaa suti nyeusi hapa kwenye kushika shilingi, kwamba stakabadhi ghalani tunaizika kesho, haiwezekani! Kesho ni msiba wa stakabadhi ghalani nchini Tanzania. Haiwezekani kabisa, nakataa. Jambo hili ukiwaona wale wakulima wanahangaika nalo.

Mheshimiwa Spika, kule Songwe kuna maghala matatu...

**MHE. KIZITO J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.



**SPIKA:** Mheshimiwa Mulugo kuna taarifa sijui ipo wapi, Mheshimiwa Mwambe, hapana Mheshimiwa Mhagama yupo nyuma yake ndiyo maana nilikuwa simuoni. *(Kicheko)*

**MHE. KIZITO J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mulugo kwamba stakabadhi ghalani inatamkwa kwa jina Tanzania, lakini *practice* ya stakabadhi ghalani Tanzania ni *collection center* ya mazao, inalenga kukusanya mapato ya Serikali, na siyo kuwasaidia wakulima wadogo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sisi Mkoa wa Dodoma, maeneo yaliyokuwa yanalima ufuta mwaka huu wameacha kabisa kulima ufuta. Wameacha kwa sababu ya kutotaka kugombana na Serikali kuhusu stakabadhi ghalani, maana ukishapata huo ufuta unaweza ukafungwa bure na zao la kwako mwenyewe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mulugo, endelea.

**MHE. PHILIP A. MULUGO:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa kwa mikono miwili na miguu miwili. Kama nilivyosema, mkulima huyu tunasema eti tunamtetea mkulima huyu. Wilaya ya Songwe ni kubwa kuliko hata Mkoa wa Songwe wenyewe ukilinganisha Wilaya ya Mbozi, Momba na Ileje, lakini tulikuwa tumewekewa *center* tatu za ukusanyaji wa ufuta, Mkwajuni, Chang'ombe na Kanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutoka Mkwajuni mpaka uende nilikozaliwa mimi Kijiji cha mwisho kabisa karibu na Ziwa Rukwa kule ni kilometa 168. Mkulima huyu anyanyue debe mbili za ufuta alete Mkwajuni aje auze, nilikataa na nilimwambia Mkuu wa Wilaya utaniweka ndani bure. Haiwezekani katika mazingira ya kawaida, lakini Serikali inaendelea kulazimisha, Mrajisi yuko pale nimemuona aseme mwenyewe aliona nini Songwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkuu wa Wilaya ya Songwe ilikuwa ukiwa na ufuta akikukamata anakuweka ndani, mpaka ninavyosema hivi, pikipiki ziko ndani, alikuwa ameshikilia

magari yote ya wakulima, haiwezekani tu katika mazingira ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo, wale watumishi wa Serikali wa Wilaya ya Songwe hasa Afisa Kilimo, alikuwa akienda vijijini anasema elimu imetolewa. Mimi ndiyo mfadhili mkubwa wa vikoba kwenye jimbo langu, wanakwenda kwa mwenyekiti wa vikoba wanasema, naomba uandike barua hapa nakupa shilingi 100,000/=, saina hapa, sema hiki Kikoba, ni Chama cha Ushirika cha Msingi, ni uongo mtupu. Haiwezekani katika mazingira ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kesho, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Bashe, tuseme kesho, stakabadhi ghalani ndio basi haiwezekani, ni jambo baya mno kwa mkulima, tuweke kama tulivyoweka kwenye ada elekezi. Serikali ilisema ije na ada elekezi kwenye shule binafsi, tukasimama kidete tukasema hivi, kila mtu ana fedha zake ampeleke mtoto anakotaka mtoto kusoma shule. Aende Kenya akasome shule, aende Marekani akasome shule, tumuache mkulima kwenye ufuta akauze anakotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nenda sasa hivi Wilaya ya Songwe wakulima wa ufuta wanauza Mbalizi, wanauza Mkwajuni, wanauza Tunduma, wanauza Mbozi *they are free*, tuwaache wawe *free* kwa sababu, ndiko wanakofaidika huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkulima katika maisha ya mwaka mzima anakopa fedha za kwenda kujitibu masikini ya Mungu, anakopa fedha kumpeleka mtoto shule mwezi wa kwanza, anakopa fedha kwa ajili ya kuendeshea mifumo ya chumvi, sabuni. Leo hii amechukua fedha pale kwa jirani yake ambapo amemuambia atamlipa ufuta wameandikishana, *butter trade* wameandikishana, leo Serikali inakuja kusema kwamba, ufuta wote mpeleke pale mkauze kwa stakabadhi ghalani, tunakupa risiti, tutakupa fedha baada ya masaa 48. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii Mbunge nalipa wakulima wangu wa pamba toka mwaka 1995 niko *form six*, watu

walikuwa wanauza pamba hawajalipwa mpaka leo na risiti ninazo, nitakuletea Mheshimiwa Bashe risiti za wakulima wa Songwe wanaodai fedha za pamba, ilikuwa ni mambo ya stakabadhi ghalani. Nazungumza kwa uchungu mkubwa sana naomba ninyamaze. Siungi hoja mkono. (Makofi)

**SPIKA:** Haya mambo Waheshimiwa Wabunge, sio utani, nilichosema ni kweli sisi Mkoa wa Dodoma, sisi wenzenu tumeachana na hiyo biashara, hulimi hilo zao unaacha unalima kitu kingine. Kwa sababu, zao lako mwenyewe linakufunga. (Makofi)

Sasa wewe debe mbili ukapeleke stakabadhi ghalani, mpaka waje wauze, siku wanayouza utaweza wapi, kilometa kwa kilometa haiwezekani baadhi ya vitu. Ndio hili tulikuwa tunasema asubuhi *government intervention*, yaani *government intervention* inatakiwa ndio iwepo, lakini *minimal* na katika nchi za wenzetu zilizoendelea, kampeni mojawapo katika uchaguzi mkuu ni kitu kinaitwa *less government*. (Makofi/Kicheko)

Yaani, *less government* katika maisha ya watu, sio ukigeuka Serikali, ukigeuka Serikali, ukigeuka Serikali, yaani Serikali iwepo kidogo kidogo watu wajimwage katika nchi yao wasikie wana nafasi. Ukilima ufuta Serikali, ukifanya hivi Serikali sasa unafanyaje? Ukilima korosho ndio kabisa, Serikali hebu rudini nyuma kidogo wapeni watu nafasi. Nyinyi ni *facilitators*, wasimamizi pale ambapo mtu anadhulumiwa na kadhalika. Lakini sio *front* sana ndio *openness* ile tuliyosema. Pole sana Mheshimiwa Mulugo, tulisikia, lakini tulikuwa tunasubiri uguswe tu lakini bahati nzuri hukuguswa sana. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Toufiq na Mheshimiwa Issa Mchungahela ajiandae.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia na nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu

Waziri kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, pongezi zangu za kazi nitawapa baada ya kumaliza matatizo ya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, pia, ninawashukuru wataalam wakiongozwa na Katibu Mkuu, kwa kweli nimepita kwenye hotuba hii kuna mambo nimeyaona mazuri mazuri hasa ujenzi wa skimu, kwa hiyo, kuna msembo mmoja wa Machame wanasema *nyamnya mwishanyo hufoo* angalau kuna mambo tumeyaona.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze kuhusu Ushirika, lakini naomba nizungumze taratibu kabisa leo Mheshimiwa Waziri kaka yangu na Naibu Waziri, wanielewe kwamba huku kuna shida. Katika maeneo yana majizi ni kwenye Ushirika na hao ndio wanaoturudisha nyuma, hao ndio wanafanya kilimo nchi hii kisiendelee. Ukisoma Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, imeeleza vizuri nia njema ya chama na Serikali kuhakikisha Ushirika unabadilisha maisha ya watanania. Naomba kwa ruhusa yako uniruhusu nisome mistari michache tu, kwenye Ilani hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ukurasa wa 30 pale wanasema, Chama Cha Mapinduzi kinaamini kuwa, Ushirika ni njia ya uhakika ya kuwezesha wanachama kuwa na uwezo mkubwa wa kutatua matatizo yao ya kiuchumi, kijamii kwa kutumia juhudi zao za pamoja katika kufikia malengo, hiyo ndio Imani ya Chama Cha Mapinduzi lakini ndio imani ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, uhalisia ni kinyume kabisa na hiki kilichoandikwa hapa, haya Maushirika sasa hivi sio Ushirika tena Mheshimiwa Waziri na wewe unajua, ni watu wachache 7 wanaitwa Bodi za Ushirika ndio wanaoendesha mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa wanaingia mikataba ya ovyo duniani hujapata ona, anakuja mtu anaitwa mwekezaji, anapewa shamba kwa bei ya kutupa, humo ndani yaliyoandikwa kwenye mikataba ni mambo ya hovyoy, ukijaribu kuwaambia naomba tuone wanakuambia sheria

ya Ushirika ya mwaka 2013 haimruhusu Mbunge kujua kinachoendelea, haimruhusu Mkuu wa Wilaya, haimruhusu Mkuu wa Mkoa, haimruhusu Mwenyekiti, haimruhusu Diwani, hii kitu gani hii! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri majuzi nilienda ziara ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaomba utulivu kidogo, endelea Mheshimiwa Saashisha.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, tumeenda kwenye ziara ile na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii na Naibu Waziri, kwenye chama kimoja cha Ushirika cha Makoa Waziri alipofika kule akaniambia Saashisha sasa nimekuelewa. Ule mkataba ni aibu, vitu vinavyofanyika pale havifai kusema hapa, maana duniani wanatusikiliza watatushangaa kwamba, Tanzania kuna kitu cha namna hii.

Mheshimiwa Spika, mtu anapewa mkataba miaka 60, miaka 30 halafu kwenye ule mkataba kuna madalali zaidi ya saba. Nilisimama pale namueleza Naibu Waziri yuko hapa, dada yangu nilikuwa naye Masanja, nawaambia hebu niambieni ninyi wataalam mmesomeshwa kwa fedha za nchi hii hiki ni nini?

Mheshimiwa Spika, mtu amepewa vibali vya kwenda kuhudumia wanyama hana *document* yoyote na Vyama hivi vya Ushirika, bado hapa tunasema watu wanaona sijui vitu gani? Ukizungumza kule Hai moja ya kero na iliyosababisha umasikini ni vyama hivi vya Ushirika. Kihistoria nilishasema nia ya Serikali ilikuwa ni nini na sisi kwenye mashamba haya kupitia Ushirika huo huo. Sisi Ushirika wetu kule unachukua Kijiji kizima wanakuwa ni sehemu ya Ushirika. Tulikuwa tunalima kwenye haya mashamba sisi hatuna ardhi ya kutosha kwa hiyo, kwetu sisi nusu heka ni kitu kikubwa mno. Kwenye nusu heka ile tulikuwa tunalima tunapata mahindi, tunapata maharage, tunapata alizeti, tunapata chakula cha ng'ombe.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, mazingira yetu ya kulima eneo letu limegawanyika kuna sehemu makazi ya watu, lakini kuna sehemu maalum ya kulima. Kule wanapolima watu ndipo ambapo mashamba haya yameshikwa na Ushirika. Asilimia 78 ya mashamba yetu yako chini ya Ushirika, yanaamuliwa na watu saba tu kitu hiki ni hatari. Ni hatari kubwa kwa sababu wao ndio wanaoamua, leo hii tunazungumza mashamba, shamba kama la *silver day* amepewa mtu pale hajalipa miaka mitatu. Lakini yumo ameshikilia na sisi hatuna pa kulima, ndio maana ilifika mahali nikasema sisi tutaenda kugawana kazi yangu rahisi sana kwasababu, mashamba tunayaona Mheshimiwa Waziri wewe unajua yaani ukifungua moyo wako unajua matatizo yaliyoko kwenye Ushirika tutaenda kugawana mashamba yale sisi wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niwape mfano mmoja, Jumapili moja nilikuwa naingia kanisani tena bahati mbaya nimeingia kwa kuchelewa. Nimefika katikati mama mmoja bibi akanishika shati nikamchekeki huyu mama vipi! Ikabidi nitoke naye nje akaniambia Saashisha sikiliza, mimi nimeshiriki kwenye vita ya Uganda niko tayari kupigana tunataka shamba letu la *Silver Day*. Huyo ni mwananchi wa kawaida tena bibi halafu mnataka Mbunge nije hapa niwasikilize, mimi kuna siku mtaniweka ndani kwenye mambo haya ya Ushirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maana kama mashamba tunayaona si tunaenda kugawana tu, hatua 20 nusu heka Masawe chukua, Kimaro chukua tunagawana halafu mtakuja kukutoa na polisi. (Kicheko)

Mheshimiwa Spika, haiwezekani namna hii watu wachache wanafanya maamuzi kwa sababu yetu, tunawaambia hapa fedha zinazolipwa kule hiyo heka moja inakodishwa kwa shilingi 65,000 dola. Tena wanatuwekea viingereza vigumu vigumu, ili kuwababaisha watu dola 65 yule mtu anaenda kumpangisha tena mwananchi kwa shilingi 300,000/= mpaka 350,000/= kwa hiyo, fedha yake aliyokuja nayo inarudi pale pale na mengine yako tupu.

Mheshimiwa Spika, hiyo fedha yenyewe dola 65 haifiki kwa mwananchi, hata kama inafika kwa mwaka kwa mfano, analipwa shilingi 45,000,000/= zinapigwa, zinapigwa mpaka kufika kwenye kile kijiji kinachohusika, inafika shilingi 5,000,000/= unaambiwa ikajenge choo cha shule. Kweli leo tunabadilishana mahindi, maharage, chakula cha ng'ombe na kuondoa ujinga maana mtu asipofanya kazi atakuwa mjinga. Vyote hivi tunabadilishana kwa kujengewa choo cha shule ya msingi! Hapana. Niiombe sasa Serikali ikubali na Mheshimiwa Waziri hili unalimudu kwani hivyo Vyama vya Ushirika kuna miungu si ni watu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwani ukitamka kuanzia leo Mkoa wa Kilimanjaro nasimamisha viongozi wote wa Ushirika tuunde upya. Nimekaa na Mrajisi nikapita naye *document* hii hapa nikamuambia Mrajisi hebu tazama yeye mwenyewe anaumia kama mimi. Nimekaa na wewe Mheshimiwa Naibu Waziri na wataalam wako unaumia kama mimi, wale wataalam wako uliosema wakachunguze kule nimekaa nao wanalia kama mimi, hivi kwa nini hatuchukui maamuzi? Kama wote tunaona tuna majizi! Hebu ifike mahali niombe Serikali iingilie kati, tufanye na sio kwamba nachukia Ushirika napenda Ushirika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha muda, unga mkono hoja. (Kicheko)

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa naunga mkono hoja kwa sababu, ameniwekea fedha za umwagiliaji, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, huyo ni Saashisha Mafuwe Mbunge wa Hai, Mheshimiwa Fatma Toufiq, nilishamtaja na Mheshimiwa Issa Mchungahela.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana nami nashukuru kwa kunipa fursa niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji

wote wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba hii. Najua muda ni mchache sana lakini nitajitahidi.

Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu kuipongeza sana Serikali, kwa kuifanya sekta ya kilimo iweze kutoa mchango mkubwa sana katika ukuaji wa kilimo, wa uchumi, lakini sambamba na hilo katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, kilimo kimechangia asilimia 65 ya malighafi za viwanda niipongeze sana Wizara kwa kufikia hatua hii.

Mheshimiwa Spika, sambamba na pongezi hizo naomba nitoe ushauri kwamba, iwapo bajeti itakuwa ya kutosha ina maana kwamba, uwezekano wa uchumi wetu kukua kutokana na kilimo unaweza ukafika zaidi ya asilimia 90. Lakini sambamba na hilo, hata katika upatikanaji wa malighafi ikipatikana pesa ya kutosha kwamba, kilimo kikawa kina tija ina maana kwamba, uchangiaji katika zile malighafi unaweza ukafika asilimia 100 na hatimaye mwisho wa siku, tunaweza tukapata ziada zaidi na tukaweza kuuza nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kubwa ninachoweza kuishauri Serikali hapa ni kwamba, kuona jinsi gani tunaweza kupata bajeti ya kutosha ili kusudi kuweza kuwekeza katika kilimo. Naomba pia, nizungumzie kuhusu kilimo cha umwagiliaji, wenzangu wengi sana wamezungumzia kuhusu kilimo cha umwagiliaji. Niipongeze sana Serikali kwa kuweza kuwa na hekta 694,715 kwa mwezi Mei, 2020 hadi hekta 695,045 mwezi Machi, 2021 hii iko katika ukurasa wa 10 wa hotuba hii. Kumbe ni kwamba tukiwekeza zaidi katika kilimo tija itakayopatikana ni kubwa sana na sasa kubwa ni kwamba, Wizara ione umuhimu wa kuhamasisha wananchi waweze kujikita zaidi kwenye kilimo cha umwagiliaji kulikoni kilimo cha mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hilo kwamba, wadau wengi zaidi waweze kuingia katika kilimo cha umwagiliaji. Naamini kabisa mapinduzi ya kilimo yanaweza yakawezekana na hatimaye, sisi tukawa ni miongoni mwa



nchi ambayo inaweza ikalisha hata nchi mbalimbali katika dunia hii. Lakini pia mazao ya biashara yanaweza yakapatikana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nilitaka kuzungumzia ilikuwa ni kuhusu bima ya kilimo, niipongeze sana Serikali kwa kuona umuhimu wa bima ya kilimo. Ninajua kabisa kwamba bima hii kutokana na taarifa ambayo nimeiona katika hotuba hii, inaweza ikasaidia wananchi wengi sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ushauri wangu mkubwa ni kwamba, Serikali sasa iharakishe kukamilisha ule Mpango wa Taifa wa bima, kwa ajili ya kilimo ili kusudi kuwanusuru wananchi wengi zaidi. Na wakulima wengi Zaidi, waweze kuelimishwa kuhusu hii bima ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo natamani kulizungumzia ni zao la zabibu. Kwanza niipongeze sana Serikali kwamba katika hotuba hii, ukiangalia ukurasa wa 27, ukurasa wa 107, ukurasa wa 131 na ukurasa wa 158, kuna *element* ya zabibu imezungumziwa pale. Kwa hiyo, hapa sasa tunaona mwanga kwamba sasa Serikali inaona kwamba, kuna umuhimu wa kuwekeza katika hili zao la zabibu, lakini sambamba na hilo nilikuwa naomba niishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna mashamba katika maeneo mbalimbali mfano katika Wilaya ya Chamwino kuna shamba, kuna maeneo ya Gawaye kuna shamba, kuna eneo la Hombolo kuna shamba na kuna baadhi ya maeneo ya Bahi na kadhalika. Ushauri wangu, Serikali ingeona umuhimu wa kuweza kufanya *block farming* katika zabibu na ikiwezekana zabibu nayo iwe ni zao la kimkakati katika Mkoa wa Dodoma. Kwa sababu, unapozungumzia zabibu, zabibu katika Dodoma ni siasa, zabibu katika Dodoma ni uchumi. Kwa hiyo, ushauri wangu ulikuwa ni huo, Serikali ijaribu kuwekeza zaidi na zaidi katika zao la kilimo kwa sababu, sisi wana Dodoma tunaona kabisa kwamba, zabibu ni fahari ya Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na ninasema hivyo kwasababu kwamba zabibu ya Dodoma yenyewe ni *unique* sana. Kwasababu imekuwa ikizaliwa kwa vipindi viwili, yaani kwa awamu mbili unaweza ukapata zabibu na hii ni *very unique*. Kwa hiyo, ninachosisitiza ni kwamba, Serikali ione umuhimu wa kulifanya kwamba zao la zabibu liwe ni zao la kimkakati katika Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwapongeze sana Wizara kwamba, katika ukurasa wa 89 wa hotuba ya Waziri, amezungumzia hatua ambayo Wizara imekuwa ikichukua, kutoa huduma ya lishe kwa wale wafanyakazi ambao wameonekana na *VVU* hongera sana kwa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara zingine, Idara za Serikali na Taasisi za Serikali, zione umuhimu pia wa kuona kwamba, wale wafanyakazi wote ambao wamejidhihirisha na wale ambao hawakujidhihirisha, tunawashauri kwamba wadhihirike, ili kusudi waweze kupata huduma ya lishe kwa ajili ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie kuhusu mazao ya bustani, mazao ya bustani bado bei ya zile mbegu ni kubwa na mbegu zinatoka nje. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kushauri kwamba ikiwezekana basi, hebu hizi taasisi zetu za ndani nazo ziweze kuzalisha mazao bustani, kama vile mbegu za nyanya, mbegu za matikiti na nyinginezo ili kusudi sasa, zikiuzwa hapa ndani kwa bei ya ndani itakuwa ni bei nafuu Zaidi, kulikoni ambayo ile inayotoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, ahsante sana kwa kunipa fursa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Fatma Toufiq kwa kuzungumzia mazao ya Mkoa wa Dodoma pia. Mheshimiwa Waziri mwaka huu kilimo cha karanga tunalima lima karanga hapa Dodoma nyingi, karanga hazikuzaa kabisa, yaani kabisa na mazingira ni ya kawaida mvua ni ya kawaida, lakini hazikuzaa sijui sababu ni nini? Ni vizuri mkawapa wataalam wakajaribu kuangalia tatizo ni nini sababu mbegu

ni zile zile za kawaida, mvua ya kawaida kila kitu cha kawaida lakini watu mwaka huu hamna karanga kabisa ni la kulitazama hilo pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Issa Mchungahela, atafuatiwa na Mheshimiwa Yahya Mhata.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikushukuru wewe mwenyewe binafsi, kwa kadri jinsi unavyoiondeshwa taasisi yako hii ya Bunge. Lakini nimshukuru pia Naibu Spika kwa kazi hiyo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze katika sekta hii ya kilimo, Sekta ya kilimo imekuwa ni sekta nzuri ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa sana uchumi wa nchi hii. Kwa muda wote sekta ya kilimo imekuwa namba moja katika uchangiaji katika uchumi wa nchi hii. Kwa mfano, mwaka 2018 sekta hii ilichangia kwa takribani asilimia 27.9 ya bajeti nzima. Lakini pia mwaka 2019 ilichangia kwa takribani asilimia 26.6 kwenye bajeti ya nchi nzima. Lakini imeendelea pia kuchangia sekta hii katika ajira, asilimia 58 ya ajira zinazopatikana katika nchi hii zinachangiwa na sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Halikadhalika asilimia 65 ya malighafi *(raw materials)* inachangiwa na sekta ya kilimo. Baada ya kuona umuhimu wote huu bado Serikali imeendelea kuwa na kigugumizi kikubwa katika kuhakikisha kwamba sekta ya kilimo inapata haki inayostahili. Serikali imekuwa haioneshi weledi wake katika kuchangia sekta hii kikamilifu. Naomba kwa namna moja au nyingine, Serikali ioneshe nguvu zake zote kwenye sekta ya kilimo kusudi tuweze kufanya mapinduzi ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi tunatumia jembe la mkono, maeneo mengi sana jembe la mkono limekuwa siyo Rafiki. Hali hii imesababisha mpaka vijana ambao ndiyo wengi katika nchi hii kushindwa kujiingiza katika sekta ya kilimo kwa sababu ya ugumu wa matumizi ya hili jembe la mkono. Kwa hiyo, naiomba Serikali itilie mkazo kwa kiasi

kikubwa kuiinua sekta hii ambayo inabeba ajira za wananchi walio wengi hasa wananchi walioko pembezoni vijijini huko.

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali pia inaona shida gani kutumia sekta zake tofauti, kwa mfano sekta ya fedha kama benki, kuyaamrisha au kuyapa taarifa kwamba wawakopeshe wananchi. Kuna ugumu gani kwa sababu hii ni sekta muhimu na kilimo kinakopesheka. Wananchi wote ambao wanashughulika na kilimo wanakopesheka.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mfano mdogo tu wa zao la korosho limetoa dola takriban bilioni 589. Hizi ni fedha nyingi sana, ni trilioni 1.3. Nashangaa kwa nini Serikali imekuwa na kigugumizi kuwekeza katika kilimo kwa sababu hii trilioni 1.3 ni takriban asilimia 4 ya bajeti nzima. Ukiangalia ni mchango mkubwa sana, sioni sababu kwa nini Serikali haijajielekeza kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, sisi pia tumejitambulisha kuwa tunataka kuendesha uchumi wa viwanda. Uchumi wa viwanda hauwezi kufanikiwa pasipokuwa na sekta ya kilimo. Kama tulivyoona pale kwamba asilimia 65 ndiyo inapeleka pale kama malighafi, sasa ugumu uko wapi?

**SPIKA:** Unajua Mheshimiwa Mchungahela, Waheshimiwa tuwe tunawasikiliza Wabunge wanaochangia. Huyu ni Mheshimiwa Issa Mchungahela wa Lulindi, unajua kule Kusini zamani neno mhasibu halikuwepo walikuwa wanaitwa wachungahela. *(Kicheko)*

Mpaka sasa hivi Mheshimiwa hueleweki kwa kweli, yaani hujajikita moja kwa moja kujaribu kueleza kitu chako, unapiga *theory*. Hebu endelea kidogo lakini shuka kwenye kitu ambacho unataka kifike.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kujikita kwenye korosho. Korosho kwa namna moja au nyingine iko wazi kabisa kwamba inachangia kiasi kikubwa kwenye uchumi lakini pia kwenye ajira ya wananchi

wa Kusini kwa sababu ni pesa nyingi sana ambazo Serikali inapata kupitia kwenye korosho.

**SPIKA:** Yaani mtu anaweza akakuuliza swali, haijajikita vizuri kiviwi, unataka kusema nini? *(Kicheko)*

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Ahaa.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Ndiyo, taarifa, nimekusikia.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Mchungahela, anaposema Serikali haijajikita ipasavyo kwenye kulisaidia zao la korosho, hivi tunavyozungumza hata Bodi ya Korosho yenyewe haijaundwa. Bodi ile ya Korosho kwa sasa inakaimu Mkurugenzi hamna analolifanya. Kwa hiyo, napenda kumpa taarifa msemaji anaposema Serikali haijajikita alijumuishe na jambo hilo la Bodi ya Korosho. *(Makofi)*

**SPIKA:** Yaani anasema lilelile nililokuwa nakushauri mwanzoni, unaposema kitu hebu fika mwisho.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** *Yes!* Napokea taarifa Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nataka kusisitiza kwamba hata jitihada zinazofanyika sasa hivi za kupeleka pembejeo, hizo pembejeo mpaka sasa kuna maeneo ya Jimbo langu ambapo ndipo panapozalishwa korosho mapema sana, sasa ni kipindi cha maandalizi ambapo pembejeo zinahitajika lakini hazijafika. Kwa hiyo, nilikuwa najaribu kuonesha pia katika mazingira hayo kwamba kwa namna moja au nyingine umakini sana unatakiwa katika utekelezaji wa yale tunayoyazungumza.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Issa Mchungahela, bahati mbaya dakika zimeisha. Nakushukuru sana sana kwa mchango wako.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Yahya Mhata atafuatiwa na Mheshimiwa Jonas Mbunda na Janejelly ajiandae.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, nami naomba nichukue nafasi hii kwanza kuipongeza sana Wizara, kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara kwa kazi kubwa waliyoifanya katika uandaaji wa bajeti hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nielezee kwa ufupi faida za korosho. Korosho tunapata tunda, katika lile tunda tunaweza tukatengeneza *juice* na *wine*. Lile bibo lilikauka unaweza ukatengeneza *spirit*, viwandani, hospitalini na kwenye maabara tuna shida kubwa ya *spirit*. Wenzetu wa Naliendele wamekwenda mbali kutengeneza *spirit* kwa kutumia bibo. Sasa hivi wamefikia asilimia 82 ya *spirit* kwa tunda lile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, korosho yenyewe unaweza ukala, wengi wenu mnajua kazi yake lakini unaweza ukatengeneza siagi. Wenzetu wa Naliendele wana siagi ya korosho na imekuwa *approved* na *TBS*. Pia ile korosho ukisaga, unaweza ukatengeneza chapati. Aidha, korosho ni tui, unaweza ukapika mboga kwa tui la korosho na ukikutana na mwanamke wa Kimakonde hutamuacha. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tumsikilize Mheshimiwa.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, *nutshell* ya ile korosho ni mafuta yanayotumika katika dawa. Unaweza ukapaka kwenye mbao kama alivyosema

mwenzangu na ile haitaliwa na mdudu yeyote. Lile bibo ukishakamua ni mashudu na ni mbolea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niulize Wizara, mambo haya walikuwa wanayajua? Viwanda vingetumia korosho hii leo tungekuwa wapi? Nina uhakika tungetengeneza *wine*...

## T A A R I F A

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mhata.

**SPIKA:** Ndiyo Mheshimiwa Cecil.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa kwamba pamoja na hayo anayoyasema, Serikali hii ilikamilisha utafiti wa haya yote anayoyasema ambao unapatikana pale Naliendele kinachosubiriwa ni kufanya *implementation*. Kwa hiyo, sasa awaulize utekelezaji wa haya yote ili kuongezea wakulima mapato kutokana na zao la korosho utaanza lini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nampa taarifa hiyo.

**SPIKA:** Taarifa hiyo unaipokea Mheshimiwa Yahya?

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, huko ndiyo nilikokuwa nakwenda, namshukuru sana mwenzangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba wenzetu wa Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara ule Mfuko wa *export levy*ndiyo ulitakiwa ufanye kazi hizi. Tuna kazi kubwa ya kufufua viwanda vyetu vya *wine*, kutengeneza viwanda vya mbolea na *juice*. Kama tungeutumia Mfuko ule vizuri kwa kuwatumia wataalam wetu wa Naliendele, miaka hii mitatu tuliousimamisha tungekuwa tuko mbali sana. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara tutumie Mfuko ule wa *export levy* ili kuwezesha wenzetu wa Naliendele wafanya utafiti wao

wa dhati kutafuta mazao mbadala ya korosho hatimaye viwanda vingi viweze kutekelezwa ndani ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala langu la pili, kule Jimboni kwetu kumeingia mtafaruku. Kuna barua iliyoandikwa na Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Korosho inayowataka wakulima wote kukatwa Sh.110 kutoka katika mauzo yao ya korosho baada ya kupewa *sulphur*. Barua ile inachanganya sana. Inasema hata mkulima akipewa mfuko mmoja akienda kuuza tani 20 atakatwa Sh.110 kwa kila kilo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mtendaji huyu amekwenda mbali kwa kujiamini kabisa kwa kuwaandikia Wakurugenzi kwamba hayo ni maagizo na lazima yatekelezwe. Hili jambo halikubaliki. Kama mwananchi anakopeshwa mfuko mmoja, kwa nini usimkate kwa mfuko mmoja? Unamkataje kwa idadi ya korosho alizoleta kwa ajili ya kuuza *go-down*? Hii kitu hakikubaliki.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Mheshimiwa Waziri, ile barua ifutwe. Mtendaji yule anasema baraka hizi amezipata kwa Wabunge, Wabunge wapi? Ni nani aliyempa idhini ya kuandika barua hiyo? Kwa kweli anatuchanganya na anawachanganya wananchi. Namuomba sana Mheshimiwa Waziri, Mtendaji huyu usipomuangalia ipo siku tutamtoa ofisini kwake kwa nguvu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala la minada, Mheshimiwa Waziri amezungumza vizuri sana asubuhi kwamba takriban minada 70 imefanyika ndani ya nchi hii kwa msimu uliopita na minada ile ni mizuri kabisa na mimi naiunga mkono. Hata hivyo, kuna upungufu kwenye minada ile.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Tandahimba imetokana na Wilaya ya Newala lakini utashangaa bei za minada zinatofautiana. Unaambiwa korosho za Tandahimba ni bora kuliko korosho za Newala ambapo jana walikuwa Wilaya moja. Leo kwa kugawanywa tu, bei zinatofautiana. Wilaya ya Nanyumbu, wilaya yangu mimi imetokana na Wilaya ya



Masasi. Mwanzo, bei ilikuwa moja kwa kugawanywa tu, bei zinatofautiana, hii ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri uwaangalie watendaji wake kuna hujuma inayofanyika. Haiwezekani korosho za Nanyumbu zikawa na bei ndogo kuliko korosho za Masasi. Wakati tulikuwa wilaya moja bei ilikuwa sawa, leo tunagawanywa, unasema kwamba bei tofauti. Hili jambo halikubaliki. Kwa hiyo, kuna hujuma inayofanyika na haitakubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Wizara, pamoja na mazuri yote wanayoyafanya, naomba muwaangalie watendaji wenu wa chini. Wenzangu wamezungumza kuhusu Bodi ya Korosho, mtendaji amepewa mamlaka makubwa sana kwa sababu hana mtu anayemdhibiti. Naomba huyu mtu aangaliwe kwa macho mawili. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Yahya.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, mwisho naishukuru sana Wizara naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Yahya Mhata, Mbunge wa Nanyumbu. Mheshimiwa Jonas Mbunda, ajiandae Mheshimiwa Janejelly.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Kilimo. Kwanza kabisa, naomba nimpongeze Waziri wa Wizara ya Kilimo, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa jinsi walivyoanza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili naomba niwapongeze kwa sababu wameleta mikakati mizuri ambayo itatusaidia kutukwamua kwenye suala hili la kilimo. Pamoja na mikakati

mizuri ambayo imetolewa na Wizara, lakini bado kuna changamoto ambazo zinatakiwa zitatuliwe ili tuweze kufikia malengo na kilimo chetu kiweze kuchangia kwenye Pato la Taifa kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitajielekeza sana kwenye upande wa utafiti. Changamoto kubwa ambayo nimeiona upande wa kilimo ni suala la utafiti. Changamoto nyingi ambazo zimetokana na suala la kilimo zinatokana na kukosa utafiti.

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza, mimi natoka Mbinga kule Milimani ni wakulima wa kahawa na takriban sasa miaka 80 kilimo cha kahawa kinaendeshwa katika milima ile ya Umatengo. Changamoto iliyopo ni kwamba udongo ule umechoka. Kwa hiyo, tunaomba tafiti ya kupima udongo ili wakulima wale sasa waweze kupata ushauri mzuri utakaowasaidia kuongeza uzalishaji katika mashamba yale yale ambayo wanatakiwa waendeleo kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utafiti unahitajika pia kwenye suala la pembejeo. Kama nilivyoeleza hapo mwanzo kwamba udongo ule umechoka na uzalishaji katika udongo ule bado ni tatizo na wakulima wale hawawezi kuhama katika maeneo yao ya asili. Kwa hiyo, leo usipopima udongo na ukajua wakulima wale wanatakiwa watumie pembejeo za aina gani ina maana wakulima watanunua pembejeo kwa kubahatisha, kitu ambacho hakitaleta tija kwenye uzalishaji wa kahawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la miche na mbegu upande wa mahindi. Unakuta kwamba kuna vituo vya utafiti havipewi nguvu za kuzalisha miche ya kutosha lakini kwenye suala la mbegu kuna kampuni nyingi sana zinazalisha mbegu lakini mkulima huyu hapewi maelekezo kwamba ni mbegu zipi sasa anatakiwa atumie ili aweze kupata mavuno mengi katika mazao yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Serikali iongeze nguvu kwenye utafiti na kama utafiti huo unafanyika,

unafanyika kwa manufaa ya nani? Kama huyu mkulima hajapata matokeo na ushauri kutoka kwenye utafiti huo, huo utafiti ambao unaendelea unafanyika kwa manufaa ya nani? Kwa hiyo, niombe Serikali ihakikishe kwamba matokeo ya utafiti na ushauri yawafikie wakulima ili waweze kuzalisha kwa tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaongelea suala la wakulima ambao wako kule vijijini lakini wanahitaji msaada wa wataalam. Kama nilivyosema mwanzo kwamba utafiti kama umekamilika wale wataalam wanatakiwa wapeleke matokeo ya utafiti kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa waziri ametuambia kwamba wataalam waliopo ni takriban 7,000 lakini ukiangalia upande wa pili unakuta wataalam wale hawana vitendea kazi, sasa watafikaje kwa wakulima na kuwapa maelekezo kwenye masuala yanayohusu kilimo? Utakuta wataalam hawa hawana pikipiki, magari na hawawezeshwi mafuta ya kufika vijijini. Ni namna gani sasa hawa wakulima wetu ambao wako vijijini watapata utalam ili waweze kuzalisha na waweze kuleta tija katika uzalishaji wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nilitaka nilielekeze kwenye suala la kilimo kama walivyosema wenzangu ni miundombinu. Miundombinu yetu ni shida kwenye suala la barabara, hata kama utafiti na mambo mengine yatafanyika, lakini bado tutapata kikwazo kwenye suala la namna gani wataalam wanafika kule vijijini kwa wakulima na ni namna gani wakulima wanatoa mazao kutoka vijijini kwenye zile *feeder roads* ambazo ziko katika hali mbaya kupeleka sokoni. Kwa hiyo, hilo bado ni tatizo kwenye upande wa kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine naomba niishauri Wizara iache utaratibu wa kubadilisha sera mara kwa mara. Sera zinavyobadilika Bodi za Mazao pamoja na vyama vya ushirika vinashindwa kusimamia mazao kwa sababu hakuna sera endelevu. Kunakuwa na tatizo kwamba sera imetolewa leo baada ya miezi sita maelekezo mengine yanatolewa.

Kwa hiyo, kwenye mpango mkakati wa muda mrefu ni vigumu kuutekeleza kwa sababu kunakuwa na mabadiliko ya maelekezo ya kiutendaji mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni masoko. Suala la soko ni tatizo kwenye mazao, kwetu ni zao la kahawa na mahindi. Kwenye zao la kahawa niipongeze Serikali imeanzisha ile minada ya kanda, lakini mpaka mkulima anapeleka mazao yake sokoni hajui gharama za uzalishaji wala hajui atauza kwa bei gani na hajui kama akiuza kwa bei ile italipa gharama zile za uendeshaji. Kwa hiyo, unaona kabisa kwamba zile tafiti kama zingekuwa zinafanyika zingekuwa zina uwezo wa kumuelekeza mkulima ili ajue zile gharama anazotumia baada ya kuuza mazao yake fedha zake zilizotumika zinarudi na mkulima huyu anakuwa amezalisha mazao haya kwa faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa mahindi kuna tatizo kubwa sana nalo linalotokana na soko kwamba wakulima wale wanalima kwa gharama kubwa na ni wakulima wadogo wadogo wanalima kwa jembe la mkono, lakini bado wanapata tatizo la soko kwenye upande wa mahindi.

Mheshimiwa Spika, kama mwaka 2020 wakulima wetu wa Mkoa wa Ruvuma, Wilaya ya Mbinga na Songea Vijijini, kwa dada yangu Mheshimiwa Jenista wametapeliwa mahindi yao ambayo ni ya thamani kubwa na mpaka sasa hivi hawajui hizo fedha zitalipwa kwa namna gani? Hawajalipwa, Serikali ipo, inaona, lakini mpaka leo wakulima wamekopa kwenye benki na...

**SPIKA:** Wametapeliwa na nani?

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Spika, wametapeliwa na mfanyabiashara mmoja anaitwa Njau na mpaka leo hawajui ni namna gani hela zao zitapatikana. Kwa hiyo, naomba wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha

hapa atamke Kauli ya Serikali kwamba inasema nini kuhusiana na hawa wakulima ambao wamepoteza mazao yao.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jonas Mbunda, kutoka kule Mbinga tunakushukuru sana. Mheshimiwa Jenejelly, atafuatiwa na Mheshimiwa Kasalali Mageni.

**MHE. JENEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yake kwa kazi nzuri mnayoifanya kuendeleza kilimo.

Mheshimiwa Spika, nijikite kwenye *block farm* katika mazao ya kimkakati. Tunajua wana mazao ya kimkakati kila mkoa. Mathalani zao la kimkakati la Dodoma tunajua ni zabibu na alizeti, lakini kama tungetafuta *block farm*, tukawagawia wakulima, tukaweka miundombinu mizuri pale, itawasaidia sana hawa wakulima kuweza kuwakopesha hata mikopo ya kuendeleza kilimo na kuwapa wataalamu wa kuwasaidia katika kilimo kile. Kwa sababu watakuwa wako pamoja, wanahudumiwa kwa pamoja na wanaweza tukazalisha vya kutosha kwa kutumia *block farm*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizo *block farm* zitatusaidia kupata masoko kwa sababu, patakuwa panafikika kwa wale wateja wanaohitaji kununua mazao yetu. Tuna imani tutakuwa tumeweka miundombinu ya kutosha ya barabara, tutakuwa tumeweka wataalamu wa kuweza kuwasaidia watu kwenye kuuza mazao, tutakuwa tumepafanya mahali ambapo ni pa soko la kuweza kuuza mazao yetu haya.

Kama hatukufanya hivyo, kwa kweli tutakaa kwenye kilimo cha ndoto ndani ya Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, juzi wakati unasainiwa Mkataba wa Mafuta, Kiongozi Mkuu wa Nchi ametuambia, Tanzania tukitaka kuendelea tuwekeze kwenye kilimo cha biashara, kwenye nishati na kwenye miundombinu. Sasa ifike wakati basi, tuone hizi *block farms* ndiyo za kututoa mahali tulipo. Hii ya kumfuata mkulima mmoja mmoja, tutachelewa kwa sababu, kwanza wataalamu wa kutosha hatuna, miundombinu kuwafuata wakulima huko waliko, ni ngumu zaidi na uwekezaji wake utakuwa mkubwa zaidi, lakini tukiwaweka pamoja, tukawahudumia kwa pamoja tunaweza tukatoka hata kwenye sakata hili la ukosefu wa mafuta, ukosefu wa masoko na wakulima wetu wakapata thamani ya kile wanachokilima.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jenejelly, mnaposema *block farm* mnamaanisha nini?

**MHE. JENEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika, ninaposema *block farm* naamisha hivi, kwa mfano Dodoma kuna ardhi ya kutosha, kwa hiyo, Serikali iende pale impimie kila mkulima. Kwa mfano, kama ilivyo Singida, katika zao la korosho wamepimiwa na kila mkulima ana sehemu yake, ana eka zake za kulima, lakini wote wako kwenye sehemu moja ambayo ni rahisi wataalamu kuifikia, ni rahisi kupata pembejeo, ni rahisi kutengeneza miundombinu ya pale na ni rahisi kutafuta soko la mahali pale kwa sababu wako sehemu moja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ndiyo ilikuwa maana yangu. Hilo ndilo litakalotutoa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tukienda kwenye kilimo cha umwagiliaji, nacho tuangalie ambapo tumeweka miundombinu ya umwagiliaji na hawa wakulima nao ziwe ni *block farm*, wawekwe kwa pamoja. Tumeona hapa Tume ya Umwagiliaji tunaambiwa imefikia wakulima 714, bado tuko mbali sana; kwa nchi nzima kufikia wakulima 714 wakati

tunasema asilimia 70 ya Watanzania ni wakulima, bado tuko mbali sana. Najua Waziri na Naibu wake na timu yake mnajitahidi sana, lakini tuendeleo kujitahidi.

Mheshimiwa Spika, haya yote yatafanyika wakipelekewa bajeti yao ya maendeleo kama tunavyoipitisha leo. Wanajitahidi sana, lakini wanakwama kwa rasilimali fedha, hatujawa *serious* kwenye kilimo kama tulivyokuwa kwenye miundombinu ya barabara. Ukiangalia bajeti ya miundombinu huwa inapelekwa asilimia 80 mpaka 70, lakini ukienda kwenye kilimo, tumeona wanapelekwa asilimia 18, 19, 20 au 26; hawawezi kufanya chochote. Kila siku tutamlaumu Waziri wa Kilimo, Naibu wake na wataalamu wake, lakini hatujawawezesha kwenye rasilimali fedha tukaweza kufanya kilimo kiweze kuwa uti wa mgongo kama kweli tunavyosema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo ulikuwa mchango wangu. Tukijikita kwenye hilo tutakwenda vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nilikuwa najjuliza kama kuna *direct correlation* kati ya kuwa na bajeti kubwa ya Wizara ya Kilimo na mkulima mmoja mmoja kule Kongwa. Najua ipo, lakini kwa kiasi gani ukiiipa Wizara ya Kilimo hela nyingi, mkulima yule wa Kongwa atafaidika kama siyo kununua *VX*, pikipiki, *computer* na vitu vya namna hiyo ambavyo... (*Kicheko*)

Mheshimiwa Kasalali Mageni, atafuatiwa na Mheshimiwa Deogratius Mwanyika.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Pia nitumie nafasi hii kuwapongeza viongozi wa Wizara ya Kilimo, Waziri na Naibu; na mahususi kabisa nampongeza na kumshukuru Naibu Waziri wa Kilimo, kaka yangu Mheshimiwa Hussein Bashe. Wakati sisi watu wa Sumve na Kwimba tulipokuwa tuna kilio chetu cha kupangiwa namna ya kuuza choroko, zao ambalo tulikuwa

tunalilima bila usaidizi wa Serikali kwa asilimia 100, alilia pamoja na sisi. Namshukuru kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kusema kwamba, sisi watu wa Sumve bado tunacho kilio chetu kikubwa katika Wizara hii ya Kilimo. Shida yetu kubwa...

**SPIKA:** Kwa hiyo, Mheshimiwa Kasalali Serikali iliingia hata kwenye choroko?

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, iliingia.

**SPIKA:** Umesikia hayo maneno! *(Kicheko)*

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, ni jambo la aibu kulisema hapa kwenye Bunge Tukufu namna hii kwa sababu, sisi Wasukuma tunalima choroko. Kwetu choroko ni kama benki. Yaani familia ambayo haina choroko ni familia ambayo haiheshimiki. Yaani tunamaanisha kwamba choroko ni kama benki zetu kwa sababu hatuko karibu na mabenki, sisi bado kule ni washamba, ni vijijini. Sasa mtoto anapougua, mimi nachukua kilo moja ya choroko naenda kwa mtu ambaye anajulikana kwamba huwa ananunua, ninampa napata pesa, naenda kununua dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali bila aibu, wakaweka choroko kwenye Stakabadhi Ghalani.

**SPIKA:** Aah, kwa hiyo, ni kangomba.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, mwaka 2020 watu wa Sumve wameteseka. Ninasema Mheshimiwa Bashe tumelianaye kwa sababu nimehangaikanaye kwenye kiti chake pale nikijitahidi kujieleza. Nimeeleza, lakini naye akichukua hatua, kuna mtu anaitwa mrajisi, sijui hawa watu wanatoka wapi? Nikafikiri labda mrajisi huyu inawezekana amezaliwa India au Denmark. Kama angekuwa amezaliwa kwetu, angeshangaa kama ulivyoshangaa wewe kuona choroko inaingizwa kwenye Stakabadhi Ghalani. *(Makofi)*



Mheshimiwa Spika, wakulima wamenyanyasika, wanalazimishwa wapeleke hizo kilo moja moja...

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam.

### TAARIFA

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, namwambia tu mzungumzaji kwamba choroko ili uipeleke katika Stakabadahi Ghalani, mtu analima eka moja anapata debe moja. Ili kujaa tani 10 mpaka uwe na wakulima 1,000. Sasa hii ni hatari sana na hao walioko kule au wale *AMCOS* na wenyewe ni majambazi hawana hata mtaji wa 2,000/=.  
(*Makofi*)

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, taarifa hii ya heshima kutoka kwa Mheshimiwa Tabasam naipokea. Nasisitiza kwamba mimi nilikuwa natamani kumwona Mrajisi. Wakati unatambulisha wageni wa Wizara ya Kilimo, nilikuwa nime-*concentrate*, lakini inaonekana ulimjumuisha kwenye Maafisa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hawa watu wanafikiria kama wako nje ya nchi. Aling'ang'ana, Mheshimiwa Naibu Waziri anatoa maelekezo mpaka akaandika barua, hawataki kuifuata. Tunalazimishwa; mwaka 2020 watu wa Sumve wamepata hasara ya mamilioni ya pesa. Kuna watu wamekamatwa, wamelipishwa *fine* zisizoelezeka.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo nitawaunga mkono bajeti yao tu endapo watakuja na maelezo ya kutosha ya kurudisha pesa zilizoibiwa kwa kutumia mgongo wa Serikali kwa wakulima wa choroko kwenye Jimbo la Sumve. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna kitu kinaitwa sijui *TMX*, sijui wanaita kitu gani. Mtu anakuja anaambiwa, kwamba sasa

mwishoni waliposumbua sana; na ninamshukuru sana Mkuu wa Mkoa wa sasa wa Dodoma alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, kidogo alifanya ubunifu ambao ulirahisisha hili tatizo ingawaje lilibaki kuwa tatizo, lakini alilirahisisha akasema, sasa kwa sababu mnawalazimisha wakulima wote wakusanye mazao yao wakakopwe, yeye akasema wanunuzi nunueni, mkishanunua, basi hiyo sijui malipo yao ya *TMX* na nini na nini wachukue Serikali. Yaani wale Ushirika, zile *AMCOS* zilikuwa zinachukua pesa ambayo hazijaifanyia kazi. Huu ni ujambazi kama ujambazi mwingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hawa watu wanatakiwa warudishe hela. Mheshimiwa Waziri tunataka hela za watu wa Sumve...

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere nimekuona, taarifa.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Wakati naendelea kumpa Taarifa mzungumzaji anayezungumza saa hizi, nikuombe hiyo sura uliyoingianayo asubuhi, uendeleo kuwanayo hivyo hivyo. Mungu akusaidie hivyo hivyo; ya kukemea mambo ambayo yanaenda ovyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *AMCOS* katika nchi yetu, mimi sielewi. Mama mmoja ana miaka karibu 75 alinihoji siku moja. Wewe ni Mbunge wa nini? Kama mnakuwepo Bungeni miaka yote, sisi wakulima wa pamba kuna kitu kinaitwa *AMCOS*, hawana hela, wanachukua hela ya pamba ya mkulima wanakula; wanachukua ushuru wanakula; hawana hela ya kununua pamba. Ananiuliza ninyi ni Wabunge wa nini? Mbona mnazungumza mambo hayaishi?

Mheshimiwa Spika, ndiyo anayozungumza mzungumzaji hapa.

**SPIKA:** Taarifa hiyo Mheshimiwa Kasalali.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, naipokea na ninasisitiza, Mheshimiwa Waziri mimi sitaunga mkono hii bajeti, urudishe pesa. Hawa watu wanaitwa *TMX* na nani waliokuwa wanachukua pesa kwa wakulima wa Sumve bila kufanya chochote na kuwasababishia matatizo kwenye uuzaji wa choroko, pesa zirudi. Halafu pili, hiki kitu kinaitwa ushirika kwenye choroko kisije kikajirudia tena. Hatuwezi kuendelea namna hii, mnaleta vitu ambavyo havipo katika hali ya kawaida na bado sasa hivi tunavuna dengi, nasikia mna mpango huo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi watu wa Sumve huo mpango hatuutaki. Tunataka tuuze tunavyotaka kwa sababu wakati wa kulima hamtuletei chochote. Tunaanza kulima wenyewe, tunahangaika; sijawahi kuona Afisa Ugani anashauri kuhusu choroko. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Yaani Mheshimiwa Kasalali Serikali ina mpango wa kuingia kwenye dengi pia! *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, wapo wamejipanga. Hawa watu wakati mwingine tuwe tunaona hata aibu, kwa sababu sisi ni viongozi na hawa wataalamu walioko huko, wanatushauri ovyo. Kwa sababu, hamwezi kushauri Serikali iweke Stakabadhi Ghalani choroko, kama kweli nyie ni watafiti. Kwa sababu, kuna wengine ni maprofesa, madokta, hizo elimu za *Ph.D* ni utafiti, sasa mnaingiaje kwenye jambo bila kulifanyia utafiti? Kwa sababu, wangepanya utafiti wasingetuletea hili tatizo. Sasa hivi wakulima wamefilisiwa, watu kule Sumve kwa kweli uchumi wetu umeyumba hapa katikati kwa sababu ya haya mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nimalizie kwa suala la pamba. Mheshimiwa Waziri Bodi ya Pamba sisi wakulima wa pamba hatuutaki. Wewe ndio unaitaka. Sasa itaanza kushughulika na pamba ya Wizarani. Kwa sababu, hii bodi imeshindwa kabisa kuwasaidia wakulima wa pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamba imeshuka, bado tuna bodi na bado tuna wataalamu. Sasa hawa wataalamu ni wa nini? Tunaendelea kuwanao wa nini? Kwa sababu, hamji na mbinu za kumsaidia mkulima wa pamba apende kulima pamba. Wakulima wa pamba wakiniuliza jimboni kwangu nawaambia waache, kwa sababu, mwisho wa siku zinaniletea matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna wakulima kwenye AMCOS kama za Kiminza, Lyoma, nakumbuka nikiwa Diwani, mpaka leo wanadai kuna hela; mpaka kuna wahasibu wamejinyonga. Sasa mnaendelea kuwa na Bodi ya Pamba ya nini? Hata hizi AMCOS, ni za nini? *(Makofi)*

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nafikiri kesho tutazungumza vizuri kama nitaunga mkono hoja au la, lakini haya mambo lazima yabadilishwe. Sisi watu wa Sumve kwa kweli hamjatutendea haki. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Kasalali Mageni, Mbunge wa Sumve nakushukuru sana kwa mchango wako. *(Makofi)*

Tunaendelea na Njombe Mjini sasa. Mheshimiwa Deogratus Mwanyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Deus Sangu.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hoja iliyopo Mezani. Nianze kwanza kwa kuunga mkono hoja, lakini niseme sekta hii ya kilimo ndiyo inabeba maisha ya Watanzania walio wengi. Kwa hiyo, ningetegemea labda wangukuwa na bajeti kubwa ya kutosha, lakini matarajio hayo na bajeti iliyopangwa ni sidhani kama itakidhi matarajio ya wengi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nianze kwa kusema bado nampongeza Waziri na Naibu Waziri na Watendaji kwa juhudi zao mpaka muda huu. Kwenye bajeti hii nilichokiona pamoja na kwamba hakuna pesa za kutosha, lakini wamejaribu kuweka maeneo ya mikakati ambayo yanakwenda kushughulikia baadhi ya matatizo.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema, itategemeana sana kama hata hiyo pesa ndogo iliyotengwa kama itapatikana. Kama isipopatikana tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu na sidhani kama kuna mafanikio yoyote ambayo yatapatikana kulinganisha na matarajio.

Mheshimiwa Spika, napenda niongelee mazao mawili ambayo ndiyo yapo katika Jimbo letu la Njombe Mjini, lakini yapo katika Ukanda mzima wa Nyanda za Juu Kusini. Tukianza na chai, wachache wameliongelea humu ndani, lakini ni zao ambalo tuna uhakika na tunaelewa kwamba kwa sasa hivi ni zao ambalo katika soko la dunia bei imetikisika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, nchi yetu uzalishaji wa chai umeshuka chini kwa maana ya majani mabichi ya chai, lakini napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Waziri, walikuja Njombe tarehe 10 mwezi wa Tatu, wakakaa na wadau wa chai, tukawaeleza matatizo yote ya chai, kwa hiyo, tukayajenga tukaweka mikakati.

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa ambalo wanalielewa ni kuhusiana na umwagiliaji. Tunahitaji tija kwenye zao la chai, tunahitaji kuwa na bajeti ya kutosha ya umwagiliaji. Nimeona katika bajeti ya leo kwamba umwagiliaji umepewa pesa kidogo. Nina matumaini makubwa kwa sababu Mheshimiwa Waziri alikuja Njombe, akayasikia mwenyewe. Katika pesa hizo atahakikisha kwamba wakulima wa chai wa eneo hilo wanaangaliwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ni la muhimu...

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa.

**MHE. JUSTINE L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nataka nimtaarifu msemaji kwamba, wakati wanahangaika na umwagiliaji pale Kilolo kuna eka zaidi ya 300 za chai. kwa miaka 30 ile michai sasa inachomwa mkaa; na hata hiyo ambayo mvua inanyesha yenyewe, bado haljafanywa kitu chochote na hakuna kiwanda na majani hayachumwi.

Mheshimiwa Spika, nampa taarifa hiyo ili aweze kujenga hoja vizuri. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa yake, nami nilikuwa naenda huko. Najua wanakwenda kuongeza uzalishaji wa chai, lakini nilisema kwamba waanze na maeneo ambayo tayari chai ilishalimwa na imeachwa porini na mojawapo ni hilo la Kilolo. Ndiyo maana naongelea Nyanda za Juu Kusini na chai.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kubwa ni miundombinu wezeshi katika zao la chai. Ni ukweli usiopingika kwamba kama hatuta-*address* tatizo la miundombinu wezeshi kwenye zao la chai hatutapata mafanikio wala hatutapata yale malengo yetu ya kuongeza uzalishaji wa chai kutoka tani 37,000 kwenda kule ambako wanataka, hatutafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni ambalo limeongelewa sana hapa, la ugani, ni jambo la muhimu sana. Naelewa kwenye chai kwenye eneo la Njombe kuna Kampuni ya *NOOSC* ambayo imeleta ushirikiano mkubwa na imesaidia, lakini kuna maeneo mengi bado tunahitaji Maafisa Ugani.

Mheshimiwa Spika, naelewa umeliongelea hapa ukielezea kwamba Serikali haiwezi kuajiri. Ni kweli haiwezi

kuajiri Maafisa Ugani wa kutosha, lakini kuna wakulima wadogo wadogo wa chai ambao wanahitaji msaada mkubwa wa Maafisa Ugani. Kwa hiyo niombe waendeleo kuliangalia na nimeona kwamba bajeti yao imeongezwa.

Mheshimiwa Spika, soko ni tatizo kubwa sana, Njombe na zao la chai soko letu sisi ni viwanda, kiwanda kikifanya kazi maana yake tuna soko. Kinachojitokeza, Njombe tuna viwanda vinne vya chai, tuna uhakika wa hilo soko, lakini kwa bahati mbaya, katika waendeshaji wa viwanda vya chai katika Mkoa wa Njombe na maeneo yote ya Njombe ni mwekezaji mmoja tu ya *Unilever* ambaye yeye anaendesha kwa ufanisi na anaweza kulipa wakulima. Waendeshaji wengine wa viwanda vya chai ni jambo la kusikitisha sana kwamba wameshindwa kabisa kuwalipa wakulima wa chai. Naelewa jambo hili Waziri Mkuu alilingilia, Mkuu wa Mkoa amelilingilia, Waziri amelisikia, lakini bado tatizo bado linaendelea. Tunaomba sana Serikali ioneshe kwamba ni Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kiwanda kilichobaki kimoja ambacho kinafanya kazi kina tatizo bado la kupata majani ya chai ya kutosha. Kuna uwezekano kama tatizo hili halitakuwa-*addressed*, kwa sababu mfumo wa kile kiwanda ilikuwa ni kupata majani ya chai kutoka kwa wakulima wadogo wadogo, majani ya chai hayatoshi. Ni kweli kwamba maeneo mengine yanayozalisha majani ya chai yanaweza yaka-*supply* kiwanda kile, lakini kwa sababu ya mikataba ambayo imeingwiwa, wakulima wale wanatakiwa wapeleke chai kwenye kiwanda au viwanda vya yule mtu ambaye hawezi kulipa ambaye ni Mkenya wa Kampuni inaitwa *DL Group*.

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo ambalo Wananjombe hatulikubali kwa sababu kama wananchi wanaweza wakapeleka majani kwenye Kiwanda cha *Unilever* ambacho kinalipa kwa nini wazuiwe. Kwa hiyo, naiomba Bodi ya Chai ifanye kazi yake, lakini namwomba vile vile Mheshimiwa Waziri naye aingilie...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Deodatus Mwanyika.

**DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deus Sangu atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Sitta.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu niliotumwa na wananchi wa Jimbo la Kwela na Mkoa wa Rukwa kwa ujumla, kuhusu sekta hii muhimu ambayo inagusa maisha ya wananchi wa Mkoa wa Rukwa. Sitakuwa nimewatendea haki wananchi wa Jimbo la Kwela na Mkoa wa Rukwa kwa ujumla kama sitaongelea hali halisi ya zao la mahindi ndani ya mkoa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kaskazini Mheshimiwa Aida amesema hapa na naomba nisisitize kwa umuhimu wake, leo hii inaonekana Mkoa wa Rukwa tumekuwa kama kichwa cha mwendawazimu. Mwaka jana nilipata masikitiko makubwa katika hotuba yake alivyokuwa anahutubia Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI wakati huo Mheshimiwa Jafo, akawa anasema kati ya mikoa ambayo yamechangia na kupata mapato ghafi kidogo sana na ya mwisho katika mikoa yote Tanzania ulikuwa Mkoa wa Rukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa iliyopelekea tukae mkiani, sio kwasababu sisi hatufanyi shughuli, ni wavivu, hatulimi wala hatujielewi, hapana, wananchi wa Mkoa wa Rukwa wanajituma sana, tunalima na sisi ndio katika *top two* katika kilimo cha mahindi nchi hii, Mkoa wa Rukwa ni mmojawapo. Nimekuwa nikifuatilia sana mijadala hapa Bungeni, mwezi Februari nilisimama katika Bunge hili Tukufu, nikaongelea suala la zao la mahindi, lakini pia kuna



Wabunge mbalimbali akiwepo Balozi Dkt. Pindi Chana aliuliza swali katika Wizara hii, lakini majibu ya Naibu Waziri yalikuwa ya kukatisha tamaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakumbuka wakati huo katika Bunge la Kumi na Moja mtu ambaye nilikuwa ninam-*rank* kama *the best of Rukwa Region* alikuwa ni Mheshimiwa Naibu Waziri Bashe, alikuwa ni *front liner* na *champion* mkubwa wa kupigania zao la mahindi, alikuwa anatoa takwimu *unit cost* ya *production per* heka na mauzo anayouza mkulima kwa heka moja. Alikuwa anasema *gross loss* ilikuwa ni Sh.150,000 kwa mkulima kila msimu. Bahati mbaya wakati huu hiyo *gross loss* anayopata Mkulima kwa heka moja imeenda mpaka Sh.300,000 yaani unapofika wakati wa mavuno, akijumlisha gharama zake za uzalishaji mkulima wa Mkoa wa Rukwa anapata hasara ya Sh.300,000, hapo hajatunza mazao, afanye *hedging* asubiri bei itakapopanda, hivi ninavyoongea Sh.18,000 gunia moja, heka moja Sh.700,000...

**SPIKA:** Mheshimiwa Deus Sangu mimi shahidi yako, nilikuwa nikikaa hapa Mheshimiwa Bashe yupo pale nyuma anashuka jinsi wakulima wa mahindi ambavyo hawatendewi sawasawa kwa hesabu kwa takwimu, sasa leo yupo wapi? (*Makofi*)

**MHE. DEUS C. SANGU:** Yuko hapa.

**SPIKA:** Haya endelea kuchangia Mheshimiwa.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniunga mkono. Kwa hiyo Mheshimiwa Bashe ni msalaba wake huu, *is your baby*, naomba leo wakiwa wa Waziri hapa Profesa waje watuambie wananchi wa Mkoa wa Rukwa na Nyanda za Juu Kusini, wanawapa habari njema. Habari ya kusema kwamba mipaka ipo wazi, hiyo sio stori *brother*, lazima waanzishe *marketing intelligent system* waende kwenye nchi hizo ambao wanadhani ni masoko, mpaka unaweza ukawa wazi, lakini sio wazi kwa Tanzania

pekee, Zambia wanaangalia hiyo mipaka iliyo wazi; Kenya wanaangalia mipaka iliyo wazi; *DRC* wanaangalia mipaka iliyo wazi na Burundi hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa wakikaa kwenye madawati huko Wizarani wanasubiria tu kwamba mipaka iko wazi *you will wait until the next coming of Jesus Christ*. Kwa hiyo namwomba sana Mheshimiwa Waziri kwa Mkoa wetu wa Rukwa, leo hii halmashauri zetu zime-*paralyze*, hazina mapato, sisi hatuna migodi ya dhahabu, hatuna jambo lolote tunalotegemea zaidi ya zao la mahindi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya hadi mpunga sasa umeshuka bei. Mwaka jana hali ilikuwa ngumu. Halmashauri zetu zote katika Mkoa wa Rukwa zimeshindwa kukusanya mapato. Tumeshindwa kujenga madarasa, tumeshindwa kujenga zahanati, tumeshindwa kuboresha vituo vyetu vya afya, maisha ni magumu watuonee huruma wananchi wa Mkoa wa Rukwa, tumechoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna *solution* zinatolewa kwamba *substitute*, twende tupeleka mikorosho na wakituletea mikorosho *its good initiative*, lakini haitoshi, wakileta mikorosho ina maana tuache kulima mahindi. Tukiacha mahindi maana yake nchi itaenda kwenye baa la njaa, baadaye wataanza kuhangaika kutafuta mahindi sehemu nyingine. Kwa hiyo, hatutaki korosho iwe ni *replacement* ya mahindi, tunataka iwe ni *alternative* tu, anayetaka ku-*jump* kwenye korosho ataenda, anayetaka ku-*jump* kwenye mazao mengine ya kimkakati ataenda, lakini hatutaki mahindi yawe *replaced*, tunataka mahindi yabaki kuwa pale pale, kwa sababu wakati wa njaa sisi ndio mkombozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi ikiingia kwenye matatizo ya njaa, Wizarani inakimbilia Rukwa, sasa hivi mazao tumefanya *over production* wanaanza kutukimbia wanatukwepa na sababu ndogo ndogo. Nilienda *front line*, tukaenda mpaka wa Waziri Mkuu tukamwambia huu ni mwezi Februari Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaomba na akaja kusema ndani

ya Bunge hili Tukufu kwamba tayari tutaunda timu itakayoenda huko Kongo na Burundi ili ku-secure hayo masoko.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa na dhamira njema na safi, lakini naona watendaji wake hawaendi na sauti ile, ilitakiwa tamko la Waziri Mkuu hapa liwaamshe, waje tukae Wabunge wa Mkoa wa Rukwa na *management* ya Mkoa wa Rukwa, twende huko, baadaye tutakuta yale masoko yameenda, hatuna soko la mahindi, *confidence* ya wakulima imepotea, wamekata tamaa.

Mheshimiwa Spika, nawaheshimiwa sana Mheshimiwa Bashe na Mheshimiwa Waziri, sitaki kesho niendeshe mgomo wa Wabunge wa Nyanda za Juu Kusini, tuwawekee mgomo wa Bajeti yao mpaka waje na kauli thabiti, kauli ambayo sasa tukirudi mwezi Julai kwenye ziara kwa wananchi, tuwe tunawaambia jambo linaloeleweka sio *stories*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, naomba tu niseme hayo kwa uchache, ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge mbona mnanitisha kuhusu kesho itabidi nitafute Mwenyekiti wa Bunge aje akae hapa au Naibu Spika, naona kesho inaweza ikawa moto hapa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Margaret Sitta, atafuatiwa na Mheshimiwa Sillo Baran.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja iliyopo mezani. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, lakini pia nawashukuru sana wananchi wa Urambo na familia yangu kwa jinsi ambavyo tunashirikiana nao. Nawaomba tuendeleo kushirikiana kwa lengo la kuendeleza Wilaya yetu.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali inayoongozwa na Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo wanachapa kazi kwa kuzingatia yaliyopo ndani ya Ilani ya Uchaguzi. Hongera sana kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii pikumpongeza Mheshimiwa Waziri, Profesa Mkenda pamoja na Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara hii na naamini wanasikiliza yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wameongea ili kesho tupate mrejesho mzuri. Ninapoongea kwa niaba ya wananchi wa Urambo siwezi kuacha kutaja tumbaku, tumbaku hoyee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumbaku ndio uhai wetu sisi kwa sababu ndio zao ambalo linatuingizia fedha na miaka ya nyuma wakati wa mauzo kama huu uliopo sasa hivi, mitaani kote watu wangekuwa wanafurahia kwa sababu tumbaku ilikuwa inauzwa tani kwa tani kadri ambavyo mkulima alivyokuwa akilima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwapongeza wenzangu wote waliotangulia kwa kusema kwamba changamoto kubwa ya Wizara ya Kilimo ni masoko, masoko ndio ambayo yanaamua mkulima alime kiasi gani na kumpa ari pia. Tumbaku bado ina changamoto kubwa sana. Kwa sasa hivi bei ambayo ingeweza kutolewa kama tungekuwa na wanunuzi wengi ingekuwa dola 1.63 lakini mpaka sasa hivi ni *JTI* tu ambao wamefikisha angalau dola moja 1.54, wakifuatiwa na wenzao ambao ni akina *Alliance* na wengineo ambao wananutua kwa dola 1.45.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo suala la soko ni la muhimu sana, tunaomba wanunuzi zaidi, tunaomba soko liwe la uhakika Zaidi. Sasa hivi tumbaku inauzwa lakini bado haijafikia *peak* ambayo tutasema kweli mkulima anapata haki yake na jasho lake alilotoa. Namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja mezani kuja ku-*wind up* yaani

anapokuwa anahitimisha atuambie kama changamoto kubwa ni soko iweje *TLTC* waondoke ambao ndio walikuwa wananunua tumbaku nyingi Mkoa wa Tabora. Kwa hiyo tunaomba atakapokuja kueleza hapa atuambie *TLTC* wapo, wameondoka na kama wameondoka kweli imeshindikana kukubaliana nao ili waendeleo kununua ili tupate wanunuzi wengi zaidi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia itakuwa ni vizuri kama Waziri atatuambia kwamba *TLTC* ndio waliokuwa wamenunua Kiwanda cha Tumbaku, *TLTC* ndio walikuwa wamechukua ma-*godown* yote, kama wanaondoka nini hatma ya ma-*godown* na kiwanda walichokuwa wanamiliki? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, ni suala la makisio, kutokana na kutokuwa na wanunuzi wengi, sasa hivi pamoja na kwamba mnasema Maafisa Ugani watembe, inasaidia nini Maafisa Ugani wakitembea, halafu baadaye unaambiwa wanunuzi wote wanataka kilo labda 1,000,000 tu, lakini tungekuwa na wanunuzi wengi wangenunua nyingi.

Mheshimiwa Spika, fikiria, sasa hivi mkulima anaambiwa wewe lima mwisho labda kilogram 100 au 200 tu, why? Sasa kuna haja gani ya kuhimiza watu walime, halafu baada ya pale wanakosa soko au wanapewa makisio madogo. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri atusaidie tunafanyaje ili wakulima walime tani yao kadri wanavyopenda kutokana na jinsi wanafundishwa kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ni la muhimu sana ni suala la mbolea. Wenzangu waliotangulia wameongea kwamba ni vizuri mbolea ikafika kwa wakati, Wazara wanajitahidi lakini bado wajitahidi zaidi ili mkulima anapoanza kuandaa shamba, sio anaanza kuuliza kwanza mbolea inakuja lini? Inabidi mbolea iwe tayari ipo nchini. Wazara imekuwa na utaratibu mzuri wanaleta katika *bulky* yaani nyingui, sawa, lakini kufika kwa wakati ili mkulima anapoandaa shamba lake mbolea iwe tayari imeshafika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo naona ni matatizo makubwa, Bodi ya Tumbaku inatusaidia kuwasiliana kuhusu bei, lakini haina vitendea kazi. Kwa hiyo tunaomba Bodi ya Tumbaku wawe na vitendea kazi. Kwa mfano, kama kwangu hata gari hawana, wakitaka kuzunguka mpaka waombe gari ya Mkurugenzi ni alibu. Kwa hiyo nadhani Bodi ya Tumbaku ipewe vitendea kazi na vingine vyote ambavyo wanajua wao hawana ili waendeleo kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, lingine, wametaja mikoa mitatu ambayo itafanyiwa utafiti wa mazao ya alizeti na kadhalika, wametaja Dodoma, Singida na Simiyu lakini wamesahau Mkoa wa Tabora, Mkoa wa Tabora ni jirani ya Singida, tupo sawasawa na wao na cha ajabu kuhusu pamba, Igunga ndio ina shamba la mbegu. Sasa mkoa ambao una shamba la mbegu wameuacha katika haya majaribio ya mikoa mitatu! Kwa hiyo naiomba sana Serikali itusaidie kuirudisha au kuiingiza Tabora katika mikoa ile mitatu ili iwe mikoa minne; kwanza kwa sababu ardhi ni sawasawa, na sisi alizeti inakubali na kama nilivyosema shamba la mbegu yaani utafiti kuhusu mbegu upo Igunga ambao ni Mkoa wa Tabora. Kwa hiyo tunaomba kwa heshima na taadhima Mkoa wa Tabora uwekwe katika mikoa ile ya majaribio.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Margaret Sitta.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sillo Baran, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Jumbe na Mheshimiwa Condester Sichalwe ajiandae.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ili niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu ya Kilimo, Wizara ambayo inachangia asilimia 27 ya pato la Taifa, asilimia 25 ya fedha za kigeni lakini inajiri Watanzania wasiopungua asilimia 65.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Serikali sasa ni Serikali ya viwanda na ni ukweli kwamba *raw materials* au malighafi zaidi ya asilimia 60 zinatoka kwenye kilimo. Kwa hiyo, niombe sana Serikali iwekeze kwenye kilimo, ikishawekeza kwenye kilimo maana yake tunapata viwanda vya kutosha, tukishapata viwanda tunaajiri Watanzania wengi, lakini pia Serikali inapata kodi. Ni ukweli usiopingika kwamba kilimo ni biashara ya chakula na ajira. Kwa hiyo niombe sana Wizara iwekeze kwenye kilimo ili tupate na wigo wa kodi pia katika Taifa letu, (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze kwa kifupi pia kuhusu wakulima wadogo hasa wa vijijini. Wakulima wa vijijini toka anaandaa shamba hadi anavuna hajawahi kutembelewa na Afisa Ugani hata mmoja. Hii ni changamoto kubwa sana kwa wakulima wa vijijini, watabaki kulima kilimo cha kujikimu, hawatapata kilimo cha tija. Kwa hiyo niombe sana Wizara iangalie sana wakulima wa vijijini, wanateseka kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, kuna mashamba yasiyoendelezwa; nchi yetu ina sera ya kubinafsisha mashamba kwa wawekezaji. Ni kweli kabisa tunawahitaji wawekezaji maana wakiwekeza watalipa kodi na wataajiri Watanzania, lakini kuna mashamba mengi katika maeneo mbalimbali nchini ambayo mtu amebinafsishiwa lakini anatomia labda robo tatu au robo tu ya eneo lote. Eneo lililobaki linabaki wazi wakati kuna wakulima wanaozunguka eneo hilo wanateseka hawana eneo la kulima. Naomba sana Wizara hii isaidiane na Wizara ya Ardhi, mashamba haya ambayo hayajaendelezwa Serikali iwagawie wananchi waweze kulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina mifano kule kwangu Babati Vijijini; kuna Bonde la Kiru, Kata za Kisangaji na Magara, kwenye msimu huu wa kilimo juzi watu walikatana mapanga kwenye Kijiji cha Magara, shamba lilikuwa na mwekezaji, mwekezaji haonekani, watu wamevamia. Kwa hiyo niombe sana Serikali itatue migogoro hiyo ili wananchi wapate maeneo ya kulima.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie masoko ya mazao. Wanachi wetu wanateseka sana na masoko ya mazao yao. Mfano mdogo tu wa kilimo kama cha mahindi, mbegu ya mahindi kilo mbili inauzwa Sh.13,000, lakini leo gunia linauzwa Sh.18,000 mpaka Sh.20,000 gunia la kilo 100. Niombe sana Wizara ya Kilimo iwasaidie Watanzania hawa wanyonge hasa wa vijijini, wanateseka mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Halmashauri yangu ya Babati Vijijini kuna wakulima wazuri sana wa mbaazi. Mwaka jana msimu uliopita mbaazi zilibaki shambani, hakuna pa kuuza kilo Sh.200, sijui Sh.300, mkulima ameteseka mwaka mzima, kwanza hajashauriwa na wataalam wa kilimo na pia masoko asipatiwe. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara ijielekeze kutafuta masoko ya mazao ya wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, kule kwangu kuna Vijiji vya Nar, Madunga, kuna wakulima wazuri sana wa vitunguu, lakini hawapati ushauri. Wanabaki kuhangaika na virobo heka vyao. Hii haiwasaidii, naomba sana Wizara iwasaidie wananchi hawa wa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kupanga ni kuchagua, niombe Wizara hii ya Kilimo ijielekeze kuchagua kuwekeza kwenye kilimo, nchi hii itatoka hapa itasonga mbele, wananchi watasogea mbele katika mapato yao na umaskini utapungua kwa wananchi wetu hasa wa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja. *(Makofi)*



**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sillo Baran. Mheshimiwa Ally Jumbe atafuatiwa na Mheshimiwa Condester.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni ume-*set standards* na sisi ni wanafunzi wako na hata tunapochangia tunajua tuko na mlinzi wetu ambaye ni wewe na sisi tutakulinda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sitachangia kwa hasira kama alivyofanya Mheshimiwa Mlugo na Mheshimiwa Tabasamu na wengine kwa sababu ninataka leo liwe ni fundisho tujifunze tusome tujue vizuri maeneo yetu tunakotoka.

Mheshimiwa Spika, nitaongelea mfumo wa pili aliosema mchangiaji wa kwanza Mheshimiwa Mhagama mfumo wa Stakabadhi Ghalani na nitahusianisha mfumo huu na zao lililoko Kyela zao la kokoa ambalo ni zao kati ya mazao muhimu yaliyowekwa katika mfumo wetu wa mazao saba Tanzania hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mfumo huu pia hata ulivyoingizwa Wilayani Kyela uliingizwa kwa ubabe hakuna aliyefanya utafiti hakuna aliyezungumza na mkulima kilichofanyika ni kwamba leo tunazungumza kesho makampuni yote yasinunue kokoa. Ilikuwa ni kitendo cha ukatili na kuna makampuni yalipoteza pesa zao. Ukiuliza wanakwambia Serikali imesema Serikali ni nani kama siyo sisi wananchi? Ndugu zangu hili lilifikia hatua ya kutuparang'anya wana Kyela tulifikia hatua ya kuanza kuichukia Serikali lakini ilikuwa ni kwa sababu ya watu wachache.

Mheshimiwa Spika, *cocoa* ni zao ambalo ni tofauti na mazao mengine yaliyoko Mtwara kama korosho ambayo yanalimwa kwa msimu. Kokoa inalimwa kwenye vivuli sisi Wanyakyusa zao la *cocoa* ni zao la heshima kuwepo nyumbani kwako. Zao lile hatulimi porini maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba huwezi ukachukua mfumo unaotumika kwenye zao la korosho ambalo ni la msimu

ukaja kwenye mfumo huo ukauleta kwenye *cocoa* ambayo inachumwa kila siku kwa msimu na kila mtu anaokota kidogo kidogo.

Mheshimiwa Spika, kilichotokea mfumo wa korosho ukahamishiwa kwenye mfumo wa *cocoa* matokeo yake ni kwamba wale wote waliokuwa wananunua *cocoa* makampuni yote yalipoteza pesa zao na hata walipokubali kilichofuata ni kwamba wale wote ambao walikuwa wananunua *cocoa* hizo walishindwa kuendelea na biashara kwasababu wengi pia walifikia kufilisika na kampuni mojawapo ni *Baoland* ambao mpaka sasa hivi hawanunui kokoa Kyela.

Mheshimiwa Spika, hili zao kwetu huwezi ukamfanya mtu asubiri kila mtu anachuma siyo zaidi ya kilo tano kwa wiki ukisema huyu mtu anayechuma kilo moja asubiri aziandae *cocoa* ndani ya siku tano kama kuna jua lakini apeleke mnadani akishapeleka mnadani anatakiwa kusubiri mwezi mzima ndipo apate pesa sasa wewe elfu 30 unaisubiri mwezi mzima kwa kweli haiingii akilini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa kinachotokea hawa watu wanashindwa kusubiri tumetengeneza tabaka la wanunuzi wa kati ambalo limejitengeneza *automatically* kwenye mfumo badala ya kununua kuuza hizo *cocoa* kwa shilingi elfu nne watu wanauza *cocoa* hizo kwa shilingi elfu tatu, na ni kwanini kwa sababu *cocoa* yao siyo *cocoa* kwa ajili ya kupata utajiri *cocoa* ya Kyela ni kwa ajili ya matumizi ya kila siku mtu anataka auze *cocoa* akamtibu mtoto, mtu anataka kuuza *cocoa* apeleke *school fees* kwa mtoto, anataka auze *cocoa* abadilishe mboga halafu auze *cocoa* angalau jioni akakae na wenzie anywe bia ndiyo kazi ya *cocoa* sasa leo unapomwambia mtu asubiri inashindikana.

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba niseme mambo machache ambayo ninaomba sana Serikali inisikilize hili zao katika dunia hii kokoa iliyopo Kyela ndiyo hamira ya *cocoa* inayotoka Ivory Coast, *cocoa* inayotoka Ghana kwa ubora kokoa yetu inaongoza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na kuna fununu...

**SPIKA:** Dakika moja ya kumaliza

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally Jumbe Mbunge wa Kyela, Mheshimiwa Condester Sichalwe atafatiwa na Mheshimiwa Jafari Chege.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii naomba kupitia Bunge lako Tukufu kwa heshima na taadhima niombe sana Serikali yangu Sikivu ya Chama Cha Mapinduzi ninaomba kwenu sana sana tunaiomba Serikali yetu tuwatazame wakulima walioko vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa kusema hayo simaanishi kwamba labda wakulima ambao wako mjini hawastahili kuombwa lakini Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi wakulima hawa ambao wako vijijini ndiyo ambao wamekuwa ni waaminifu kwetu mno katika kutupa kura na sehemu zingine hawaamini hata vyama vya upinzani wanaelewa ni CCM tu. Kwa hiyo, fadhila ya kuwalipa wakulima hawa ni sisi kuwatazama wakulima hawa jamani Benki ya Kilimo haiwafikii huko vijijini Benki ya Kilimo haiwafikii ndiyo maana wamegubikwa na wimbi la hawa watu ambao wanaitwa *AMCOS*. *AMCOS* mmewapa watu wa vijijini wawasaidie spidi ya watu wa vijijini hawafanani kabisa na spidi ya watu wa *AMCOS*, *AMCOS* ni waongo samahani Waheshimiwa wengine wametumia lugha na kusema ni matapeli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwenyewe nimehusika katika kusimamia kuendelea kuwaombea mkopo wapiga kura wangu wa Jimbo la Momba ambao walikuwa wameomba *AMCOS* nimepiga simu kwa mameneja kadhaa wa Branchi husika za wilaya mpaka kwa mameneja wa kanda kwa ajili ya kuendelea kuomba mkopo wananchi wameahidiwa kupewa mkopo kuanzia mwezi wa 12 mpaka sasa wanaendelea kuomba kilimo kinaanza kulimwa kuanzia

mwezi wa 11 mpaka wa 12 watalima nini? Hivyo Serikali yangu naomba kwa kuwa iko Benki ya Kilimo ambayo riba yake ni nafuu kwa wapiga kura hawa waaminifu wa Chama Cha Mapinduzi ambao tukienda tunapiga magoti na kugaragara kwao kuwaambia Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ni Sikivu basi tuwape kitu ambacho kinafanana na uelewa wao ambao ni Benki ya Kilimo na inatoa riba nafuu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ukisikia mchele mzuri ambao unalimwa Kamsamba unalimwa ndani ya Jimbo la Momba achilia tu kwamba tunalima na kusambaza kwenye mikoa mingine ambayo iko hapa Tanzania lakini mchele ambao tunalima ndani ya Jimbo la Momba tunasambaza mpaka nchi ambazo ziko SADC. Lakini cha kushangaza ndani ya Jimbo la Momba ikiwa kama lilivyo jimbo lenyewe tuna bonde kubwa kabisa ambalo linabeba na mto wa Momba lakini cha kusikitisha tuna skimu moja tu ya umwagiliaji na ambayo na yenyewe haifanyi kama ambavyo inatajikana. Skimu ya umwagiliaji ya Naming'ong'o.

Mheshimiwa Spika, lakini Pamoja na hayo Serikali imeshawahi kutoa kwenye skimu nyingine ya umwagiliaji ambayo iko lyendo, Kata ya Kapele Zaidi ya pesa milioni 800 na Wizara ya Kilimo wakaunda Tume kwa ajili ya kwenda kukagua skimu hii lakini mpaka sasa tunavyoongea hatujawahi kupewa hata majibu na hatujui nini kinaendelea kuanzia niko *Form four* na mpaka sasa ni Mbunge, jamani Serikali tunaomba wananchi hawa na wapiga kura hawa ni waadilifu na ni wachapakazi tunaomba tuwawezeshe. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini skimu ya umwagiliaji Naming'ong'o kaka angu Bashe nimekufuata mara kadhaa hii skimu Serikali imetoa hela nyingi Zaidi ya bilioni 4.7 ina matatizo kadhaa *farm layout* kuna shida *designing* na *drawings* zina changamoto *leveling farm roads* mwenyewe nimeitembelea ile skimu mara kadhaa mara nyingi nimeitembelea hakuna mifereji ambayo inaonyesha inatoa maji na inaingiza maji, zile njia zote za kupitishia maji kwenye

skimu zimejaa matope basi tunaomba mtupe *excavator* ili hata wataalamu ambao wako kule tuweze kukwangua wenyewe ile mifereji tunaomba sana.

Mheshimiwa Spika, lakini bonde hili lina zaidi karibu hekta 100,000 za kulima mpunga pamoja na mazao mengine ya umwagiliaji na mbogamboga. Lakini cha kushangaza ndiyo skimu hizo ambayo hata iliyopo yenyewe ni mbovu tunaomba kabisa tupate skimu ya umwagiliaji Kamsamba tupate skimu ya umwagiliaji Msangano, tupate skimu ya umwagiliaji Kasinde, tupate skimu ya umwagiliaji kubwa zaidi kwenye Mto Tesa tunaomba mtuongeze. Kwa sababu mazao yote ambayo tunayazalisha pale kwenye Jimbo la Momba ni tija kwa Mkoa ni tija kwa mikoa mingine lakini Taifa linakusanya mapato ya kutosha kwenye zile nchi za Jirani ambazo tunazitegemea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimekuwepo Zambia muda mrefu wanatumia mchele wa kutoka Tanzania tu na kama Jimbo la Momba ndiyo tuko pale mpakani Kongo wanatumia mchele wa Tanzania tu lakini hata nchi zingine ambazo ziko huko Kusini wanatumia mchele wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini siyo hayo tu kama ambavyo ameongea Mheshimiwa Deus Sangu tunalima pia mahindi yamkini tungeweza kulima hata mara tatu kwa mwaka lakini tutafanyaje mkopo hatupewi tumepewa matapeli *AMCOS*. Umwagiliaji hakuna sasa huyu mkulima huyu tunamtazamaje aliyepo vijijini? Tunamtazamaje.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho tunaishukuru sana Serikali kwa kutupa soko la mifugo na mazao pale Kakozi lakini tuna vijiji 72 na jiografia jamani ni ngumu. Jiografia ya Jimbo la Momba ni changamoto wapo Waheshimiwa Wabunge ambao wamefika hapo wanajua ile vijiji 72 ghala moja tu. Mtu aliyoko kule Kamsamba Usoche ili atoe mazao yake kabla yajafikisha kule juu Kakozi hayo maghala hakuna tuna

maghala mawili tu na lingine hili halijakamilika liko toka kipindi hicho. Tunaiomba Serikali tunaomba kuongezewa maghala hata kama hayatafika 72 kwenye kila Kijiji lakini angalau basi yafike hata 26 kwa kuanzia tunaomba sana Serikali ili tuweze kupandisha mazao yetu kufika pale Kakozi.

Mheshimiwa Spika, na jambo lingine la kumaliza tunaomba Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi tuwekewe mkakati mzuri namna gani hawa wakulima hawa wapimiwe ardhi zao ili wawe wanakopesheka na kwenye benki wenyewe wakienda peke yake ardhi ni *potential* tuko mpakani tunaishia tu kugawa ardhi kwa wazambia na Watanzania kwa sababu hakuna muundombinu mzuri ambao Serikali imeweka kwa wapiga kura hawa, naunga mkono. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Condester Sihalwe Mheshimiwa Jafari Chege utumalie *session* ya leo jioni.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru nichukue nafasi hii kukushukuru kabisa kwa kunipa nafasi kuchangia Wizara hii nyeti. Lakini pia nachukua nafasi hii kumshukuru Waziri, Naibu Waziri Pamoja na watendaji wote wa Wizara wakitambua kwamba wanaongoza Wizara ambayo ni mtambuka ni Wizara ambayo katika sekta ni Wizara toka tunapata uhuru tunazungumzia Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni Wizara ambayo ukitaja sekta zingine zote unaweza ukasema zimeanza baada ya Wizara hii ya Kilimo. Lakini nichukue nafasi hii kuwapongeza kwa kazi kubwa mnayoifanya changamoto ni nyingi wakati mwingine kuzimaliza kwa muda mfupi yawezekana isiwe kazi ya rahisi lakini tuna imani kwa sababu sasa tumempata Waziri kijana ambaye ni *Professor*, tumempaka Naibu Waziri kijana ni imani yangu sasa mtakwenda kubadilisha kilimo kutoka kwenye nadharia sasa iende kwenye vitendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kwamba kwa miaka yote toka uhuru hakuna ambacho hakijawahi kuandikwa kwa maana ya *research* kama utafiti kwenye zao lolote la kilimo nchi hii. Kazi kwenu sasa kwenda kutumia *research* zilizoandikwa na wataalamu hao ili sasa kutumia nafasi zenu za vijana muiondoe nadhania hii ya kilimo ambayo imekuwa ikizungumzwa na wananchi na Pamoja na Waheshimiwa Wabunge iende kuwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, lakini Wizara hii haiwezi kufanya mazuri kama haina fedha angalia tazama bajeti tunayoajadili sasa ni bilioni 2.9 kama haitaenda yote maana yake haya tunayozungumza ukiacha nje ya mifumo hii ambayo Wabunge wamekuwa wakilalamikia, maana yake bado haiwezi kufanya vizuri vile ambavyo wananchi wanahitaji. Nichukue nafasi hii kuiomba sana Serikali hii bilioni 2.9 iliyoombwa na Wizara hii wapeni yote ili angalau tunaporudi bajeti ya mwakani tuweze sasa kushikana mashati sawasawa tukiwa tumewapa fedha sasa za utekelezaji na uendelezaji wa utekelezaji wa Wiza hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie maeneo yangu mawili ndani ya jimbo langu eneo la kwanza ni eneo la kilimo cha umwagiliaji mradi wa Chereche nilikuwa naangalia taarifa ya Mheshimiwa Waziri hotuba yake na randama sijaona ikitajwa. Chereche ni mradi ambao wa umwagiliaji una heka Zaidi ya 350 unahudumia zaidi ya wananchi ambao walikuwa wakifanya shughuli pale Zaidi ya watu 300 na kitu.

Mheshimiwa Spika, mradi huu wa umwagiliaji umeanza toka mwaka 2002, lakini toka mwaka 2018 umesimama una miaka minne tunakwenda miaka mitano umesimama na haufanyikazi yoyote unaweza ukaona wananchi waliokuwa wanafanya shughuli za kiuchumi pale mpaka leo wanaenda wapi. Lakini nimeangalia kwenye bajeti humu nilikuwa naangalia kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri haupo tuna mradi wa umwagiliaji upo Kijiji cha Rabol Kata ya Rabol, Tarafa ya Loimbo una zaidi ya heka 250 kwa mara ya kwanza Serikali iliamua kufufua mwaka 2012 kwenda mwaka 2013 wakaitengea bajeti 2016

kwamba sasa tunakwenda kuufufua huu mradi ili uwanufaishe wananchi wa maeneo yale Kijiji cha Loimbo. Hivi ninavyozungumza mpaka leo ile bajeti 2016 haikwenda kwenye utekelezaji nimeangalia kwenye bajeti ya Serikali bajeti ya Mheshimiwa Waziri haimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuna mradi wa umwagiliaji Ochuna wananchi wanalima mpunga kule ni mradi wa umwagiliaji ambao wananchi masikini ya Mungu wanahangaika lakini wanachangamoto zao za miundombinu ndani ya ule mradi haipo ni imani yangu Mheshimiwa Waziri atakapokuwa amesimama kesho kufanya majumuisho aniambie na kwa sababu nimekwisha zungumza naye kabla ya hapa haina haja ya sisi tena kurudi kule na wakati ninaye Waziri ndani ya Bunge hili. Atoe tamko na atoe maelekezo wale watendaji wote ambao wamesahau kuingiza kwenye bajeti ili angalau sasa nitakaporudi na mimi Jimboni nirudi nikijua hawa wananchi wanatokaje hapa na wanakwendaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jafari Chege Waheshimiwa Wabunge niwashukuru sana wale wote ambao mmeweza kuchangia kutwa nzima ya leo na kwasababu tutaendelea na Wizara hii kesho pia wale ambao hamjapata nafasi leo basi mtapata nafasi kesho japo kwa kweli leo tumechukua wengi kadri tulivyoweza.

Kwa hiyo, bado kuna mikoa mingine haijasikika ya kutosha nilikuwa najaribu kusikiliza tangu asubuhi hapa sijasikia vizuri Kigoma, Mara ndiyo ameongea Mheshimiwa Jafari peke yake Kagera ameongea Mheshimiwa Conchester peke yake Singida hakuna aliyeongea Dodoma wameongea Mheshimiwa Toufiq peke yake, Iringa yote iko kimya Morogoro yaani ndiyo kabisa wako likizo, Tanga hamna kitu nafikiri hata nyinyi wenyewe mnaweza mkaona kabisa kwamba Pwani wako kimya, Iringa wakulima wakubwa hawasikiki wakisema chochote. *(Makofi)*



Waheshimiwa Wabunge, hata hivyo, *at least* watu wa korosho wameongea, watu wa tumbaku wameongea, watu wa mahindi wameongea na mazao mengine madogo madogo. Kwa hiyo, hata kwenye uwakilishi kwa upande wa waongeeji ni vizuri pakawa na hawa wa mikoa hii mingine nao wakapata nafasi ya kuongea pia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kesho tutajaribu kwenda hivyo ili tuone namna gani. Lakini pia Wabunge wanawake walioongea wachache sana na mimi kila wakati huwa nawaambia Waheshimiwa Wabunge wanawake hamjaja kukaa hapa mmekuja kusemea matatizo ya wananchi na wanawake mnaowawakilisha sehemu kubwa asilimia kubwa ni wakulima. Kwa hiyo, ni wakati wenu wa kusema siyo kusema kwa sababu usikike lakini kama huna cha kusema basi kaa kimya, lakini ni vizuri mka-*prove everybody wrong* kwa kwa *active* katika Wizara zile ambazo kwa kweli zinagusa Maisha kwa siku ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Kamati ya Kilimo nafikiri mmefuatilia mchango na michango mbalimbali ambayo inaendelea humu ndani mna kazi kubwa ya kufanya ku-*pick up* baadhi ya haya mambo ambayo yamejitokeza hapa kwa sababu sisi tutamalizana na Wizara kesho lakini ninyi ni jukumu lenu sasa kuyabeba na kuona hamuwezi kubeba yote ni mambo gani ambayo mnaona mnaweza kujikita ambayo kupitia hayo yanaweza yakawa na unafuu mkubwa Zaidi kwa upande wa uchumi wa wananchi wetu wa Tanzania. Jambo kama hili la masoko tuendeleo kuibana Serikali sababu ni kweli kwamba soko likikaa vizuri lina *trigger* karibu kila kitu kwenda kule chini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Mawaziri tufanye *network* ya kujua majirani zetu na masoko ya majirani zetu ili tuweze ku-*penetrate* huko na ni ukweli usiopingika hatuwezi kufanya hivyo kwa kukaa tu hapa. Tutakuwa tunapiga kelele hivi hivi maana vitu vingine vinataka *rapport* mara kunywa chai kidogo na wanaohusika, kahawa kidogo na nini huku mambo yanakwenda namna hiyo.

Kwa hiyo tuna nia njema ukiona wakulima hawa wanaongea Waheshimiwa Wabunge wanaongea kwa uchungu kwa kweli iko haja ya kufanya kitu fulani ili kilimo chetu kiweze kwenda mbele ndiyo ajira kubwa katika nchi yetu kilimo ndiyo tarajio la hii kundi kubwa la vijana wanaoitwa hawana ajira ajira yao kubwa ni kilimo. Kwa kweli kilimo kinalipa sana kuliko kijana anatafuta ajira ya shilingi laki tatu kwa mwezi anaweza akafanya kilimo akapata zaidi ya milioni moja kwa mwezi huyo huyo akawa na Maisha bora zaidi.

Niliwahi kuwapa mfano wa kijana mmoja ambaye tulimtembelea kule, nirudie tena, enzi hizo tulimtembelea kijana mmoja kule Uganda na yeye alikuwa anafuga ng'ombe wa maziwa hawazidi 50 katika eneo fulani karibu na kule kwa Rais Museveni, kule kwa Kitura maeneo fulani jirani na kule, ana kaeneo kake ambako wala ekari 30 au 40 hazifiki sana ana nyumba nzuri na gari nzuri iko pale. Kule Uganda gari ya maana sana ni Prado enzi hizo hata sasa nafikiri.

Tukamuuliza unadhani Serikali ikufanyie nini ili mambo yako yakae vizuri zaidi. Akasema *what Government? Government do what*, lakini nadhani Serikali inge... Akasema *no I don't need government* mimi sihitaji Serikali likawa ni jibu la ajabu sana. Mtanzania ukimtaji Serikali kwa hiyo tukamdodosa zaidi wewe huna kitu ambacho Serikali akasema nimekumbuka kitu kimoja *security* yaani pakiwa na usalama ng'ombe wangu wasiibiwe wala nini mimi ninachohitaji usalama tu pakishakuwepo usalama mengine yote niachieni mwenyewe namudu.

Kwa kweli Serikali ikishaweka usalama sasa wewe unataka nini tena changamka tu uweze kwenda mbele. Tunachohitaji Serikali ikishaweka usalama sasa ipunguze *interference* basi ipunguze *interference* kwamba akitaka kufanya hivi umefika akilima choroko umefika, akilima dengi upo, akilima mahindi wewe kwa sababu bahati nzuri kwenye Tanzania usalama tumefanikiwa sana kwa kiwango kikubwa sasa tuwape watu nafasi ya kupumua basi nyinyi mtashangaa

kuona tu maendeleo ambayo yanajitokeza yatakuwa ni makubwa sana kwa vijana wetu. *(Makofi)*

Kwa sababu tuna kila sifa ya kuweza kuendelea kwasababu usalama wetu tuchukue nafasi hii kuvipongeza sana vyombo vya ulinzi na usalama kwa sababu hiyo ndiyo *basic*. Ukishakuwa uko salama mali yako iko salama shamba lako liko salama ng'ombe wako yuko salama anazaa vizuri nakadhalika yaliyobaki yaliyo mengi unaweza kufika mbali sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri tuko na nyinyi wala hakuna wasiwasi lengo letu ni jema tunajua na nyinyi mnajitahidi usiku na mchana kupambana na hii hali ili tuweze kuvuka hapo tulipo na ndiyo maana kwa kumaliza huwa tunasemaga ile *blue print* sijui kitu gani ile ije. Tuone ni maeneo gani ambayo yanatakiwa tuyafanyie kazi ambayo yatatoa unafuu mkubwa zaidi katika biashara zetu katika masuala ya biashara za mazao ya kilimo nakadhalika ili tuweze kwenda mbele kwa spidi zaidi kama nchi.

Kwa kuwa shughuli zilizopangwa leo zimekamilika zote basi kwa hatua hii niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.50 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 25 Mei, 2021, Saa Tatu Asubuhi)*